16 APRILI, 2025

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Saba – Tarehe 16 Aprili, 2025

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa, tuketi.

Katibu.

NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

WAZIRI WA FEDHA:

Ripoti Kuu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia tarehe 30 Juni, 2024 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Central Government for the Financial Year Ending 2023/2024);*

Ripoti Kuu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia tarehe 30 Juni, 2024 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General*

on the Local Government Authorities for the Financial Year Ending 2023/2024);

Ripoti Kuu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia tarehe 30 Juni, 2024 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Development Projects for the Financial Year 2023/2024);*

Ripoti Kuu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia tarehe 30 Juni, 2024 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of the Public Authorities and Other Bodies for the Financial Year Ending 2023/2024);*

Ripoti ya Jumla ya Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalumu kwa Kipindi Kinachoishia tarehe 31 Disemba, 2024 *(The Annual General Report on the Performance and Specialized Audits for the Period Ending 31st December, 2024);*

Ripoti Kuu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia tarehe 30 Juni, 2024 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Information Systems for the Financial Year Ending 2023/2024);*

Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Huduma za Vivuko *(The Performance Audit Report on the Management of Ferry Operations);*

Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Baharini *(The Performance Audit on the Regulation of Maritime Transport Services);*

Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utoaji wa Msaada na Udhibiti wa Tiba za Asili *(The Performance Audit Report on the Provision of Support and Regulation of Traditional Medicine);*

Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Utoaji wa Vyeti vya Vizazi na Vifo *(The Performance Audit Report on the Identification, Registration and Issuance of Birth and Death Certificates);*

Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Data za Kijiosayansi katika Sekta ya Uchimbaji Madini *(The Performance Audit Report on the Management of Geoscientific Data in the Mining Sector);*

Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utekelezaji wa Mradi wa Kujenga Kesho Bora – Mpango wa Vijana kwa Biashara ya Kilimo *(BBT – YIA) (The Performance Audit Report on the Implementation of Building a Better Tomorrow – Youth Initiative for Agribusiness (BBT – YIA));*

Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utoaji wa Huduma za Ugani kwa Rasilimali za Mifugo *(The Performance Audit Report on the Provision of Extension Services to Livestock Resources);*

Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Huduma za Hali ya Hewa *(The Performance Audit Report on the Management of Meteorological Services);*

Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Vifaa vya Kielekitroni vya Kodi katika Kukusanya Mapato *(The Performance Audit Report on the Management of Electronic Fiscal Devices (EFDs) in Revenue Collection);*

Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Biashara ya Kaboni *(The Performance Audit Report on the Management of Carbon Trade);*

Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Kukabiliana na Hali ya Jangwa *(The Performance Audit Report on the Implementation of the National Action Plan for Combating Desertification);*

Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi na Matumizi ya Teknolojia za Habari na Mawasiliano katika Mamlaka za Udhibiti katika Utoaji wa Huduma za Udhibiti *(The Performance Audit Report on the Management and Utilization of ICT in Regulatory Authorities in the Delivery of Regulatory Services);*

Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Gharama za Mifumo ya TEHAMA ya Serikali iliyotengenezwa Ndani *(The Performance Audit Report on Cost-effectiveness of Internally Developed Government ICT System);*

Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Mafuriko *(The Performance Audit Report on the Management of Floods);* na

Taarifa ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi za Ufanisi zilizofanyika na Kuwasilishwa Bungeni Mwaka 2021 *(The Follow-up Report on the Implementation of the Controller and Auditor General's Recommendations from the Fourteen Performance Audit Reports Issued and Tabled to the Parliament in April, 2021*).

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

SPIKA: Ahsante sana.

Katibu.

NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali, Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 82

Idadi ya Madaktari na Wauguzi Maeneo ya Vijijini

MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza idadi ya madaktari na wauguzi hasa maeneo ya vijijini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutenga bajeti na kuajiri watumishi wa kada mbalimbali za afya nchini. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 – 2024/2025, jumla ya watumishi wa kada mbalimbali za afya 34,720 wameajiriwa. Wataalamu hao ni pamoja na madaktari 1,851; wauguzi 10,213 pamoja na kada nyingine 22,656. Aidha, zaidi ya 70% ya watumishi hawa wamepangiwa kazi kwenye vituo vya maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti na kuajiri watumishi wa kada mbalimbali za afya na kuwapanga katika maeneo yenye upungufu hususan vijijini katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Munira, swali la nyongeza.

MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza ninapenda kuipongeza Serikali kwa majibu mazuri, lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, watumishi wengi hasa kada ya afya wanaopangiwa maeneo ya vijijini wanakuwa wanaomba uhamisho pindi tu wanapopata ajira hizo; je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wanaboresha makazi kwa watumishi wa kada ya afya, hasa maeneo ya vijijini ili kuweza kuwaruhusu watumishi hawa wanapoajiriwa kubakia kwenye vituo vyao vya kazi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ni kweli, kama alivyosema Mheshimiwa Munira Mustapha kwamba kumekuwa na changamoto ya baadhi ya watumishi wanaoajiriwa maeneo ya vijijini kuomba kuhamia maeneo ya mijini. Sasa hivi Serikali imeweka utaratibu kwanza kwa kuhakikisha kwamba tunadhibiti wimbi la uhamisho wa watumishi kutoka vijijini kwenda mijini kwa sababu wana hoja ya msingi kwamba wananchi wa vijijini pia wanahitaji kupata huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hilo, moja ya hatua ambazo Serikali imechukua ni pamoja na kuboresha mazingira ya kazi ya vituo vya vijijini kwa maana ya ujenzi wa vituo bora zaidi vya kisasa, vilevile kujenga nyumba za watumishi (madakatari na wauguzi).

Mheshimiwa Spika, katika miaka hii mitatu, jumla ya nyumba 270 *three in one* zimejengwa ambazo zina uwezo wa kuchukua kaya 810 za watumishi wa sekta ya afya. Zoezi hili ni endelevu, hivyo tutaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kujenga nyumba za watumishi maeneo ya vijijini, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, swali la nyongeza.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kuniona, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, katika Jimbo la Makambako Kituo cha Afya Lyamkena na kule Kitandililo hatuna watumishi.

Je, ni lini Serikali itapeleka watumishi ili wananchi waweze kupata huduma?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Serikali imekuwa ikiajiri watumishi na kuwapeleka katika Halmashauri ya Makambako na halmashauri zote kote nchini. Kama ambavyo jibu langu la msingi linasema, katika miaka hii minne Serikali imeajiri zaidi ya watumishi 34,720 na Halmashauri ya Makambako imeendelea kupata watumishi.

Mheshimiwa Spika, ninafahamu kuwa ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Kitandililo na Lyamkena bado vina upungufu wa watumishi. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kila kibali cha ajira kitakapotoka tutahakikisha tunapeleka watumishi katika vituo hivyo vya afya. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 83

Wanawake na Watoto Kulazwa Wodi Moja Kituo cha Afya Iramba – Serengeti

MHE. GHATI Z. CHOMETE aliuliza: -

Je, kwa nini katika Kituo cha Afya Iramba wanawake na watoto wanalazwa katika wodi moja?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Iramba katika Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti kinahudumia wananchi wapatao 77,027. Serikali inatambua upungufu wa miundombinu katika vituo vya afya, hali inayopelekea baadhi ya vituo kukosa miundombinu ya msingi ikiwemo wodi za kulaza watoto, wanawake na wanaume.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti imetenga shilingi milioni 75 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa wodi ya watoto, wanawake na wanaume katika Kituo cha Afya cha Iramba.

SPIKA: Mheshimiwa Ghati Chomete, swali la nyogeza.

MHE. GHATI Z. CHOMETE: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana, lakini pia ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Kituo cha Afya cha Iramba ni kituo cha muda mrefu ambacho mpaka sasa miundombinu ni mibovu sana.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujua; je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha inaondoa tatizo hili la watoto na wanawake wa Kituo cha Afya cha Iramba kulala pamoja, yaani wodi moja?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Kituo cha Afya cha Ikizu kina changamoto kama hiyo hiyo kwamba wanawake wanaosubiri kujifungua, wanawake waliojifungua na waliofanyia *operation* wanalala wodi moja.

Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuondoa tatizo hilo katika Kituo cha Afya cha Ikizu? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika,

ahsante sana, ninamhakikishia Mheshimiwa Zephania Chomete kwamba kwanza Serikali ilishafanya tathmini na kuorodhesha vituo vyote vya afya chakavu na kongwe na tayari tunakwenda kuandaa mpango mkakati wa ukarabati na upanuzi wa vituo hivyo vya afya. Katika hatua hiyo tutahakikisha pia kwamba Kituo cha Afya cha Iramba kinazingatiwa na kupewa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba kuna upungufu wa wodi za wananume na wanawake. Serikali imeshaanza kuchukua hatua kwa kutenga shilingi milioni 75 katika mwaka wa fedha ujao wa fedha wa 2025/2026. Tutaanza ujenzi wa wodi hizo kupitia mapato ya ndani, lakini Serikali Kuu pia itatenga fedha kwa ajili ya kwenda kujenga wodi hizo.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, kuhusiana na Kituo cha Afya cha Ikizu, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa suala la Kituo cha Afya cha Ikizu linafahamika na limeshawasilishwa, limewekwa kwenye Mpango wa Benki ya Dunia kwa ajili ya kwenda kukitanua na kuongeza majengo, kwa maana ya wodi za wanawake, watoto pamoja na wananume.

SPIKA: Mheshimwa Twaha Mpembenwe, swali la nyongeza.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, wapigakura wangu wa Kata ya Bungu wanataka kujua; je, ni lini Serikali itakamilisha ile ahadi ya kupeleka shilingi milioni 200 ili kuboresha miundombinu katika kituo kile cha afya?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Bungu ni moja ya vituo ambavyo vinahudumia wananchi wengi na Serikali ilishapeleka fedha kwa hatua za mwanzo. Ninamhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba

tutapeleka fedha kwa ajili ya kukitanua Kituo cha Afya cha Bungu ili kiweze kutoa huduma bora sana kwa wananchi. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge wa Babati Mjini, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Flatei Massay.

Na. 84

Wakulima Kulipishwa *Crop Cess* Zaidi ya Mara Moja

MHE. FLATEI G. MASSAY K.n.y. MHE. PAULINE P. GEKUL aliuliza:-

Je, ipi kauli ya Serikali kwa wakulima na wafanyabiashara kulipishwa *crop cess* zaidi ya mara moja wanapovusha mazao yao halmashauri nyingine?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ushuru wa mazao katika halmashauri hutozwa kwa mujibu wa kifungu cha 16(1)(a) na (b) *(cash crops and food crops)* cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290. Sheria hiyo imeweka kiwango cha asilimia tatu ambacho hutozwa kwa mazao yanayozidi tani moja yanayosafirishwa kwenda nje ya halmashauri. Aidha, ushuru wa mazao hutozwa mara moja kwa wafanyabiashara wanaonunua mazao kutoka kwa wakulima na kuyasafirsha nje ya halmashauri.

Mheshimiwa Spika, mfanyabiashara anapaswa kuwa na stakabadhi ya ushuru aliolipia muda wote wa usafirishaji wa mzigo ili kuepuka usumbufu. Baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu wamekuwa wakisafirisha mazao hayo kidogo kidogo kwa hutumia maguta, pikipiki na bajaji ili yasifikie ujazo wa tani moja ambayo hulipiwa ushuru. Wafanyabiashara hao wanapobainika hutozwa ushuru wa mazao kulingana na wingi wa mazao waliyoyasafirisha.

Mheshimiwa Spika, aidha, mamlaka zote za Serikali za Mitaa zihakikishe zinasimamia utoaji wa ushuru wa mazao kwa mujibu wa sheria.

SPIKA: Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tabia hii imekuwa inajitokeza mara nyingi, hasa kwenye Halmashauri ya Babati Mjini na Babati Vijijini, na Halmashauri ya Mbulu, kwa sababu ziko karibu karibu na wameweka mageti: -

Je, una mpango gani wa kuwaelekeza moja kwa moja wakurugenzi ili kutotoza ushuru huu mara mbili?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuna wengine wanachukua mazao shambani kuleta nyumbani: -

Je, ni nini kauli ya Serikali kuhusu hili na hawa hawasafirishi, wanapeleka ghalani (nyumbani) kama matumizi ya kawaida?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza nitumie nafasi hii kuwasisitiza wakurugenzi wote kote nchini, lakini hususan Wakurugenzi wa Halmashauri ya Babati Mjini, Vijijini na Mbulu pamoja na halmashauri nyingine zote za Mkoa wa Manyara wahakikishe wanatoza ushuru wa mazao kwa kufuata sheria. Wananchi wote ambao ni wakulima wanaosafirisha mazao hayo kupeleka nyumbani hawatakiwi kutozwa ushuru wa mazao, isipokuwa kwa wale ambao wanasafirisha nje ya halmashauri zaidi ya tani moja na kwa maana ya shughuli za kibiashara.

Mheshimiwa Spika, suala la pili kuhusu wananchi ambao ni wakulima katika halmashauri hizo wanafahamika, kwa hiyo, ikiwa mwananchi anasafirisha mazao yake kutoka shambani kwa maana ya ujazo wa zaidi ya tani moja kupeleka nyumbani hatakiwi kutozwa ushuru na kwa sababu viongozi wa halmashauri

wa vijiji wanawafahamu wakulima hao, basi ninatumia nafasi hii kuwashauri wakulima wahakikishe wanatoa taarifa katika vijiji vyao kwamba wanasafirisha mazao hayo kupeleka nyumbani kwa maana ya kuepuka ushuru, lakini pia na changamoto nyingine, lakini nitumie nafasi hii kuwasisitiza wakurugenzi kusimamia ushuru huo kwa kufuata sheria.

SPIKA: Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, utekelezaji wa sheria hii ya kukusanya ushuru katika halmashauri zetu umekuwa na changamoto kutoka eneo moja hadi eneo lingine. Je, Serikali sasa ipo tayari kuboresha kwa kutunga sheria au kuleta maboresho ya sheria hii ya *cess?*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, utozaji wa ushuru wa mazao *crop cess* upo kwa mujibu wa sheria na halmashauri zote zinalazimika na zinawajibika kufuata sheria hiyo. Tunafahamu kuna mapungufu ya baadhi ya halmashauri kutozingatia utozaji wa ushuru huu kwa mujibu wa sheria. Ninaomba nitumie nafasi hii nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tumeshatoa maelekezo kwa Makatibu Tawala wa Mikoa, tumeshatoa maelekezo kwa wakurugenzi na wataalamu wote katika halmsahauri zetu kuhakikisha wanazingatia utozaji kwa kufuata sheria. Ofisi ya Rais, TAMISEMI itaendelea kufuatilia kwa karibu na pale ambapo utapata changamoto kwenye halmashauri Waheshimiwa Wabunge watatufikishia taarifa na wananchi ili tuweze kuchukua hatua na kudhibiti changamoto hiyo, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri, tumehamasisha vijana kujiunga katika vikundi na kupata mikopo ya halmashauri, wapo wanaobeba ndizi kutoka Wilaya la Rungwe na kupeleka Dar es Salaam pale Mahakama ya Ndizi kuuza, lakini sheria hii inawaathiri sana na hasa pale Mikumi kwa sababu magari mengi yanasimamishwa na mazao haya yanaharibikia njiani.

Mheshimiwa Spika, mnaonaje sasa kama kuna haja ya Bunge lijalo kuweza kubadilisha sheria na hasa kwa wale tuliowashawishi kuchukua mikopo ya halmashauri, kwa sababu wanashindwa kurudisha kutokana na sheria hii?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ninaomba tupokee hoja ya Mheshimiwa Mwakagenda ni hoja ya msingi na nzuri na sisi Serikali tukaifanyie tathmini kuona uwezekano wa kuiboresha au kuweka mazingira mazuri zaidi hususan kwa maeneo hayo ambayo wananchi wanasafirisha mazao kutoka halmashauri moja kwenda katika masoko makubwa Dar es Salaam na maeneo mengine.

SPIKA: Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Ulyankulu, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Omari Kigua.

Na. 85

Ukarabati wa Shule za Msingi – Ulyankulu

MHE. OMARI M. KIGUA K.n.y. MHE. REHEMA J. MIGILLA aliuliza:-

Je, lini Serikali itafanya ukarabati wa Shule za Msingi Taba, Mkindo, Kaswa, Mbeta na Milambo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, mwaka 2024/2025 Serikali ilitoa shilingi milioni 380 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya Shule za Msingi za Seleli, Makingi, Ntyemo, Kagunga, Kabanga, Unampanda na Kashishi za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua. Katika mpango na bajeti ya mwaka 2025/2026 Serikali inatarajia kutumia shilingi milioni 270 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya shule za msingi 10 zikiwemo Shule za Milambo, Ichemba, Kaswa, Mbeta, Taba na Mkindo. Serikali itaendelea kutenga fedha ya ukarabati wa miundombinu ya shule chakavu zikiwemo Shule za Msingi Taba, Mkindo na Milambo kadiri ya upatikanaji wa fedha.

SPIKA: Mheshimiwa Omari Kigua, swali la nyongeza.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Rehema, niipongeze Serikali kwa majibu na matumaini makubwa kwa wananchi wa Ulyankulu lakini pamoja na hayo ni kwamba Shule ya Msingi Mkindi katika Jimbo hilo la Ulyankulu ni kwamba mvua iliyonyesha tarehe 10 Aprili, iliezua madarasa matano. Je, nini mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba madarasa yale yanarejeshwa katika hali ya kawaida?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Shule ya Msingi Masagalu katika Wilaya ya Kilindi ni shule yenye historia kubwa ambayo ilijengwa mwaka 1948 ikiwa ni *middle school,* lakini shule ile imechakaa, nini mpango mkakati wa kuikarabati shule ile? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA): Mheshimiwa Spika, ni kweli tarehe 10 Aprili, 2025 mvua na upepo mkali uliezua madarasa matano katika Shule ya Msingi ya Mkindu. Kwa kweli Mheshimiwa Rehema Migilla amekuwa akifanya ufuatiliaji wa hali ya juu kuhakikisha kwamba zinachukuliwa hatua kwa ajili ya kurejesha

miundombinu katika shule hizo ili pale shule zitakaporejea wanafunzi waweze kutumia madarasa haya matano.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kuchukua hatua za dharura kutumia mapato ya ndani kwenda kurekebisha madarasa hayo matano ili madarasa hayo yaweze kutumika pindi shule zitakapofunguliwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali la pili la Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na shule chakavu katika Jimbo lake la Kilindi, ninaomba niendelee kutoa taarifa kwamba Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi cha miaka minne imefanya uwekezaji wa zaidi ya shilingi trilioni 5.1 katika sekta ya elimu msingi na sekondari. Katika kipindi cha miaka hiyo shule 832 chakavu za msingi zimekarabatiwa.

Kwa hiyo, ninaomba nitumie nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea na jitihada hizo na itafika katika shule hii katika Jimbo lako kwa ajili ya kuhakikisha inafanyiwa ukarabati ili iweze kuwa katika hadhi nzuri na wanafunzi wetu wapate sehemu nzuri ya kusoma.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, aah, utaratibu ni ule ule jamani tunaelekea Bunge la mwisho hili, anaposimama muuliza swali ndipo unaposimama na wewe mwenye nia, ukisimama baadaye wewe keti tu. Nitawaita wale waliosimama mwanzoni kuonesha nia hiyo, lakini nenda moja kwa moja kwenye swali. Maswali yawe mafupi, majibu pia mafupi.

Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, swali la nyongeza.

MHE. JONAS V. ZEELAND: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Shule ya Msingi Mnyanza, Shule ya Msingi Mbogo, Masalaka, Mvomero, Kisimagulu, Kichangani, Kikeo na Melela hizi ni shule kongwe sana na zina madarasa chakavu sana...

SPIKA: Swali.

MHE. JONAS V. ZEELAND: Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani sasa kutenga fedha kwa ajili ya kuzikarabati na kuongeza vyumba vipya vya madarasa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA): Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa swali hili ambalo nia yake ni kuhakikisha miundombinu katika shule hizi za msingi inaweza kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kuendelea kuwakumbusha Wakurugenzi wa Halmashauri kufanya tathmini katika shule hizi chakavu na kuweka katika mpango na bajeti na kwa kuanzia kwenye mapato ya ndani ili shule hizi ziweze kufikiwa na kufanyiwa ukarabati. Kwa hiyo, kwa nafasi hii ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itafika katika shule hizi chakavu ili iweze kuzirekebisha na ziwasaidie wanafunzi wetu.

SPIKA: Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza, aah samahani Mheshimiwa Samweli Hhayuma, swali la nyongeza.

MHE. SAMWELI X. HHAYUMA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itapeleka fedha Shule ya Msingi Bassodesh ambayo ni shule maalumu kwa watoto wa wafugaji na ni shule ya bweni ila majengo yake yaweze kukarabatiwa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA): Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi cha miaka minne imefanya uwekezaji mkubwa wa zaidi shilingi trilioni 5.1 katika upande wa kuboresha elimu msingi na elimu sekondari. Ninaomba

nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge dhamira ya Serikali ni kufika katika shule nyingi zaidi kuziboresha kwa ajili ya kuhakikisha watoto wetu wanapata maeneo mazuri ya kujifunzia na walimu pia wanapata maeneo mazuri ya kufundishia. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali itafika katika shule alizozitaja katika jimbo lake kwa ajili ya kuhakikisha zinakarabatiwa na zinakuwa katika hadhi nzuri.

SPIKA: Mheshimiwa Shabani Shekilindi, swali la nyongeza.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, je, ni lini Serikali itapeleka pesa za ukarabati katika Shule ya Msingi Makanya pamoja na Shule ya Msingi Kwayi maana shule hizi zimechoka na ni za zamani mno tangu mkoloni?

Mheshimiwa Spika, ninaomba majibu kwa Mheshimiwa Naibu Waziri.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA): Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Shekilindi kwamba katika kipindi cha miaka minne shule za msingi chakavu 832 zimefikiwa. Nimhakikishie kuwa Serikali tayari imeshaanza kuzifikia shule hizi chakavu na itaendelea kufikia shule nyingi zaidi. Nimhakikishie kwamba na yeye katika jimbo lake Serikali itafika kwa ajili ya kufanya ukarabati katika shule alizozitaja.

SPIKA: Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato, Mbunge wa Bukoba Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 86

Barabara ya *Lake Oil* - Ijuganyodo hadi Kyamunene - Bukoba Mjini

MHE. STEPHEN L. BYABATO aliuliza: -

Je, lini Barabara ya *Lake Oil* - Ijuganyodo hadi Kyamunene itajengwa kwa kiwango cha lami?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/2025 Barabara ya *Lake Oil* – Ijuganyodo hadi Kyamunene imetengewa shilingi milioni 40 kwa ajili matengenezo ya changarawe urefu wa kilometa 2.078 na ujenzi wa mifereji mita 800. Aidha, mkandarasi wa kazi hiyo ameshapatikana na anatarajiwa kuanza hivi karibuni. Katika mwaka 2025/2026 barabara hiyo pia imewekwa kwenye mpango wa bajeti kwa kutengewa shilingi milioni 33 kwa ajili ya matengenezo ya kiwango cha changarawe urefu wa kilometa mbili ili kukamilisha urefu wa kilometa 4.078.

SPIKA: Mheshimiwa Stephen Byabato, swali la nyongeza.

MHE. STEPHEN L. BYABATO: Mheshimiwa Spika, ahsante, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali madogo mawili.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni ya kimkakati kwa Manispaa yetu ya Bukoba inaenda kwa mwekezaji mkubwa wa shule ambazo zinafanya vizuri kitaifa za Kaizirege na Kemebos na yeye amekuwa akishirikiana na Serikali kutengeneza barabara hii. Sasa ninaomba *commitment* ya Serikali kwamba ni lini itawekewa lami ili iendelee kuhudumia vizuri mwekezaji huyu, lakini na wakazi wengine wa maeneo hayo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nilimwomba juzi Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwamba Mradi wa *TACTIC* utakapokamilika basi usainiwe pale Bukoba Mjini ili Wana-Bukoba Mjini waweze kuona kwamba jambo hili linaanza kufanyika. Sasa ninaomba kujua ni lini mradi huo utasainiwa ili barabara zaidi ya kilometa 10 ziweze kutekelezwa katika Jimbo la Bukoba Mjini? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA): Mheshimiwa Spika, ninaomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake ambayo nia ya kimsingi anataka kuona miundombinu ya barabara inaboreshwa katika jimbo lake. Kuhusiana na swali lake la mwanzo kama nilivyotangulia kujibu katika majibu ya msingi kwamba barabara hii ya *Lake Oil* - Ijuganyodo ipo katika mpango wa kufanyiwa ukarabati lakini lengo na nia ni kuijenga barabara hii katika hadhi ya lami.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika kipindi cha miaka minne tayari katika Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba jumla ya shilingi bilioni 9.6 zimewekezwa kwa ajili ya kukarabati na kujenga barabara za lami na mtandao wa lami umeongezeka kutoka kilometa 34.29 mpaka sasa mtandao wa lami ni kilometa 43.54. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kuongeza mtandao huu wa lami na itaifikia barabara hii muhimu kabisa ya *Lake Oil* – Ijuganyodo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili Mheshimiwa Mbunge ameulizia kuhusiana na utekelezaji wa Mradi wa *TACTIC,* ni kweli Manispaa ya Bukoba Mjini na yenyewe ni miongoni mwa miji 45 ambayo inanufaika na Mradi huu wa *TACTIC*. Kwa awamu hii au kwa wakati huu tuliokuwa nao tayari mradi wa ujenzi wa barabara kilometa 10 katika jimbo la Mheshimiwa Mbunge unaendelea na *evaluation* na tunatarajia mwezi Mei tutasaini mikataba ili mkandarasi sasa aweze kukabidhiwa *site* na aanze ujenzi.

Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge yeye na wananchi wake wa Manispaa ya Bukoba Mjini wakae mkao wa mapokeo, barabara hizi zinakuja kujengwa kupitia Mradi wa *TATIC* pamoja na miundombinu mingine ya soko na stendi. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa barabara ya kutoka Kahama - Nyang'olongo – Bukwimba - Kharumwa mpaka Busolwa magari makubwa na mazito yameharibu barabara hiyo. Je, Serikali itapeleka lini fedha kwa ajili ya kufanya matengenezo ya kawaida?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA): Mheshimiwa Spika, katika Serikali ya Awamu ya Sita bajeti ya *TARURA* imeongezeka maradufu kutoka bajeti ya shilingi bilioni 275 kwa mwaka mpaka sasa bajeti ya *TARURA* imefikia shilingi bilioni 710. Lengo ni kufikia mtandao mkubwa zaidi wa barabra hizi ambazo zinahudumiwa na *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunatambua umuhimu mkubwa wa barabara aliyoitaja hasa kiuchumi, lakini kwa kuwasaidia wananchi kufikia huduma za kijamii. Nimhakikishie kuwa Serikali itafika kuja kutengeneza barabara hii.

SPIKA: Mheshimiwa Subira Mgalu. Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, swali la nyongeza.

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Ujenzi wa Barabara ya Akeri hadi Ndoombo kwa kiwango cha lami umesimama sasa hivi kwa takribani mwaka mmoja na nusu; je, ni lini Serikali inakwenda kupeleka pesa sasa hivi kwa ajili ya kumaliza hiyo kazi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA): Mheshimiwa Spika, ninaomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, amekuwa akifuatilia kwa ukaribu sana kuhakikisha katika jimbo lake miundombinu ya barabara hizi zinazohudumiwa

na *TARURA* zinaweza kujengwa ziwe kwenye hadhi nzuri na kuweza kuwasaidia wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa tutaendelea kufuatilia ili kuhakikisha mradi huu kama kuna changamoto yoyote unakwamuliwa ili uweze kuendelea na uweze kukamilika na uweze kuwanufaisha wananchi wako.

SPIKA: Mheshimiwa Priscus Tarimo, swali la nyongeza.

MHE. PRISCUS J. TARIMO: Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana, kwa kuwa Serikali imeshatoa fedha kwa ajili ya barabara mbili kutoka *Clock Tower* kuja *YMCA* na kwa kuwa Barabara ya Arusha nayo imeshafikia hatua ya utangazaji kwa ajili ya *double road*. Je, ni lini Serikali itazirejesha fedha kwa ajili ya *double road* kutoka *YMCA* mpaka *KCMC* ambazo zilisombwa kutokana na mafuriko yaliyotokea na hiyo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA): Mheshimiwa Spika, ninaomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri na niendelee kumhakikishia kwamba ahadi za viongozi wakuu ni kipaumbele namba moja katika mipango ya utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Ninaomba nimhakikishie kwamba Serikali tutafuatilia kuhakikisha kwamba barabara hizi alizozitaja zinaweza kupatiwa fedha na zinaweza kujengwa ziwe katika hadhi nzuri ili ziweze kuwanufaisha wananchi wake.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 87

Mafunzo kwa Watumishi Kabla ya Kustaafu

MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kufuatilia waajiri ili wawe wanatoa mafunzo kwa watumishi kabla ya kustaafu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa maelekezo kwa waajiri kupitia Kanuni G.1(7) ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za mwaka 2009, kuhakikisha wanaandaa mipango ya mafunzo kwa watumishi na kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo *(training need assessment),* kutenga bajeti na kusimamia utekelezaji wake. Katika kutekeleza maelekezo hayo, kwa kipindi cha mwaka 2022/2023 hadi mwaka 2024/2025, jumla ya watumishi 3,036 kutoka kwa waajiri mbalimbali walipatiwa mafunzo kabla ya kustaafu katika Chuo cha Utumishi wa Umma. Hata hivyo, Serikali itaendelea kuwasisitiza waajiri kuhakikisha suala la mafunzo kwa watumishi kabla ya kustaafu linapewa kipaumbele katika utumishi wa umma, ninakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage, swali la nyongeza.

MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE: Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuhusisha mifuko ya hifadhi ya jamii hata kutoa elimu kwa wastaafu watarajiwa kwa sababu wanasema wanatoa kwa muda mfupi na kwao unaona haina tija, kwa hiyo hili

pengine ni gharama hii mifuko inayohifadhi fedha zao kwa nini isihusishwe ikawa muhusika mkuu wa kutoa elimu kwa hawa wastaafu watarajiwa kwa kipindi cha kutosha?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Serikali ina mpango gani kutoa upendeleo kwa wastaafu ili kupata uwekezaji katika hatifungani za *BOT* kama ilivyo kwa baadhi ya taasisi chache? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Alice kwa namna anavyofuatilia masuala ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza, ameuliza ni namna gani Serikali tuna mpango wa kuihusisha mifuko ya jamii katika kutoa elimu ya wastaafu kabla hawajastaafu.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge jambo hili tumeliweka kwenye utekelezaji na taasisi za waajiri zimeanza sasa kuweka mpango wa kushirikiana na mifuko hii ya hifadhi ya jamii kutoa elimu. Pia tunahakikisha sasa tumetoa maelekezo kama Serikali, elimu hii inatolewa mapema kwa sababu wengine wamekuwa wakitoa elimu hiyo kwa wastaafu mwezi mmoja kabla ya kustaafu ambayo inakuwa haiwasaidii, sasa tumejipanga kutoa elimu hii mapema ili kumpa nafasi mstaafu anapostaafu anakuwa tayari anajua afanye nini baada ya kumaliza utumishi wake wa umma.

Mheshimiwa Spika, juu ya kuwekeza kwenye hatifungani; Serikali pamoja na elimu ambayo tumesisitiza kutoa kwa wastaafu ni kuwekeza kwenye hatifungani kwa maana ni sehemu ambapo *risk* yake ni ndogo. Kupitia mfuko wetu wa *UTT AMIS* tumeanzisha *product* ya *Wekeza Bond* kwa maana ya *Bond Fund* ambayo inatoa masharti nafuu kabisa na ambayo inamwezesha mstaafu kupata gawio lake kila mwezi.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, swali la nyongeza.

MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA: Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na mpango mzuri wa Serikali ambao upo kwa ajili ya watumishi wanaotarajia kustaafu sasa; je, ni nini hatua ya Serikali kwa wale ambao walistaafu zamani na hawakuwa na bahati ya kupata haya mafunzo, lakini bado wanadai mafao yao hawajayapata wakiwemo wale waliokuwa watumishi wa *East Africa? (Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mabula, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna baadhi ya wastaafu ambao hawakupata faida ya mafunzo haya, lakini kama Serikali tumeweka mkakati na mwingine, bado wanaendelea kudai mafao haya. Tutakapokuwa tunashughulikia masuala hayo tutahakikisha pia tunaongea na waajiri wao wa zamani kuhakikisha wanapewa mafunzo ili tutakapokamilisha kuwalipa fedha hizi waende kuwekeza mahali ambapo patakuwa na tija zaidi na kutokuwaacha *stranded. (Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Sangu ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Msalala, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Santiel Kirumba.

Na. 88

Kuwaunganishia Umeme Wateja Waliolipia Kabla ya Mabadiliko ya Bei

MHE. SANTIEL E. KIRUMBA K.n.y. MHE. IDDI K. IDDI aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaunganishia umeme wateja waliolipia kabla ya mabadiliko ya bei katika Halmashauri ya Msalala?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii kwa niaba ya Wizara ya Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* imekamilisha kupeleka umeme vijijini na sasa inaendelea na kupeleka umeme vitongojini ambapo katika maeneo haya wananchi wanaunganishiwa umeme kwa gharama ya shilingi 27,000.

SPIKA: Mheshimiwa Santiel Kirumba, swali la nyongeza.

MHE. SANTIEL E. KIRUMBA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Halmashauri ya Msalala imeshatenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa ofisi na Mheshimiwa Mbunge ametoa tofali 1,000 za kuanzia ujenzi. Je, Serikali imejipangaje kukamilisha ujenzi wa ofisi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ofisi hii ya ki-*TANESCO* imekuwa na changamoto ya watumishi na vitendea kazi, Serikali imejipangaje kupeleka vitendea kazi pamoja na watumishi? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge yote kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali inawapongeza wananchi kwa jitihada hizi walizozifanya za kusaidia katika ujenzi wa ofisi hii na pili, tunashukuru kwa taarifa hiyo, tunaichukua na tutawatuma wataalamu wetu waende kuona kazi ambayo imeanza kufanyika, halafu jambo hili tutaliweka kwenye mipango yetu. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, Wilaya ya Ngorongoro imekuwa na changamoto kubwa ya kukatika katika kwa umeme mara kwa mara. Nimekuwa nikiongea hapa na Serikali imekuwa ikiniahidi kutatua kero hii ambayo ni kubwa sana kwa wananchi wa Ngorongoro Mkoa wa Arusha.

Mheshimiwa Spika, ninataka kufahamu ni lini sasa Serikali itatatua kero hii kubwa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika maeneo kadhaa nchini tuna tatizo la kukatika katika kwa umeme na tatizo hili linatokana na uchakavu wa miundombinu ya kusafirishia umeme. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge waendelee kuwa na subira wakati Serikali inafanya kazi kubwa sana ya kuboresha miundombinu hii. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Spika, ninashukuru, ni kwa nini sasa Serikali isitoe mwongozo wa kuonesha tofauti ya malipo ya kuvuta umeme kwa kiwango cha shilingi 27,000 na shilingi 300,000 kulingana na maeneo? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali imekwisha kutoa mwongozo huo. Tunachoweza kufanya sasa ni kuendelea kutoa elimu ili jambo hili liweze kueleweka kwa upana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 89

Wakulima Kupata Mikopo ya Mbolea ya Ruzuku

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itawezesha wakulima wasio na fedha taslimu kupata mikopo ya mbolea ya ruzuku?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Silinde, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa sasa Serikali inatoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima ambapo mkulima huchangia gharama wakati wa ununuzi. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025

tani 388,619.8 za mbolea zenye thamani ya ruzuku ya shilingi bilioni 131.66 imeuzwa kwa utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya tathmini ya namna ya kutoa ruzuku ya mbolea kwa njia ya mkopo ili kuwawezesha wakulima wasio na fedha taslimu kupata mbolea hiyo. Wakati tunakamilisha tathmini hiyo, tunashauri wakulima ambao hawana fedha taslimu kujiunga na Vyama vya Ushirika *(AMCOS* au *SACCOS)* ili waweze kukopa pembejeo kupitia vyama hivyo. Aidha, wakulima hao pia wanaweza kupata mikopo ya riba nafuu kupitia Benki ya Maendeleo ya Ushirika, Mfuko wa Pembejeo za Kilimo *(AGITF)* na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania *(TADB)*.

SPIKA: Mheshimiwa Kakunda, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Spika, kwanza, ninafurahi sana kwa majibu ya Serikali hasa wanaposema wanaandaa tathmini, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; je, Serikali ipo tayari kuandaa na kutoa mwongozo pamoja na elimu itakayowezesha wakulima kupata mikopo kwenye hizi Benki za Ushirika na Benki ya Wakulima *(TADB)* kwa sababu wakulima wengi hawana habari na hawajui utaratibu wa kufikia kupata mikopo hiyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; mikopo ya Mfuko wa Pembejeo za Kilimo imekuwa ikichelewa sana tangu mwombaji aombe wakati mwingine inachukua hata miaka miwili; je, Serikali haioni kwamba hatua hizo zinakatisha tamaa wakulima?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, mimi nimpongeze Mheshimiwa Mbunge na nimthibitishie tu kwamba Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni makini sana katika kumsaidia mkulima. Tutakuwa tayari kuendelea kutoa mwongozo kwa mkulima wa kuzisisitiza hizi taasisi ambazo tunazisimamia ziweze kuongeza elimu maana yake

waongeze bajeti ili waweze kuwafikia watu wengi. Kwa hiyo, tutalifanya hivyo ili tuweze kuwafikia wakulima kama ambavyo umeshauri.

Mheshimiwa Spika, hukusu mikopo ya Mfuko wa Pembejeo *(AGITF)* kuendelea kuchelewa, nitoe tu maelekezo kwa Mkurugenzi Mkuu wa *AGITF* kwamba ahakikishe mikopo wanaitoa kwa haraka. Sisi kama Wizara moja ya wajibu wetu ni kufuatilia kuona mikopo hiyo inawafikia wakulima kwa sababu fedha hiyo tunayo. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Justin Nyamoga, swali la nyongeza.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru; kwenye kilimo cha mazao ya mboga mboga hasa nyanya, viazi, vitunguu na mazao mengine yanayofanana, tatizo kubwa ni viuatilifu yaani dawa zinazotumika ambazo ni gharama kubwa sana.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka ruzuku kwenye viuatilifu hivyo ili wakulima hao pia wapate nafuu katika shughuli zao za kilimo? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ninakubaliana na pendekezo la Mheshimiwa Nyamoga, lakini sasa hivi sisi kama Serikali tunatekeleza huu mpango wa ruzuku kwa awamu na ndiyo maana unaona tumefanya kwenye mbolea, kwenye upande wa mazao kwa mfano ya chakula kama mahindi na tunafanya viuatilifu kwenye mazao ya biashara kama vile korosho.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni mpango endelevu ambao tumekuwa tukifanya. Kwa hiyo, tunakwenda hatua kwa hatua tukiangalia changamoto zinazojitokeza ili tuhakikishe sasa baadaye tutawafikia na hao. Kwa hiyo, jambo hilo tumelipokea na tutalifanyika kazi.

SPIKA: Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, swali la nyongeza.

MHE. MOHAMED L. MONNI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kuna ucheleweshaji mkubwa wa pembejeo hasa mbolea za ruzuku pamoja na mbegu katika Jimbo zima la Chemba, ninataka kujua kauli ya Serikali juu ya ucheleweshaji huo, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, niseme tu kwamba sisi kama Serikali, kama kuna kipindi tumejitahidi kupeleka mbolea kwa wakati ninafikiri katika msimu huu uliopita hususani mbolea za kawaida kwa wakulima. Baada ya kutambua zile changamoto zilizojitokeza katika msimu uliopita mwaka huu tutaongeza idadi ya mawakala kwa ajili ya kusambaza pembejeo. Vilevile kutumia vyama vya ushirika ili kuhakikisha mbolea za ruzuku zinawafikia wakulima. Kwa hiyo, tutalizingatia hilo hususani katika Jimbo lako la Chemba. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi, sasa aulize swali lake.

Na. 90

Changamoto ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo

MHE. MWANTATU MBARAK KHAMIS aliuliza: -

Je, Serikali imewezaje kutatua changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP I)?*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo

Awamu ya Kwanza *(ASDP I)* ni pamoja na miundombinu duni ya kilimo kwa maana ya barabara, maghala na miundombinu ya umwagiliaji; upatikanaji mdogo wa pembejeo kama mbegu bora, mbolea na viuatilifu; huduma duni za ugani; ushirikishwaji mdogo wa sekta binafsi; na upungufu wa takwimu sahihi za kilimo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Serikali imezingatia katika kutatua changamoto hizo kupitia mipango inayoendelea kutekelezwa ukiwemo Mpango wa Muda Mrefu wa Mageuzi ya Sekta ya Kilimo kwa maana ya *Tanzania Agricultural Master Plan - 2050*. Maeneo ya kipaumbele yanayoendelea kutekelezwa kwa sasa ni kuendelea kuwekeza kwa kuimarisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo, huduma za ugani, utafiti, uzalishaji wa mbegu, kuongeza uwezo wa kuhifadhi mazao, upatikanaji wa masoko, kuimarisha upatikanaji wa takwimu na kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi ambao ulikuwa wa chini wakati wa utekelezaji wa *ASDP I*.

SPIKA: Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis, swali la nyongeza.

MHE. MWANTATU MBARAK KHAMIS: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake, lakini kwa kuzingatia changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa programu hii; je, katika mipango inayoendelea mmejipanga vipi katika suala zima la kuboresha, kuratibu, kufuatilia pamoja na kufanya tathmini ili kuhakikisha mafanikio ya programu hii yanapatikana kwa lengo la kuboresha sekta ya kilimo nchini? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, mimi pia nimpongeze Mheshimiwa Mwantatu kwani amekuwa ni mfuatiliaji mzuri sana wa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, ni kweli sisi kama Wizara sasa hivi tumeandaa Kitengo cha *M and E* kwa ajili ya kuhakikisha inafuatilia mipango yote ambayo inatekelezwa katika Wizara

yetu. Kwa hiyo, tunataka ufuatiliaji pamoja na utekelezaji wake uende kama vile ambavyo Serikali imepanga na kukusudia. Kwa hiyo, tutaongeza nguvu pamoja na bajeti kuhakikisha yale yote tuliyokusudia yanatekelezeka. Kwa hiyo, nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa hilo. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, swali la nyongeza.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamaja na umuhimu wa sekta ya kilimo, inakabiliwa na changamoto nyingi lakini changamoto hizo tunaweza kupunguza kama tukianzisha Mfuko wa Kilimo na ukiwa na vyanzo vya uhakika. Nini kauli ya Serikali kuanzisha mfuko huu? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ni kwamba tayari tumeshaanzisha Mfuko wa Kilimo ambao tunaita Mfuko wa Pembejeo za Kilimo. Moja ya jukumu kubwa tulilonalo sasa hivi ni kuendelea kuuongezea fedha na bahati nzuri tulishapata *grants* kwa ajili ya mfuko huo karibu dola milioni 15. Kwa hiyo, tutaendelea kuongeza fedha ambazo zitawafanikisha kuwafikia wakulima wengi. Kwa hiyo, tupo katika utekelezaji.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Deo Mwanyika.

Na. 91

Ununuzi wa Meli Kubwa ya Uvuvi Ziwa Nyasa

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA K.n.y. MHE. JOSEPH Z. KAMONGA aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kupeleka meli ya Uvuvi Ziwa Nyasa ili kuvua samaki wanaoishi kwenye kina kirefu ambao kwa sasa wanakufa kwa uzee?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa ina mpango wa kununua meli kwa ajili ya uvuvi wa Bahari Kuu. Vilevile Serikali imeweka msukumo mkubwa kwenye ununuzi wa boti za kisasa kwa ajili ya kuvua kwenye maziwa yote nchini ambapo kwa mwaka 2022/2023 Wizara imefanikiwa kupeleka Ziwa Nyasa boti nne za kisasa pamoja na zana za kuvulia samaki.

Mheshimiwa Spika, boti zilizopelekwa Ziwa Nyasa zina urefu wa mita 7.06, mita 10 na mita 12. Kati ya boti hizo nne, boti mbili zenye urefu wa mita 10 na ile ya mita 12 zina uwezo wa kuvua kwenye kina kirefu cha Ziwa Nyasa. Boti hizo zilitolewa kupitia ushirikiano baina ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania *(TADB)* kupitia mikopo isiyo na riba kwa vikundi vya wavuvi, makampuni, vyama vya wavuvi, vyama vya ushirika na mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, boti hizo nne zilizopelekwa Ziwa Nyasa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 zilitolewa kwa *Kyela Education Improvement Foundation* (Kyela), Christopher N. Ndunguru (Nyasa), Hubbert Authur Wayotile (Ludewa) na Godfred Raphael Mwasoka (Ludewa). Aidha, utoaji wa boti hizo ni endelevu hivyo Wizara inahamasisha wavuvi na vikundi vya wavuvi kuendelea kuomba mikopo hiyo ili waweze kunufaika na fursa hiyo, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninashukuru sana kwa majibu mazuri na tunawashukuru sana Serikali kwa mpango huo wa boti ambao tayari zimeshaanza kupelekwa kule, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; tunafahamu wazi kwamba tija kubwa inatokana hasa na boti, lakini kuwa na vizimba. Ni lini Serikali itapeleka vizimba ili viweze kuwasaidia vijana waweze kuvua kwa urahisi katika Ziwa Nyasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Halmashauri ya Mji Njombe haina kituo ambacho kingetumika kama shamba darasa kwa ajili ya kutunza vifaranga na kufanya *multiplication.* Ni lini sasa Serikali itatengeneza au itaweka mpango wa kuwa na shamba darasa kwa ajili ya Halmashauri ya Mji Njombe? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa Ziwa Nyasa bado Serikali haijaweka utaratibu maalumu kuhusiana na vizimba kwa sababu tayari imeshaanza utafiti wa namna gani na wapi ambako vizimba vinaweza vikawekwa katika Ziwa letu Nyasa na tayari tumeshakamilisha utafiti huo juu ya kujua wapi tunaweza tukaweka vizimba ili vitakapoenda vizimba hivyo viwe na tija kwa wafugaji wetu wa samaki katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumeshakamilisha utafiti huo na baada ya utafiti huo basi sasa tutakwenda kutoa semina kwa wavuvi wetu juu ya wapi panafaa kuwekwa vizimba katika Ziwa Nyasa. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tumeshakamilisha utafiti na baada ya hapo tutatuma wataalamu kwa ajili ya kutoa elimu juu ya vizimba, lakini na wapi ambapo vizimba vinaweza vikafaa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na shamba darasa tumelipokea hili la Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakwenda kuwafundisha wavuvi wetu wa eneo hilo. Tutakwenda kuweka shamba darasa kwa ajili ya kuendelea kufanya *demonstration* kwa wavuvi wetu katika eneo hilo. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumelichukua na tutakwenda kulifanyia kazi ili tuweze kuweka tija katika eneo. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali kwa kifupi. Mheshimiwa Phillipo Mulugo, swali la nyongeza.

MHE. PHILLIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, Ziwa Rukwa ni ziwa kubwa sana toka limepimwa mwaka 1978 na Serikali ilipandikiza samaki aina ya Singida enzi hizo tukiwa watoto wadogo kabisa, lakini mpaka leo samaki wa Ziwa Rukwa wamedumaa kabisa. Serikali ina mpango gani wa kupandikiza samaki wengine kwa ajili ya kuleta ustawi wa Ziwa Rukwa? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, wazo la Mheshimiwa Mbunge tunaomba tukalifanyie kazi, tutatuma wataalamu waende kuhakikisha na kuangalia kama kweli samaki wamedumaa katika Ziwa hilo halafu tuone tunaweza kufanya nini ili kuweza kunusuru samaki katika ziwa hilo, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, swali la nyongeza.

MHE. ALLY A. J. M. JUMBE: Mheshimiwa Spika, mmoja wa wanufaika wa mpango wa maboti ya kuvulia yupo Kyela, lakini tangu amepewa boti hilo, vifaa vyote havijakamilika na ni miaka miwili sasa. Kazi yake anayofanya ni kusafirisha abiria; je, ni lini sasa Serikali itampelekea vifaa vyote ili aweze hata kulipa mkopo wake kwa kuvua samaki? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, wakati tunatoa vifaa hivi boti pamoja na vifaa vyake vilikuwa vimekamilika, labda kama kuna tatizo la mmoja mmoja hilo ni jambo lingine. Tupo tayari kukutana na Mheshimiwa Mbunge na huyo mvuvi ili tuone namna ya kwenda kumtatulia tatizo lake. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, swali la nyongeza.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru.

Mheshimiwa Spika, wavuvi wa Bunda Mjini wamejiunga kwenye vikundi hasa wa eneo la Tahiro na Guta, lakini mpaka sasa hivi hawajapata boti ambayo itawawezesha kuvua kisasa. Ni lini sasa na wenyewe watapatiwa? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba Mheshimiwa Rais alishazindua ugawaji wa boti hizi na vifaa vyake. Tupo tayari kupeleka pale Bunda kama tutapata maombi maalumu. Nafikiri baada ya Bunge hili nikutane na Mheshimiwa Mbunge anipe vikundi hivyo ambavyo vinahitaji boti na vifaa vya uvuvi ili tuweze kupewa mkopo huo kwa sababu vifaa vipo na tayari Mheshimiwa Rais amesharuhusu vigawiwe katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

MHE. CHARLES M. KAJEGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, wavuvi wa Mwibara wamechoka kufukuzana na samaki majini; je, ni lini watapatiwa vizimba ili waweze kuvua samaki wengi? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, tunaendelea na ugawaji wa vizimba katika maeneo mbalimbali na hata sasa tumeshaanza ugawaji wa vizimba awamu ya pili, tunamhakikishia Mheshimiwa Mbunge tutakwenda kugawa vizimba katika vikundi vyake vya Mwibara, bahati nzuri tumeshawasiliana na Mheshimiwa Mbunge kwa mara nyingi zaidi kwamba tumeshamwelekeza namna sahihi ya kufanya ili tuweze kwenda kugawa vizimba katika Jimbo lake, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako, ahsante sana.

Tunaenda na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Katani Ahmad Katani, Mbunge wa Tandahimba, haya, Mbunge aliyesimama ni yule ambaye ameshapata fursa ya kuuliza swali la nyongeza tayari, lakini hakuna mwingine aliyesimama, Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali.

Na. 92

Halmashauri ya Tandahimba Kurejeshewa Fedha Zilizochukuliwa na Hazina

MHE. CECILIA D. PARESSO K.n.y. MHE. KATANI A. KATANI aliuliza: -

Je, lini Serikali itarejesha fedha za miradi iliyochukuliwa na Hazina ili miradi hiyo iweze kukamilishwa?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA FEDHA alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 29 cha Sheria ya Bajeti, Sura 439, fedha ambazo hazijatumika hadi mwisho wa mwaka zinakoma matumizi yake mwisho wa mwaka unapofika. Lengo kuu la kanuni hiyo ni kusimamia uwajibikaji na uwazi katika matumizi ya fedha zilizotengwa katika bajeti.

Mheshimiwa Spika, hivyo, iwapo kuna miradi ama shughuli ambayo haijakamilika, Fungu husika linatakiwa kutenga bajeti na kuwasilisha maombi kwa kuambatisha hati za madai au nyaraka za utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali ni kuhakikisha kuwa miradi yote inatekelezwa ili kuleta maendeleo kwa wananchi.

SPIKA: Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni utamaduni sasa kila inapofika mwisho wa mwaka wa Serikali ndiyo fedha nyingi sana zinaanza kutoka kiasi ambacho kinafanya inakuwa *carried forward* miaka mingine, lakini pia wakati mwingine ndiyo mwanya wa matumizi mabaya ya fedha.

Je, kwa nini Serikali isijipange vizuri fedha ziwe zinatoka kila awamu bila kukaribia mwisho wa mwaka? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, tunapokea ushauri, ni ushauri mzuri. Mara nyingi ambacho huwa kinasababisha ni pale ambapo bajeti inapopitishwa kunakuwa na taratibu za kuweza kukamilisha masuala ya manunuzi ili miradi ianze kutekelezwa na fedha zianze kupelekwa kwa ajili ya kulipia miradi hiyo, lakini miradi ambayo huwa inakuwa tayari ipo kwenye utekelezaji mara tu baada ya mwaka wa fedha kuanza, huendelea kupata fedha. Kwa hiyo, kwa ile ambayo imechelewa kuanza shughuli zake za utekelezaji mara nyingi fedha hufuatia baada ya hapo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo wazo lililotolewa na Mheshimiwa Mbunge ni wazo la msingi na Serikali tutaendelea kuzingatia utoaji wa fedha kwa kila awamu ili kuweza kuhakikisha fedha zinazotengwa ndani ya mwaka husika zinatumika. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani wa kupeleka fedha ili kwenda kuwalipa wakandarasi wanaojenga barabara kwa kiwango cha changarawe na lami kupitia *TARURA* na *TANROADS* ili miradi iendelee?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa fedha zinazotakiwa kwenda kutekeleza miradi ya barabara ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja kupitia *TARURA* na *TANROADS*, tunavyoongea katika wiki mbili hadi mwezi mmoja tumepeleka fedha kwa ajili ya *TARURA* na kwa ajili ya *TANROADS* kwa ajili ya kuendelea kutekeleza miradi ambayo wakandarasi wapo *site* na wanatakiwa wapate fedha ili waendelee na utekelezaji wa miradi.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya, Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, Mbunge wa Viti Maalum.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Spika, …

SPIKA: Hujaitwa bado, lakini leo umekwishapata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza labda kama umepewa majibu na Mheshimiwa Mbunge. Kati ya ninyi mliosimama nani ana majibu ya Mheshimiwa Mbunge?

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Spika, naomba nimuulizie mimi hapa.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Spika, mimi ninatokea Singida.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Spika, sina majibu naomba niulize.

SPIKA: Nani ana majibu? Hakuna mwenye majibu? Basi wa kwanza kusimama alikuwa Mheshimiwa Ritta.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Spika, mimi ninatokea Singida.

SPIKA: Ni sawa, Mheshimiwa Mbunge wa kwanza kusimama alikuwa Mheshimiwa Ritta Kabati.

Na. 93

Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida

MHE. DKT. RITTA E. KABATI K.n.y. MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Hospitali ya Mkoa Singida unatekelezwa kwa awamu ambapo hadi sasa Serikali imeshatoa fedha kiasi cha shilingi bilioni 9.3 ambapo awamu ya kwanza zilitolewa shilingi bilioni sita na awamu ya pili shilingi bilioni 3.3.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi bilioni nne kwa ajili za ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Singida ikiwa ni awamu ya III *(Phase III)*. Ujenzi huu unatarajia kukamilika ifikapo mwezi Januari, 2027.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake.

Je, katika ujenzi huo wa hospitali ya rufaa, Serikali imeweza kuweka na maeneo kwa ajili ya nyumba za madaktari wa hospitali hiyo, kwa sababu imekuwa ni changamoto kwenye hospitali nyingi?

Swali langu la pili, Hospitali ya Mkoa wa Iringa madaktari wanapata shida sana kwa sababu hawana nyumba za kuishi na mara nyingi madaktari wamekuwa wakipata shida kwenda kuhudumia wagonjwa wa dharura inapotokea.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, kwenye mpango huu wa shilingi bilioni nne zinazokwenda, mkakati wa nyumba za madaktari umewekwa, lakini siyo mkakati tu wa nyumba za madaktari, pia vyumba vya kupumzikia madaktari wakati wanasubiri kama kutatokea dharura. Kitakachofanywa kule Singida ndicho kitakachotokea upande wa mkoa wa Hospitali ya Iringa. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Asha Juma, swali la nyongeza.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Hivi Serikali inaweza kulieleza Bunge hili kwa zile hospitali za rufaa ambazo zimekamilika ni zote zimepata vifaa muhimu vya hospitali ya rufaa kama *MRI, scanners, x-rays, mortuary* za kisasa na kadhalika?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, hospitali zote za rufaa ambazo zimekamilika ambazo ni hospitali za mikoa kwenda Taifa zimepata vifaa kulingana na *level* ya hospitali yenyewe na mahitaji kwa wakati huo, kwa maana ya *capacity* ya wataalamu

waliopo *site* na kila wakati uhitaji unapoibuka zinaongezwa. Kwa sasa kwa maana ya mashine kama *MRI* ambayo umeisema hapa hiyo haipo kwenye hospitali za mikoa, utaikuta kwenye hospitali za kanda na Taifa na kwenye hospitali za mikoa utakuta *CT-Scan*.

SPIKA: Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru sana Serikali kwa kutujengea hospitali yetu ya Mkoa wa Sogwe; je, ni lini mtatujengea wodi za jumla kwa ajili ya kulaza wagonjwa kwa sababu kuna upungufu mkubwa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, nimtoe Mheshimiwa Mbunge wasiwasi, miezi mitatu iliyopita nilikuwepo kwenye Hospitali ya Mkoa wa Songwe, hospitali hiyo kwa majengo yaliyopo na vitanda bado wala wagonjwa hawajaweza kujaza, lakini ni kweli huo, *wing* inahitajika kwenye Hospitali yako ya Mkoa wa Songwe na kwenye bajeti ya mwaka huu ni mojawapo ya mipango inayopagwa kwa ajili ya kujenga *wing* hiyo, lakini kwa uhakika kwamba wagonjwa watapata shida au vitanda havitatosha kwa majengo yaliyopo bado vitanda ni vingi kuliko wagonjwa.

SPIKA: Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Felista Njau. Hebu ngoja, ninao ujumbe hapa, ninadhani Mheshimiwa Sylvia ndiyo una majibu ya Mheshimiwa Nancy? Mheshimiwa Felista utauliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi Mbunge wa Viti Maalum Swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Sylvia Sigula.

Na. 94

Tatizo la Udumavu Nchini

MHE. SYLVIA F. SIGULA K.n.y. MHE. NANCY H. NYALUSI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza tatizo la udumavu nchini?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu: -

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na tatizo la udumavu nchini Serikali inatekeleza mpango kazi jumuishi wa masuala ya lishe wa mwaka 2021/2022 – 2025/2026 ambapo baadhi ya afua zinazotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Uhamasishaji na umuhimu wa ulishaji sahihi wa watoto ikiwemo unyonyeshaji.

(ii) Utoaji wa elimu ya lishe katika vituo vya afya na uhamasishaji wa jamii kupitia vyombo vya habari.

(iii) Kwa wajawazito na wazazi/walezi wanapohudhuria kliniki.

(iv) Utoaji wa matone ya Vitamini A na dawa za minyoo kwa watoto wa umri wa chini ya miaka mitano.

(v) Uongezwaji wa virutubishi (madini na vitamini) katika vyakula hasa mafuta ya kula, unga wa ngano, unga wa mahindi na chumvi.

(vi) Utoaji wa vidonge vya madini chuma na asidi ya foliki kwa wanawake wajawazito.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Sylvia Sigula, swali la nyongeza.

MHE. SYLVIA F. SIGULA: Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kutoka kwenye ripoti ya Serikali mikoa inayoongoza kwa uzalishaji wa chakula ndiyo mikoa inayoongoza kwa udumavu, ikiwemo Iringa, Rukwa, Katavi pamoja na Ruvuma. Je, Serikali haioni kuna haja sasa ya kufanya utafiti ili kujua pamoja na uzalishaji huo changamoto ni nini suala la udumavu lipo juu? *(Makofi)*

Swali la pili, mikoa hii ambayo nimeitaja ni mikoa ambayo ina idadi kubwa ya watu; je, Serikali haioni haja ya kuja na mkakati maalumu wa kupambana na changamoto ya udumavu katika mikoa hii niliyoitaja? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake hili, lakini niseme tu, Serikali imeshafanya utafiti na kilichoonekana, moja ni kweli kwamba mikoa hii inazalisha chakula, lakini ni asilimia tisa tu ya watu wanakula chakula mchanganyiko, kwa hiyo, maana yake asilimia nyingine yote inakula chakula cha aina moja. Unakuta mtu anaweza akatengeneza makande halafu yakawekwa, yakaliwa kwa muda mrefu kidogo badala ya kula vyakula vingine.

Mheshimiwa Spika, pia unakuta ule ulishaji kwenye yale makuzi ya watoto mwanzo wanapozaliwa, kuanzia kulisha ujauzito, mama mjamzito anavyolishwa, lakini pia wakati mtoto akiwa mchanga mpaka anafikisha miaka mitano, maeneo hayo kuna matatizo. Kwa hiyo, sasa hivi nguvu zimeelekezwa kwenye kubadilisha hiyo tabia.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili niseme tu kwamba pia kuhusu kutoa hamasa kwa jamii na idadi ya watu. Kwa kweli nguvu sasa hivi imeelekezwa na Serikali, lakini na mashirika

mbalimbali na utaona kwenye Mkoa wa Njombe, ninampongeza Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Mheshimiwa Mtaka amefanya kazi nzuri sana. Wakati wa siku ya afya juzi Mkoa wa Njombe ndiyo uliongoza karibu kila kitu katika kufanya vizuri, wakati mkoa huu kwa masuala haya ya udumavu unashika namba mbili ukiongozwa na Mkoa wa Iringa, maana yake hii mikoa sasa imeanza kuongeza nguvu kwenye masuala ya afya na masuala mbalimbali na tunaamini baada ya muda mtaona mabadiliko makubwa. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali mafupi, muda wetu umeshakimbia sana. Mheshimiwa Felista Njau, swali la nyongeza.

MHE. FELISTA D. NJAU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, *SUA* wanazalisha wataalamu wa lishe wengi sana lakini mtaani hawapo, hawajaajiriwa. Ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kila kijiji, kila kata kunakuwa na mtaalamu wa lishe ili kuepuka adha ya udumavu? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, ni kweli *SUA* wanazalisha wataalamu wa aina mbalimbali na wazuri sana na ambao wanafikiri vizuri sana kisayansi, lakini kuna mambo ambayo tunatakiwa tujadiliane na wenzetu wa Wizara ya Utumishi, baadhi wengine kwenye muundo hawapo, lakini wengine ni kwamba kuna vibali vinavyotoka tutaendelea kuwaajiri wale ambao wapo kwenye muundo, lakini wale ambao inaonekana kwenye muundo hawapo ili waweze kuingia na waweze kusaidia kutatua hayo matatizo. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kuwa ni miaka 64 sasa baada ya uhuru na bado tatizo hili ni kubwa.

Je, Serikali haioni kwamba ni muhimu kila hospitali ikawa na kitengo cha lishe wakati akina mama wanapoenda kliniki wakaweza kupata huduma hiyo endelevu? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, kwa sasa kitengo cha lishe kwenye hospitali zetu kimeanza, ukienda kwenye Hospitali za Mikoa, Taifa utakuta Afisa Lishe, tutaendelea kuongeza nguvu na utaona hata kila Wilaya kuna Afisa Lishe lengo ni kuhakikisha hayo mambo yanafanyika. Kikubwa ninachosema ni kwamba tutaongeza nguvu kuhakikisha pia lishe ni sehemu ya mtu anatoka kabisa kama anakwenda kwa daktari anaingia chumba na anamsikiliza daktari kabla ya kuondoka hospitalini. Tumeanza kila mama anapoingia kliniki wakati wa kliniki lishe ni jambo ambalo ni lazima lizungumziwe kabla ya mama kuondoka kiliniki. Tunalichukua hilo iwe ni kitu ambacho kabla haujaondoka hospitali basi uwe umemwona Afisa Lishe na muongee mambo mbalimbali.

SPIKA: Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, ahsante lakini swali langu lilishaulizwa na muuliza swali.

SPIKA: Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, swali la nyongeza.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, kwa kuwa suala la upatikanaji wa chakula shuleni limebaki kuwa suala la hiari. Kuna maeneo mengine wazazi wasipochangia watoto hawapati chakula na huo ndiyo mwanzo wa udumavu kwa sababu hawapati chakula kwa wakati.

Ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha chakula kinapatikana mashuleni na pale ambapo wazazi hawawezi kuchangia Serikali iweze kuhusika kusaidia upatikanaji wa chakula mashuleni?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRII WA AFYA: Mheshimiwa Spika, moja ni suala tu la kuhamasishana kwamba unapozungumzia suala la lishe huzungumzii suala la lishe tu pale mtoto anapokuwa ameanza shule, ni toka mama anapobeba ujauzito na ndipo unapopata mtoto mwenye *GB* za kutosha na mwenye uwezo mzuri wa akili na mwenye uwezo wa kupambana. Kila mzazi anahitaji mwanae aweze kupambana na masuala mbalimbali baadaye maishani na hata Taifa letu liweze ku-*compete* na mataifa mengine katika *arena* ya sayansi na ugunduzi.

Mheshimiwa Spika, sasa suala la kula, kama mtoto wako ameondoka nyumbani chakula cha mchana kile ambacho angekula mchana ukampelekea shuleni sioni kwamba ni tatizo. Wilaya ya Siha tumekubaliana, mtoto angekula nyumbani mchana, hicho chakula chake cha mchana kinahamishiwa tu shuleni na wazazi wamekubali wote na hakuna tatizo la lishe mashuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ninalipokea suala lako kwamba pamoja na kuhamasisha wananchi kwamba lazima tuchangie chakula shuleni, lakini pia panapotokea matatizo basi tutashauriana na Wizara ya Elimu tuone *way forward,* lakini ukweli ni kwamba siyo sawa ukashindwa kuhakikisha mtoto wako anakula shuleni kwa sababu mchana angekuwa nyumbani ungemlisha chakula. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, swali la nyongeza kwa kifupi.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi; kwa kuwa bado udumavu ni changamoto kubwa hapa nchini kwetu, kwa kurejea kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri umesema kwamba Serikali inatekeleza ule mpango jumuishi wa lishe, Shirika la Chakula na Lishe Tanzania *(TFNC)* limekuwa likifanya kazi kubwa katika eneo hili.

SPIKA: Uliza swali Mheshimiwa.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Spika, je, Wizara ya Afya haioni ipo haja ya hii Taasisi ya Chakula na Lishe *(TFNC)* kuendelea kuwepo badala ya vile Serikali ilivyoamua kuifuta? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, kwanza nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, *TFNC* haijafutwa, lakini imeboreshwa ili iweze kutenda vizuri zaidi na kuweza kutenda kwa namna ambayo inaweza kusimamiwa kirahisi zaidi. Sasa *TFNC* inaenda kuwa idara kamili na itasimamiwa vizuri sana na kuhakikisha inatekeleza majukumu yake kwa usahihi zaidi. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Lucy John Sabu, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 95

Kuongeza Vituo vya Ushauri wa Afya ya Akili na Programu za Uhamasishaji

MHE. LUCY J. SABU aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuongeza vituo vya ushauri na programu za uhamasishaji ili kusaidia vijana na tatizo la afya ya akili?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali katika kupambana na tatizo la afya ya akili kama ifuatavyo: -

(i) Serikali inatoa huduma ya ushauri nasaha wa afya ya akili na uhamasishaji katika vituo vya afya 701 na hospitali zote za

rufaa za mikoa pamoja na Hospitali ya Afya ya Akili Mirembe.

(ii) Serikali imefanya mafunzo kwa wataalamu 2,840 wakiwemo madaktari na wauguzi ili kuwawezesha kutambua na kushughulikia changamoto za magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo afya ya akili.

(iii) Serikali imeanzisha huduma ya *call centre 115* ambapo pamoja na huduma nyingine, jamii inapata huduma ya ushauri nasaha ya afya ya akili kwa njia ya simu, lengo likiwa ni kuwafikia vijana wengi zaidi, kuwasaidia kwa haraka na pia kupunguza unyanyapaa kwa wale wasiopenda kwenda hospitalini moja kwa moja.

(iv) Serikali imeanzisha vituo 1561 vya kutoa huduma rafiki kwa vijana katika mikoa yote, ikiwemo huduma za afya ya akili kupitia Mkakati Jumuishi wa Vijana *(NAIA)*.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Lucy Sabu, swali la nyongeza.

MHE. LUCY J. SABU: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja dogo la nyongeza. Kumekuwepo na changamoto kubwa kwa vijana ambao wamekosa ajira, hivyo kusababisha kuwa na msongo wa mawazo na afya ya akili. Je, Serikali ina mpango gani wa kuzuia tatizo la afya ya akili kabla kijana hajakumbwa na changamoto hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, vilevile Serikali inatumia gharama kubwa katika kuwahudumia vijana hawa. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha kwamba changamoto hii inakwisha kabisa? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, matatizo ya akili yanayosababishwa na ukosefu wa ajira, ninafikiri tunaweza tukayakabili. Moja, kwa kuelemishana namna sahihi ya kufikiri na kuyatazama maisha. Ndiyo maana Serikali imekuja na mtaala mpya wa kuyarekebisha masuala ya elimu, ili mtu toka akiwa mtoto, chekechea, basi ajitambue na ajue kwamba, unaposoma hata usipoajiriwa kuna namna nyingine ya kufanya ukaweza kuzalisha na ukaishi.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali.

Waheshimiwa Wabunge mliosimama kule nyuma mtafute viti mketi.

Ninalo tangazo la wageni walio Bungeni asubuhi hii. Tutaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika; tunao wageni wanne ambao ni wageni wangu. Hawa ni Watendaji Wakuu kutoka *Access Bank;* wapo Ndugu Imani John, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji; Ndugu Joyce Malai, Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wadogo.

Ukitajwa unasimama; sijui kama hao wageni wako humu ndani ama hawapo? Hawapo? Sawa. *(Makofi)*

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika, ni Wageni wa Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Tutaanza na Ndugu Adolf Ndunguru, ambaye ni Katibu Mkuu. Wapo pia Ndugu Sospeter Mtwale, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Mhandisi Rogatus Mativila, Naibu Katibu Mkuu Miundombinu; na Ndugu Atupele Mwambene, Naibu Katibu Mkuu Elimu, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia Ndugu Hawa Ghasia, Mwenyekiti wa Bodi Shirika la Masoko Kariakoo na Mhandisi Victor Seff, Mkurugenzi Mkuu wa *TARURA*. Haya ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, makofi hayo ninajua huwa hayapigwi kawaida. Kwa hiyo, tunakupongeza Mhandisi Victor Seff kwa kazi nzuri ambayo unaifanya kuhakikisha Barabara za *TARURA* zinapitika katika maeneo ya uwakilishi, ambayo Waheshimiwa Wabunge hawa wametambua mchango wako mkubwa. Kwa hiyo, tunakupongeza sana. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, pia, wapo Dkt. Athumani Kihamia, ambaye ni Mtendaji Mkuu wa *DART*; na Ndugu Robert Shilingi, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Elimu Kibaha, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo vile vile Alhaj Mustafa Rajab Shaban, Sheikh wa Mkoa wa Dodoma; na Padre Wenceslaus Bamugasheki, Askofu wa Kanisa Katoliki Dodoma. Ahsante sana. *(Makofi)*

Haya, yupo *CPA* Samweli Wado, Afisa Mtendaji Mkuu Benki ya Kibiashara ya Uchumi, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Mchengerwa, ambao ni familia yake kutoka Rufiji amba oni Ndugu Nadra Rashid na Sebabili Duranya, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba, ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Hawa ni Ndugu Mary Chatanda, Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania; Ndugu Suzan Kunambi, Katibu Mkuu wa UWT. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia, leo wapo wageni sita wa Bunge kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Tutaanza na Ndugu Charles Kichere, ambaye ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Tunashukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

Wapo Ndugu Kubela Mwakatundu, Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; Ndugu Benja Majura, Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; Ndugu Salhina Mkumba, Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; Ndugu Wendi Massoy, Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Ndugu George Haule, Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Karibuni sana Bungeni na tunawashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo mnafanya kwa niaba yetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni sita wa Mheshimiwa Naibu Spika, ambao ni Waheshimiwa Madiwani Wanawake kutoka Kata saba za Jiji la Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Edward Ole-Lekaita Kisau, ambao ni mtoto na mdogo wake kutoka Kilimanjaro. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge; tutaanza na wageni 17 wa Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Hawa ni Wanakwaya ya Dorcas Maswa kutoka Mkoani Simiyu, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Khamisi Hamza Khamis, ambaye ni Naibu Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Hawa ni Wakurugenzi na Wenyeviti wa Mabaraza Miji Zanzibar. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Deus Sangu, ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Manajimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; hawa ni marafiki zake na familia yake, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, ambao ni ndugu zake kutoka Mkoani Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia, tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Ravia Idarus Faina, ambao ni Viongozi wa Tawi la CCM, Nganani, Makunduchi, Mkoa wa Kusini Zanzibar, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 11 wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Mabula, ambao ni Viongozi na Wanachama wa *ATAPE* kutoka Ilemela Mkoani Mwanza, wakiongozwa na Sarah Ng'wani, ambaye ni Diwani wa Kata ya Buswelu, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 34 wa Mheshimiwa Sylivia Francis Sigula. Hawa ni wanakwaya kutoka Sumbawanga, Mkoani Rukwa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia, wageni nane wa Mheshimiwa Suleiman Haroub Suleiman, ambao ni Wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Mkoani Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge, kwa ajili ya mafunzo; viongozi wanne na Wanafunzi 75 wa Chama cha Skauti kutoka Wilaya ya Kinondoni, Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 41 na Walimu wawili wa Shule ya Awali na Msingi Jitegemee ya Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wafanyakazi nane kutoka *Phinu Media*, Katavi, karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile upo Uongozi wa Jamii Mpya 41 kutoka Jijini Dar es Salaam. Kwa hiyo, hii 41 ni idadi? Sawa.

Tunao wageni 41 ambao ni Uongozi wa Jamii Mpya kutoka Jijini Dar e Salaam. Karibuni sana. Japo sijajua hii Jamii Mpya inamaanisha nini, lakini tunawatakia kila la heri katika hiyo Jamii Mpya. Sijui ni katika kuanzisha jamii mpya ama katika hiyo, Jamii mpya? Tunawatakia kila la heri. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni tulionao Bungeni na wengine tutaendelea kuwatangaza kwa kadri watakavyopata nafasi ya kuingia hapa ndani. Sasa tutaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, sasa aje awasilishe hoja yake. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ninaomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Fungu Na. 56; Tume ya Utumishi wa Walimu, Fungu Na.2 na Mafungu 26 ya mikoa, ikijumuisha halmashauri 184 kwa mwaka 2024/2025. Aidha, ninaomba Bunge lako lijadili na kuidhinisha Mpango wa Utekelezaji, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha, kwa ajili ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Tume ya Utumishi wa Walimu na Mafungu 26 ya Mikoa, ikijumuisha halmashauri 184 kwa mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu ina sehemu nne. Ninaomba uridhie sehemu zote za hotuba yangu ziingie kwenye Kumbukumbu Rasmi ya Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa taarifa kuwa, hotuba hii itaonesha utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 kwa kipindi cha kuanzia Novemba, 2020 hadi Machi, 2025. Aidha, hotuba hii ni ya mwisho katika utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wa Miaka Mitano 2021/2022...

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, subiri kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, tupunguze sauti. Mnajadili mambo ya msingi, lakini tuwape nafasi Waheshimiwa Wabunge wanaotaka kumsikiliza Mheshimiwa Waziri, wamsikilize kwa utulivu.

Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: ....2021/2022 – 2025/2026; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 pamoja na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026) na Kipindi cha Kwanza cha Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu shukrani na pongezi; ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kunijalia kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu. Ninapenda kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake wenye dira, maono na dhamira ya kuwaletea wananchi maendeleo kwa vitendo. Miongozo, maelekezo na usimamizi wake umeendelea kututia moyo sisi wasaidizi wake na tunamuahidi kufanya kazi bila kuchoka ili kuboresha maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imekuwa heshima kwangu kuhudumu chini ya uongozi wake mahiri, akinipa nafasi ya kutumikia katika Serikali ikiwa ni Wizara yangu ya nne. Pia, imenipa nafasi ya kutumikia mihimili yote ya dola, yaani Mahakama ya Tanzania kwa miaka 13 kama Afisa Mwandamizi, miaka 10 ndani ya Bunge lako hili Tukufu na Serikali kwa miaka minne. Sasa ikiwa ni miaka 23 ya utumishi wa umma katika nafasi andamizi katika mihimili yote ya dola, ambapo nina hakika kwa nafasi hii na maono ya Mheshimiwa Raisi wetu amethibitisha kuwa, uongozi siyo nafasi tu, bali ni jukumu la kusukuma mbele gurudumu la maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuteuliwa kuwa mgombea wa nafasi ya Urais kwa

kipindi cha pili, Awamu ya Sita, kupitia Chama Cha Mapinduzi katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba, 2025. Tunamuamini na tunaendelea kuamini ataendelea kuleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi na kijamii katika nchi yetu. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa mgombea mwenza. Mwenyezi Mungu awape afya njema, hekima na maarifa katika kutekeleza majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwashukuru Waheshimiwa, Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati kwa uongozi wao thabiti na kujitolea kwa dhati katika kutimiza majukumu yao. Miongozo na maelekezo yao ya mara kwa mara yenye hekima na busara yamenisaidia sana katika majukumu yangu ya usimamizi wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshiwiwa Spika, kipekee ninaomba nikushukuru wewe binafsi, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani, kwa kuliongoza Bunge kwa weledi na umahiri wa hali ya juu. Umeonesha uongozi bora kwa kuhakikisha majadiliano yenye tija yanakuwa msingi kwenye Bunge letu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza pia Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kukusaidia kuendesha Shughuli za Bunge. Vilevile, ninawapongeza Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Madaba; Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum kwa umakini wao wa kuliongoza Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ninamshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Jimbo la Kilolo;

Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Jafari Chege Wambura, Mbunge wa Jimbo la Rorya; Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge za Hesabu za Serikali za Mitaa; Sheria Ndogo; Hesabu za Serikali; Uwekezaji Mitaji ya Serikali; Bajeti na Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge. Ninawiwa kusema, kazi zenu ni za thamani na zina mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa na ustawi wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara mbalimbali ambao wameendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kufanya kazi kwa pamoja ya kuwaletea maendeleo Watanzania. Ninathamini sana mchango wao na kwa pamoja tutaendelea kujenga Taifa lenye nguvu na ustawi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwashukuru viongozi wenzangu na wataalam wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Ninatambua mchango wao katika kuhakikisha wananchi wanahudumiwa katika nyanja zote.

Mheshimiwa Spika, kipekee ninawashukuru Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange, Naibu Waziri anayeshughulikia Afya na Mbunge wa Jimbo la Wanging'ombe; Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba, Naibu Waziri anayeshughulikia Elimu na Mbunge wa Viti Maalum. Ndugu Adolf Ndunguru, Katibu Mkuu; Naibu Makatibu Wakuu, Ndugu Sospeter Mtwale (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa), Mhandisi Rogatus Mativila (Miundombinu) na Ndugu Atupele Mwambene (Elimu); Mwalimu Paulina Nkwama, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu; Watendaji Wakuu wa Taasisi, Wakuu wa Mikoa ambao leo wako hapa mbele ya Bunge lako Tukufu, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri, ambao pia, tunao ndani ya Bunge lako hili Tukufu na watumishi wote chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa ninaendelea kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Rufiji kwa imani yao kwangu. Ninaendelea kuwaahidi kuwa nitafanya kazi bila kuchoka ili kutimiza ahadi ambazo tumeziweka kwa pamoja. Nitumie nafasi hii kuwaambia kuwa, mara zote ninapoiwaza Rufiji napata matumaini, imani, nguvu na ari ya kujitoa zaidi kwa mustakabali bora wa jimbo letu. Niwahakikishie, sichukulii dhamana waliyonipa kwa urahisi hata kidogo. Imani yao ni deni kwangu; sauti zao daima zitaongoza matendo yangu. Nitaendelea kuwahudumia kwa uadilifu, uwazi na uwajibikaji. Ninawashukuru sana. Wahenga walisema, "Asiyekumbuka kwao ni mtumwa". *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hiki kipindi cha utumishi wangu kwa wananchi wa Rufiji na taifa kwa ujumla nimepata faraja na msukumo mkubwa kutoka kwenye kumbukumbu ya baba yangu mpendwa ambaye alifariki dunia akiwa kwenye Ibada Tukufu huko Makka. Hii ni bajeti yangu ya kwanza kuiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu tangu kumpoteza baba yangu. Ni tukio lenye uzito wa kipekee katika maisha yangu ya uongozi kwani kila hatua ya safari yangu katika utumishi wa umma imekuwa ikiambatakana na maombi, ushauri na baraka zake. Ingawa ni huzuni kubwa kumpoteza, maisha yake yamebaki kuwa ni dira kwenye nguvu kwangu na kwa wengi waliomfahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baba yangu alikuwa ni mtu wa maono, msimamo, heshima na hekima. Alinilea katika misingi ya maadili, kujituma na kumheshimu kila mwanadamu; misingi ambayo imekuwa msingi wa uongozi wangu leo. Alinihimiza kuwa kiongozi mwenye kusikiliza ni mwenye kujifunza kila siku na mwenye kumtanguliza Mungu katika kila hatua ya maisha. Maisha yake yalijaa ibada, kujitoa kwa jamii na kusimama katika haki, katika mambo madogo madogo. Haya yote yamekuwa nguzo imara ya mtazamo wangu wa kulihudumia Taifa kwa moyo wote.

Mheshimiwa Spika, pamoja na huzuni ya kumpoteza, moyo wangu unafarijika na kujazwa nguvu kila ninapoyaona matunda ya kazi inayofanywa na ofisi ninayoiongoza chini ya mwongozo wa Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mambo makubwa na ya kihistoria yanaendelea kufanyika kutoka kwenye maboresho ya miundombinu, utoaji wa huduma kwa jamii hadi mageuzi ya kimfumo yanayolenga kuleta maendeleo kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, japo kifo chake kimeniacha na pengo kubwa moyoni pia kimeniacha na kumbukumbu hai ya kiongozi wa kweli niliyemjua tangu utoto. Ni kumbukumbu inayonipa msukumo wa kuendelea kufanya kazi kwa bidii, kwa kujitoa, kwa uadilifu na kwa upendo kwa watu wangu. Kwa sababu ninajua kule alipo, angependa kuona mwanawe akiendeleza dhamira yake ya kuwatumikia watu kwa moyo mmoja.

Mheshimiwa Spika, salamu za pole; ninatoa pole kwa Bunge lako kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, Mkoani Dar es Salaam na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika, Mwenyezi Mungu ampe pumziko la milele.

Mheshimiwa Spika, kuhusu jukumu la Ofisi ya Rais, TAMISEMI; TAMISEMI ina jukumu la kuratibu na kusimamia Mafungu 28 yanayojumuisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI (Fungu Na. 56) pamoja na Taasisi zilizo chini yake ambazo ni Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini *(TARURA)*; Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka *(DART)*; Chuo cha Serikali za Mitaa; Shirika la Elimu Kibaha; Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa; na Shirika la Masoko la Kariakoo. Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na.2) na Mafungu 26 ya mikoa ikijumuisha halmashauri 184.

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa majukumu yaliyolewa na Hati Idhini ya Rais *(Presidential Instrument)* ya tarehe 30 Agosti, 2023 yameainishwa katika aya ya 15 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 kuanzia Novemba, 2020 hadi Machi, 2025. Katika kipindi cha miaka mitano bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na mafungu yake imekuwa ikiongezeka kutoka shilingi trilioni 7.01 mwaka 2020/2021 hadi shilingi trilioni 10.53 mwaka 2024/2025. Hii

ni sawa na ongezeko la 50.21%. Ofisi ya Rais, TAMISEMI inamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona umuhimu wa Serikali za Mitaa na kuziongezea bajeti. Hii inaonyesha namna anavyowajali wananchi kwa kupeleka maendeleo kwa vitendo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, ongezeko hili si tu la fedha ni ushahidi wa mabadiliko bali ni matumaini mapya kwa wananchi wa hili Taifa kupata huduma bora. Ni daraja jipya linalounganisha maendeleo na maisha ya kila siku. Ni shule mpya, zahanati, barabara, maji safi na juu ya yote ni heshima kwa utu wa Mtanzania wa kawaida. Leo hii tunapopitia haya mafanikio tunasema kwa sauti kubwa Serikali ya Awamu ya Sita inatekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa vitendo; na sisi sote, kama wawakilishi wa wananchi tuna dhamana ya kuendeleza hii kasi kwa mshikamano, uadilifu na moyo wa kizalendo. Tanzania mpya inawezekana na inaendelea kujengwa mbele ya macho yetu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imetekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu mwaka 2020 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi na uendeshaji wa Elimumsingi na Sekondari ibara ya 80 ya Ilani. Elimu ni urithi wa kizazi, urithi usioharibika, usioibwa na usiozeeka. Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano aliweka msingi imara aliposema, "Ni jukumu letu kuimarisha elimu ya ufundi na mafunzo ili vijana wetu wawe na ujuzi wa kukabiliana na ajira". Kauli hii si tu kauli ya kisera, bali ni mwamko wa kiroho na kijamii, mwamko wa Taifa linalojua kuwa maendeleo ya kweli hayaanzi na barabara wala majengo, bali na maarifa yaliyowekezwa kwa watu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ninapowasilisha mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI katika utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa upande wa elimumsingi na sekondari, ninatoa ushahidi wa mabadiliko ya kweli, mabadiliko ya shule zilizofufuliwa, walimu walioajiriwa, watoto

waliowezeshwa na matumaini mapya yaliyochipuka kila pembe ya nchi yetu. Kwa sababu katika Taifa lenye maono, kila darasa linalojengwa si tu ukuta bali ni mlango wa maisha mapya kwa mtoto wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu hilo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imetekeleza ilani katika huduma ya elimu kama ifuatavyo:-

(i) Kuboresha shule 28 za mchepuo wa elimu ya ufundi na amali kwa kuzikarabati na kutoa vifaa vya kisasa. Aidha, kuboresha shule 274 za michepuo ya kilimo na 28 za michepuo ya biashara;

(ii) Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu ya msingi na sekondari imeongezeka kutoka miundombinu 582,733 hadi 754,075. Miundombinu hiyo inajumuisha vyumba vya madarasa, shule za msingi, shule za sekondari, matundu ya vyoo kwa shule za msingi na sekondari, nyumba za walimu, maabara, mabweni na mabwalo;

(iii) Ruzuku ya Elimu Bila Ada imeongezeka kutoka shilingi bilioni 249.66 hadi shilingi bilioni 484.27 kwa mwaka sawa na 93.97%;

(iv) Uandikishaji wa watoto wenye mahitaji maalum umeongezeka kutoka wanafunzi 28,482 hadi 78,429 sawa na 175%. Aidha, madarasa 44, matundu ya vyoo 132 na mabweni 172 yamejengwa kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum;

(v) Walimu 44,527 wameajiriwa wakiwemo walimu 447 wa elimu maalum; na

(vi) Kutoa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ambapo uandikishaji umeongezeka kutoka 28,482 hadi 78,429 sawa na 175%. Aidha, madarasa 44, matundu ya

vyoo 132 na mabweni 172 yamejengwa kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Spika, matokeo haya si tu mafanikio ya kiutawala bali ni ushindi wa kitaifa. Kuongeza miundombinu ya elimu; kuwekeza takribani shilingi bilioni 500 katika elimu bila ada na kuongeza idadi ya wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa 175% haya ni matendo yanayosema kwa sauti kubwa kuliko maneno, kwamba Serikali hii haikuja kuahidi tu, bali kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, wapo waliokuwa na mashaka, wapo waliokuwa wamesahau matumaini lakini leo tuna ushahidi kuwa pale ambapo kuna nia njema kuna njia, na katika kila kona ya Tanzania kuna darasa, mwalimu na mwanafunzi anayesimama kama ushahidi wa mabadiliko haya. Hivyo, ninaomba nitamke kauli ambayo itakumbukwa kwa miaka mingi ijayo: Mtoto wa Kitanzania, popote alipo hawezi tena kuzuiwa na umbali na hawezi tena kusahaulika kwa sababu ya ulemavu; elimu sasa ni haki ya kila Mtanzania na Tanzania mpya inaanzia darasani. Kwa misingi hiyo, tunaamini kabisa kuwa elimu yetu, uhai wa Taifa Letu; elimu yetu ni uhai wa Taifa Letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio zaidi yameanishwa katika aya ya 21 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uratibu na usimamizi wa huduma za afya ya msingi ibara ya 83. Hayati Benjamin William Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu aliwahi kusema "Tusiposhughulikia masuala ya afya ya msingi hatutaweza kupiga hatua kubwa katika maendeleo".

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza kauli hiyo, Awamu ya Sita chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kuimarisha huduma za afya ya msingi ambapo imetekeleza ilani katika eneo hilo kama ifuatavyo: -

(i) Kuongeza vituo vya kutolea huduma ya afya ya msingi kutoka 6,081 hadi 7,713 sawa na ongezeko la vituo

1,632 au 26.80%. Kati ya vituo hivyo, zahanati ni 1,158, vituo vya afya 345 na hospitali za halmashauri 129;

(ii) Kujenga hospitali mpya za halmashauri 129 ikiwa ni ongezeko la 31.63% ya lengo la kujenga hospitali 98;

(iii) Kuajiri wataalam wa afya 34,720 ambapo Madaktari ni 1,851; Matabibu 6,546; Wauguzi 10,213; Watekinolojia Mionzi, Macho, Maabara, Meno na Dawa 1,488; Wafamasia 993; Maafisa Lishe 328; Maafisa Ustawi 224; Fundi Sanifu Vifaa Tiba 239 na kada nyingine watumishi 12,838; na

(iv) Ongezeko la akinamama wanajifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya kutoka akinamama 52,585 mwaka 2020 hadi kufikia akinamama 141,386 mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, tumeyaishi kwa vitendo maneno ya Hayati Mzee wetu, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Awamu ya Pili aliyesema "Tuwekeze katika afya ya mama na mtoto kwa kuwa wao ni msingi wa kizazi kijacho chenye nguvu."

Mheshimiwa Spika, mafanikio zaidi yameainishwa katika aya ya 25 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma za lishe Ibara ya 86(a) – (d). Mheshimiwa Hayati Ali Hassan Mwinyi Rais wa Awamu ya Pili aliwahi kusema: "Lishe bora na usafi wa mazingira ni silaha madhubuti za kupambana na magonjwa yanayozuilika."

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeendelea kuyaenzi maneno hayo kwa kusimamia utekelezaji wa ahadi hiyo kwa Watanzania ambapo imetekeleza ilani katika eneo la lishe kama ifuatavyo:-

(i) Watoto 7,454,996 walipimwa hali ya lishe kwenye vijiji na mitaa nchini ambapo watoto 149,308 walipatiwa matibabu ya utapiamlo mkali. Aidha, wazazi na

walezi milioni 11.44 walipatiwa elimu na unasihi wa lishe;

(ii) Wajawazito 7,440,632 walipatiwa vidonge vya kuongeza wingi wa damu. Aidha, watoto 8,944,200 wenye umri chini ya miaka mitano walipatiwa nyongeza ya matone ya vitamini A kupitia kampeni za kitaifa zinazofanyika mara mbili kila mwaka; na

(iii) Kutenga shilingi 1000 au zaidi kwa kila mtoto chini ya umri wa miaka mitano kutoka mapato ya ndani ambapo jumla ya shilingi bilioni 48.56 zilitolewa na kutumika kutoa huduma katika afua za lishe katika mikoa na halmashauri.

Mheshimiwa Spika, mafanikio zaidi yameanishwa katika aya ya 27 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma za ustawi wa jamii Ibara ya 91 ya Ilani. Hayati Mzee Benjamini William Mkapa Rais wa Awamu ya Tatu aliwahi kusema "Maendeleo ya kweli hayawezi kupatikana kama hatuwekezi katika afya, elimu, na ustawi wa jamii. Taifa imara linajengwa kwa kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma bora na fursa sawa za maendeleo."

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeendelea kuyaishi maneno hayo ambapo utekeleza ilani katika huduma za ustawi wa jamii umeendelea kama ifuatavyo:-

(i) Kutambua wazee 4,975,473 (wanawake 2,682,210 na wanaume 2,293,263) na kutoa huduma za matibabu bila malipo;

(ii) Kushughulikia ukatili wa kijinsia ambapo mashauri 517,286 ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto yameshughulikiwa;

(iii) Watu wenye Ulemavu 821,763 (wanawake 410,442 na wanaume 411,321) walipatiwa huduma za msaada wa kisaikolojia; na

(iv) Watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi 2,592,963 (wanawake 1,450,949 na wanaume 1,142,014) walitambuliwa na kupatiwa huduma mbalimbali zikiwemo mafunzo ya ufundi stadi, kadi za bima ya afya ya jamii na vifaa vya shule.

Mheshimiwa Spika, mafanikio zaidi yameanishwa katika aya ya 29 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi, ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya barabara na usafirishaji ibara 57 ya Ilani; Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)*. Ofisi ya Rais, TAMISEMI imetekeleza ilani katika ujenzi, ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya barabara kupitia *TARURA* kama ifuatavyo: -

(i) Ujenzi wa barabara za changarawe ambao umeongezeka kutoka kilomita 24,493 hadi kilomita 44,372.21 sawa na ongezeko la 81.16%. Urefu wa barabara za vijijini na mijini zilizojengwa kwa kiwango cha lami umeongezeka kutoka kilomita 2,025 hadi kilomita 3,467, sawa na ongezeko la 71.22%. Aidha, kuongeza mtandao wa barabara kutoka kilomita 108,946 hadi kilomita 144,429.7 sawa na ongezeko la 32.57%;

(ii) Kutekeleza kazi za ujenzi wa miundombinu ya barabara kwa kutumia teknolojia mbadala ambapo barabara zenye urefu wa kilomita 61.7 zinaendelea kufanyiwa utafiti ili kupunguza gharama za ujenzi, matengenezo na ukarabati; na

(iii) Tulipotoka kulikuwa na vumbi, lakini leo tunatembea kwenye lami. Tulipotoka kulikuwa na miteremko isiyopitika, leo tuna barabara zinazounganisha

ndoto na fursa. Kuongezeka kwa barabara za changarawe kwa 81.16% na lami kwa 71.22% ni ushahidi wa nchi inayojenga msingi wa maendeleo kwa kila Mtanzania, kuanzia kijijini hadi mjini. Huu siyo mradi wa barabara tu, huu ni mradi wa matumaini.

Mheshimiwa Spika, kila kilomita mpya ya barabara iliyojengwa ni daraja kati ya umaskini na maendeleo; ni njia ya mtoto kufika shuleni, mama kufika hospitali, mkulima kupeleka mazao sokoni na Taifa kusonga mbele. Kuongeza mtandao wa barabara kutoka kilomita 108,946 hadi zaidi ya 144,000 si takwimu tu ni mabadiliko ya kweli yanayoonekana, yanayogusika na yanayogusa maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara hizi ni sauti ya Serikali inayosema "Hatukuwaacha Nyuma". Hizi ni njia zinazotufikisha kwenye Tanzania ya viwanda, fursa na mshikamano wa kitaifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka. Ofisi ya Rais, TAMISEMI imetekeleza ilani kwa kutoa huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka kupitia *DART* kama ifuatavyo:-

(i) Kusambaza kadi janja 62,000 kati ya 200,000 katika awamu ya kwanza na kusimika mageti janja kwenye vituo vyote 27;

(ii) Kusimika Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji Nauli ambao utafungamanishwa na mfumo wa kuongozea magari ambao upo kwenye hatua ya ununuzi; na

(iii) Kununua watoa huduma watatu wa uendeshaji kwa njia ya ubia wa mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili na mikataba imeshasainiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu watu wa Jiji la Dar es Salaam wamekuwa wakisubiri, wengine kwa matumaini, wengine kwa mashaka lakini wote kwa kiu ya mabadiliko. Leo kwa mara

ya kwanza tunasema kwamba subira yao haikuwa ya bure. Kupitia ubia kati ya Serikali na sekta binafsi tumefanikisha hatua ya kihistoria, kusaini mikataba na watoa huduma watatu wa uendeshaji wa awamu ya pili ya mabasi yaendayo haraka. Hili ni tukio la mwanzo wa zama mpya siyo tena hadithi ya ahadi zisizotekelezwa, bali ya huduma bora zinazoonekana na kuguswa.

Mheshimiwa Spika, "*great things take time*." Wanafalsafa wanasema, "Mambo Makubwa Yanahitaji Muda." Hatua hii si tu ununuzi wa huduma, bali ni ununuzi wa matumaini mapya kwa wakazi wa Jiji letu la Dar es Salaam. Hatutaki kurudia makosa ya jana, bali tunajenga mfumo imara, unaozingatia ubora, ufanisi na heshima kwa muda na maisha ya abiria.

Mheshimiwa Spika, Mzee Desmond Tutu aliwahi kusema; "*Hope is being able to see that there is light despite all the darkness.*"

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi wananchi wamepitia usumbufu, wananchi foleni zisizokwisha na huduma zisizoeleweka, lakini leo, tunasema kwa sauti ya matumaini nuru inaanza kuonekana. Mabasi haya hayatakuwa tu magari ya kusafirisha watu yatakuwa magari ya kusukuma uchumi, kuunganisha fursa na kupunguza mzigo wa maisha ya kila siku. Bwana Khalil Gibran aliwahi kusema: "*Progress is not in enhancing what is, but in advancing towards what will be.*"

Mheshimiwa Spika, mradi huu unaonesha jinsi tunavyotoka kwenye kilichozoeleka: foleni na ajali, uchakavu na kuelekea kwenye kile kinachowezekana, usafiri wa kisasa wa heshima na wa watu wote. Tunajenga mfumo wa usafiri wa umma ambao utaweka heshima kwa abiria, uwajibikaji kwa watoa huduma na thamani kwa kila senti inayowekezwa. Awamu hii mpya ni jibu la kilio cha miaka mingi, ni ushahidi kuwa Serikali ya Awamu ya Sita haikosei mwelekeo, tunasonga mbele kwa busara, kwa maono na kwa nia njema ya kuwahudumia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, utawala bora, kujenga uwezo, usimamizi wa rasilimali, ujenzi wa majengo ya utawala na makazi ya

viongozi Ibara za 18 ya Ilani. Ofisi ya Rais, TAMISEMI imetekeleza ilani kwenye eneo la utawala bora kama ifuatavyo:-

(a) Kero 282,124 zimepokelewa na kusikilizwa katika ngazi ya mikoa na wilaya ambapo jumla ya kero 263,893 zimetatuliwa sawa 93.54% na 6.46% ya kero zilizobaki zipo katika hatua mbalimbali za utatuzi;

(b) Kuajiri Maafisa Tarafa, Wahandisi, Wakadiriaji wa Majengo na wataalamu wa ununuzi na kupangwa katika mikoa; na

(c) Kufanya ujenzi na ukarabati wa majengo mbalimbali ikiwemo ujenzi wa Ikulu Ndogo 23, Ofisi 26 za Wakuu wa Mikoa, Ofisi 85 za Wakuu wa Wilaya, ofisi 141 za Maafisa Tarafa, nyumba 21 za Wakuu wa Mikoa, nyumba 22 za Makatibu Tawala wa Mikoa, nyumba 73 za Wakuu wa Wilaya, nyumba 56 za Makatibu Tawala Wasaidizi na nyumba 62 za Makatibu Tawala wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, mafanikio zaidi yameainishwa katika aya ya 40 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, ulinzi wa mazingira, uhifadhi wa maliasili mabadiliko ya tabianchi na biashara ya kaboni ibara za 68 ya Ilani. Shilingi bilioni 45 zimepokelewa kutoka Kampuni ya Kaboni Tanzania kutokana na uuzaji wa *carbon*. Fedha hizo zimenufaisha wananchi wa halmashauri 10 ambazo ni Tanganyika, Kiteto, Mbulu, Karatu, Kyerwa, Karagwe, Misenyi, Muleba, Ngara na Bukoba Mjini. Shughuli zilizotekelezwa kutokana na fedha zilizopatikana zimeainishwa katika aya ya 43 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaendelea na utekelezaji wa mkakati wa Serikali wa kupunguza matumizi ya kuni na mkaa kwa lengo la kupunguza kasi ya uharibifu wa mazingira. Hadi Machi, 2025 taasisi 903 zikiwemo shule za msingi 83, sekondari 650 na taasisi zingine 170 zimeanza kutumia mfumo wa nishati safi. Kuimarisha Mamlaka za Serikali za Mitaa Ibara za 19, 32, 122. Ofisi

ya Rais, TAMISEMI imetekeleza ilani katika uimarishaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ifuatavyo:-

(a) Kutoa mikopo ya shilingi bilioni 158.50 kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambapo shilingi bilioni 63.40 zimetolewa kwa vikundi 8,576 vya wanawake; shilingi bilioni 63.40 zimetolewa kwa vikundi 4,981 vya vijana; na shilingi bilioni 31.70 zimetolewa kwa vikundi 2,319 vya watu wenye ulemavu;

(b) Bajeti ya mapato ya ndani ya halmashauri imeongezeka kutoka shilingi bilioni 814.96 hadi shilingi trilioni 1.35 sawa na ongezeko la 66.65%. Aidha, fedha za mapato ya ndani zilizoidhinishwa katika miradi ya maendeleo zimeongezeka kutoka shilingi bilioni 333.09 hadi shilingi bilioni 454.41 hii sawa na ongezeko la 36.42%.

Mheshimiwa Spika, mafanikio zaidi yameainishwa katika aya ya 46 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uendelezaji Miji Ibara ya 76 na 122. Ofisi ya Rais, TAMISEMI imetekeleza ilani katika uendelezaji miji katika maeneo yafuatayo:-

(a) Kuandaa na kuidhinisha Mipango Kabambe ya miji 33 ya Mamlaka za Upangaji ikiwemo miji yote ya Makao Makuu ya Mikoa 26 ambayo iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji; na

(b) Kuandaa Mpango Kabambe Jumuishi wa Jiji la Kibiashara na Uwekezaji la Kwala, Mkoa wa Pwani wa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, mafanikio zaidi yameainishwa katika aya ya 48 hadi 51 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uendelezaji wa miji midogo inayochipukia Ibara ya 122. Ofisi ya Rais, TAMISEMI imefanya utambuzi wa miji midogo inayochipukia 4,103 hii ni sawa na 91.5%

ya miji yote nchini ili kupunguza kasi ya ukuaji kiholela na kuongeza kasi ya urasimishaji wa makazi na biashara vijijini.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mwaka 2024 Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilipanga kutekeleza mpango wa bajeti kwa kuzingatia vipaumbele 11 vilivyoainishwa katika aya ya 55 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukusanyaji wa Kodi ya Majengo, Maduhuli na Mapato ya Ndani ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI (Mafungu 28) Mwaka 2024/2025. Hadi Machi, 2025 shilingi trilioni 1.11 zimekusanywa, hii ni sawa na 53.15% ya lengo la kipindi hicho. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 61.21 ni kodi ya majengo, shilingi trilioni 1.04 ni mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, shilingi bilioni 16.23 ni mapato ya ndani ya Taasisi na shilingi milioni 201.60 ni maduhuli ya mikoa. Makusanyo hayo yalitokana na ada za wanachuo, tozo, ukusanyaji wa madeni, mauzo ya bidhaa mbalimbali na ushuru unaotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kulingana na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290.

Mheshimiwa Spika, kuhusu taarifa ya fedha za matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Mwaka 2024/2025, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na taasisi zilizo chini ya Ofisi hii (Fungu Na. 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na.2) na Mafungu 26 ya mikoa (yakijumuisha halmashauri 184) ilipanga kutumia shilingi trilioni 10.53 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya hizo matumizi ya kawaida ni shilingi trilioni 6.94 ambapo mishahara ni shilingi trilioni 5.52 na matumizi mengineyo ni shilingi trilioni 1.42 yanayojumuisha shilingi bilioni 815.06 za mapato ya ndani ya halmashauri. Aidha, shilingi trilioni 3.58 ni fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2025 Mafungu 28 yamepokea na kukusanya shilingi trilioni 7.53 hii ni sawa na 71.47% ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 5.39 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida yakijumuisha mishahara shilingi trilioni 4.08 na matumizi mengineyo shilingi trilioni 1.31. Aidha, shilingi trilioni 2.13 ni fedha za miradi ya maendeleo ikijumuisha shilingi trilioni 1.74 fedha za ndani na shilingi bilioni 385.83 ni fedha

za nje. Kati ya fedha zilizopokelewa shilingi bilioni 312.30 ni za mapato ya ndani ya halmashauri ambazo zimetumika kwenye Miradi ya Maendeleo iliyoainishwa katika Kiambatisho Na.3 cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafanikio ya utekelezaji ya bajeti kwa mwaka 2024/2025. Mwaka 2024/2025 Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zimefanikiwa kutekeleza shughuli mbalimbali. Kuhusu shughuli zilizotekelezwa kupitia fedha za mapato ya ndani ya halmashauri; Mheshimiwa Spika, Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema: "Tunahitajika kuongeza juhudi zetu katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ili tuweze kufikia malengo yetu ya maendeleo."

Mheshimiwa Spika, mwaka 2024/2025, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilipanga kutumia shilingi bilioni 541.27 za mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya kuchangia utekelezaji wa shughuli za maendeleo. Hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 312.30 sawa na 57.70% zimetolewa na shughuli mbalimbali zimetekelezwa. Matengenezo ya barabara yenye urefu wa kilometa 435.75 kwa kiwango cha lami ambapo kilometa 180.75 matengenezo yamekamilika na kilometa 255 ujenzi unaendelea, ujenzi wa madaraja, makalavati mafanikio zaidi yameainishwa katika aya ya 62 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024. Mwaka 2024/2025 Ofisi ya Rais, TAMISEMI iliidhinishiwa shilingi bilioni 254.82 kwa ajili ya kuratibu na kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 247.03 ni fedha kutoka Serikali Kuu na shilingi bilioni 7.78 ni fedha za mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya uchaguzi. Uchaguzi huu ulihusisha uchaguzi wa viongozi katika ngazi ya msingi ambao ni Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa, Vitongoji, Wajumbe wa Halmashauri za Vijiji na Wajumbe wa Kamati za Mitaa. Tunampongeza kila Mtanzania kwa kushiriki kwa amani na utulivu mkubwa katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliyokuwa wa viwango vya hali ya juu. Shughuli zaidi zilizotekelezwa zimeanishwa katika aya ya 64 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uratibu na usimamizi wa huduma za afya ya msingi. Katika mwaka 2024/2025, Ofisi ya Rais, TAMISEMI iliidhinishiwa kutumia shilingi bilioni 357.85 za ruzuku ya fedha za maendeleo za Serikali Kuu na Washirika wa Maendeleo katika uratibu na usimamizi wa huduma za afya ya msingi, ustawi wa jamii na lishe. Hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 166.38 zimepokelewa hii sawa na 46.49% ya fedha iliyoidhinishwa. Shughuli zifuatazo zimetekelezwa ni pamoja na:-

(a) Ukarabati na ukamilishaji wa hospitali 89 za wilaya kati ya 118 zilizopangwa ambapo hospitali 65 zipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji wa ujenzi na hospitali 24 zipo katika hatua za ununuzi; na

(b) Ukamilishaji wa vituo 16 vya afya ambapo vituo 13 vipo katika hatua za ununuzi na vituo vitatu vipo katika hatua za ukamilishaji wa ujenzi kwa miundombinu iliyopelekewa fedha ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Spika, umefanyika ununuzi wa vifaa tiba kwa ajili ya hospitali 119 kati ya 136 za wilaya, vituo 41 kati ya 44 vya afya katika halmashauri 18. Vifaatiba kwa ajili ya zahanati 356 kati ya 386 katika halmashauri 164. Shughuli nyingine zilizotekelezwa zimeainishwa katika aya ya 66 ya hotuba yangu. Utekelezaji wa shughuli za usimamizi na uendeshaji wa elimumsingi na sekondari.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaratibu usimamizi na uendeshaji wa elimu ya awali, msingi na sekondari nchini kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mwaka 2024/2025 Ofisi ya Rais, TAMISEMI iliidhinishiwa kutumia shilingi trilioni 1.02 kupitia ruzuku ya Serikali Kuu na Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli katika Sekta ya Elimu. Hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 663.29 zimepokelewa hii ni sawa na 66% ya fedha iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafanikio ya mpango wa elimumsingi bila ada. Maafisa Elimu kata 3,931, Wakuu wa Shule za Msingi 18,021 na Sekondari 4,944 walipokea Posho ya Madaraka, jumla ya wanafunzi 376,052 wamepata ruzuku ya

chakula ambapo wanafunzi 330,325 wa bweni na wanafunzi 45,727 wa kutwa; wanafunzi 12,285,382 wamepata ruzuku ya uendeshaji kwa shule za msingi 18,021. Vilevile, jumla ya wanafunzi 305,906 wa sekondari walipata ruzuku ya chakula na fidia ya ada ya bweni, fidia ya ada ya kutwa kwa wanafunzi 2,761,311 na ruzuku ya uendeshaji wanafunzi 3,067,217 kwa shule za sekondari 4,944 imetolewa. Mafanikio zaidi yaliyopatikana kwenye Sekta ya Elimu Msingi na Sekondari yameainishwa katika aya ya 70 hadi 84 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi na ukamilishaji wa miundombinu ya shule. Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaendelea na umaliziaji wa maboma yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi na miradi viporo katika shule za msingi na sekondari. Ukamilishaji unaoendelea ni madarasa 1,897, mabwalo 241, mabweni 126, majengo ya utawala matatu, hosteli 11, maabara 42 na nyumba za walimu sita.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ununuzi wa vifaa vya kujifunzia; Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaendelea na taratibu za ununzi wa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya shule za msingi 600 ambavyo ni *Smart Blackboard 416, All in One Computers 8,672, Multifunction Photocopier (Black & White) 600, Laptop Computer 600, UPS 4,936, AI Smart Classroom 184.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu utawala bora, usimamizi wa rasilimali, ujenzi wa majengo ya utawala na makazi ya viongozi, utatuzi wa kero za wananchi katika mikoa na wilaya. Hayati Benjamini William Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu aliwahi kusema: "Utawala bora ni msingi wa maendeleo endelevu; bila yake, hatuwezi kufikia malengo yetu." Kwa muktadha huo Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeendelea kusimamia shughuli za utawala bora na utatuzi wa kero za wananchi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaendelea kuyaenzi maneno hayo ambapo mwaka 2024/2025, Ofisi za Wakuu wa Mikoa ziliidhinishiwa shilingi bilioni 4.56 kwa ajili ya shughuli za ufuatiliaji, utatuzi wa kero na uhamasishaji wa shughuli

za maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 4.03 zimetolewa sawa na 88.37%. Aidha, katika kipindi hicho kero 70,432 zimeshughulikiwa ambapo kero 52,201 mashauri yake yamefungwa na kero 18,231 zinaendelea na utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu Mstaafu Hayati Edward Moringe Sokoine tarehe 26 Machi, 1983 alisema: "Ole wake kiongozi mzembe na asiye na nidhamu nitakayemkuta, viongozi wazembe na wabadhirifu wahesabu siku zao, labda tusiwajue. Hawa Hatuna sababu ya kuwapa imani, kuwa tutawalinda kama vitendo vyao viovu." Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kutokuwa na muhali na watendaji wote wazembe na wabadhirifu wa mali za umma ambapo mwaka 2024/2025 watumishi 2,297 wamechukuliwa hatua za kinidhamu, kati yao Wakurugenzi ni tisa, Wakuu wa Idara na Vitengo 81, watumishi wa sekta ya ujenzi 43 na watumishi wa kawaida 2,164 wa kada nyingine. Ofisi ya Rais, TAMISEMI itaendelea kusimamia nidhamu na uwajibikaji wa utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwezeshaji wa ngazi za msingi za Mamlaka za Serikali za Mitaa; katika kutekeleza dhana ya ugatuaji madaraka kwa wananchi, Serikali imeendelea kuboresha utendaji kazi katika ngazi za msingi ili kuimarisha utawala bora, maendeleo endelevu na ushiriki wa wananchi katika maamuzi yanayogusa maisha yao. kwa kutambua umuhimu huo, Serikali katika mwaka 2024/2025 ilitenga shilingi bilioni 1.73 za matumizi mengineyo kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya posho ya mawasiliano kwa Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa. Hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 1.15 zimetolewa hii ni sawa na 66.47% ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya posho ya mawasiliano katika halmashauri 165 ambazo mapato yake ni chini ya shilingi bilioni 5.0 katika vijiji 12,263 na mitaa 2,161.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu; Rais wetu, Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema: "Mikopo ya 10% ni njia mojawapo ya kusaidia jamii katika kuleta usawa wa kijamii na kiuchumi".

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2024/2025, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilipanga kutoa mikopo ya shilingi bilioni 227.96 ambapo shilingi bilioni 63.67 ni fedha za marejesho zilizokuwa zikiendelea kukusanywa kutokana na mikopo iliyotolewa kabla ya kusimamishwa. Aidha, shilingi bilioni 63.24 ni fedha zilizokuwa zinatengwa kwa ajili ya mikopo na shilingi bilioni 101.05 ni fedha ambazo zimekadiriwa kutokana na makisio ya makusanyo ya mapato ya ndani ya mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 82.84 zimekopeshwa kwa vikundi 8,275 vya wanawake, vijana na wenye ulemavu. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 40.71 ya vikundi 4,557 vya wanawake, shilingi bilioni 36.64 ya vikundi 2,827 kwa vijana na shilingi bilioni 5.48 kwa vikundi 891 vya watu wenye ulemavu. Aidha, hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 14.04 zimerejeshwa kutoka vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Miundombinu; Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia *TARURA* kwa kushirikiana na Benki ya *CRDB* imeratibu uanzishwaji wa Hatifungani ya Miundombinu iitwayo *Samia Infrastructure Bond* iliyolenga kukusanya zaidi ya shilingi bilioni 150 ambapo hadi sasa shilingi bilioni 323 sawa na 215.33% zimekusanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia *TARURA* iliidhinishiwa shilingi bilioni 71.46 kwa ajili ya kugharamia barabara zilizoathiriwa na mafuriko ya maji ya mvua. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 50 ni fedha za bajeti ya nyongeza ya bajeti ya Mwaka 2024/2025. Hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 8.01 zimepokelewa sawa na 11.28%.

Mheshimiwa Spika, Muhtasari wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2025/2026. Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mwaka 2025/2026, yamezingatia Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026); Mipango Mikakati ya Taasisi; Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania aliyoitoa wakati akilihutubia Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021; Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/2026; Sheria ya Bajeti Sura 439; Sera za Kisekta; Maelekezo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; malengo yaliyomo katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 - 2025/2026; na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, mikoa na halmashauri vimeambatanishwa katika aya ya 140 hadi 143 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutumia fursa hii kuwaelekeza Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa kuwasimamia Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzingatia vipaumbele nilivyoainisha katika hotuba yangu.

(i) Kuhakikisha ukusanyaji wa mapato unafikia malengo;

(ii) Kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya afya ya msingi, elimu msingi na sekondari kulingana na mipango iliyowekwa;

(iii) Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Uchumi wa Kidijiti ikiwemo uwekezaji na matumizi ya mifumo na miundombinu ya TEHAMA katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na vituo vya huduma za afya na elimu;

(iv) Kuhakikisha mapato katika mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa yanakusanywa kupitia mifumo ya TEHAMA ya Serikali pamoja na kufanya ufuatiliaji wa karibu wa mifumo hiyo ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato;

(v) Mikoa na mamlaka za Serikali za mitaa kuhakikisha inatekeleza Mikakati ya Uchumi wa Buluu, nishati safi ya

kupikia na mabadiliko ya tabianchi na utunzaji wa mazingira;

(vi) Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa iendelee kuimarisha mifumo stahimilivu na endelevu ya utoaji wa huduma bora za afya, ustawi wa jamii na lishe ili kuboresha huduma ambayo ni nguzo muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote; na

(vii) Wakuu wa Mikoa na Wakurugenzi wahakikishe watoto walio chini ya miaka mitano wanajiunga kwenye vituo vya jamii vya kulelea watoto wadogo mchana.

Mheshimiwa Spika, aidha, kila halmashauri itapimwa utekelezaji wa vipaumbele hivi kwa kuzingatia miradi iliyotengewa bajeti kwa Mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, nitumie fursa hii kuwashukuru wadau mbalimbali walioshirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kufanikisha utekelezaji wa mpango na bajeti ya 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ninawashukuru wadau wote ambao wametoa ahadi za kuchangia utekelezaji wa bajeti ya 2025/2026 kwa mafungu 28. Wadau hao ni pamoja na: Benki ya Dunia, *UNICEF, Global Fund, Twiga Barrick Tanzania, European Union, JICA, KOICA, UNCDF, CDC, SIDA, UNDP, UNFPA, UN Women, Carbon Tanzania, UNEP, WHO, AfDB, WWF, FCDO, DANIDA, CANADA, SDC SWISS*, Shirika la Korea, Serikali ya Shirikisho la Ujerumani, Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kupitia *FOCAC, Global Facility Financing* na *GAVI. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, ninawashukuru viongozi wa Chama Cha Mapinduzi katika ngazi zote kwa kutekeleza wajibu wao wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 katika maeneo yao, watendaji wote wa ngazi za msingi bila kusahau Wenyeviti wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa, Watendaji wa Mitaa na Vijiji, Watendaji wa Kata,

Maafisa Tarafa, Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakurugenzi wa Halmashauri, Makatibu Tawala wa Wilaya, Waheshimiwa Madiwani, Waheshimiwa Wabunge, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Mikoa na watumishi wote wa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa utendaji kazi wao mzuri.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine ninawashukuru tena wananchi wa Jimbo la Rufiji kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya kitaifa na jimbo na kuniombea kila siku. Ninaahidi kuendelea kuwatumikia na kushirikiana nao kila hatua katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee, ninaishukuru kwa dhati familia yangu kwa upendo wao, uvumilivu na maombi yao wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yangu ya kitaifa. Ninawashukuru kwa kusimama nami katika safari hii ya kuleta maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2025/2026 ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI; Makadirio ya Makusanyo ya Kodi ya Majengo, Maduhuli na Mapato ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2025/2026, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, taasisi zilizo chini yake, mikoa 26 ikijumuisha halmashauri 184 inaomba idhini ya kukusanya kodi ya majengo, maduhuli na mapato ya ndani ya shilingi 1,925,881,323,464.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha hizo, shilingi 56,108,174,064 ni mapato ya ndani ya taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, shilingi 306,079,400 ni maduhuli ya mikoa na shilingi 1,680,506,764,000 ni za mapato ya ndani ya halmashauri. Aidha, shilingi 188,960,306,000 ni kodi ya majengo ambayo itakusanywa na mamlaka za serikali za mitaa ambazo zimepewa uwakala wa kukusanya kodi hiyo na kuwasilisha makusanyo hayo Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali; Jedwali Na.1.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi Ofisi ya Rais; sasa ninaomba Bunge lako likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2025/2026 yenye jumla ya shilingi 11,000,782,984,200 kwa ajili ya Ofisi ya Rais TAMISEMI.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, subiri kidogo, hebu soma upya hiyo jumla.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, ninaomba Bunge lako likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2025/2026 yenye jumla ya shilingi 11,782,984,202,000 kwa ajili ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na taasisi zilizo chini yake Fungu Na. 56, Tume ya Utumishi wa Walimu - Fungu Na.2 na Mafungu 26 ya Mikoa yakijumuisha Halmashauri 184.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha zinazoombwa, shilingi 7,836,140,708,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida yanayojumuisha mishahara, shilingi 6,292,557,648,000 ni matumizi mengineyo, shilingi 1,543,583,060,000 ikijumuisha shilingi trilioni moja…

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, hiyo *figure* tusomee tena.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, shilingi 1,543,583,060,000 ikijumuisha shilingi 1,067,065,328,000 za mapato ya ndani ya halmashauri.

Mheshimiwa Spika, shilingi 3,946,843,494,000 zinaombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo kati ya fedha hizo, shilingi 2,498,981,476,000 ni fedha za ndani, ikijumuisha shilingi 613,441,436,000 za mapato ya ndani ya halmashauri na shilingi 1,447,912,018,000 ni fedha za nje kama Jedwali Na.2 linavyoonesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii, yapo majedwali ambayo yamefafanua kwa kina makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa ajili ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na taasisi

zilizo chini yake Fungu Na. 56, Tume ya Utumishi wa Walimu - Fungu Na.2 na Mafungu 26 ya Mikoa yote nchini yakijumuisha Halmashauri 184.

Mheshimiwa Spika, ninapohitimisha hotuba hii ya bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ninaomba tusimame pamoja si tu kama viongozi wa leo, bali kama warithi wa kesho tunaojenga Tanzania mpya kwa misingi ya uwajibikaji, ushirikishwaji na maendeleo yanayogusa maisha ya kila Mtanzania kuanzia mijini hadi vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii tumewasilisha si tu makadirio ya mapato na matumizi, bali tumeweka mbele yetu dira ya matumaini, ramani ya maendeleo na ahadi ya uongozi unaowajibika. Kama alivyoandika Nelson Mandela, "*Education is the most powerful weapon which you can use to change the world.*" Tumewekeza katika elimu kwa watoto wetu wote, bila ubaguzi. Pia, kama alivyosema John F. Kennedy, "*Let us not seek the Republican answer or the Democratic answer, but the right answer.*" TAMISEMI hatutafuti sifa ya kisiasa, tunatafuta suluhisho sahihi kwa maisha ya Mtanzania wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, "Maendeleo hayataletwa na mtu Mmoja, Maendeleo ni kazi ya pamoja." Hivyo, kwa kauli moja, tunatoa wito kwa mikoa, mamlaka za serikali za mitaa na wananchi wote: tushirikiane, tusonge mbele kwa mshikamano.

Mheshimiwa Spika, kwa dhamira hii na kwa imani kubwa katika maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunawasilisha bajeti hii kama zana ya kazi, dira ya matumaini na silaha ya mapinduzi ya kiutawala, kiuchumi na kijamii. Kwa hiyo, tunasema kwa ujasiri mkubwa: "TAMISEMI ndiyo Msingi wa Maendeleo Endelevu, Kila Shilingi ina Jukumu, kila Kiongozi ana Wajibu na kila Mwananchi ana Nafasi."

Mheshimiwa Spika, hotuba hii inapatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambayo ni www.tamisemi.go.tz.

16 APRILI, 2025

HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, MHESHIMIWA MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2025/26 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 Utangulizi

1. ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ninaomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Fungu Na. 56); Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 02) na mafungu 26 ya mikoa, ikijumuisha halmashauri 184 kwa mwaka 2024/25. Aidha, ninaomba Bunge lako lijadili na kuidhinisha mpango wa utekelezaji, makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa ajili ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu na mafungu 26 ya mikoa ikijumuisha halmashauri 184 kwa mwaka 2025/26.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa taarifa kuwa, hotuba hii itaonesha utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 kwa kipindi cha kuanzia Novemba, 2020 hadi Machi, 2025. Aidha, hotuba hii ni ya mwisho katika utekelezaji wa: Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 pamoja na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26; na Kipindi cha Kwanza cha Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

1.1 Shukrani na Pongezi

3. ***Mheshimiwa Spika,*** ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kunijalia kusimama mbele ya Bunge hili. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake wenye dira, maono na dhamira ya kuwaletea wananchi maendeleo kwa vitendo. Miongozo, maelekezo na usimamizi wake umeendelea kututia moyo sisi wasaidizi wake na tunamuahidi kufanya kazi bila kuchoka ili kuboresha maisha ya watanzania. Imekuwa heshima kwangu kuhudumu chini ya uongozi wake mahiri, na hakika amethibitisha kuwa, uongozi si nafasi bali ni jukumu la kusukuma mbele gurudumu la maendeleo.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuteuliwa kuwa mgombea wa nafasi ya urais kwa kipindi cha pili Awamu ya Sita kupitia Chama cha Mapinduzi katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba, 2025, tunamuamini na tunaendelea kuamini ataendelea kuleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi na kijamii katika nchi yetu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa mgombea mwenza. Mwenyezi Mungu awape afya njema, hekima na maarifa katika kutekeleza majukumu yao.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kuwashukuru waheshimiwa: Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati kwa uongozi wao thabiti na kujitolea kwa dhati katika kutimiza majukumu yao, pamoja na miongozo na maelekezo yao ya mara kwa mara yenye hekima na busara ambayo yemenisaidia sana katika majukumu yangu ya usimamizi wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali kwa ufanisi mkubwa.

6. ***Mheshiwiwa Spika,*** kipekee ninaomba nikushukuru wewe binafsi, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani, kwa kuliongoza Bunge kwa weledi na umahiri wa hali ya juu. Umeonesha uongozi bora kwa kuhakikisha majadiliano yenye tija yanakuwa msingi kwenye Bunge letu. Pia, ninampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, kwa kukusaidia kuendesha shughuli za Bunge. Vilevile, ninawapongeza Wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb.), Jimbo la Madaba, Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika (Mb.), Jimbo la Njombe Mjini na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.), wa Viti Maalum kwa umakini wao wa kuliongoza Bunge lako.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** Ninamshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Jimbo la Kilolo; Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Jafari Chege Wambura, Mbunge wa Jimbo la Rorya; Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge za: Hesabu za Serikali za Mitaa; Sheria Ndogo; Hesabu za Serikali; Uwekezaji Mitaji ya Serikali; Bajeti; na Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge. Ninawiwa kusema kazi zenu ni za thamani na zina mchango mkubwa katika maendeleo ya taifa na ustawi wa wananchi.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru waheshimiwa mawaziri, naibu mawaziri, makatibu wakuu, naibu makatibu wakuu na watendaji wote wa wizara mbalimbali ambao wameendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kufanya kazi kwa pamoja ya kuwaletea maendeleo watanzania. Ninathamini sana mchango wao, kwa pamoja tutaendelea kujenga taifa lenye nguvu na ustawi zaidi.

9. ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba kuwashukuru viongozi wenzangu na wataalamu wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Ninatambua mchango wao katika kuhakikisha wananchi wanahudumiwa katika nyanja zote. Kipekee ninawashukuru: Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange, Naibu Waziri anayeshughulikia afya na Mbunge wa Jimbo la Wanging'ombe, Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba, Naibu Waziri anayeshughulikia elimu na Mbunge wa Viti Maalum, Ndg. Adolf Ndunguru, Katibu Mkuu; Naibu Makatibu Wakuu: Ndg. Sospeter Mtwale (TAMISEMI), Mhandisi Rogatus Mativila (Miundombinu) na Ndg. Atupele Mwambene (Elimu); Mwl. Paulina Nkwama Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu; watendaji wakuu wa taasisi,

wakuu wa mikoa, makatibu tawala wa mikoa, wakuu wa wilaya, makatibu tawala wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri na watumishi wote.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee kabisa ninaendelea kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Rufiji kwa imani yao kwangu. Ninaendelea kuwaahidi kuwa nitafanya kazi bila kuchoka ili kutimiza ahadi ambazo tumeziweka kwa pamoja. Nitumie nafasi hii kuwaambia kuwa, mara zote ninapoiwaza Rufiji napata matumaini, imani, nguvu na ari ya kujitoa zaidi kwa mustakabali bora wa jimbo letu. Niwahakikishie, sichukulii dhamana waliyonipa kwa urahisi hata kidogo. Imani yao ni deni kwangu; sauti zao daima zitaongoza matendo yangu. Nitaendelea kuwahudumia kwa uadilifu, uwazi na uwajibikaji. Nawashukuru sana. Wahenga walisema, "***Asiyekumbuka kwao ni mtumwa".***

11. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki cha utumishi wangu kwa wananchi wa Rufiji na Taifa kwa ujumla, nimepata faraja na msukumo mkubwa kutoka kwenye kumbukumbu ya baba yangu mpendwa, ambaye alifariki dunia akiwa kwenye ibada tukufu huko Makka. Hii ni bajeti yangu ya kwanza kuiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu tangu kumpoteza baba yangu. Ni tukio lenye uzito wa kipekee katika maisha yangu ya uongozi, kwani kila hatua ya safari yangu katika utumishi wa umma imekuwa ikiambatana na maombi, ushauri, na baraka zake. Ingawa ni huzuni kubwa kumpoteza, maisha yake yamebaki kuwa dira yenye nguvu kwangu na kwa wengi waliomfahamu. Baba yangu alikuwa mtu wa maono, msimamo, heshima na hekima. Alinilea katika misingi ya maadili, kujituma, na kuheshimu kila mwanadamu – misingi ambayo imekuwa msingi wa uongozi wangu leo. Alinihimiza kuwa kiongozi mwenye kusikiliza, mwenye kujifunza kila siku, na mwenye kumtanguliza Mungu katika kila hatua ya maisha. Maisha yake yalijaa ibada, kujitoa kwa jamii, na kusimamia haki hata katika mambo madogo. Haya yote yamekuwa nguzo imara ya mtazamo wangu wa kulihudumia Taifa kwa moyo wote.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na huzuni ya kumpoteza, moyo wangu unafarijika na kujazwa nguvu kila ninapoyaona matunda

ya kazi inayofanywa na ofisi ninayoiongoza chini ya mwongozo wa Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mambo makubwa na ya kihistoria yanaendelea kufanyika – kutoka kwenye maboresho ya miundombinu, utoaji wa huduma kwa jamii, hadi mageuzi ya kimfumo yanayolenga kuleta maendeleo kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, japo Kifo chake kimeniacha na pengo kubwa moyoni, pia kimeniacha na kumbukumbu hai ya kiongozi wa kweli niliyemjua tangu utoto. Ni kumbukumbu inayonipa msukumo wa kuendelea kufanya kazi kwa bidii, kwa kujitoa, kwa uadilifu na kwa upendo kwa watu wangu – kwa sababu najua, kule aliko, angependa kuona mwanaye akiendeleza dhamira yake ya kuwatumikia watu kwa moyo mmoja.

1.2 Salamu za Pole

13. ***Mheshimiwa Spika,*** natoa pole kwa Bunge lako kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, Mkoani Dar es Salaam na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika. Mwenyezi Mungu ampe pumziko la milele.

1.3 Majukumu ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI

14. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI ina jukumu la kuratibu na kusimamia mafungu 28 yanayojumuisha: Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Fungu Na. 56) pamoja na Taasisi zilizo chini yake ambazo ni Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini, Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka, Chuo cha Serikali za Mitaa, Shirika la Elimu Kibaha, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa na Shirika la Masoko ya Kariakoo; Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 02) na Mafungu 26 ya mikoa ikijumuisha halmashauri 184.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** maelekezo ya mgawanyo wa majukumu yaliyotolewa na Hati Idhini ya Rais *(Presidential Instrument)* ya tarehe 30 Agosti, 2023 yanaainisha majukumu ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI kama ifuatavyo: -

(i) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Ugatuaji wa Madaraka (D by D), tawala za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa, maendeleo vijijini na mijini;

(ii) Kuziwezesha tawala za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kutekeleza majukumu yake ya kisheria;

(iii) Kuratibu shughuli za utoaji wa huduma mijini kama vile usafiri, usafirishaji na usafi wa mazingira;

(iv) Kusimamia shughuli za Tume ya Utumishi wa Walimu;

(v) Kusimamia shughuli za elimumsingi na sekondari;

(vi) Kusimamia na kuratibu shughuli za utoaji wa huduma za afya ya msingi, ustawi wa jamii na lishe;

(vii) Kuratibu na kusimamia mifumo na miundombinu ya TEHAMA katika ofisi za wakuu wa mikoa, mamlaka za serikali za mitaa na taasisi;

(viii) Kuwatambua na kuwaendeleza wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo;

(ix) Kutambua vipaji na kuviendeleza;

(x) Kujenga uwezo wa watumishi wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, ofisi za wakuu wa mikoa na mamlaka za serikali za mitaa; na

(xi) Kusimamia utendaji wa mashirika, taasisi, programu na miradi iliyo chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

SEHEMU YA PILI

2.0 Utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 kuanzia Novemba, 2020 hadi Machi, 2025

16. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka mitano (5) bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI pamoja na mafungu yake imekuwa ikiongezeka kutoka shilingi trilioni 7.01 Mwaka 2020/21 hadi shilingi trilioni 10.53 Mwaka 2024/25 sawa na ongezeko la asilimia 50.21. Ofisi ya Rais - TAMISEMI inamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona umuhimu wa Serikali za Mitaa na kuziongezea bajeti. Hii inaonesha namna anavyowajali wananchi kwa kupeleka maendeleo kwa vitendo katika maeneo yao.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** ongezeko hili si tu la fedha; ni ushahidi wa mabadiliko. Ni matumaini mapya kwa mwananchi wa taifa hili kupata huduma bora. Ni daraja jipya linalounganisha maendeleo na maisha ya kila siku. Ni shule mpya, zahanati, barabara, maji safi – na juu ya yote, ni heshima kwa utu wa mtanzania wa kawaida. Leo hii, tunapopitia mafanikio haya, tunasema kwa sauti kubwa: Serikali ya Awamu ya Sita inatekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa vitendo. Na sisi sote, kama wawakilishi wa wananchi, tunayo dhamana ya kuendeleza kasi hii – kwa mshikamano, uadilifu na moyo wa kizalendo. Tanzania mpya inawezekana – na inaendelea kujengwa mbele ya macho yetu!

18. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imetekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 katika maeneo yafuatayo;

2.1 Usimamizi na Uendeshaji wa Elimumsingi na Sekondari

19. ***Mheshimiwa Spika,*** ibara ya 80 (a - j) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 inaelekeza: Kujenga na kukarabati miundombinu ya elimu pamoja na kuhifadhi na kuendeleza mazingira ya shule hizo; Kuendeleza Mpango wa Kutoa Elimu bila Ada kwa Shule za Msingi

na Sekondari ili kuwawezesha vijana wenye sifa kuanza na kuendelea na masomo bila kikwazo; Kuhakikisha kuwa kila shule ya msingi inatoa elimu ya awali kwa ufanisi katika mazingira na miundombinu iliyoboreshwa; Kuimarisha utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum; Kuimarisha ufundishaji wa Masomo ya Sayansi ya Hisabati, Fizikia, Kemia na Baiolojia na kuongeza upatikanaji wa walimu wa kufundisha masomo hayo; Kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji wa masomo ya stadi za kazi na lugha ikiwemo lugha za alama katika elimu ya msingi; na Kuimarisha shule zote za michepuo ikijumuisha Elimu ya Ufundi, Kilimo na Biashara kwa kuzipatia vifaa vya kisasa.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** elimu ni urithi wa kizazi – urithi usioharibika, usioibwa, na usiozeeka. Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano, aliweka msingi imara aliposema, ***"Ni jukumu letu kuimarisha elimu ya ufundi na mafunzo ili vijana wetu wawe na ujuzi wa kukabiliana na ajira"***.

Kauli hii si tu kauli ya kisera, bali ni mwamko wa kiroho na kijamii – mwamko wa taifa linalojua kuwa maendeleo ya kweli hayaanzi na barabara wala majengo, bali na maarifa yaliyowekezwa kwa watu wake.

Mheshimiwa Spika, leo ninapowasilisha mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Ofisi ya Rais – TAMISEMI katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa upande wa Elimumsingi na Sekondari, ninatoa ushahidi wa mabadiliko ya kweli – mabadiliko ya shule zilizofufuliwa, walimu walioajiriwa, watoto waliowezeshwa, na matumaini mapya yaliyochipuka kila pembe ya nchi yetu. Kwa sababu katika taifa lenye maono, kila darasa linalojengwa si tu ukuta – bali ni mlango wa maisha mapya kwa mtoto wa kitanzania.

21. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kutekeleza jukumu hilo, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetekeleza ilani katika huduma ya elimu kama ifuatavyo:

(i) Kujenga na kukarabati miundombinu ya elimu, ambapo kumekuwa na ongezeko la vyumba vya madarasa kutoka

191,708 hadi 254,393, sawa na asilimia 32.69; shule za msingi kutoka shule 16,406 hadi 17,986 sawa na ongezeko la asilimia 9.63; shule za sekondari kutoka shule 3,863 hadi 4,894 sawa na asilimia 26.68; ongezeko la matundu ya vyoo kutoka 206,670 hadi 278,911 (shule za msingi) sawa na asilimia 34.95; na kutoka matundu 92,724 hadi 120,970 (shule za sekondari) sawa na asilimia 30.43. Aidha, nyumba za walimu zimeongezeka kutoka 58,637 hadi 60,429 sawa na ongezeko la asilimia 3.05; maktaba kutoka 1,537 hadi 2,665 sawa na ongezeko la asilimia 73.38; maabara kutoka 8,072 hadi 8,710 sawa na asilimia 7.90; mabweni kutoka 2,245 hadi 3,245 sawa na asilimia 44.54; na mabwalo kutoka 871 hadi 1,004 sawa na asilimia 15.26. Vilevile, shule 868 zimekarabatiwa zikiwemo za msingi 794 na za sekondari 74;

(ii) Kuendeleza Mpango wa Kutoa Elimu bila Ada kwa shule za msingi na sekondari ili kuwawezesha vijana wenye sifa kuanza na kuendelea na masomo bila kikwazo, ruzuku ya Elimu Bila Ada imeongezeka kutoka shilingi bilioni 249.66 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 484.27 mwaka 2024/25 kwa mwaka sawa na asilimia 93.97;

(iii) Kutoa elimu ya awali katika shule za msingi kwa ufanisi katika mazingira na miundombinu iliyoboreshwa, idadi ya wanafunzi katika shule za awali imeongezeka kutoka 1,278,886 (wavulana 647,609 na wasichana 631,277) hadi 1,558,549 (wavulana 791,520 na wasichana 767,029) sawa na asilimia 21.87, na shule zenye madarasa ya awali zimeongezeka kutoka 16,355 hadi 18,011 sawa na asilimia 10.12;

(iv) Kutoa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ambapo uandikishaji umeongezeka kutoka 28,482 hadi 78,429 sawa na asilimia 175. Aidha, madarasa 44, matundu ya vyoo 132 na mabweni 172 yamejengwa kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu;

(v) Kufundisha Masomo ya Sayansi ya Fizikia, Kemia, Baiolojia na Hisabati na kuongeza upatikanaji wa walimu wa kufundisha masomo hayo. Idadi ya Wanafunzi wanaosoma Masomo ya Sayansi na Hisabati katika shule za sekondari kuanzia

kidato cha tatu imeongezeka kutoka 2,497,450 hadi 2,792,584 sawa na ongezeko la wanafunzi 295,134;

(vi) Ujifunzaji na ufundishaji wa masomo ya stadi za kazi na lugha ikiwemo lugha za alama katika elimu ya msingi ambapo walimu 127 wa lugha za alama wameajiriwa na kusambazwa katika shule 127;

(vii) Imeboresha shule 28 za mchepuo wa elimu ya ufundi/amali kwa kuzikarabati na kutoa vifaa vya kisasa. Aidha, shule 274 za michepuo ya kilimo na 28 za michepuo ya biashara zimeboreshwa ***(Kiambatisho Na.1)***;

(viii) Kuajiri walimu 45,804 wakiwemo walimu 447 wa elimu maalumu;

(ix) Kutoa mafunzo kazini kwa walimu 106,806 ikiwa ni pamoja na walimu 29,399 wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Teknolojia kwa lengo la kuimarisha ufundishaji wa masomo hayo;

(x) Kununua na kusambaza vitabu vya kiada na ziada 66,553,455 kwa shule za msingi na sekondari;

(xi) Kuandikisha wanafunzi wa Darasa la Kwanza ambapo uandikishaji umeongezeka kwa asilimia 14.87 kutoka wanafunzi 1,621,724 (wavulana 811,401 na wasichana 810,323) hadi 1,862,539 (wavulana 937,260 na wasichana 925,279), idadi ya wanafunzi katika shule za msingi za umma imeongezeka kutoka 10,460,785 hadi 10,739,975 sawa na asilimia 2.69 na elimu ya sekondari kutoka 2,172,257 hadi 2,999,530 sawa na asilimia 38.01; na

(xii) Kuimarika kwa matokeo ya mitihani ya kitaifa ambapo Darasa la Saba ufaulu umefikia asilimia 80.87, Kidato cha Nne asilimia 92.37 kutoka 85.8 na Kidato cha sita ufaulu umefikia asilimia 99.99 kutoka 99.90.

22. ***Mheshimiwa Spika***, matokeo haya si tu mafanikio ya kiutawala ni ushindi wa kitaifa. Kuongeza miundombinu ya elimu;

kuwekeza karibu shilingi bilioni 500 katika Elimu Bila Ada; na kuongeza idadi ya wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa asilimia 175 haya ni matendo yanayosema kwa sauti kubwa kuliko maneno: kwamba serikali hii haikuja kuahidi tu, bali kutekeleza.

23. ***Mheshimiwa Spika***, wapo waliokuwa na mashaka, wapo waliokuwa wamesahau matumaini lakini leo, tuna ushahidi kuwa pale ambapo kuna nia njema, kuna njia na katika kila kona ya Tanzania, kuna darasa, mwalimu na mwanafunzi anayesimama kama ushahidi wa mabadiliko haya. Hivyo, ninaomba nitamke kauli ambayo itakumbukwa kwa miaka mingi ijayo: **Mtoto wa Kitanzania, popote alipo hawezi tena kuzuiwa na umbali na hawezi tena kusahaulika kwa sababu ya ulemavu;** elimu sasa ni haki ya kila mmoja na Tanzania mpya inaanzia darasani. ***Na kwa misingi hiyo, tunaamini kabisa: Elimu Yetu, Uhai wa Taifa Letu.***

2.2 Uratibu na Usimamizi wa Huduma za Afya ya Msingi

24. ***Mheshimiwa Spika,*** ibara ya 83 (d, f, l, q, u na z) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 imeelekeza kutekeleza mambo yafuatayo: Kujenga na kuimarisha vituo vya kutolea huduma za afya ili viweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi. Hadi kufikia 2025 Serikali itaongeza vituo vya kutolea huduma za afya kwa asilimia 20 ya vituo 8,446 vilivyopo sasa; vipaumbele vitawekwa katika ujenzi wa vituo vya afya na ukamilishaji wa maboma kwa kuzingatia uwiano wa kijografia, idadi ya watu na wingi wa magonjwa; Kuanza awamu ya pili ya ujenzi wa hospitali 98 za halmashauri; Kuajiri wataalamu wa kutosha wenye ujuzi na kuboresha mazingira ya kazi; Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za afya ikiwemo tiba mtandao, mafunzo, utawala, usimamizi wa fedha, dawa na bidhaa zote za dawa pamoja na uboreshaji wa ukusanyaji na matumizi ya takwimu za afya katika hospitali za halmashauri, hospitali ngazi ya wilaya, vituo vya afya na zahanati; Kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya na kuzifanya rafiki kwa wanawake, wanaume na vijana ikiwemo kutoa huduma ya msingi ya dharura ya afya ya uzazi na mtoto, huduma tembezi na mkoba; Kuimarisha mfumo wa upelekaji wa fedha moja kwa moja

kwenye akaunti za vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya msingi kwa kushirikisha wadau wote wanaotekeleza afua za afya.

25. ***Mheshimiwa Spika, Hayati Mheshimiwa Benjamin Wiliam Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu alisema: "Tusiposhughulikia masuala ya afya ya msingi, hatutaweza kupiga hatua kubwa katika maendeleo."*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetekeleza ilani katika huduma za afya ya msingi kama ifuatavyo:

(i) Kujenga na kuimarisha vituo vya kutolea huduma za afya ili viweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi ambapo Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeongeza vituo vya kutolea huduma ya afya ya msingi kutoka 6,081 hadi 7,713 sawa na ongezeko la vituo 1,632 au asilimia 26.80. Kati ya vituo hivyo, zahanati ni 1,158, vituo vya afya 345 na hospitali za halmashauri 129;

(ii) Ujenzi wa hospitali mpya za halmashauri 129 ikiwa ni ongezeko la asilimia 31.63 ya lengo la kujenga hospitali 98. Kati ya hospitali hizo, 67 zimejengwa majengo 14 ambayo ni; jengo la utawala, jengo la huduma kwa wagonjwa wa nje, jengo la maabara, jengo la mionzi, wodi ya wazazi, jengo la kutunzia dawa, jengo la kufulia, wodi ya magonjwa mchanganyiko (*medical ward*) wanawake na wanaume, wodi ya watoto, jengo la upasuaji, wodi ya upasuaji wanaume na wanawake na jengo la kuhifadhia maiti; hospitali 86 kati ya hizo zimejengwa majengo ya kuhudumia wagonjwa wa dharura *(Emergence Medical Department- EMD)* na hospitali 30 zimejengwa majengo ya kuhudumia wagonjwa mahututi *(Intensive Care Unit - ICU)* na kufanya idadi ya majengo yaliyokwisha jengwa kwa baadhi ya hospitali kufikia kati ya 14 hadi 16; na hospitali 62 zinaendelea na ujenzi wa majengo hayo katika hatua mbalimbali. Aidha, hospitali 128 kati ya 129 zimesajiliwa na tayari zinatoa huduma muhimu za awali, ikiwemo huduma kwa wagonjwa wa nje na huduma za uzazi;

(iii) Wataalamu wa afya 34,720 wameajiriwa ambapo madaktari ni 1,851, matabibu 6,546, wauguzi 10,213,

watekinolijia mionzi, macho, maabara, meno na dawa 1,488, wafamasia 993, maafisa lishe 328, maafisa ustawi 224, fundi sanifu vifaa tiba 239 na kada nyingine watumishi 12,838, wameajiriwa na kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya ya msingi. Aidha, watumishi 700 wameajiriwa kwa mkataba wa miaka mitatu (3) na watumishi 150 wa mkataba wa UVIKO;

(iv) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA kwa kuboresha mfumo wa uendeshaji na usimamizi wa utoaji wa huduma za afya (GoTHOMIS) katika vituo vya kutolea huduma za afya ambapo vituo 4,915 au asilimia 67.88 ya vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya msingi vinatumia mfumo. Kati ya vituo hivyo, hospitali za halmashauri ni 186, vituo vya afya 848, zahanati 3,860, kliniki 3 na hospitali teule za wilaya 7 na vituo vingine 11 vinavyomilikiwa na taasisi za umma;

(v) Kusimamia na kuratibu Mfumo wa Huduma ya Usafiri wa Dharura kwa akina Mama Wajawazito na Watoto Wachanga (M-MAMA) ambapo wateja 135,526 wamehudumiwa katika mfumo huo (kinamama wajawazito 110,722; watoto wachanga 24,537 na mama na mtoto 267). Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya na kuzifanya rafiki kwa wanawake, wanaume na vijana ikiwemo kutoa huduma ya msingi ya dharura ya afya ya uzazi na mtoto, huduma tembezi na mkoba ambapo yafuatayo yamefanyika:

(a) Uimarishaji wa huduma za afya na utoaji wa huduma za mkoba zimeongeza idadi ya kinamama kuhudhuria kliniki. Aidha, akina mama wajawazito wanaohudhuria kliniki mahudhurio manne wameongezeka kutoka 2,374,666 mwaka 2020 kufikia 3,143,332 mwaka 2024, pia idadi ya wajawazito waliohudhuria hudhurio la kwanza kliniki kabla ya wiki 12 imeongezeka kutoka 848,149 mwaka 2020 hadi 1,186,812 mwaka 2024;

(b) Uimarishaji wa huduma za akinamama katika vituo vya kutolea huduma na kuzifanya kuwa rafiki umechangia ongezeko la akina mama wanaojifungua katika vituo vya kutolea huduma za afya. Katika mwaka 2020 akina mama 52,585 walijifungua katika vituo vya kutolea huduma za afya msingi hadi kufikia akina mama 141,386 mwaka 2024;

(c) Kuimarisha huduma za wajawazito ambapo uimarishaji wa huduma kwa mama wajawazito kumesaidia kuongeza idadi ya watoto wachanga waliozaliwa hai ambapo imeongezeka kutoka 1,392,634 mwaka 2020 hadi 1,828,285 mwaka 2024. Pia, Serikali imejenga vyumba maalumu 114 kwa ajili kutoa huduma za dharura kwa watoto wachanga (*Neonatal Care Unit - NCU* na Kangaroo Mother Care - KMC);

(d) Utoaji wa huduma kwa vijana unaendelea kufanyika na halmashauri 22 kati ya 184 zimeshaanzisha vituo maalumu kwa ajili ya huduma rafiki kwa vijana; tumeyaishi kwa vitendo maneno ya ***Hayati Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi Rais wa Awamu ya Pili aliyosema, "Tuwekeze katika afya ya mama na mtoto kwa kuwa wao ni msingi wa kizazi kijacho chenye nguvu";*** na

(vi) Kuratibu upelekaji wa fedha moja kwa moja katika vituo vya kutolea huduma za afya ambapo vituo vinavyopokea fedha moja kwa moja vimeongezeka kutoka vituo 5,913 hadi 7,295. Aidha utaratibu huu umeboresha upatikanaji wa fedha katika ngazi ya vituo vya kutolea huduma za afya ya msingi hivyo kuboresha huduma zinazotolewa.

2.3 Huduma za lishe

26. ***Mheshimiwa Spika,*** ibara ya 86 (a, b, c na d) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka

2020 inaelekeza: Kutekeleza mikakati ya kupunguza idadi ya watoto chini ya miaka mitano wenye udumavu na ukondefu kwa kasi kubwa zaidi; Kupunguza idadi ya watoto wanaozaliwa na uzito pungufu yaani chini ya uzito wa kilogramu 2.5 ili iwe chini ya asilimia 50; na kupunguza kwa asilimia 50 viwango vya upungufu wa damu kwa wanawake walio katika umri wa kuzaa yaani miaka 15 – 49.

Mheshimiwa Spika, Hayati Ali Hassan Mwinyi Rais wa Awamu ya Pili aliwahi kusema, "Lishe bora na usafi wa mazingira ni silaha madhubuti za kupambana na magonjwa yanayozuilika."

27. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetekeleza ilani katika huduma za lishe kama ifuatavyo:

(i) Kusimamia utoaji wa huduma mbalimbali za lishe zinazolenga kupunguza udumavu, uzito pungufu wa kuzaliwa na uzito uliozidi kwa watoto. Miongoni mwa huduma zilizotolewa ni kutathimini hali ya lishe ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Takribani watoto 7,454,996 walipimwa hali ya lishe kwenye vijiji na mitaa nchini. Upimaji huo uliwezesha kuwabaini na kuwapa matibabu ya utapiamlo mkali watoto 149,308 kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya msingi. Huduma nyingine zilizotolewa ili kudhibiti udumavu ni pamoja na ukaguzi wa ubora na usalama wa vyakula na utoaji wa elimu ya lishe kwa jamii. Wazazi na walezi 11,449,738 walipatiwa elimu na unasihi wa lishe na kuhimizwa kuboresha taratibu za ulishaji wa watoto ili kupunguza udumavu;

(ii) Kutoa vidonge vya madini chuma na vitamini ya foliki kwa wanawake wajawazito ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa damu unaochangia vifo vya wanawake vitokanavyo na uzazi. Wajawazito 7,440,632 walipatiwa vidonge vya kuongeza wingi wa damu katika vituo vya kutolea huduma ya afya ngazi ya msingi. Aidha, vidonge vya Vitamini A ya nyongeza vimetolewa kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano (5) ili kuimarisha kinga

ya mwili na kupunguza kasi ya maambukizo ya magonjwa yanayochangia tatizo la udumavu. Watoto 8,944,200 wenye umri chini ya miaka mitano walipatiwa nyongeza ya matone ya Vitamini A kupitia kampeni za kitaifa zinazofanyika mara mbili kila mwaka; na

(iii) Kutenga shilingi 1,000 au zaidi kwa kila mtoto chini ya umri wa miaka mitano (5) kutoka mapato ya ndani ya halmashauri ambapo shilingi bilioni 48.56 zilitolewa na kutumika kutoa huduma katika afua za lishe. Aidha kiwango cha utoaji wa shilingi 1,000 au zaidi kwa kila mtoto mwenye umri chini ya miaka mitano katika mikoa na halmashauri nchini kimefikia wastani wa kitaifa wa shilingi 1,546.

2.4 Huduma za Ustawi wa Jamii

28. ***Mheshimiwa Spika,*** ibara za 91(a, e na f), 93(b, c, f, i na l) na 95(i na h) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 zinaelekeza: Kuimarisha huduma za matibabu bila malipo kwa wazee; Kutoa huduma za matunzo na kisaikolojia kwa wazee na watu wenye ulemavu; Kuimarisha mabaraza ya wazee maeneo yote nchini; Kuunda kamati za ulinzi wa wanawake na watoto na kuzijengea uwezo ili kuhakikisha kuwa zinatekeleza afua za ulinzi na usalama wa wanawake na watoto na kulinda maadili chanya ya taifa; Kusimamia, kufuatilia na kuimarisha uanzishaji na uendelezaji wa vituo vya kulelea watoto wadogo na vituo vya maendeleo ya awali ya mtoto katika ngazi ya jamii ili kuboresha malezi na makuzi ya kila mtoto; Kuimarisha huduma kwa watoto walio katika mkinzano na sheria kwa kuboresha mahabusu za watoto; Kuimarisha huduma za usuluhisho wa migogoro ya ndoa na matunzo kwa watoto; Kuboresha rejista ya watu wenye ulemavu itakayotoa taarifa sahihi za watu wenye ulemavu ili kuimarisha utoaji wa huduma na misaada; pamoja na kuboresha na kusimamia utoaji wa msaada wa kisaikolojia kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, "Maendeleo ya kweli hayawezi kupatikana kama hatuwekezi katika afya, elimu, na ustawi wa

jamii. Taifa imara linajengwa kwa kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma bora na fursa sawa za maendeleo." - Hayati Benjamini William Mkapa Rais wa Awamu ya Tatu

29. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetekeleza ilani katika huduma za ustawi wa jamii kama ifuatavyo:

(i) Kutambua wazee 4,975,473 (wanawake 2,682,210 na wanaume 2,293,263) na kutoa huduma za matibabu bila malipo. Kati ya wazee waliotambuliwa wazee 2,199,588 (wanawake 1,189,512 na wanaume 1,010,076) wamepatiwa vitambulisho/bima ya afya kwa ajili ya msamaha wa matibabu. Aidha, vituo 7,300 vya kutolea huduma ya afya, vimeanzisha madirisha 4,574 ya kutolea huduma za afya kwa wazee. Vilevile, kutokana na uhaba wa vyumba maalumu kwa huduma za wazee vituo 2,726 vinazingatia ujumbe wa "Mpishe mzee kwanza" ili apatiwe huduma katika vituo vilivyopo kwenye halmashauri zote 184;

(ii) Kuunda na kuimarisha mabaraza 20,768 ya ushauri ya wazee katika ngazi za mikoa 26, halmashauri 184, kata 3,956, vijiji 12,333 na mitaa 4,269. Aidha, kamati za watu wenye ulemavu 2,449 ziliundwa. Kupitia kamati hizo, wazee na watu wenye ulemavu wanapatiwa huduma za matunzo na kisaikolojia;

(iii) Kuunda kamati 20,768 za ulinzi na usalama wa mwanamke na mtoto, uanzishwaji wa vituo vya huduma kwa pamoja *(one stop centre)* katika vituo vya kutolea huduma za afya ambapo vituo vya huduma kwa pamoja vimeongezeka kutoka 21 hadi 25. Aidha, vituo vya kulelea watoto wadogo mchana vimeongezeka kutoka 2,378 hadi 3,362;

(iv) Kuanzisha vituo 206 vya kulelea watoto wadogo vinavyotoa huduma kwa watoto 11,675 (wanaume 4,833 na wanawake 6,842). Aidha, vituo binafsi vilivyosajiliwa ni

3,862 vinavyohudumia watoto 397,935 (wanaume 175,517 na wanawake 222,418);

(v) Kushughulikia ukatili wa kijinsia ambapo mashauri 517,286 ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto yameshughulikiwa. Kati ya mashauri hayo, ya ngono na ulawiti yalikuwa 53,925, ya kupigwa au kuumizwa 180,047, ya kuumizwa kihisia 272,571 na kutelekezwa 10,743. Aidha, migogoro ya ndoa na familia 97,234 imeshughulikiwa na kati ya migogoro hiyo, migogoro 15,414 ilipelekwa mahakamani kwa usuluhishi zaidi;

(vi) Watu wenye Ulemavu 821,763 (wanaume 411,321 na wanawake 410,442) walipatiwa huduma za msaada wa kisaikolojia. Kati ya hao, watu wenye Ualbino 67,502 walipatiwa msaada wa kisaikolojia wakati wa uendeshaji wa kliniki za uchunguzi wa saratani ya ngozi katika mikoa 24 na halmashauri 172; na

(vii) Watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi 2,592,963 (wanaume 1,142,014 na wanawake 1,450,949) walitambuliwa na kupatiwa huduma mbalimbali zikiwemo mafunzo ya ufundi stadi, kadi za bima ya afya ya Jamii na vifaa vya shule. Kati ya watoto hao, waliotambuliwa wanaoishi na kufanya kazi mitaani ni 18,291 (wanaume 9,448 na wanawake 8,843), ambapo watoto 21 waliweza kuunganishwa na vyuo vya ufundi na wengine 18,270 waliunganishwa na familia zao. Aidha, jumla ya watoto 4,207,796 walio na umri chini ya miaka mitano (5) wamesajiliwa na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa sawa na asilimia 45.7 ya jumla ya watoto wa kundi hilo.

2.5 Ujenzi, Ukarabati na Matengenezo ya Barabara

30. ***Mheshimiwa Spika,*** Ibara 57 (c-d) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 inaelekeza kuongeza kiwango cha barabara za changarawe kutoka kilomita 24,493 hadi kilomita 35,000; kuongeza urefu wa barabara za vijijini na mijini zilizojengwa kwa kiwango cha lami kutoka kilomita 2,025

hadi kilomita 3,100; na kuongeza mtandao wa barabara toka kilomita 108,946.19, mwaka, 2020 hadi kufikia kilomita 143,881 mwaka 2025.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetekeleza ilani katika ujenzi, ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya barabara kupitia TARURA kama ifuatavyo:

(i) Ujenzi wa barabara za changarawe ambao umeongezeka kutoka kilomita 24,493 hadi kilomita 44,372.21 sawa na ongezeko la asilimia 81.16. Urefu wa barabara za vijijini na mijini zilizojengwa kwa kiwango cha lami umeongezeka kutoka kilomita 2,025 hadi kilomita 3,467.30 sawa na ongezeko la asilimia 71.22. Aidha, kuongeza mtandao wa barabara kutoka kilomita 108,946.19 hadi kilomita 144,429.77, sawa na ongezeko la asilimia 32.57;

(ii) Kufanya tafiti kwa kutekeleza kazi za ujenzi wa miundombinu ya barabara kwa kutumia teknolojia mbadala *(ecoroads, ecozyme na polymer)* ambapo barabara zenye urefu wa kilomita 61.7 zinaendelea kufanyiwa tafiti ili kupunguza gharama za ujenzi, matengenezo na ukarabati. Teknolojia hiyo huimarisha tabaka la chini la barabara na hivyo kuzifanya kuwa stahimilivu dhidi ya uharibifu wa mapema unaotokana na maji na uzito. Aidha, kwa kutumia malighafi zinazopatikana mahali pa kazi ujenzi wa miundombinu ya barabara kilomita 28.92 na madaraja 395 kwa kutumia mawe katika barabara za wilaya umekamilika; na

(iii) Tulipotoka kulikuwa na vumbi, lakini leo tunatembea kwenye lami. Tulipotoka kulikuwa na miteremko isiyopitika, leo tuna barabara zinazounganisha ndoto na fursa. Kuongezeka kwa barabara za changarawe kwa asilimia 81.16 na lami kwa asilimia 71.22 ni ushahidi wa nchi inayojenga msingi wa maendeleo kwa kila mtanzania – kuanzia kijijini hadi mjini. Huu siyo mradi wa barabara tu, huu ni mradi wa matumaini! Kila kilomita mpya ya

barabara iliyojengwa ni daraja kati ya umaskini na maendeleo; ni njia ya mtoto kufika shuleni, mama kufika hospitali, mkulima kupeleka mazao sokoni na taifa kusonga mbele. Kuongeza mtandao wa barabara kutoka kilomita 108,946 hadi zaidi ya 144,000 si takwimu tu – ni mabadiliko ya kweli yanayoonekana, yanayogusika na yanayogusa maisha. Barabara hizi ni sauti ya serikali inayosema: **'Hatukuwaacha Nyuma**.' Hizi ni njia zinazotufikisha kwenye Tanzania ya viwanda, fursa na mshikamano wa kitaifa.

2.6 Huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka

32. ***Mheshimiwa Spika,*** ibara ya 57(e) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 inaelekeza kuimarisha utoaji wa huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka katika Jiji la Dar es Salaam.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetekeleza ilani kwa kutoa Huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka kupitia DART kama ifuatavyo:

(i) Kusambaza kadi janja 62,000 kati ya 200,000 katika awamu ya kwanza na kusimika mageti janja kwenye vituo vyote 27;

(ii) Kusimika Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji Nauli *(Automated Fare Collection System-AFCS)* ambao utafungamanishwa na mfumo wa kuongozea magari *(Intelligent Transport System - ITS)* ambao upo kwenye hatua ya ununuzi; na

(iii) Wakala imenunua watoa huduma watatu (3) wa uendeshaji kwa njia ya ubia (PPP) wa mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili na mikataba imeshasainiwa.

34. ***Mheshimiwa Spika***, kwa muda mrefu watu wa Jiji la Dar es Salaam wamekuwa wakisubiri – wengine kwa matumaini, wengine kwa mashaka lakini wote kwa kiu ya mabadiliko. Leo,

kwa mara ya kwanza tunasema: subira yao haikuwa ya bure. Kupitia ubia kati ya Serikali na sekta binafsi (PPP), tumefanikisha hatua ya kihistoria – kusaini mikataba na watoa huduma watatu (3) wa uendeshaji wa Awamu ya Pili ya Mabasi Yaendayo Haraka. Hili ni tukio la mwanzo wa zama mpya – siyo tena hadithi ya ahadi zisizotekelezwa, bali ya huduma bora zinazoonekana na kuguswa." "*Great things take time*."

35. ***Mheshimiwa Spika***, wanafalsafa wanasema, "**Mambo Makubwa Yanahitaji Muda**." Hatua hii si tu ununuzi wa huduma, bali ni ununuzi wa matumaini mapya kwa wakazi wa jiji letu. Hatutaki kurudia makosa ya jana, bali tunajenga mfumo imara, unaozingatia ubora, ufanisi na heshima kwa muda na maisha ya abiria.

> *"**Hope is being able to see that there is light despite all the darkness**." – **Desmond Tutu.***

36. ***Mheshimiwa Spika***, kwa miaka mingi wananchi wamepitia usumbufu, foleni zisizokwisha na huduma zisizoeleweka. Lakini leo, tunasema kwa sauti ya matumaini: nuru inaanza kuonekana. Mabasi haya hayatakuwa tu magari ya kusafirisha watu – yatakuwa magari ya kusukuma uchumi, kuunganisha fursa na kupunguza mzigo wa maisha ya kila siku.

> "***Progress is not in enhancing what is, but in advancing toward what will be***." – ***Khalil Gibran*.**

37. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unaonesha jinsi tunavyotoka kwenye kilichozoeleka – foleni, ajali, uchakavu na kuelekea kwenye kile kinachowezekana: usafiri wa kisasa, wa heshima, wa watu wote. Tunajenga mfumo wa usafiri wa umma ambao utaweka heshima kwa abiria, uwajibikaji kwa watoa huduma na thamani kwa kila senti inayowekezwa.

38. ***Mheshimiwa Spika***, awamu hii mpya ni jibu la kilio cha miaka mingi, ni ushahidi kuwa Serikali ya Awamu ya Sita haikosei mwelekeo – tunasonga mbele kwa busara, kwa maono, na kwa nia njema ya kuwahudumia Watanzania."

2.7 Utawala Bora, Kujenga Uwezo, Usimamizi wa Rasilimali, Ujenzi wa Majengo ya Utawala na Makazi ya Viongozi

39. ***Mheshimiwa Spika,*** ibara za 18 (b) (vii), 122 (a, e, l) na 235 (a, e) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 zimeelekeza kutekeleza mambo yafuatayo: Kuimarisha mifumo ya kitaasisi na uwezo wa viongozi na watendaji wa mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kwenda vijijini kusikiliza na kushughulikia kero na malalamiko ya wananchi kwa wakati, haki na uadilifu. Aidha, kuwapokea, kuwasikiliza na kuwahudumia wananchi wanaotembelea ofisi hizo kwa weledi, hekima na busara; Kujenga uwezo wa mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kwa kutoa mafunzo, mifumo na vitendea kazi ili kuiwezesha kutoa huduma kwa wananchi; na Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kujenga ofisi za wakuu wa mikoa, wilaya, tarafa, kata na vijiji pamoja na nyumba za watumishi kwa kuweka kipaumbele katika maeneo ambayo hayana ofisi na nyumba za viongozi na watumishi.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetekeleza ilani kwenye eneo la utawala bora kama ifuatavyo:

(i) Kero 282,124 zimepokelewa na kusikilizwa katika ngazi ya mikoa na wilaya ambapo jumla ya kero 263,893 zimetatuliwa na kero 18,231 zipo katika hatua mbalimbali za utatuzi, baadhi ya kero zilizotatuliwa ni pamoja na masuala ya ardhi, barabara, umeme na maji;

(ii) Mafunzo yanayohusu uongozi katika usimamizi wa rasilimaliwatu na fedha yalitolewa kwa wakuu wa mikoa 26, makatibu tawala wa mikoa 26, wakuu wa wilaya 139, makatibu tawala wa wilaya 139. Aidha, makatibu tawala wasaidizi wa mikoa 208 walipatiwa mafunzo kuhusu uandaaji wa mpango mkakati, uchumi mahalia, mkataba wa huduma kwa mteja, uendeshaji wa mabaraza ya biashara, ukaguzi na ufuatiliaji wa fedha, usimamizi na uendeshaji wa shughuli za elimu na afya;

(iii) Kuajiri maafisa tarafa 72, wahandisi 52, wakadiriaji majenzi 25 na wataalamu wa ununuzi 12 na kupangiwa katika ofisi za wakuu wa mikoa;

(iv) Ujenzi wa majengo 289 na ukarabati wa majengo 220, ambapo ujenzi wa ikulu ndogo 7 na ukarabati wa ikulu ndogo 16, ujenzi wa ofisi sita (6) na ukarabati wa ofisi 20 za wakuu wa mikoa, ujenzi wa ofisi 34 na ukarabati wa ofisi 51 za wakuu wa wilaya, ujenzi wa ofisi 133 na ukarabati wa ofisi nane (8) za maafisa tarafa, ujenzi wa nyumba nane (8) na ukarabati wa nyumba 13 za wakuu wa mikoa, ujenzi wa nyumba tano (5) na ukarabati wa nyumba 17 za makatibu tawala wa mikoa, ujenzi wa nyumba 31 na ukarabati wa nyumba 42 za wakuu wa wilaya, ujenzi wa nyumba 47 na ukarabati wa nyumba tisa (9) za makatibu tawala wasaidizi, ujenzi wa nyumba 18 na ukarabati wa nyumba 44 za makatibu tawala wa wilaya umefanyika; na

(v) Ununuzi wa magari 346 kati ya hayo 18 ya wakuu wa mikoa, 14 ya makatibu tawala wa mikoa, 120 ya wakuu wa wilaya na 68 ya idara katika ofisi za wakuu wa mikoa na 126 ya wakurugenzi wa halmashauri na ununuzi wa pikipiki 1,206 za watendaji wa kata.

2.8 Ulinzi wa Mazingira, uhifadhi wa Maliasili, Mabadiliko ya Tabianchi na Biashara ya Kaboni

41. ***Mheshimiwa Spika***, Ibara za 68(c) na 235(e) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 zimeelekeza kuimarisha ushiriki wa jamii katika usimamizi wa rasilimali za misitu kwa kutekeleza programu zinazolenga kuzalisha ajira na kuongeza kipato; na Kubuni na kuweka mikakati ya kupunguza matumizi ya kuni na mkaa kwa lengo la kupunguza kasi ya uharibifu wa mazingira kwa kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala ikiwemo gesi na umeme.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** shilingi bilioni 45 zimepokelewa kutoka kampuni ya Carbon Tanzania Ltd na Kaderes Peasant Development PLC kutokana na uuzaji wa kaboni. Fedha hizo

zimenufaisha wananchi wa Halmashauri 10 za Mikoa ya Katavi (Tanganyika), Manyara (Kiteto na Mbulu), Arusha (Karatu), Kagera (Kyerwa, Karagwe, Misenyi, Muleba, Ngara na Bukoba Vijijini).

43. ***Mheshimiwa Spika,*** shuguli zilizotekelezwa kutokana na fedha zilizopatikana kutokana na biashara ya kaboni ni kama ifuatavyo:

(i) Ujenzi vyumba vya madarasa 64 katika shule za msingi na sekondari;

(ii) Ujenzi wa matundu ya vyoo 160 katika zahanati na shule;

(iii) Ujenzi wa nyumba 26 za watumishi;

(iv) Ukamilishaji wa masoko 6 ya vijiji na vivuko 3;

(v) Ukamilishaji wa vituo 4 vya polisi na majosho 2 kwa ajili ya mifugo;

(vi) Ujenzi wa jiko na stoo kwa shule za msingi 6; na

(vii) Ujenzi na ukamilishaji wa mabweni 8 yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 960 katika shule za Sekondari za Mwese, Ndedo na Domaga.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza mkakati wa kupunguza matumizi ya kuni na mkaa kwa lengo la kupunguza kasi ya uharibifu wa mazingira kwa kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala ikiwemo gesi na umeme Ofisi ya Rais - TAMISEMI imehamasisha matumizi ya nishati safi ambapo taasisi 903 zikiwemo shule za msingi 83, sekondari 650 na taasisi zingine 170 zimeanza kutumia mfumo wa nishati safi.

2.9 Mamlaka za Serikali za Mitaa

45. ***Mheshimiwa Spika,*** ibara za 19(a) (ii), 32 (s) na 122 (c, d, e, h, i, j, l, m, n), ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi

Mkuu wa Mwaka 2020 zinaelekeza yafuatayo: Kuimarisha huduma za kifedha kwa wananchi kutokana na kutungwa kwa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2017 na kanuni zake za mwaka 2019 pamoja na kuboresha usimamizi wa taasisi za kifedha na maadili ya watumishi wa taasisi hizo ili kumlinda mteja; Kuhakikisha kwamba halmashauri zote nchini zinaendelea kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kwa mujibu wa sheria ili kuwezesha vijana na makundi mengine katika jamii zetu kupata mikopo isiyo na riba; Kuimarisha makusanyo ya mapato ya ndani ya halmashauri ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi; Kuimarisha serikali za mitaa ili ziendelee kuwa chombo cha kuwapa wananchi uwezo na sauti ya kuamua na kushiriki kwa karibu katika shughuli za maendeleo; Kujenga uwezo wa mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kwa kutoa mafunzo, mifumo na vitendea kazi ili kuiwezesha kutoa huduma kwa wananchi; Kubuni na kuibua miradi ya kimkakati ambayo itaboresha utoaji wa huduma katika mamlaka za serikali za mitaa na kuongeza mapato ya ndani na kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu; Kuimarisha utekelezaji wa maboresho ya serikali za mitaa kupitia sera na sheria mbalimbali ili kuendana na dhana ya kupeleka madaraka karibu na wananchi; Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kujenga ofisi za wakuu wa mikoa, wilaya, tarafa, kata na vijiji na nyumba za watumishi kwa kuweka kipaumbele katika maeneo ambayo hayana ofisi na nyumba za viongozi na watumishi; Kuboresha mazingira ya kufanyia biashara na uwekezaji katika mamlaka za serikali za mitaa kwa kutenga maeneo ya uwekezaji na kuzipatia ufumbuzi kero za wafanyabiashara ndogondogo; na kusimamia kikamilifu suala la utawala bora, uadilifu, uwajibikaji na matumizi sahihi ya rasilimali za umma pamoja na miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika mamlaka hizo ili itekelezwe kwa kiwango kinachokusudiwa na kuhakikisha kuwa ubora wa miradi unalingana na thamani ya fedha iliyotumika.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetekeleza ilani katika mamlaka za serikali za mitaa kama ifuatavyo:

(i) Kusajili vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha ambapo vikundi 57,364 vimesajiliwa katika halmashauri zote nchini;

(ii) Kutoa mikopo ya shilingi bilioni 158.50 kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambapo shilingi bilioni 63.40 ni wanawake (vikundi 8,576), shilingi bilioni 63.40 ni vijana (vikundi 4,981) na shilingi bilioni 31.70 watu wenye ulemavu (vikundi 2,319);

(iii) Bajeti ya mapato ya ndani ya halmashauri imeongezeka kutoka shilingi bilioni 814.96 hadi shilingi trilioni 1.35 sawa na asilimia 60; Aidha, fedha za mapato ya ndani zilizoidhinishwa katika miradi ya maendeleo zimeongezeka kutoka shilingi bilioni 333.09 hadi bilioni 454.41 sawa na asilimia 36.42;

(iv) Makusanyo halisi ya mapato ya ndani ya halmashauri yameongezeka kutoka shilingi bilioni 757.05 mwaka 2020/21 hadi shilingi trilioni 1.15 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 77 mwaka 2024 ***Kielelezo Na. 1.*** Aidha, fedha za mapato ya ndani zilizopelekwa katika miradi ya maendeleo zimeongezeka kutoka shilingi bilioni 276.69 hadi shilingi bilioni 313.26 sawa na asilimia 13.21.

Kielelezo Na.1: Mwenendo wa Bajeti na Makusanyo Halisi ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri Mwaka 2020/21 – Machi, 2024/25



(v) Miradi 30,928 imeibuliwa na wananchi ambapo sekta za elimu 16,080, afya 7,472, barabara 1,232, maji 608 na utawala 5,536 kupitia Mfumo wa Fursa na Vikwazo vya

Maendeleo Ulioboreshwa *(Improved Oportunities and Obstacles to Develepment - O&OD);*

(vi) Mafunzo elekezi kuhusu Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo Ulioboreshwa (*improved O&OD*) yalitolewa kwa wakurugenzi 184, vikosi kazi vya halmashauri zote 184 vyenye maafisa 1,288 na maafisa TEHAMA 184. Aidha, mafunzo hayo yametolewa kwa wawezeshaji kata 207 kutoka halmashauri 20 na kwa maafisa ugani 249 wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma (123), Manispaa ya Morogoro (6) na Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa (120);

(vii) Miradi ya kimkakati 251 imebuniwa katika mamlaka za serikali za mitaa ikiwemo stendi za mabasi, maegesho ya malori, masoko, viwanja vya michezo, maduka ya biashara, kiwanda cha chaki na machinjio. Kati ya hiyo, miradi 48 imekidhi vigezo na imeanza utekelezaji ambapo miradi 22 imekamilika na imeanza kutoa huduma na shilingi bilioni 37.55 zimekusanywa kutoka kwenye miradi hiyo;

(viii) Ujenzi, ukarabati na ukamilishaji wa majengo 122 ya utawala ya halmashauri. Kati ya hayo, 66 yamekamilika na 56 ujenzi upo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Pia, ofisi 4,960 za vijiji, ofisi 737 za mitaa, na nyumba 156 za viongozi na watumishi zimejengwa, kukamilishwa na kufanyiwa ukarabati;

(ix) Kutenga maeneo yenye ukubwa wa ekari 22,000 katika mamlaka za serikali za mitaa kwa ajili ya wafanyabiashara ndogondogo. Aidha, kero 1,849 za wafanyabiashara ndogondogo zimetatuliwa ambapo wachuuzi 4,899 na watoa huduma wadogo wamesajiliwa pamoja na wafanyabiashara ndogondogo na kati 3,565 wametambuliwa. Vilevile, vituo vya kutoa huduma kwa pamoja 65 zimeanzishwa katika mamlaka za serikali za mitaa;

(x) Watumishi 8,097 wameajiriwa katika kada zifuatazo; uhandisi 443, wakadiriaji majenzi 122, watendaji wa kata na vijiji/mtaa 4,070, maendeleo ya jamii 2,241, wasanifu majengo 22, mafundi sanifu na maafisa ugani 1,199; na

(xi) Watumishi 3,680 katika mamlaka za serikali za mitaa (wakiwemo wakurugenzi, wakuu wa idara na vitengo) kutoka mamlaka za serikali za mitaa wameweza kupatiwa mafunzo mbalimbali yakiwemo usimamizi wa masuala ya kinidhamu, maadili, ugavi kutumia mfumo wa NeST, sheria, kaguzi, uibuaji wa miradi/vyanzo vya mapato, uandishi wa miradi, na uandaaji wa miradi ya kimkakati.

2.10 Uendelezaji Miji

47. ***Mheshimiwa Spika,*** Ibara ya 76(b) na 122(k) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 zimeelekeza kuratibu, kusimamia, kufuatilia na kutoa ushauri wa kitalaamu katika utekelezaji wa Mipango Kabambe na Mifumo ya Kijiografia ili kuwezesha mifumo ya ukusanyaji na uchakataji taarifa za kodi za majengo, mabango, pango la ardhi na vibali vya ujenzi.

48. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetekeleza ilani katika maeneo yafuatayo:

(i) Mipango Kabambe ya miji 33 imeandaliwa na kuidhinishwa na mamlaka za upangaji ikiwemo miji yote ya makao makuu ya mikoa 26 na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Mamlaka hizo ni Majiji matano (5) (Dodoma, Mwanza, Arusha, Dar es Salaam na Mbeya), Manispaa 12 (Musoma, Singida, Iringa, Shinyanga, Tabora, Bukoba, Songea, Sumbawanga, Mtwara-Mikindani, KigomaUjiji, Mpanda na Lindi) na Miji sita (6) (Kibaha, Korogwe, Babati, Njombe, Bariadi na Geita); na

(ii) Kuandaa Mpango Kabambe Jumuishi wa Jiji la Kibiashara na Uwekezaji la Kwala, Mkoa wa Pwani 2024 –

2054 ambao umetangazwa katika Gazeti la Serikali Na: 633 la tarehe 28 Oktoba, 2022. Ukubwa wa Jiji hilo ni hekta 130,831, limechukua jumla ya vijiji 30 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe vitano (5), Kibaha (16) na Chalinze tisa (9) ambalo ukubwa wa eneo lake unakaribia ukubwa wa Mkoa wa Dar es Salaam wenye ukubwa nchi kavu pekee wa hekta 139,300. Jiji hilo limelengwa kuwa kitovu shindani cha biashara, uwekezaji, utalii, viwanda na uendeshaji wa mifumo ya fedha kwenye Ukanda wa Magharibi mwa Bahari ya Hindi.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** Jiji la Kwala litapunguza na hatimaye kuondosha changamoto za msongamano zilizopo katika Mkoa wa Dar es Salaam. Hatua hiyo ni jitihada za Serikali za kuongeza ufanisi wa ushushaji na uondoshaji mizigo kwenye bandari ya Dar es Salaam ambapo mizigo inayotoka bandari ya Dar es Salaam imeanza kupakuliwa, kuhamishiwa na kukabidhiwa kwa wateja kwenye bandari kavu ya Kwala iliyoko Vigwaza. Aidha, nalipongeza Shirika la Reli Tanzania kwa kuanzisha huduma kwenye bandari kavu ya Kwala, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Shirika la Viwango Tanzania kwa kufungua matawi yake kwenye bandari kavu ya Kwala na kuanza kutoa huduma. Kufanya hivyo kumelenga kuboresha muonekano wa Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** Miongozo ya utekelezaji wa Mpango Kabambe na Mfumo wa Taarifa za Kijiografia *(Geographical Information System – GIS)* ilisambazwa kwenye Mikoa 12 katika halmashauri 56 pamoja na kuzijengea uwezo timu za menejimenti za halmashauri kama ifuatavyo: - Songwe tano (5), Rukwa tatu (3), Kigoma sita (6), Mwanza nne (4), Mara tano (5), Kagera tano (5), Dodoma tano (5), Mtwara tano (5), Singida mbili (2), Iringa tano (5), Arusha sita (6) na Tanga tano (5).

51. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa *Green and Smart Cities – SASA* 2022 – 2027, unatekelezwa kwenye Halmashauri za Majiji ya Tanga na Mwanza na Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ambapo wanufaika 913 walijengewa uwezo katika Mfumo wa Taarifa za Kijiografia pamoja na Miongozo ya Utekelezaji wa Mpango

Kabambe katika Halmashauri inayotekeleza mradi. Mgawanyo wa wanufaika hao ni vijana 337, wanawake 485 na makundi maalumu 91. Aidha, wataalamu 78 kutoka Ofisi za Wakuu wa Mikoa ya Mwanza na Tanga na halmashauri ya Jiji la Mwanza na Tanga na Manispaa ya Ilemela pia walijengewa uwezo. Aidha, ilihusisha kuwajengea uwezo watalaamu wengine 1,672 wa Halmashauri mbalimbali kwenye mikoa 12 kuhusu matumizi ya Mfumo wa Taarifa za Kijiografia; na Andiko dhana la mapendekezo ya rasimu ya Sera ya Maendeleo Vijijini na Mijini limeandaliwa;

2.11 Uendelezaji wa Miji Midogo Inayochipukia

52. ***Mheshimiwa Spika,*** Ibara ya 122 (k) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 inaelekeza sera ya maendeleo ya miji na kuendelea na utekelezaji wa programu ya uendelezaji wa miundombinu katika majiji, manispaa na miji ili iwe ya kisasa itakayochangia ukuaji wa uchumi na maendeleo ya nchi. Kipaumbele kitakuwa ni kuendeleza miji inayochipukia ili kuzuia uendelezaji usiozingatia taratibu za mipango miji;

53. ***Mheshimiwa Spika,*** miji inayochipukia ni 4,103 sawa na asilimia 91.5 ambayo ipo kwenye halmashauri za wilaya na vijiji miji (*urban villages*), 379 sawa na asilimia 8.5 ipo kwenye halmashauri za miji. Fursa mbalimbali za kiuchumi, mazingira na kijamii za miji hiyo zilibainishwa kikanda, mikoa na halmashauri kwa kutumia mfumo wa taarifa za kijiografia na hivyo kuweza kuainishia miji hiyo aina ya huduma na uwekezaji utakaokuwa na tija kulingana na maliasili zilizoko kwenye maeneo hayo.

54. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI imedhamiria kuimarisha miji hii kwa kuwa inaweka msawazo katika utangamano kijamii na kiuchumi na kuchochea mapinduzi kwenye ngazi hiyo katika uwekezaji, biashara, matumizi ya ufundi, teknolojia na TEHAMA yenye manufaa kwa pande mbili hizo. Aidha, miji hiyo ndiyo msingi wa ukuaji wa miji ya baadaye na inaimarisha shughuli za maendeleo kwenye halmashauri za wilaya.

SEHEMU YA TATU

3.0 Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Mafungu 28) Kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025

3.1 Vipaumbele vya Bajeti kwa Mwaka 2024/25

55. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2024/25, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilipanga kutekeleza mpango na bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo: -

(i) Kusimamia masuala ya utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma (D by D);

(ii) Kuratibu na kusimamia uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2024;

(iii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa huduma za jamii;

(iv) Kuratibu na kusimamia mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato na kudhibiti matumizi yasiyo na tija katika ngazi zote ikijumuisha kuongeza kasi ya biashara ya kaboni;

(v) Kuratibu na kusimamia mifumo na miundombinu ya TEHAMA;

(vi) Kuendeleza rasilimaliwatu katika ngazi zote za Ofisi ya Rais - TAMISEMI;

(vii) Kuratibu na kusimamia shughuli za kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa;

(viii) Kuratibu na kusimamia masuala ya michezo katika shule za msingi na sekondari;

(ix) Kuratibu na kusimamia utendaji kazi wa taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI;

(x) Kuratibu na kusimamia ujenzi wa miradi ya maendeleo katika ngazi zote za Ofisi ya Rais - TAMISEMI; na

(xi) Kuratibu na kusimamia shughuli za uendelezaji wa vijiji na miji kwenye mamlaka za serikali za mitaa.

3.2 Ukusanyaji wa Kodi ya Majengo, Maduhuli na Mapato ya Ndani ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Mafungu 28) Mwaka 2024/25

56. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2024/25, Ofisi ya Rais – TAMISEMI na taasisi zilizo chini yake, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa iliidhinishiwa kukusanya kodi ya majengo, maduhuli na mapato ya ndani ya shilingi trilioni 1.60. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 188.96 ni makadirio ya kodi ya majengo ambayo yatakusanywa na mamlaka za serikali za mitaa zilizopewa uwakala wa kukusanya kodi hiyo na kuwasilisha makusanyo Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali, shilingi bilioni 55.42 ni mapato ya ndani ya taasisi. Aidha, shilingi milioni 315.93 ni maduhuli ya mikoa na shilingi trilioni 1.35 ni za mapato ya ndani ya halmashauri.

57. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2025 shilingi trilioni 1.11 zimekusanywa sawa na asilimia 93.15 ya lengo la kipindi hicho. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 61.21 ni kodi ya majengo, shilingi trilioni 1.04 ni mapato ya ndani ya mamlaka za serikali za mitaa ***(Kiambatisho Na. 2)***, shilingi bilioni 16.23 ni mapato ya ndani ya taasisi na shilingi milioni 201.60 ni maduhuli ya mikoa. Makusanyo hayo yalitokana na ada za wanachuo, tozo, ukusanyaji wa madeni, mauzo ya bidhaa mbalimbali na ushuru unaotozwa na mamlaka za serikali za mitaa kulingana na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290.

3.3 Taarifa ya Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

58. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2024/25, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na taasisi zilizo chini yake (Fungu Na. 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 02) na mafungu 26 ya mikoa (yakijumuisha halmashauri 184) ilipanga kutumia shilingi trilioni 10.53 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kati ya hizo Matumizi ya Kawaida ni shilingi 6.94 ambapo Mishahara ni shilingi trilioni 5.52 na Matumizi Mengineyo ni shilingi trilioni 1.42 yanayojumuisha shilingi bilioni 815.06 za mapato ya ndani ya halmashauri. Aidha, shilingi trilioni 3.58 ni fedha za maendeleo, kati ya hizo shilingi trilioni 2.44 ni fedha za ndani ikijumuisha shilingi bilioni 541.27 ni Mapato ya Ndani ya Halmashauri na shilingi trilioni 1.14 ni fedha za Nje.

59. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2025 Mafungu 28 yamepokea na kukusanya shilingi trilioni 7.53 sawa na asilimia 71.47 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 5.39 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida yakijumuisha Mishahara shilingi trilioni 4.08 na Matumizi Mengineyo shilingi trilioni 1.31. Aidha, shilingi trilioni 2.13 ni fedha za Miradi ya Maendeleo ikijumuisha shilingi trilioni 1.74 Fedha za Ndani na shilingi bilioni 385.83 ni Fedha za Nje.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya fedha zilizopokelewa shilingi bilioni 312.30 ni za mapato ya ndani ya halmashauri ambazo zimetumika kwenye Miradi ya Maendeleo ***(Kiambatisho Na. 3).***

3.4 Mafanikio ya Utekelezaji ya Bajeti kwa Mwaka 2024/25

61. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2024/25 Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, ofisi za wakuu wa mikoa na halmashauri zimefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo:

3.5 Shughuli Zilizotekelezwa Kupitia Fedha za Mapato ya Ndani ya Halmashauri *Mheshimiwa Spika, Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema "Tunahitajika kuongeza juhudi zetu katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ili tuweze kufikia malengo yetu ya maendeleo."*

61. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2024/25 Ofisi ya Rais - TAMISEMI ilipanga kutumia shilingi bilioni 541.27 za mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya kuchangia utekelezaji wa shughuli za maendeleo. Hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 312.30 sawa na asilimia 57.70 zimetolewa na shughuli zifuatazo zimetekelezwa:

(i) Ujenzi wa hosteli 24 umekamilika na 105 zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji, vyumba vya madarasa 122 vimekamilika na 202 vipo katika hatua za ukamilishaji, ujenzi wa nyumba za walimu 15 umekamilika na 140 zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji, ofisi za walimu 14 zimekamilika na 36 utekelezaji unaendelea, ujenzi wa shule 175 umekamilika na 117 zipo hatua mbalimbali za utekelezaji, matundu ya vyoo 534 yamekamilika na 1,966 ujenzi unaendelea, madawati 17,429 yamekamilika na 11,533 yanaendelea kutengenezwa;

(ii) Ujenzi wa hospitali mbili (2) za Manispaa ya Temeke na Jiji la Dodoma unaendelea, uendelezaji wa hospitali 22 upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji, usimikaji wa mfumo wa GoTHOMIS katika vituo vya afya 21 unaendelea, ujenzi wa vichomea taka 10 ambapo vitatu (3) vimekamilika na saba (7) vipo hatua mbalimbali za utekelezaji, ujenzi wa vituo vya afya 162, ambapo vituo 29 vimekamilika na 133 ujenzi unaendelea, ujenzi wa nyumba 114 za watumishi wa afya ambapo nyumba nane (8) zimekamilika na nyumba 106 zipo katika hatua mbalimbali, ujenzi na uendelezaji wa majengo 28 ya wagonjwa wa nje ambapo manne (4) yamemekamilika na yanatumika na 24 ujenzi unaendelea, ujenzi na ukamilishaji wa zahanati 347 ambapo zahanati 28 zimekamilika na 319 utekelezaji upo katika hatua

mbalimbali na ujenzi wa wodi 93 ambapo wodi 21 zimekamilika na 72 ujenzi unaendelea;

(iii) Matengenezo ya Barabara yenye urefu wa kilomita 435.75 kwa kiwango cha lami ambapo kilomita 180.75 matengenezo yamekamilika na kilomita 255 ujenzi unaendelea, ujenzi wa madaraja mawili (2) Manispaa ya Kinondoni unaendelea, ujenzi wa Kalavati tatu (3) Halmashauri ya Wilaya ya Kyela unaendelea, ujenzi wa vivuko vitatu (3) Manispaa ya Morogoro na Wilaya ya Arusha unaendelea, ununuzi magreda 11 kwa ajili ya kuchonga barabara ambapo magreda mawili (2) yamenunuliwa na tisa (9) yapo hatua ya ununuzi, uwekaji wa taa 153 za barabarani ambapo taa 115 zimewekwa na 38 ujenzi unaendelea;

(iv) Ujenzi wa machinjio 48 ambapo sita (6) yamekamilika na 42 ujenzi unaendelea, ujenzi wa fremu za maduka 354, fremu 48 zimekamilika na 306 ujenzi unaendelea, ujenzi wa maghala 10 ambapo matatu (3) yamekamilika na saba (7) yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji, ujenzi wa vitega Uchumi 15 ambavyo vipo katika hatua mbali mbali za utekelezaji, uanzishwaji wa viwanda vidogo 21 ambapo saba (7) vimekamilika na vinafanya kazi na 14 ujenzi wake unaendelea, ujenzi wa vituo vidogo 54 vya mabasi ambapo vituo 17 vimekamilika na vinatumika na 37 ujenzi unaendelea, ujenzi wa masoko 71 ambapo 16 yamekamilika na yanatumika na 55 ujenzi unaendelea na ujenzi wa maeneo ya minada 27 ambapo mitatu (3) imekamilika na 24 ujenzi upo katika hatua mbalimbali;

(v) Ununuzi wa magari 26 ambapo sita (6) yamenunuliwa na 20 yapo hatua mbalimbali za ununuzi, kulipa madeni ya wazabuni katika miradi 71, ujenzi wa ofisi za kata 117 ambapo saba (7) zimekamilika na 110 ujenzi unaendelea, ofisi za vijiji 49 ambapo sita (6) zimekamilika na 43 zipo hatua mbalimbali, ofisi za mitaa 87 ambapo 36 zimekamilika na 51 zipo hatua mbalimbali za utekelezaji

na ukarabati wa majengo ya utawala 77 ambapo 27 yamekamilika na 55 ukarabati unaendelea na ununuzi wa POS 266 ambapo 211 zimenunuliwa na 55 zipo hatua ya ununuzi;

(vi) Kuanzisha mashamba darasa 261 ambapo 29 yamekamilika na 232 yapo katika hatua mbalimbali ya uanzishwaji, kutoa chanjo 101,551 ya mifugo, ujenzi wa mabwawa tisa (9) upo hatua za ukamilishaji, majosho sita (6) yamejengwa na 23 yapo hatua mbalimbali za ujenzi, mbegu tani 3,211 za mazao ya kimkakati zimegawiwa kwa wakulima, miche 135,546 imegawiwa kwa wakulima kwa ajili ya kuimarisha sekta ya kilimo;

(vii) Kuendelea na ukamilishaji wa vituo 77 vya polisi kata ambapo 48 vinaendelea kukamilishwa na 29 vipo kwenye hatua za awali za utekelezaji. Shughuli hii inafanywa kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; na

(viii) Hati miliki za ardhi 2,220 zimetolewa, wananchi 84 wamelipwa fidia kupisha ujenzi wa miundombinu ya umma, viwanja 324 vimepimwa na 719 vinaendelea kupimwa, kuandaa michoro ya mipango miji, ununuzi wa vifaa vya kupimia ardhi, matumizi bora ya ardhi na utekelezaji wa zoezi la anuani za makazi.

3.6 Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024

63. ***Mheshimiwa Spika***, Mwaka 2024/25 Ofisi ya Rais – TAMISEMI iliidhinishiwa shilingi bilioni 254.82 kwa ajili ya kuratibu na kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 247.03 kutoka serikali kuu na shilingi bilioni 7.78 ni fedha za mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya uchaguzi. Uchaguzi huu ulihusisha uchaguzi wa viongozi katika ngazi ya msingi ambao ni wenyeviti wa vijiji, mitaa, vitongoji, wajumbe wa halmashauri za vijiji na wajumbe wa kamati za mitaa.

64. ***Mheshimiwa Spika***, shughuli zilizotekelezwa ni uhakiki wa maeneo ya utawala yaliyojumuisha kata 3,956, vijiji 12,333, mitaa 4,269 na vitongoji 64,274; uandaaji wa nyaraka, uhamasishaji na utoaji wa elimu ya mpiga kura; ununuzi na usambazaji wa vifaa; na uratibu wa usimamizi, ufuatiliaji na uratibu wa upigaji kura kwa ajili ya kuchagua viongozi wa ngazi za vijiji, mitaa na vitongoji katika mamlaka za serikali za mitaa. Aidha, mamlaka za serikali za mitaa zilifanya uandikishaji wa wapiga kura, uteuzi wa wagombea na kampeni.

3.7 Uratibu na Usimamizi wa Huduma za Afya ya Msingi

65. ***Mheshimiwa Spika***, Mwaka 2024/25, Ofisi ya Rais - TAMISEMI ilipanga kutumia shilingi bilioni 357.85 za ruzuku ya fedha za maendeleo za serikali kuu na washirika wa maendeleo katika Uratibu na Usimamizi wa Huduma za Afya ya Msingi, Ustawi wa Jamii na Lishe.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2025 bilioni 166.38 zimepokelewa sawa na asilimia 46.49. Shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

(i) Hospitali 89 za Wilaya kati ya 118 zilizopangwa kujengwa, kukarabatiwa na kukamilishwa zinaendelea na utekelezaji ambapo hospitali 24 zipo katika hatua za ununuzi na 65 zipo katika hatua za ukamilishaji wa ujenzi;

(ii) Ukamilishaji wa Vituo vya Afya 16 ambavyo ni Kazima, Lusaba, Mwayaya, Mgunzo, Nyakiobe, Isangawana, Kilasilo, Mahongole, Igava, Kifunda, Isange, Mpata, Ntaba, Nabweko, Senga na Kasu katika Halmashauri 10 za Manispaa ya Mpanda na Halmashauri za Wilaya za Buhigwe, Kakonko, Chunya, Kyela, Mbarali, Busokelo, Ukerewe, Sumbawanga, na Nkasi. Aidha, vituo vya afya vitatu (3) vipo katika hatua za ukamilishaji wa ujenzi wa miundombinu iliyopelekewa fedha za ukamilishaji na vituo vya afya 13 vipo katika hatua za ununuzi na;

(iii) Ununuzi wa vifaa tiba kwa ajili ya hospitali 119 kati ya 136 za Halmashauri; vituo 41 kati ya 44 vya afya katika halmashauri 18 za Jiji la Tanga, Manispaa ya Songea, Musoma, Halmashauri za Wilaya za Makete, Ludewa, Rufiji, Mkuranga, Nsimbo, Hanang, Nyasa, Mbogwe, Nyang'hwale, Tarime, Kwimba, Buhigwe, Kakonko, Kibondo, na Songwe. Vifaa tiba kwa ajili ya zahanati 356 kati ya 386 katika halmashauri 164. Aidha, vifaa na vifaa tiba vimenunuliwa na MSD inaendelea na taratibu za kukamilisha usambazaji;

(iv) Ujenzi wa miundombinu ya maji 183 na vyoo 183 katika vituo vya kutolea huduma za afya katika mamlaka za serikali za mitaa 137;

(v) Huduma za chanjo katika mamlaka za serikali za mitaa 184 kwa watoto chini ya miaka mitano (5) zimetolewa kupitia vituo vya kutolea huduma za afya na kwa njia ya huduma za mkoba (*outreach*) watoto 1,610,303 kati ya 1,556,556 sawa na asilimia 103 walipata chanjo ya *pentavalent* dozi ya tatu (*Penta* 3) na watoto 1,526,884 kati ya 1,556,556 sawa na asilimia 98 walipata chanjo ya surua dozi ya pili;

(vi) Ukamilishaji wa ujenzi wa zahanati tano (5) ambapo tatu (3) zipo katika hatua za ununuzi, na mbili (2) zipo katika hatua ya plasta, rangi na uwekaji wa milango. Aidha zahanati tano (5) za Idaho, Makutupa, Kinango, Nyamahanga na Ulumi zinajengwa katika Halmashauri za Wilaya ya Mpwapwa, Magu na Kalambo;

(vii) Kupitia Programu ya Uwekezaji katika Afya ya Mama na Mtoto Tanzania *(Tanzania Maternal Child Health Investment Programme - TMCHIP)* watumishi 300 wa mkataba wameajiriwa katika vituo vya kutolea huduma za afya, ukarabati wa vituo vya afya 25 na zahanati 2, wasimamizi wa miradi 209 walipata mafunzo kutoka ngazi ya mkoa na halmashauri, na magari mawili (2) ya usimamizi yamenunuliwa; na

(viii) Kupitia Programu ya Kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria (*Global Fund*) mafunzo kazini yametolewa kwa waganga wakuu wa halmashauri 53, wasimamizi wakuu 40 na wataalamu 60 wa mionzi kutoka katika vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, usimamizi shirikishi katika afua za UKIMWI, kifua kikuu na malaria umefanyika katika halmashauri 184.

3.8 Usimamizi na Uendeshaji wa Elimumsingi na Sekondari

67. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI inaratibu usimamizi na uendeshaji wa elimu ya awali, msingi na sekondari nchini kupitia mamlaka za serikali za mitaa ambapo shule zenye madarasa ya awali ni 20,607 (18,011 za Serikali na 2,596 zisizo za Serikali); idadi ya shule za msingi 20,533 (18,055 za Serikali na 2,478 zisizo za Serikali) zikiwemo shule maalumu za msingi 37 za bweni na vitengo maalumu 710. Aidha, idadi ya shule za sekondari ni 6,269 (4,905 za Serikali na 1,364 zisizo za Serikali).

68. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2024/25 Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilipanga kutumia shilingi trilioni 1.02 kupitia ruzuku ya Serikali Kuu na washirika wa maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli katika sekta ya elimu.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2025 bilioni 663.29 zimepokelewa sawa na asilimia 66.00. Shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

(i) **Uandikishaji wa Wanafunzi wa Elimu ya Awali, Darasa la Kwanza na Kidato cha Kwanza**

70. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2025 Wanafunzi wa Darasa la Awali walioandikishwa ni 1,501,368 (wavulana 754,902 na wasichana 746,466) wakiwemo wenye mahitaji maalum 3,048 (wavulana 1,649 na wasichana 1,399) sawa na asilimia 80.11 ya watoto 1,873,927 wenye umri wa miaka mitano (5) waliotarajiwa kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi, 2022.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa masomo wa 2025, wanafunzi 1,729,180 walitarajiwa kuandikishwa darasa la kwanza, ambapo hadi Machi, 2025 wanafunzi walioandikishwa ni 1,778,461 (wavulana 890,056 na wasichana 888,405) wakiwemo wenye mahitaji maalumu 3,904 (wavulana 2,143 na wasichana 1,761) sawa na asilimia 102.84 ya lengo.

72. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2025 wanafunzi 20,665 (wavulana 11,311 na wasichana 9,354) wakijumuisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu 107 (wavulana 56 na wasichana 51) waliandikishwa katika Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA). Aidha, uandikishaji umeongezeka kwa asilimia 4.04 ikilinganishwa na wanafunzi 19,863 (wavulana 10,775 na wasichana 9,088) walioandikishwa Mwaka 2024.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2025 wanafunzi 889,773 (wavulana 411,046 na wasichana 478,727) wakijumuisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu 2,184 (wavulana 1,074 na wasichana 1,110) waliandikishwa kujiunga na kidato cha kwanza sawa na asilimia 91.15 ya lengo.

(ii) **Upimaji na Mitihani ya Kitaifa**

74. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeratibu na kusimamia mitihani ya upimaji wa kitaifa wa darasa la nne na kidato cha pili na mitihani ya kuhitimu darasa la saba, kidato cha nne na sita.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2024, wanafunzi 1,530,911 (wavulana 733,220 na wasichana 797,691) walifanya mitihani ya upimaji wa darasa la nne. Aidha, wanafunzi 1,320,227 (wavulana 620,326 na wasichana 699,901) kati ya 1,530,805 wenye matokeo sawa na asilimia 86.24 walifaulu. Mwaka 2023 Wanafunzi waliofaulu walikuwa 1,287,934 sawa na asilimia 83.34. Hivyo, kumekuwa na ongezeko la ufaulu kwa asilimia 2.90 kwa wanafunzi waliopata fursa ya kuendelea na darasa la tano ikilinganishwa na Mwaka 2023.

76. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2024 wanafunzi 1,204,899 (wavulana 548,739 na wasichana 656,160) walifanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi, ambapo watahiniwa 1,024,229 (wavulana 449,057 na wasichana 525,172) sawa na asilimia 80.87 ya watahiniwa wenye matokeo walifaulu ikiwa ni ongezeko la asilimia 0.29 la ufaulu wa asilimia 80.58 Mwaka 2023. Aidha, wanafunzi wote waliofaulu walipata nafasi ya kuendelea na elimu ya sekondari.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2024 wanafunzi 801,564 (wavulana 369,731 na wasichana 437,833) walifanya mtihani wa upimaji wa kitaifa wa kidato cha pili, ambapo wanafunzi 680,574 (wavulana 313,117 na wasichana 367,457) kati ya 796,825 wenye matokeo ambao ni sawa na asilimia 85.41 walifaulu kuendelea na Kidato cha Tatu. Mwaka 2023 wanafunzi waliofaulu walikuwa 592,741 sawa na asilimia 85.31.

78. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2024, wanafunzi 517,460 (wavulana 245,542 na wasichana 271,918) walifanya mtihani kidato cha nne. Aidha, watahiniwa wa shule 477,262 (wavulana 228,184 na wasichana 249,078) kati ya 516,695 wenye matokeo ambao ni sawa na asilimia 92.37 walifaulu. Mwaka 2023 watahiniwa waliofaulu walikuwa 471,427 sawa na asilimia 89.36. Hivyo, ufaulu umeongezeka kwa asilimia 3.01. Kati yao wanafunzi 215,245 (wavulana 117,132 na wasichana 98,113) walikuwa na sifa za kujiunga kidato cha tano au vyuo vya kati.

79. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2024, wanafunzi 103,812 (wavulana 57,019 na wasichana 46,793) walifanya mtihani wa taifa wa kidato cha sita, ambapo watahiniwa wa shule waliofaulu ni 103,252 (wavulana 56,637 na wasichana 46,615) sawa na asilimia 99.92 ikilinganishwa na ufaulu wa Mwaka 2023 ambao ulikuwa asilimia 99.90.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** ufaulu wa mitihani ya kitaifa unadhihirisha jitihada kubwa zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau kwa kuboreshwa kwa mazingira ya kujifunzia na kufundishia. Aidha, ninawapongeza walimu kwa jitihada kubwa wanazozitoa katika ufundishaji wa wanafunzi.

(iii) **Michezo kwa Shule za Msingi na Sekondari**

81. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuratibu michezo kwa kuhimiza na kusimamia maendeleo yake katika shule za msingi na sekondari. Mwaka 2024 mashindano ya michezo ya Umoja wa Michezo na Taaluma Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) na Umoja wa Michezo Shule za Sekondari Tanzania (UMISSETA) yalifanyika mkoani Tabora tarehe 05 hadi 26 Juni, 2024.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Michezo ya UMITASHUMTA yenye lengo la kutambua na kuendeleza vipaji, jumla ya wanafunzi 3,188 (wavulana 1,600 na wasichana 1,588) walishiriki michezo mbalimbali. Aidha, wanafunzi 3,164 (wavulana 1,591 na wasichana 1,573) walishiriki mashindano ya UMISSETA. Michezo hii ilihusisha wanafunzi kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. Vilevile, wanafunzi 423 (wavulana 206 na wasichana 217) walishiriki Mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wanafunzi wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Agosti, 2024 nchini Uganda.

83. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mbalimbali yamefikiwa katika usimamizi wa michezo shuleni. Miongoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA yameendelea kuwa na mchango mkubwa kwa upatikanaji wa wachezaji wa timu za vijana wa chini ya miaka 15, 17 na 20 kwa michezo yote inayoshindaniwa Tanzania.

84. ***Mheshimiwa Spika,*** Mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wanafunzi wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania imekuwa bingwa katika michezo ya mpira wa wavu wasichana, mpira wa goli wavulana na wasichana, mshindi wa pili netiboli na soka wasichana kwenye mashindano ya wanafunzi wa shule za msingi. Vilevile Tanzania imeshiriki katika mashindano ya Shule ya Dunia ya Mbio za Nyika yaliyofanyika nchini Kenya na kushika nafasi ya tatu kwa wanamichezo wa umri wa miaka 12 kati ya mataifa 22 yaliyoshiriki mashindano hayo.

(iv) **Mpango wa Elimumsingi Bila Ada**

85. ***Mheshimiwa Spika,*** maafisa elimu kata 3,931, wakuu wa shule za msingi 18,021 na sekondari 4,944 walipokea posho ya madaraka; jumla ya wanafunzi 376,052 wamepata ruzuku ya chakula ambapo wanafunzi 330,325 wa bweni na wanafunzi 45,727 wa kutwa; na wanafunzi 12,285,382 wamepata ruzuku ya uendeshaji kwa shule za msingi 18,021. Vilevile, jumla ya wanafunzi 305,906 wa sekondari walipata ruzuku ya chakula na fidia ya ada ya bweni, fidia ya ada ya kutwa kwa wanafunzi 2,761,311 na ruzuku ya uendeshaji wanafunzi 3,067,217 kwa shule za sekondari 4,944 imetolewa.

(v) **Ujenzi na Ukamilishaji wa Miundombinu ya Shule**

86. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea na umaliziaji wa maboma yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi na miradi viporo katika shule za msingi na sekondari. Ukamilishaji unaoendelea ni madarasa 1,897, mabwalo 241, mabweni 126, majengo ya utawala tatu (3), hosteli 11, maabara 42 na nyumba za walimu sita (6). Aidha, serikali inaendelea na ujenzi wa matundu ya vyoo 2,365 pamoja na miundombinu ya kunawia mikono, kuvunia maji ya mvua na ununuzi wa matanki katika shule za msingi 139 zilizopo katika Mikoa tisa (9) ya Mara, Shinyanga, Njombe, Tabora, Iringa, Dodoma, Kagera, Tanga na Simiyu.

(vi) **Ununuzi wa Vifaa vya Kujifunzia na Kufundishia**

87. ***Mheshimiwa Spika,*** serikali imenunua na kusambaza kemikali za maabara katika shule za sekondari za kata 231. Aidha, vifaa vya maabara kwa shule 486 vimenunuliwa katika awamu mbili (2). Vifaa vya awamu ya kwanza vimesambazwa katika shule 231 zikiwemo shule nane (8) kati ya 26 za mikoa za wasichana. Vifaa vya maabara na kemikali kwa awamu ya pili kwa ajili ya shule 255 zilizobaki vinatarajiwa kupokelewa na kusambazwa kabla ya tarehe 30 Juni, 2025.

88. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea na taratibu za ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya shule za msingi 600

ambavyo ni *Smart Blackboard 416, All in One Computers 8,672, Multifunction Photocopiers (Black & White) 600, Laptops 600, UPSs 4,936, AI Smart Classrooms 184, LAN (Local Area Network) Equipment and Accessories 184 na Data Cabinets* 1,104. Aidha, vitabu 12,442,258 vikijumuisha vitabu 9,082,650 vya shule za msingi na vitabu 3,359,608 vya shule za sekondari vimenunuliwa na kusambazwa.

3.9 Utawala Bora, Usimamizi wa Rasilimali, Ujenzi wa Majengo ya Utawala na Makazi ya Viongozi

89. ***Mheshimiwa Spika, Hayati Benjamini William Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu aliwahi kusema "utawala bora ni msingi wa maendeleo endelevu; bila yake, hatuwezi kufikia malengo yetu"*** kwa muktadha huo Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kusimamia shughuli za utawala bora na utatuzi wa kero za wananchi katika mamlaka za serikali za mitaa kama ifuatavyo:

(i) Utatuzi wa Kero za Wananchi katika Mikoa na Wilaya

Mheshimiwa Spika, Hayati Julius Kambarage Nyerere Rais wa Awamu ya Kwanza alisema "Wananchi wanapotoa malalamiko yao, siyo uadui bali ni wajibu wao wa msingi. Ni lazima wasikilizwe na kushughulikiwa"

90. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2024/25 ofisi za wakuu wa mikoa ziliidhinishiwa shilingi bilioni 4.56 kwa ajili ya shughuli za ufuatiliaji, utatuzi wa kero na uhamasishaji wa shughuli za maendeleo katika mamlaka za serikali za mitaa. Hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 4.03 zimetolewa sawa na asilimia 88.37. Aidha, katika kipindi hicho kero 70,432 zimeshughulikiwa ambapo kero 52,201 mashauri yake yamefungwa na kero 18,231 zinaendelea na utekelezaji.

(ii) Usimamizi wa Rasilimali Watu

Mheshimiwa Spika, ***Hayati Waziri Mkuu Edward Moringe Sokoine alisema "Ole wake kiongozi mzembe na asiye na nidhamu nitakayemkuta, viongozi wazembe na wabadhirifu wahesabu siku***

zao. Labda tusiwajue. Hawa hatuna sababu ya kuwapa imani, kuwa tutawalinda kama vitendo vyao viovu".

91. ***Mheshimiwa Spika***, serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kutokuwa na muhali na watendaji wote wazembe na wabadhirifu wa mali za umma ambapo Mwaka 2024/25 watumishi 2,297 wamechukuliwa hatua za kinidhamu, kati yao wakurugenzi ni 09, wakuu wa idara na vitengo 81, watumishi wa sekta ya ujenzi 43 na watumishi 2,164 wa kada nyingine. Hivyo Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kusimamia nidhamu na uwajibikani wa utumishi wa umma.

(ii) **Usimamizi wa Kituo cha Huduma kwa Wateja**

92. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI ina Kituo cha Huduma kwa Wateja kwa lengo la kushughulikia malalamiko na kero za wananchi. Hadi Machi, 2025 kituo kimehudumia wananchi 43,710. Aidha, masuala mengi yaliyopokelewa na kusikilizwa kutoka kwa wananchi yalikuwa katika sekta za afya, elimu na ardhi. Kituo kimekuwa msaada kwa wananchi katika kupunguza na kutatua changamoto zinazowakabili na kupata taarifa sahihi. Wananchi wanakaribishwa kupiga simu Kituo cha Huduma kwa Wateja kupitia namba **0735 160 210** au **0262 160 210** kuanzia saa mbili asubuhi mpaka saa tisa jioni kwa siku za kazi.

(iii) **Uwezeshaji Ngazi za Msingi za Mamlaka za Serikali za Mitaa**

93. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza dhana ya Ugatuaji Madaraka kwa Wananchi, serikali imeendelea kuboresha utendaji kazi katika ngazi za msingi ili kuimarisha utawala bora, maendeleo endelevu, na ushiriki wa wananchi katika maamuzi yanayogusa maisha yao.

94. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu huo, serikali katika Mwaka 2024/25 ilitenga shilingi bilioni 1.73 za Matumizi Mengineyo kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya posho ya mawasiliano kwa wenyeviti wa vijiji na mitaa. Hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 1.15 zimetolewa sawa na asilimia 66.47 ya fedha zilizoidhinishwa

kwa ajili ya posho ya mawasiliano katika halmashauri 165 ambazo mapato yake ni chini ya shilingi bilioni 5 katika vijiji 12,263 na mitaa 2,161.

(iv) **Ununuzi wa Magari**

95. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha utekelezaji wa miradi na shughuli za maendeleo zinafanyika na kufuatiliwa kwa karibu, serikali imeendelea kuwezesha upatikanaji wa magari ambapo hadi Machi, 2025 jumla ya magari 102 yamenunuliwa na kusambazwa katika taasisi, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa. Kati ya magari hayo 39 ni kwa ajili ya usimamizi wa miundombinu ya barabara inayosimamiwa na TARURA; nane (8) wakuu wa mikoa; saba (7) makatibu tawala mikoa, 43 wakuu wa wilaya na matano (5) wakurugenzi wa halmashauri.

(vi) **Ushirikishwaji wa Wananchi kupitia Mfumo wa O&OD Ulioboreshwa**

96. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuhamasisha wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo katika ngazi za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kwa kutumia Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo Ulioboreshwa. Hadi Machi, 2025 jumla ya mikoa 26 na halmashauri 184 zimepata mafunzo kuhusu mfumo ulioboreshwa wa fursa na vikwazo kwa maendeleo ambao umewezesha halmashauri kuandaa mipango na bajeti kwa Mwaka 2025/26.

(vii) **Ujenzi wa Majengo ya Utawala na Makazi ya Viongozi**

97. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2024/25, shilingi bilioni 171.34 ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa ofisi za wakuu wa mikoa 16, ukarabati wa ofisi za wakuu wa wilaya 22, ikulu ndogo nane (8), ofisi za maafisa tarafa 19, nyumba 124 za wakuu wa mikoa, makatibu tawala wa mikoa, makatibu tawala wasaidizi wa mikoa, wakuu wa wilaya, makatibu tawala wa wilaya, maafisa tarafa, wakurugenzi na wakuu wa idara wa halmashauri; ujenzi wa majengo ya utawala katika halmashauri

72, pamoja na ununuzi wa samani za majengo ya utawala katika halmashauri 50.

98. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 53.14 zimepokelewa, sawa na asilimia 84.00 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa majengo ya utawala katika halmashauri 73 ambayo yako katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, majengo 32 yamekamilika na yanatumika. Kazi zinazoendelea katika majengo hayo ni kazi za nje ikiwemo kujenga uzio, *landscaping*, kibanda cha mlinzi na mgahawa. Majengo 15 yapo katika hatua ya ukamilishaji na baadhi yameanza kutumika wakati shughuli za ukamilishaji zikiendelea, majengo manne (4) yapo hatua ya kuta, majengo matatu (3) yapo hatua ya kupaua, majengo nane (8) yapo hatua ya kumwaga zege la sakafu ya kwanza. Majengo sita (6) yapo hatua ya msingi na majengo matano (5) yapo hatua za ununuzi. Vilevile ununuzi wa samani za majengo ya utawala katika halmashauri 19 unaendelea. Aidha, ukamilishaji wa nyumba 24 za wakurugenzi wa halmashauri unaendelea.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 36.09, sawa na asilimia 73.99 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa majengo ya utawala na makazi ya viongozi na watumishi katika ofisi za wakuu wa mikoa. fedha hizo zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa ikulu ndogo moja (1), ujenzi wa nyumba mbili (2) za viongozi na ukarabati wa ikulu ndogo nne (4), ukamilishaji wa ofisi za wakuu wa mikoa sita (6), ukarabati wa ofisi za wakuu wa mikoa 15, ujenzi wa nyumba za wakuu wa mikoa minne (4) na ukarabati wa nyumba za wakuu wa mikoa mitano (5). Ujenzi wa nyumba za makatibu tawala wa mikoa miwili (2) na ukarabati wa nyumba za makatibu tawala wa mikoa mitatu (3). Ujenzi wa nyumba nne (4) za makatibu tawala wasaidizi. Vilevile, fedha hizo zimetumika kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa ofisi za wakuu wa wilaya 11, ujenzi wa uzio katika ofisi za wakuu wa wilaya nne (4) na ukarabati wa ofisi za wakuu wa wilaya nne (4). Ujenzi wa nyumba za wakuu wa wilaya nne (4), ujenzi wa uzio katika nyumba za wakuu wa wilaya mbili (2) na ukarabati wa nyumba za wakuu wa wilaya za 12. Pia ujenzi wa nyumba za makatibu tawala wa wilaya sita (6) na ujenzi wa uzio katika nyumba za

makatibu tawala wa wilaya 14. Ujenzi wa ofisi za tarafa 48 na nyumba za maafisa tarafa sita (6).

3.10 Usimamizi wa Mifumo ya TEHAMA

Mheshimiwa Spika, Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema "Tunahitaji kuwekeza katika TEHAMA ili kuweza kujenga uchumi wa kidijitali ambao utawafaidisha wananchi wote."

100. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2024/25, mifumo ya TEHAMA imeendelea kuboreshwa na kujengwa ili kukidhi mahitaji stahiki katika maeneo ya kiutendaji yanayosimamiwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI na kuwezesha utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

101. ***Mheshimiwa Spika****,* Ofisi ya Rais -TAMISEMI imetekeleza maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa Mwaka 2024 ya uunganishaji wa mifumo ya TEHAMA. Hadi Machi, 2025 Ofisi ya Rais -TAMISEMI imeunganisha mifumo yake na mifumo ya taasisi 24 za serikali na sekta binafsi ili kuongeza ufanisi wa kumhudumia mwananchi, kuwezesha upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wakati, kudhibiti upotevu wa mapato na kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma.

102. ***Mheshimiwa Spika****,* Mifumo inayosimamiwa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI ni pamoja na Mfumo wa Uendeshaji na Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Afya yaani GoTHOMIS. Mfumo huu umeboreshwa na unaendelea kuunganishwa katika vituo vya kutolea huduma za afya ambapo hadi Machi, 2025, jumla ya vituo 5,505, sawa na asilimia 74.93 ya vituo vya umma ngazi ya afya ya msingi vinatumia mfumo huo. Vituo hivyo ni hospitali teule za wilaya tisa (9), hospitali za wilaya 188, vituo vya afya 883, zahanati 4,431 na kliniki tatu (3). Aidha, wagonjwa zaidi ya milioni sita wamepatiwa huduma kupitia Mfumo wa GoTHOMIS, kufanikisha rufaa 13,329, kusimamia mapato yanayotokana na uchangiaji, upatikanaji wa taarifa za magonjwa na ugonjwa pamoja na usimamizi wa madawa.

103. ***Mheshimiwa Spika,*** lengo la Ofisi ya Rais -TAMISEMI ni kuweka Mfumo wa GoTHOMIS katika vituo vyote vya ngazi ya msingi ifikapo Juni, 2025. Vilevile, mfumo huu unatumiwa na vituo vya kutoa huduma ya afya vilivyo chini ya Benki Kuu ya Tanzania, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, baadhi ya vituo vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na taasisi nyingine.

104. ***Mheshimiwa Spika,*** Mfumo mwingine ulio chini ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI ni Mfumo wa TAUSI ambao umeongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ya halmashauri. Aidha, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kupitia Mfumo wa TAUSI imewezesha:

(i) Kupunguza matumizi ya fedha mbichi na ucheleweshaji wa kuwasilisha fedha benki;

(ii) Kumwezesha mwananchi kununua viwanja vinavyouzwa na halmashauri nchini;

(iii) Kumwezesha mteja kujihudumia mwenyewe hata akiwa nje ya nchi na kupata huduma pasipo kufika ofisi za halmashauri;

(iv) Kupunguza muda wa kupata huduma za leseni na vibali na kuwezesha utoaji wa leseni na vibali kielektroniki;

(v) Kuwa na taarifa sahihi za walipakodi na watumiaji kwa kutumia Namba ya Utambulisho ya Taifa (NIDA) na Namba ya utambulisho wa mlipa kodi yaani *TIN*; na

(vi) Kukusanya mapato kupitia *Control Number* Jumuishi.

105. ***Mheshimiwa Spika,*** Mfumo wa TAUSI unasomana na mifumo ya Mamlaka ya Serikali Mtandao, Wizara ya Fedha, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma, Baraza la Sanaa Tanzania, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Zoezi linaendelea kuziunganisha taasisi za Mfuko wa Bima ya Afya, Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi, Mamlaka ya Usafirishaji Nchi Kavu na Jeshi la Polisi Tanzania.

106. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeanza utoaji wa mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kwa kutumia Mfumo wa Wezesha. Matumizi ya mfumo huu yamesaidia kuondoa changamoto zilizokuwepo awali ikiwa ni pamoja na kudhibiti uwepo wa vikundi hewa, watu kujisajili katika kikundi zaidi ya kimoja na wakopaji hewa. Vilevile, mfumo umeimarisha usimamizi, usajili wa vikundi, utoaji na urejeshaji wa mikopo, upatikanaji wa taarifa sahihi za mikopo kwa wakati, kuondoa upendeleo na kuongeza uwazi na uwajibikaji. Mfumo huu utaunganishwa na mifumo ya benki kuwezesha kutoa mikopo hii kwa halmashauri 10 zitakazotumia mabenki.

107. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea kuboresha utoaji wa huduma bora za afya kidijitali, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Vodacom *Foundation* imeendelea kuboresha Mfumo wa Huduma ya Usafiri wa Dharura kwa Mama Wajawazito na Watoto Wachanga yaani M-MAMA ambapo gharama za usafiri wa dharura zimepungua kwa asilimia 33 ikilinganishwa na matumizi ya magari ya kubebea wagonjwa peke yake. Matumizi ya mfumo huu yamepunguza muda wa kumhudumia mgonjwa kwa asilimia 50 sambamba na watumiaji kuongezeka kutoka 45,000 hadi 70,000 kwa mwaka. Aidha, Mfumo wa M-MAMA ni moja kati ya afua zilizochangia kupunguza vifo vya kinamama kutoka vifo 504 kwa vizazi hai 100,000 hadi vifo 104.

108. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imekamilisha uboreshaji na kuanza matumizi ya Mfumo wa Taarifa za Shule unaosaidia kupata taarifa za shule kwa wakati, kufuatilia maendeleo ya wanafunzi kimasomo, kung'amua vihatarishi vya utoro kwa wanafunzi vinavyoweza kusababisha wanafunzi kuacha shule na hivyo kuwezesha waalimu kuchukua hatua mapema. Mfumo huu unatumika katika shule zote za umma na zisizo za umma nchini katika ngazi ya elimumsingi na sekondari.

109. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuiwezesha serikali kuwa na picha kamili ya nguvu kazi ya walimu kote nchini, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imebuni

na kuanza ujenzi wa kanzidata (Mwalimu *Data Lake*) itakayotunza taarifa za uzalishaji wa walimu, ajira na uendelezaji wao.

110. ***Mheshimiwa Spika***, Mfumo wa *Mwalimu Data Lake* utaunganishwa na mifumo kutoka Sekretarieti ya Ajira (Ajira *Portal*), Tume ya Vyuo Vikuu (Mfumo wa UIMIS), Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo - NACTVET (Mfumo wa TVET-MIS), Wizara ya Elimu, Sayansi na Tekinolojia (Mfumo wa TCMS na TE-MIS), Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (Mfumo wa OS-MIS), Tume ya Utumishi ya Walimu (Mfumo wa TSC-MIS) pamoja na Taasisi ya Elimu – TIE (Mfumo wa Kusimamia Taarifa za Uendelezwaji wa Walimu).

111. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma katika ngazi ya msingi na vituo vya kutoa huduma zaidi ya elfu hamsini kupitia Mfumo wa Uhasibu na Utoaji wa Taarifa katika Vituo vya Kutolea Huduma yaani FFARS. Mfumo huu unaongeza uwazi, uwajibikaji, na ufanisi wa usimamizi wa rasilimali za umma. Aidha, mfumo huu unaziwezesha shule na vituo vya afya kutoa taarifa za fedha (mapato na matumizi) kwa wakati halisi na kuongeza ufanisi wa upangaji wa bajeti.

112. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Wizara ya Fedha, mfumo unaboreshwa ili kuendelea kusomana na mifumo mingine kama Mfumo wa Uhasibu Serikalini, Mfumo wa Mipango na Bajeti na benki kwa kuzingatia mahitaji na maelekezo mapya na kuimarisha usimamizi bora wa fedha za umma. Huu ni uthibitisho wa dhamira ya Serikali katika kujenga mifumo thabiti ya uwajibikaji kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu. Dhamira ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI katika Mwaka 2025/26 mfumo huu utumike kwenye kata, vijiji, mitaa, shule na vituo vyote vya kutoa huduma za afya.

113. ***Mheshimiwa Spika,*** Februari, 2025 Ofisi ya Rais - TAMISEMI ilifanikiwa kupata tuzo nane (8) za TEHAMA zilizoandaliwa na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Tuzo hizi zinadhihirisha mafanikio makubwa ya mapinduzi ya TEHAMA yanayofanywa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI katika utoaji wa

huduma kwa wananchi. Kwa ufafanuzi wowote wa namna ya kutumia mifumo hii ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, wananchi wanakaribishwa kupiga simu Kituo cha Huduma kwa Wateja.

3.11 Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu

Mheshimiwa Spika, Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema "Mikopo ya asilimia 10 ni njia mojawapo ya kusaidia jamii katika kuleta usawa wa kijamii na kiuchumi".

114. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2024/25 serikali ilitarajia kutoa mikopo ya shilingi bilioni 227.96, ambapo shilingi bilioni 63.67 ni fedha za marejesho zilizokusanywa kutokana na mikopo iliyotolewa kabla ya kusimamishwa. Aidha, shilingi bilioni 63.24 ni fedha zilizokuwa zinatengwa kwa ajili ya mikopo na shilingi bilioni 101.05 ni fedha ambazo zimetengwa kutokana na makadirio ya makusanyo ya mapato ya ndani ya Mwaka 2024/25.

115. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 82.84 zilikopeshwa kwa vikundi 8,275 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 40.71 kwa vikundi 4,557 vya wanawake, shilingi bilioni 36.64 kwa vikundi 2,827 vya vijana na shilingi bilioni 5.48 kwa vikundi 891 vya watu wenye ulemavu. Aidha, hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 14.04 zimerejeshwa kutoka vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

3.12 Huduma Ndogo za Fedha

116. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2024/25 mamlaka za serikali za mitaa ziliidhinishiwa shilingi bilioni 4.76 kwa ajili ya uratibu wa huduma ndogo za fedha ambapo hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 3.17 zimetolewa sawa na asilimia 66.59 kwa ajili ya uratibu wa huduma ndogo za fedha kwenye sekta ndogo ya fedha ambapo vikundi 58,271 vimesajiliwa.

3.13 Usimamizi wa Mazingira, Uhifadhi wa Maliasili na Mabadiliko ya Tabianchi

117. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea na uratibu wa shughuli za usimamizi wa mazingira, ulinzi maliasili pamoja na uratibu wa mabadiliko ya tabianchi. Mafunzo kwa wataalamu 45 wa mikoa sita (6) na halmashauri 15 zilizoanza utekelezaji wa Biashara ya Kaboni na uhifadhi wa bioanuwai yametolewa. Aidha, mafunzo ya kuhimili athari ya mabadiliko ya tabianchi yametolewa kwa wenyeviti/mameya wa halmashauri, wakurugenzi, wakuu wa idara za mipango wa halmashauri 184 na makatibu tawala wasaidizi wa sehemu ya mipango na uratibu wa mikoa 26.

118. ***Mheshimiwa Spika*** hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 12.93 zimepokelewa kutokana na mauzo ya hewa ya kaboni yaliyoishia Mwezi Novemba, 2024 kutokana na uhifadhi wa Maliasili kwa Halmashauri za Tanganyika, Mbulu, Kiteto na Karatu. Mapato hayo yametolewa na Kampuni ya Kaboni Tanzania kwa kuzingatia Kanuni ya Udhibiti na Usimamizi wa Kaboni nchini za Mwaka 2022.

3.14 Uendelezaji Vijiji na Miji

119. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI imesimamia ofisi za wakuu wa mikoa na mamlaka za upangaji kwa kushirikiana na wizara za kisekta, sekta binafsi, wadau wa maendeleo wa jamii kwa jumla katika kuandaa na kutekeleza mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 3,641 sawa na asilimia 29.52 kati ya vijiji 12,333 vilivyopo nchini. Aidha, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imezielekeza halmashauri za wilaya zisimamie ipasavyo uendelezaji wa maeneo ya visiwa na fukwe kwenye maeneo yao ya utawala.

120. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi imeweza kufuatilia urejeshwaji wa mkopo wa bilioni 49.47 ambao ulikopeshwa kwa halmashauri 51 kwa ajili ya Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha (KKK) ambao unalenga kuboresha utoaji wa huduma za ardhi. Hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 32.21 kati ya bilioni 49.47, sawa na asilimia 65.11

ya fedha zilizokopeshwa zimerejeshwa. Ofisi ya Rais - TAMISEMI inaendelea kufuatilia halmashauri ambazo bado hazijakamilisha kulipa mikopo hiyo na kuhakikisha zinalipa katika bajeti ya Mwaka 2025/26.

3.15 Ujenzi, Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Wilaya

121. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2024/25 ziliidhinishwa shilingi bilioni 908.16 kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara kupitia Mfuko wa Barabara, Tozo ya Mafuta, Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali na washirika wa maendeleo. Hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 468.40 zimetolewa kwa ajili ya miundombinu ya barabara na usafirishaji, sawa na asilimia 55.68 ya fedha zilizoidhinishwa.

122. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kunukuu maneno ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyasema akiwa Wilaya ya Kalambo Mkoa wa Rukwa Julai, 2024.

"Ninatoa wito kwa wasafirishaji wote nchini pamoja na wananchi kuhakikisha wanalinda miundombinu ya barabara inayojengwa na Serikali kwa kutofanya shughuli za kijamii kama kulima, kuchimba pembezoni mwa barabara pamoja na kazi nyingine zinazoathiri barabara. Ujenzi wa barabara ni gharama sana, ukijenga kilomita moja ya barabara ni sawa na kujenga vituo vitatu vya afya pamoja na kuweka vifaa tiba ndani yake, hivyo niwaombe sana tutunze barabara zetu."

123. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita kwa kulitambua hilo, imeendelea kutoa fedha kupitia TARURA kwa ajili ya ujenzi, matengenezo na ukarabati wa barabara kutoka shilingi bilioni 275 Mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 772.19 Mwaka 2024/25 sawa na ongezeko la asilimia 180.80 ya fedha za ndani.

124. ***Mheshimiwa Spika,*** ongezeko hili la fedha limewezesha kujenga barabara za lami kilomita 1,442.30, barabara za changarawe kilomita 19,879.21 na madaraja 3,195 yanayohudumiwa. Kutokana na ongezeko la fedha, kazi

zimeongezeka ambapo makandarasi wa ndani wamenufaika na ongezeko hilo la fedha, hivyo wastani wa mikataba 844 ya kazi za barabara imeongezeka na kufikia wastani wa mikataba 1,167.

125. ***Mheshimiwa Spika,*** Shughuli zilizotekelezwa hadi Machi, 2025 ni kama ifuatavyo:-

(i) Fedha za Mfuko wa Barabara zimetumika kufanya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 4,057.74, ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilomita 2.75, barabara za changarawe zenye urefu wa kilomita 32.36 na ukarabati wa madaraja 15, makalavati 52 na mifereji ya kuondoa maji barabarani yenye urefu wa mita 23,972.14 katika wilaya 139 za Tanzania Bara;

(ii) Fedha za tozo ya mafuta zimetumika kujenga barabara za lami zenye urefu wa kilomita 8.0, ujenzi wa barabara za changarawe zenye urefu wa kilomita 992 na ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua yenye urefu wa mita 7,338. Fedha za Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali zimetumika kujenga barabara za lami zenye urefu wa kilomita 61.77, ujenzi wa barabara za changarawe kilomita 435.26 na makalavati 90;

(iii) Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia TARURA kwa kushirikiana na Benki ya CRDB imeratibu uanzishwaji wa Hati Fungani ya Miundombinu iitwayo Samia *Infrastructure Bond* iliyolenga kukusanya zaidi ya shilingi bilioni 150 ambapo hadi dirisha la ununuzi wa hisa lilipofungwa shilingi bilioni 323.00 sawa na asilimia 215.33 zimekusanywa na zitatumika kuwakopesha (kwa masharti nafuu) makandarasi watakaoingia mikataba ya kazi na TARURA. Hii itamrahisishia mkandarasi kupata haraka fedha za kuanza kazi kwa miradi ambayo haina kipengele cha malipo ya awali. Aidha, itawezesha uwepo wa fedha zinazoweza kukopwa (kwa masharti nafuu) na mkandarasi mwenye mkataba na TARURA na kuwezesha kukamilisha mradi kwa wakati na hivyo kuepuka gharama za

kuhudumia mradi zaidi ya muda uliopangwa na hivyo mkandarasi kupata faida zaidi;

(iv) Programu ya Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii Nchini *(Roads to Inclusion and Socioeconomic Opportunities – RISE)* inaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa barabara za lami za Wenda – Mgama kilomita 19 na Mtili – Ifwagi kilomita 14 zilizopo Halmashauri za Wilaya ya Iringa na Mufindi mtawalia. Aidha, taa za barabarani 170 kwenye barabara hizo zinaendelea kuwekwa. Vilevile, madaraja 35 kati ya madaraja 130 yamekamilika na kazi nyingine zinaendelea zikiwa zimefikia asilimia 70 kupitia Miradi ya Uondoaji Vikwazo vya Upitikaji. Ujenzi wa barabara awamu ya pili za Halmashauri za Wilaya za Handeni, Ruangwa na Mbogwe tayari nyaraka za zabuni zinasubiri kupitishwa baada ya marekebisho toka Benki ya Dunia;

(v) Mradi wa Kuboresha Miundombinu Shindanishi katika Miji 45 Tanzania - *Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness (TACTIC)* unatekelezwa kama ifuatavyo:

(a) Kuendelea na ujenzi wa barabara kilomita 147.54 katika halmashauri 12 na mitaro ya maji ya mvua kilomita 24.66 katika Miji ya Dodoma, Kahama, Mbeya, Kigoma na Morogoro ambapo kilomita 25.23 sawa na asilimia 17 zimekamilika. Aidha, mikataba ya ujenzi wa masoko tisa (9), stendi za mabasi tano (5), stendi ndogo mbili (2) na ujenzi wa ghala la kuhifadhia mazao imeisainiwa na makandarasi wameanza ujenzi;

(b) Kazi iliyofanyika kundi la pili la mradi katika halmashuri za miji 15 ni ununuzi wa makandarasi unayotarajiwa kukamilishwa Aprili, 2025. Aidha, utekelezaji wa kundi la pili utakapokamilika itajengwa miundombinu ya barabara za lami kilomita 141.56, daraja moja (1), mifereji kilomita 31.15, masoko 12,

maeneo mawili (2) ya kupumzikia na stendi za mabasi sita

(c) Kazi iliyofanyika kundi la tatu katika Halmashauri za miji 18 ni maandalizi ya kuanza usanifu wa miradi inayotarajiwa kutekelezwa katika miji hiyo. Aidha, awamu hii inatarajia kujenga barabara za lami zenye urefu wa kilomita 89.40, mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa kilomita 5.0, masoko 16 na stendi za mabasi 14;

(vi) Mradi wa Uendelezaji wa Bonde la Mto Msimbazi upo katika hatua za utekelezaji ambapo kazi zinazoendelea kutekelezwa ni pamoja na taratibu za ununuzi wa mkandarasi wa kuchimba na kujenga kingo za Mto Msimbazi na mtaalamu mshauri atakayesimamia kazi;

(vii) Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam Awamu ya Pili *(Dar es Salaam Metropolitan Development Project II – DMDP II)* unaendelea ambapo kazi zinazotekelezwa ni pamoja na ukamilishaji wa taratibu za ununuzi wa ujenzi wa barabara kilomita 148 zitakazojengwa katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuingia mikataba 17 yenye thamani ya shilingi bilioni 411.00. Aidha, malipo ya awali ya shilingi bilioni 28.53 kwa makandarasi nane (8) watakaotekeleza miradi hiyo yamefanyika;

(viii) Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia TARURA inaendelea na utekelezaji wa miradi kwa teknolojia za *Ecoroads, Ecozyme* na *GeoPolymer*. Hadi sasa kwa kutumia teknolojia ya *Ecoroads,* ujenzi wa barabara ya Itilima Oil – Ikindilo kilomita 5.2 Wilaya ya Itilima kwa kutumia teknolojia ya *Ecozyme* umefikia asilimia 95 na utekelezaji wa ujenzi wa barabara ya Himo - Makuyuni - Lotima kilomita 6.16 Wilaya ya Moshi kwa kutumia teknolojia ya *Ecoroads* unaendelea na umefikia asilimia 65 ya utekelezaji;

(ix) Madaraja 82 yamejengwa kwa kutumia malighafi ya mawe inayopatikana karibu na eneo la ujenzi kwa gharama ya shilingi bilioni ambapo ingekuwa shilingi bilioni 17.4 kama yangejengwa kwa zege; na

(x) Mradi wa *Agriconnect* unaendelea na unahusisha ujenzi wa barabara za Itulahumba - Igwachanya (kilomita 19.25) - Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Ndulilo - Itete (kilomita 8.9) - Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Lwangwa - Kejo Gas (kilomita 6.41) - Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo, Kidabaga - Bomalang'ombe (kilomita 1.10) - Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, Bomalang'ombe Mwatasi - Kibengu Road (kilomita 13.3) Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, Ilolo - Ndolezi (kilomita 11.01) - Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, *Park at Old Airport* (kilomita 1.5) - Halmashauri ya Jiji la Mbeya na Utili - Mahande (kilomita 14.414) - Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.

126. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia TARURA iliidhinishiwa fedha za dharura shilingi bilioni 71.46 kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya miundombinu ya barabara zilizoathiriwa na mafuriko ya maji ya mvua. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 50 ni nyongeza ya bajeti kwa Mwaka, 2024/25. Hadi Machi, 2025 shilingi bilioni 8.01 zimepokelewa sawa na asilimia 11.28.

127. ***Mheshimiwa Spika,*** Shughuli zilizotekelezwa kwa fedha za dharura za ndani ni pamoja na kurekebisha barabara zenye urefu wa kilomita 78 na daraja moja (1) la waenda kwa miguu. Aidha, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutoa fedha ili kurejesha hali ya barabara za vijijini na mijini ambazo huathiriwa na maji ya mvua za msimu.

128. ***Mheshimiwa Spika,*** kuanzia mwishoni mwa Mwaka 2023 nakuendelea mpaka Mei, 2024, kulijitokeza mvua nyingi zisizo za kawaida ambazo ziliharibu miundombinu mingi ya barabara na kusababisha kukatika kwa mawasiliano. Fedha zilizohitajika kutengeneza miundombinu hiyo ni takribani shilingi bilioni 250.

Kupitia miradi ya Benki ya Dunia inayoendelea hapa nchini chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Benki ya Dunia kupitia madirisha ya *Contingent Emergency Response Component* (CERC) chini ya mradi wa DMDP2 na *Crisis Response Window* (CRW) chini ya mradi wa RISE imetoa jumla ya shilingi bilioni 235 kwa ajili ya kutengeneza miundombinu ya barabara iliyoharibika. Kupitia CERC shilingi bilioni 170 zimeidhinishwa na CRW shilingi bilioni 65 zimeidhinishwa. Miradi hii itatekelezwa katika mikoa yote 26 Tanzania Bara. Utekelezaji wa CERC kupitia DMDP2 umeanza ambapo hadi sasa mikataba 30 ya jumla ya shilingi bilioni 12 imesainiwa kwa ajili ya matengenezo na taratibu za ununuzi zinaendelea kwa miradi mingine inayohitaji usanifu wa kina.

3.16 Huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka

129. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia DART inaendelea na usimikaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji Nauli (*Automated Fare Collection System-AFCS)* ambao utafungamanishwa na Mfumo wa Kuongozea Magari *(Intelligent Transport System - ITS)* ikiwa ni sehemu ya maboresho endelevu ya huduma hii kwa wananchi waishio mijini, na pia kuondoa mianya ya upotevu wa mapato yatokanayo na nauli.

130. ***Mheshimiwa Spika,*** Hadi Machi, 2025 Wakala imesambaza kadi janja 62,000 kati ya 200,000 za kukusanyia mapato na kusimika mageti janja kwenye vituo vyote 27. Aidha, mapato yanatarajiwa kuongezeka kutoka shilingi milioni 100 hadi milioni 120 kwa siku baada ya kuanza kutumia kadi janja.

3.17 Shirika la Masoko ya Kariakoo

131. ***Mheshimiwa Spika,*** shirika lilipanga kuboresha mazingira ya kufanyia biashara ambapo wafanyabiashara watapangwa katika jengo jipya lenye ghorofa nane na jengo lililokarabatiwa. Hadi Machi, 2025 Shirika limetekeleza shughuli zifuatazo;

(i) Wafanyabiashara 1,520 waliohakikiwa na kukidhi vigezo vya kurejeshwa sokoni tayari wameshapangiwa maeneo ya kufanyia biashara kwenye Mfumo wa TAUSI.

Aidha, maeneo mengine 387 yatatangazwa katika Mfumo wa TAUSI kwa ajili ya kuingizwa katika mnada;

(ii) Kamera 40 zimesimikwa kwa ajili kuimarisha ulinzi na usalama katika soko;

(iii) Kutenga maeneo manne (4) ya mashine za kutolea fedha na maeneo mawili (2) kwa ajili ya huduma za kibenki;

(iv) Kutenga eneo la maegesho ya magari lenye uwezo wa kuegesha magari 138;

(v) Kuboresha mpangilio wa maeneo 1,907 ya biashara katika soko linalokarabatiwa na linalojengwa tofauti na hapo awali kwa kuzingatia aina ya biashara zinazofanana kuuzwa katika eneo moja *market segmentation*;

(vi) Kwa kushirikiana na Shirika la Nyumba la Taifa tumefanya upembuzi yakinifu wa awali kwa ajili ya mradi wa uwekezaji wa kibiashara katika eneo la Mbezi Beach Makonde;

(vii) Kuboresha mikataba ya Shirika na wafanyabiashara ambayo itatumika kwenye Soko la Kariakoo ili kuendana na mabadiliko ya soko, mahitaji ya kibiashara na kupunguza migogoro ya baadae;

(viii) Kuwajengea uwezo watumishi 29 juu ya matumizi ya mifumo mbalimbali ya kiutendaji na utekelezaji wa shughuli za Shirika ikiwemo Mfumo wa TAUSI na Mfumo wa Mpango na Bajeti; na

(ix) Ukarabati wa nyumba tatu (3) ambapo nyumba moja (1) Mbezi Beach Makonde na nyumba mbili (2) Tabata Bima.

3.18 Chuo cha Serikali za Mitaa

132. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo kilipanga kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa waheshimiwa madiwani, wenyeviti wa vijiji, wenyeviti wa mitaa pamoja na wenyeviti wa vitongoji katika halmashauri zote 184 nchini katika masuala mbalimbali yanayohusu uendeshaji wa mamlaka za serikali za mitaa; Kufanya tafiti 30 na kutoa ushauri elekezi kwa serikali kuu, mamlaka za serikali za mitaa, mashirika na watu binafsi juu ya masuala mbalimbali ya maendeleo na kuimarisha mifumo ya TEHAMA; Kuandaa Mtaala wa Shahada ya Kwanza ya Nyaraka na Kumbukumbu; Kuendeleza watumishi 27 katika ngazi mbalimbali za elimu; na kujenga miundombinu ya chuo ikiwemo ofisi ndogo, jengo la mhadhara lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 200 na nyumba ya mtumishi.

133. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2025 Chuo kimetekeleza shughuli zifuatazo;

(i) Kudahili wanafunzi wa mwaka wa kwanza 6,805 kati ya 9,300;

(ii) Kutoa mafunzo kwa wenyeviti wa vijiji 8,117, wenyeviti wa mitaa 3,126 na wenyeviti wa vitongoji 37,237 katika halmashauri 116 kati ya 184 waliochaguliwa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika Novemba, 2024. Aidha, chuo kimetoa mafunzo kwa waheshimiwa madiwani 68 kutoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita na Halmashauri ya Mji Babati. Lengo la mafunzo haya ilikuwa kuwajengea uwezo washiriki kuhusu maadili ya viongozi, usimamizi wa mapato, kuibua miradi na kusimamia utekelezaji wake, uendeshaji wa vikao vya kisheria na uendeshaji wa shughuli katika mamlaka za serikali za mitaa;

(iii) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa kutumia Mfumo wa Ujifunzaji Kielekitroniki (MUKI) kwa waheshimiwa madiwani 1,570 na watendaji wa vijiji na mitaa 2007 kutoka katika halmashauri 31;

(iv) Kufanya tafiti mbili (2) na machapisho 30 ya kitaaluma katika majarida ya kitaifa na kimataifa yenye lengo la kuboresha utendaji katika mamlaka za serikali za mitaa;

(v) Kufungamanisha mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji mapato na udahili wa wanafunzi ili kuongeza ufanisi katika utoaji huduma na kudhibiti mapato;

(vi) Kuandaa na kukamilika kwa mtaala wa Shahada ya Kwanza ya Nyaraka na Kumbukumbu ambapo masomo yataanza kutolewa mwaka wa masomo 2025/26;

(vii) Kuendeleza kitaaluma watumishi 27 katika shahada za uzamivu 11, uzamili 11 na shahada ya kwanza watano (5); na

(viii) Ukarabati wa miundombinu ya maji na umeme katika mabweni ya wanafunzi na nyumba za watumishi umefanyika ambapo shilingi milioni 61.37 zimetumika.

3.19 Shirika la Elimu Kibaha

134. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika lilipanga kutoa elimumsingi kwa wanafunzi 3,141 na elimu ya sekondari kwa wanafunzi 329; Kukamilisha, kuandaa na kusimamia mfumo wa mafunzo kwa njia ya mtandao; Kutoa elimu ya sekondari mubashara kwa shule za sekondari nchini; Kuboresha utoaji wa elimu kwa wahudumu wa afya 512 katika fani ya utabibu na uuguzi kupitia Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Kibaha.

135. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile chuo kilipanga kutoa elimu ya afya dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza kwa wananchi; kutoa elimu na mafunzo ya stadi za ujuzi na ubunifu katika fani za umeme wa majumbani, ufundi wa magari, uundaji na uungaji vyuma, ujenzi (useremala, uashi na bomba), kilimo, mifugo, upishi, na ushonaji kwa vijana 400 kwa kozi za muda mrefu na wananchi 1,000 kwa kozi za muda mfupi kwa mafunzo ya ana kwa ana na

kwa njia ya mtandao; na kufanya ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha.

136. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2025 Shirika limetekeleza shughuli zifuatazo;

(i) Elimumsingi imetolewa kwa wanafunzi 3,282 sawa na asilimia 104 ya lengo na elimu ya sekondari imetolewa kwa wanafunzi 315 sawa na asilimia 96 ya lengo. Aidha, Shirika limetoa huduma za maktaba kwa wananchi 25,496 ambapo wananchi 24,221 walisoma vitabu na machapisho mbalimbali ndani ya maktaba na wananchi 1,275 waliazima vitabu kwa ajili ya kwenda kujisomea nyumbani;

(ii) Kukamilisha maandalizi ya mada za nadharia kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa Mradi wa Utoaji wa Elimu ya Sekondari kwa njia ya masafa. Aidha, Shirika limeendelea kusimamia ufundishaji wa elimu ya sekondari mubashara kupitia madarasa janja yaliyopo Shule ya Sekondari Kibaha ambapo wanafunzi wa shule tatu (03) za sekondari ambazo ni Shule ya Sekondari Dodoma (Dodoma), Shule ya Sekondari Tumekuja (Zanzibar) na Shule ya Sekondari Dkt. Samia (Dodoma) wa masomo ya sayansi wameendelea kufundishwa kwa njia ya mtandao mubashara kwa siku za Jumatano na Ijumaa;

(iii) Mafunzo kwa kada mbalimbali za afya yametolewa kwa wanachuo 564 sawa na asilimia 110 ya lengo. Kati ya hizo kada ya uuguzi na ukunga kwa wanachuo 240, utabibu kwa wanachuo 285 na uhudumu wa afya ngazi ya jamii kwa wanachuo 39. Kada ya uhudumu wa afya ngazi ya jamii ni kozi mpya iliyoanza kutolewa Mwezi Septemba, 2024 na ina mwitikio mkubwa;

(iv) Elimu ya afya dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza ilitolewa kwa wananchi 324 sawa na asilimia 65 ya lengo; na

(v) Elimu na mafunzo ya stadi za ujuzi na ubunifu katika fani za umeme wa majumbani, ufundi wa magari, uundaji na uungaji vyuma, ujenzi (useremala, uashi na bomba), kilimo, mifugo, upishi, na ushonaji imetolewa kwa vijana 315 sawa na asilimia 79 ya lengo kwa kozi za muda mrefu. Aidha, kwa upande wa kozi za muda mfupi, elimu ya ujasiriamali na udereva ilitolewa kwa wahitaji 154.

3.20 Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa

137. ***Mheshimiwa Spika***, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa ilipanga kukusanya marejesho ya mikopo yenye jumla ya shilingi bilioni 1.25; Kukusanya michango ya shilingi bilioni 2.62; Kutoa mikopo kwa Halmashauri zitakazokidhi vigezo vya kukopeshwa na kufanya uwekezaji kwenye Taasisi za fedha, Kukamilisha mapitio ya sheria ili kuboresha utendaji wa Bodi; Kutoa mafunzo kwa ajili ya kuboresha usimamizi na utoaji wa mikopo katika mamlaka za serikali za mitaa na kuweka mikakati ya kuboresha mtaji kwa kuandika maandiko ili kupata fedha kwa ajili ya kuongeza Mtaji. Hadi kufikia Machi, 2025 Bodi imetekeleza shughuli zifuatazo;

(i) Ufuatiliaji wa Marejesho ya mikopo yenye jumla ya shilingi bilioni 1.25 umefanyika kwenye Halmashauri saba (7) kati ya Halmashauri 10 zilizokopeshwa na Taasisi. Katika ufuatiliaji huo, jumla ya shilingi milioni 517.26 sawa na asilimia 41.22 ya lengo zilikusanywa kutoka Halmashauri za Manispaa ya Singida na Morogoro, Halmashauri ya Mji wa Mbinga na Halmashauri ya Wilaya za Kishapu, Ruangwa, Mlele na Mbinga. Aidha, Halmashauri ya Manispaa ya Singida imemaliza kulipa mkopo wake wa shilingi milioni 28, Pia Halmashauri ya Manispaa ya Songea na Halmashauri za Miji ya Kasulu na Makambako bado zinaendelea na utekelezaji wa miradi hivyo muda wa kuanza kurejesha bado haujafika;

(ii) Ufuatiliaji wa Mchango wa Akiba na Nyongeza ya Mtaji wenye jumla ya shilingi bilioni 2.62 umefanyika kwenye Halmashauri 40 kati ya Halmashauri 114 ambazo bado hazijakamilisha michango. Katika ufuatiliaji huo, jumla ya

shilingi milioni 73.77 sawa na asilimia 2.82 ya lengo zimekusanywa kutoka Halmashauri 10 za Manispaa ya Morogoro, Halmashauri ya Mji wa Bunda na Halmashauri ya Wilaya za Itilima, Ikungi, Bukoba, Makambako, Itigi, Rungwe, Songea na Urambo. Aidha, katika kipindi hiki, Halmashauri ya Wilaya za Njombe, Songea, Mbinga na Itigi ziliweza kukamlisha michango yao;

(iii) Bodi inaendelea na marekebisho ya sehemu ya (V) ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura ya 290 inayohusu usimamizi na uendeshaji wa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa;

(iv) Bodi imewekeza shilingi milioni 827.00 kwenye Soko la Hisa kwenye Benki ya CRDB ambapo inatarajia kupata gawio la wastani wa shilingi milioni 65.00 kwa mwaka; na

(v) Bodi imeidhinisha mikopo yenye jumla ya shilingi milioni 537.21 ambapo shilingi milioni 270.00 ni kwa ajili ya mradi wa kiwanda cha kutengeneza kuni mbadala kwa ajili ya kupikia kwa Halmashauri ya Wilaya ya Nyangh'wale na shilingi milioni 267.21 ni mkopo wa nyongeza kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Soko la Kisasa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo.

3.21 Tume ya Utumishi wa Walimu

138. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2025 Tume imetumia shilingi bilioni 16.04 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zifuatazo;

(i) Wilaya 139 zilifanya vikao viwili (2) vya kisheria kila wilaya, ambapo jumla ya tuhuma za kinidhamu 1,379 zilipokelewa na mamlaka ya nidhamu ngazi ya wilaya kutoka kwa waajiri. Kati ya mashauri hayo, mashauri ya nidhamu 1,141 yalifanyiwa uchunguzi na mashauri 238 yapo katika hatua mbalimbali za maamuzi;

(ii) Vikao vitatu (3) vya kisheria vilifanyika ambapo rufaa 64 zilitolewa uamuzi;

(iii) Walimu 158,916 walipandishwa vyeo sawa na asilimia 214 ya waliokasimiwa. Vilevile, walimu 2,358 walibadilishiwa muundo baada ya kujiendeleza kati ya walimu 5,027 walioomba;

(iv) Mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi makao makuu unaendelea na umefikia asilimia 51 ya utekelezaji;

(v) Usimikaji wa miundombinu ya TEHAMA kwenye ofisi 139 za wilaya umekamilika;

(vi) Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu wanaoajiriwa kwenye Utumishi wa Umma umeandaliwa na kukamilika; Mwongozo huu unatarajia kusambazwa kwa walimu wapya 14,648;

(vii) Uandaaji wa mwongozo wa mafunzo kwa ajili ya kuwajengea uwezo watumishi wa tume katika uendeshaji wa mashauri ya nidhamu na rufaa kwa walimu umekamilika; na

(viii) Kutoa mafunzo ya kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu kwenye wilaya 34 za mikoa 13; wakuu wa shule 3,066 kati ya 17,463 walishiriki mafunzo kuhusu haki, wajibu, miiko na maadili ya kazi ya ualimu ambao ni mamlaka ya nidhamu katika ngazi ya shule; wajumbe tisa (9) wa tume na wajumbe 417 wa kamati za wilaya walijengewa uwezo ili waweze kutekeleza majukumu yao baada ya kuteuliwa; Wajumbe 14 wa menejimenti ya tume walipatiwa mafunzo ya uongozi na utawala bora.

SEHEMU YA NNE

4.0 Makadirio ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26

139. ***Mheshimiwa Spika,*** Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mwaka 2025/26, yamezingatia Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26; Mipango Mikakati ya Taasisi; Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati akilihutubia Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021; Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26; Sheria ya Bajeti Sura 439; Sera za Kisekta; Maelekezo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; malengo yaliyomo katika Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26; na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

4.1 Vipaumbele vya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26 Fungu Namba 56

140. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepanga kutekeleza Mpango na Bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:

(i) Kusimamia shughuli za utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma (D by D);

(ii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa Huduma za jamii;

(iii) Kuratibu na kusimamia mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato na kudhibiti matumizi yasiyo na tija katika ngazi zote;

(iv) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mikoa, mamlaka za serikali za

mitaa na taasisi zinazosimamiwa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI;

(v) Uratibu wa usimamizi wa mifumo ya TEHAMA;

(vi) Kuendeleza rasilimali watu katika ngazi zote za Ofisi ya Rais - TAMISEMI;

(vii) Kuratibu na kusimamia shughuli za kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa;

(viii) Kuratibu na kushiriki michezo ya shule za msingi (UMITASHUMTA), sekondari (UMISSETA) na mashindano ya michezo ya shule za sekondari za Afrika Mashariki;

(ix) Kuratibu shughuli za utendaji wa kazi wa taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI;

(x) Kuratibu na kusimamia ujenzi wa miradi ya maendeleo katika ngazi zote za Ofisi ya Rais - TAMISEMI;

(xi) Kuratibu uibuaji wa miradi ya kimkakati na miradi inayopaswa kutekelezwa kwa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika mamlaka za serikali za mitaa;

(xii) Kusimamia na kuratibu shughuli za utunzaji wa mazingira na uhifadhi wa maliasili katika mikoa na mamlaka za serikali za mitaa;

(xiii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa afua za mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa utalii, uhamasishaji wa nishati safi ya kupikia na uendelezaji wa Biashara ya Kaboni katika mikoa na mamlaka za serikali za mitaa; na

(xiv) Kuratibu shughuli za uendelezaji wa vijiji na miji kwenye mamlaka za serikali za mitaa.

4.2 Vipaumbele vya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26 Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Na. 2

141. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Utumishi wa Walimu inatarajia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo;

(i) Kusimamia ajira, maadili, nidhamu na maendeleo ya walimu kwa kuhakikisha walimu wanasajiliwa, kwa wale wenye sifa wanathibitishwa kazini na wanapandishwa vyeo/wanabadilishiwa vyeo kwa wakati kwa walimu wa shule za msingi na sekondari katika utumishi wa umma;

(ii) Kufanya utafiti na kutathmini hali ya walimu nchini;

(iii) Uwezeshaji wa matumizi ya mifumo ya TEHAMA;

(iv) Kuboresha utunzaji wa nyaraka na kumbukumbu za walimu;

(v) Kuwajengea uwezo watumishi wa tume; na

(vi) Kuwezesha mazingira bora ya kufanyia kazi.

4.3 Vipaumbele vya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26 Mafungu 26 ya Mikoa ikijumuisha Halmashauri 184

142. ***Mheshimiwa Spika,*** ofisi za wakuu wa mikoa zinatarajia kutekeleza vipaumbele mbalimbali kama ifuatavyo:

(i) Usimamizi wa masuala ya usalama;

(ii) Uimarishaji wa utawala bora, uwajibikaji na uwazi kwa kufanya vikao vyote vya kisheria;

(iii) Uratibu na usimamizi wa utoaji wa huduma za jamii;

(iv) Uratibu wa uwezeshaji wananchi kiuchumi;

(v) Uboreshaji wa mazingira ya kufanyia kazi na makazi ya viongozi na watumishi wa mikoa na wilaya;

(vi) Uendelezaji wa rasilimaliwatu katika mikoa;

(vii) Kusimamia na kuratibu miradi inayotekelezwa kwa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika mamlaka za serikali za mitaa;

(viii) Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

(ix) Kusimamia na kuratibu shughuli za utunzaji wa mazingira na uhifadhi wa maliasili katika mamlaka za serikali za mitaa;

(x) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa afua za mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa utalii, uhamasishaji wa nishati safi ya kupikia na uendelezaji wa Biashara ya Kaboni katika mamlaka za serikali za mitaa;

(xi) Ufuatiliaji na utatuzi wa kero na malalamiko ya wananchi; na

(xii) Uratibu wa utekelezaji wa sera za kisekta.

143. ***Mheshimiwa Spika***, mamlaka ya serikali za mitaa zinatarajia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

(i) Kusimamia na kutoa huduma za jamii na shughuli za kiuchumi;

(ii) Kusimamia na kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani ya halmashauri;

(iii) Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji;

(iv) Kusimamia na kutekeleza miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi;

(v) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

(vi) Kuwezesha wananchi kiuchumi;

(vii) Kuendeleza vijiji, miji na miji inayochipukia;

(viii) Kuimarisha huduma za ugani na ushirika;

(ix) Kusimamia na kuratibu shughuli za utunzaji wa mazingira na uhifadhi wa maliasili katika ngazi za msingi;

(x) Kutekeleza afua za mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa utalii, uhamasishaji wa nishati safi ya kupikia na uendelezaji wa Biashara ya Kaboni katika ngazi za msingi;

(xi) Kutambua na kuwapanga wafanyabiashara ndogondogo;

(xii) Ukamilishaji wa miradi viporo iliyoanzishwa na nguvu za wananchi;

(xiii) Kulipa madeni ya watumishi na wazabuni;

(xiv) Kuanzisha miradi mikubwa inayotekelezwa na mapato ya ndani ya halmashauri;

(xv) Ulipaji wa madeni na michango ya mikopo ya Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa pamoja na mkopo wa KKK; na

(xvi) Kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji.

4.4 Makadirio ya Kodi ya Majengo, Maduhuli na Mapato ya Ndani ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri Mwaka 2025/26

144. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2025/26, Taasisi za Ofisi ya Rais - TAMISEMI, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa zinakadiria kukusanya kodi ya majengo, maduhuli na mapato ya ndani ya shilingi trilioni 1.92 ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.60 iliyoidhinishwa Mwaka 2024/25, sawa na ongezeko la shilingi bilioni 324.83 au asilimia 20.29. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 56.10 ni za taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, shilingi milioni 306.07 ni Maduhuli ya Mikoa na shilingi trilioni 1.68 ni za mapato ya ndani ya halmashauri (***Kiambatisho Na. 4).***

145. ***Mheshimiwa Spika,*** shilingi bilioni 188.96 ni Kodi ya Majengo ambayo itakusanywa na mamlaka za serikali za mitaa ambazo zimepewa uwakala wa kukusanya kodi hiyo na kuwasilisha makusanyo hayo Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

4.5 Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Mafungu 28) kwa Mwaka wa Fedha 2025/26

146. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2025/26, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zilizo chini yake (Fungu Na. 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2) na Mafungu 26 ya Mikoa (yakijumuisha Halmashauri 184) yanaomba kuidhinishiwa shilingi trilioni 7.83 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Mishahara ni shilingi trilioni 6.29 na Matumizi Mengineyo shilingi trilioni 1.54 yanayojumuisha shilingi trilioni 1.06 za mapato ya ndani ya halmashauri (***Kiambatisho Na. 4).***

4.6 Makadirio ya Mpango na Bajeti ya Maendeleo ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI (Mafungu 28) kwa Mwaka 2025/26

147. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2025/26, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zilizo chini yake (Fungu Na. 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2) na Mafungu 26 ya Mikoa (yakijumuisha Halmashauri 184) inaomba kuidhinishiwa shilingi trilioni 3.94 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo,

shilingi trilioni 2.49 ni fedha za ndani ikijumuisha shilingi bilioni 613.44 za mapato ya ndani ya halmashauri (***Kiambatisho Na. 4)*** na shilingi trilioni 1.44 ni fedha za nje. Fedha hizi zimepangwa kutekeleza miradi na program mbalimbali.

4.7 Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Mafungu 28) kwa Mwaka 2025/26

(i) Shughuli zitakazotekelezwa kupitia Fedha za Mapato ya Ndani ya Halmashauri

148. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2025/26 Ofisi ya Rais – TAMISEMI imepanga kutumia shilingi bilioni 613.44 za mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya kuchangia utekelezaji wa shughuli za maendeleo kama ifuatavyo:

(a) Ujenzi wa hospitali za halmashauri tatu (3) katika Manispaa ya Temeke, Jiji la Ilala na Mwaza na ukamilishaji wa hospitali moja (1) katika Manispaa ya Kahama;
(b) Ujenzi wa vituo vya afya 28 na ukamilishaji wa vituo vya afya 72;
(c) Ujenzi wa zahanati 32 na ukamishaji wa zahanati 325;
(d) Ujenzi wa majengo matatu (3) ya *x-ray* katika vituo vya afya katika Halmashauri ya Wilaya za Kibaha (2), Geita (1) na ukamilishaji majengo matano (5) katika Halmashauri ya Jiji la Tanga (2), Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni (1), Halmashauri za Wilaya ya Mbarali (1) na Mufindi (1);
(e) Ujenzi wa wodi 15 na ukamilishaji wa wodi 49 katika vituo vya afya;
(f) Ujenzi wa jengo la huduma za dharura katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya na ujenzi wa Hosteli moja (1) ya wahudumu wa Afya Wilaya ya Mbinga,
(g) Ujenzi wa majengo 14 na ukamilishaji wa majengo 20 ya wagonjwa wa nje katika vituo vya afya;
(h) Ununuzi wa vifaa na vifaa tiba;

(i) Ujenzi wa vyumba vya madarasa 880 na ukamilishaji 1,919;

(j) Kuanza ujenzi wa shule za msingi tisa (9) na sekondari 40 mpya na ukamilishaji wa miundombinu katika shule mpya 52 ambapo msingi 32 na sekondari 20 na ukarabati wa shule nne (4) za sekondari;

(k) Ujenzi wa matundu ya vyoo 4,125 na ukamilishaji 1,528 katika shule za msingi na sekondari;

(l) Ujenzi wa hosteli 10 na ukamilishaji 10, ujenzi wa mabweni 12 na ukamilishaji 52, ujenzi wa ofisi za walimu tano (5) na ukamilishaji 60, utengenezaji wa viti na meza 47,979, madawati 71,482, ujenzi wa maabara 105 na ukamilishaji 194, ukamilishaji wa maktaba 15, ujenzi wa Mabwalo manne (4) na ukamilishaji 11 na ununuzi wa vitanda 504;

(m) Ujenzi wa barabara kilomita 1,028.02 ambapo kilomita 15.92 kwa kiwango cha lami nyepesi na kilomita 1,012.1 kwa kiwango cha changarawe, kuchonga mifereji yenye urefu wa kilomita 806.32 ununuzi wa mitambo 11 kwa ajili ya kufanya matengenezo ya miundombinu ya barabara, ujenzi wa daraja moja (1), makalavati mawili (2), vivuko 29 vya waenda kwa miguu na ujenzi wa taa za barabarani 590;

(n) Ulipaji wa fidia kwa wanachi 504 katika maeneo yatakayotwaliwa na serikali kwa ajili ya kupisha ujenzi wa miundombinu.;

(o) Upimaji wa viwanja 7,538, kuandaa michoro ya mipango miji na mipango kabambe, kufanya matumizi bora ya ardhi, kurasimisha makazi yaliyojengwa kiholela, kuendeleza zoezi la kuandaa anuani za makazi na ununuzi wa vifaa vya upimaji wa ardhi na utoaji wa hatimiliki 6,711;

(p) Ujenzi wa vitega uchumi 16 na uendelezaji wa vitega uchumi 18. Baadhi ya vitega uchumi hivyo ni; ujenzi wa bandari kavu katika Jiji la Tanga, vituo vya mafuta, kituo cha kibiashara Jiji la Arusha, ununuzi wa eneo la uwekezaji na uwanja wa mpira

Manispaa ya Kinondoni, ujenzi wa eneo la biashara Sinza Manispaa ya Ubungo na Manispaa ya Iringa. Ujenzi wa viwanda saba (7) na ukamilishaji wa viwanda 21, ujenzi wa machinjio matatu (3) na ukamilishaji na ukarabati wa machinjio 120, ujenzi wa minada 16 na uendelezaji wa minada 19, ujenzi wa masoko 26 na uendelezaji wa masoko 130, ujenzi wa vituo vya mabasi 32 na uendelezaji wa vituo 68 na ujenzi wa vibanda vya biashara 512 kwa ajili ya wafanyabiashara wakubwa, wakati na wadogo;

(q) Ujenzi wa nyumba za viongozi na watumishi 80 na ukamilishaji wa nyumba 358, ununuzi wa magari 99, pikipiki 114, bajaji 27, boti 12, lori sita (6) na trekta tano (5). Ulipaji wa madeni ya wazabuni ya miaka ya nyuma, ujenzi wa ofisi za watendaji wa kata 211, vijiji 88, mitaa 78, ujenzi wa majengo mawili (2) ya utawala katika Jiji la Dodoma na Arusha, ujenzi wa vituo vya polisi vya kata 35 na uendelezaji vituo 36 na ukarabati wa majengo 69 ya utawala; na

(r) Uanzishaji wa mashamba 188 na mashamba darasa 88 katika halmashauri, kuanzisha skimu 18 za umwagiliaji, kuimarisha huduma ya ugani kwa kutoa mafunzo kwa wakulima, wavuvi na wafugaji, kutoa mbegu tani 142,917 kwa wakulima wa mazao ya kimkakati, kugawa miche 90,508 ya mazao ya biashara kwa wakulima, ujenzi wa majosho 66, mabanio 34, ujenzi wa malambo mawili (2) katika Halmashauri ya Manispaa ya Geita na kuanzisha maeneo ya malisho kwa ajili ya mifugo.

149. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa miradi hiyo utaboresha upatikanaji wa huduma mbalimbali kwenye mamlaka za serikali za mitaa ikiwemo afya, elimu, barabara, kilimo, mifugo, uvuvi na kurahisisha uendeshaji wa shughuli mbalimbali za serikali na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi.

(iii) **Uratibu na Usimamizi wa Huduma za Afya ya Msingi, Ustawi wa Jamii na Lishe**

150. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2025/26, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepanga kutumia shilingi bilioni 502.09 za ruzuku ya matumizi mengineyo, fedha za maendeleo za Serikali Kuu na washirika wa maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali.

151. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na:

(a) Kuendelea na ujenzi wa hospitali za halmashauri 43;

(b) Ununuzi wa vifaa tiba katika hospitali za halmashauri 142, vituo vya afya 184 na zahanati 184;

(c) Kutoa chanjo kwa watoto chini ya miaka mitano (5), kutoa vitamin A na madini ya chuma kwa wajawazito katika halmashauri 184, kuratibu Mkakati wa Kimataifa wa 95-95-95 (asilimia 95 ya watu wanaoishi na VVU wanajua hali zao za VVU, asilimia 95 ya watu wanaojua hali zao wanapata matibabu ya kurefusha maisha na asilimia 95 ya watu wanaopata matibabu wamevifubaza virusi hivyo) kwa lengo la kutokomeza UKIMWI, kutoa vyandarua kwa watoto chini ya miaka mitano (5) na wajawazito katika halmashauri 184;

(d) Kutoa huduma za lishe zilizoainishwa kwenye Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe (2020/21 - 2025/26) kwa makundi yote ya jamii wakiwemo wanawake walio katika umri wa uzazi, akinamama wajawazito na wanaonyonyesha, watoto, vijana, wanaume na wazee;

(e) Usimamizi shirikishi wa utekelezaji wa huduma endelevu za maji na usafi wa mazingira vijijini katika mikoa 25 na halmashauri za wilaya 137 kupitia Programu ya Usafi wa Maji na Mazingira;

(f) Usimamizi na uratibu wa utoaji wa huduma za chanjo katika halmashauri 184 kupitia Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Utoaji wa Huduma za Chanjo;

(g) Ufuatiliaji wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za afya kupitia Programu ya Kuimarisha Mifumo ya Afya;

(h) Kuratibu na kusimamia Utekelezaji wa Mafunzo Jumuishi ya Kitaifa ya Ukuaji wa Awali wa Mtoto kwa halmashauri 184;

(i) Kuwajengea uwezo wataalamu wa ustawi wa jamii kuhusu usimamizi wa kesi za ulinzi wa mtoto katika halmashauri 184 ili kuboresha huduma za ulinzi wa watoto;

(j) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa afua za lishe kwenye mikoa na mamlaka za serikali za mitaa, kwa kuwajengea uwezo watumishi kuhusu kupanga na kusimamia bajeti za huduma za lishe, kuwajengea uwezo watendaji wa kata na vijiji/mitaa na kutathmini utekelezaji wake;

(k) Kuwezesha upatikanaji wa watumishi 400 wa mkataba watakaofanya kazi katika vituo vya kutolea huduma za afya, kuratibu ujenzi na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya 175 (hospitali 25, vituo vya afya 50 na zahanati 100) na ununuzi wa vifaa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma ya afya ya msingi 175 (hospitali 25, vituo vya afya 50 na zahanati 100) vitakavyokarabatiwa au kujengwa kupitia Programu ya Uwekezaji katika Afya ya Mama na Mtoto Tanzania (Tanzania Maternal Child Health Investment Programme - TMCHIP); na

(l) Kutoa mafunzo kazini kwa watumishi wa vituo vya kutolea huduma za afya, kufanya usimamizi shirikishi katika afua za UKIMWI, kifua kikuu na malaria katika

halmashauri 184 kupitia Programu ya Kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria (Global Fund).

(iv) **Usimamizi na Uendeshaji wa Elimumsingi na Sekondari**

152. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2025/26, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepanga kutumia shilingi trilioni 1.44 za ruzuku ya matumizi mengineyo, fedha za maendeleo za serikali kuu na washirika wa maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli katika sekta ya elimu.

153. ***Mheshimiwa Spika,*** Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na:

(a) Ujenzi wa madarasa 8,402 kati ya hayo 8,057 ni shule za msingi na 345 ni sekondari, matundu ya vyoo 19,095, umaliziaji wa maboma ya maabara 350; mabweni 129 kwenye shule za sekondari na maboma ya madarasa 700 shule za msingi;

(b) Ujenzi wa shule mpya 184 za sekondari, nyumba za walimu 211 (*two in one*). Kati ya hizo 184 ni za sekondari na 27 za msingi;

(c) Ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwenye shule za sekondari 400;

(d) Ununuzi wa vifaa na kemikali za maabara katika shule mpya 300 za sekondari;

(e) Utoaji wa ruzuku ya Elimu Bila Ada kwa shule za msingi 18,055 na sekondari 4,905;

(f) Ununuzi wa vifaa saidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu na vifaa vya elimu ya awali katika halmashauri 184;

(g) Uratibu na usimamizi wa shughuli za mitihani katika mikoa yote 26;

(h) Kutoa mafunzo endelevu ya walimu kazini (MEWAKA) kwenye shule za awali na msingi kwenye halmashauri 184;

(i) Kutekeleza mpango wa shule salama kwenye shule za awali na msingi 1,500;

(j) Kuanzisha madarasa janja (*smart classes*) saba (7) kwa ajili ya ufundishaji mubashara katika shule za sekondari saba (7) Halmashauri za Manispaa ya Mpanda moja (1), Kigoma moja (1), Sumbawanga moja (1), Shinyanga moja (1), Geita moja (1) na Halmashauri za Wilaya za Pangani moja (1), na Mbinga moja (1); na

(k) Kuratibu michezo ya shule za msingi (UMITASHUMTA), sekondari (UMISSETA) na mashindano ya michezo ya shule za sekondari za Afrika Mashariki (FEASSA).

(v) **Utawala Bora, Usimamizi wa Rasilimali, Ujenzi wa Majengo ya Utawala na Makazi ya Viongozi**

154. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2025/26, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepanga kutumia shilingi bilioni 204.90 kwa ajili ya: Ununuzi wa magari ya viongozi wa mikoa, wilaya na halmashauri; Ujenzi, ukarabati na ukamilishaji wa miundombinu ya mikoa, wilaya, halmashauri na tarafa ikiwemo majengo ya utawala, ikulu ndogo na makazi ya viongozi.

155. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na:

(a) Ununuzi wa magari 91 ya viongozi, kati ya magari hayo, magari 6 ya Wakuu wa Mikoa ya Simiyu, Geita, Arusha, Dodoma, Ruvuma, Kagera; magari 11 ya Makatibu Tawala wa Mikoa ya Simiyu, Geita, Arusha, Dodoma, Lindi, Mara, Morogoro, Mwanza, Tabora, Tanga, Kagera; gari moja (1) la katibu tawala msaidizi Mkoa wa Lindi; magari mawili (2) ya Wakuu wa Wilaya za Temeke na Ubungo; magari 71 ya wakurugenzi wa halmashauri. Lengo la ununuzi wa magari haya ni kuongeza ufanisi katika usimamizi na utekelezaji wa

shughuli za serikali katika maeneo yao ikiwemo ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo na utatuzi wa kero za wananchi; na

(b) Ujenzi wa ofisi za wakuu wa mikoa minne (4), ukarabati wa ofisi za wakuu wa mikoa 12, ukamilishaji wa Ofisi za wakuu wa mikoa minne (4); ujenzi wa ofisi za wakuu wa wilaya 31, ukamilishaji wa ofisi za wakuu wa wilaya 11, ukarabati wa ofisi za wakuu wa wilaya 26, ujenzi/ukarabati wa ikulu ndogo sita (6); ujenzi wa nyumba za wakuu wa mikoa miwili (2), ukamilishaji wa nyumba za wakuu wa mikoa minne (4), ukarabati wa nyumba za wakuu wa mikoa minne (4); ujenzi wa nyumba za makatibu tawala wa mikoa mitano (5), ukamilishaji wa nyumba za makatibu tawala wa mikoa mitatu (3), ukarabati wa nyumba za makatibu tawala wa mikoa sita (6), ukamilishaji wa nyumba za makatibu tawala wasaidizi wanne (4), ukarabati wa nyumba za makatibu tawala wasaidizi wa mikoa minne (4); ujenzi wa nyumba za wakuu wa wilaya 20, ukamilishaji wa nyumba za wakuu wa wilaya 12, ukarabati wa nyumba za wakuu wa wilaya 26, ukamilishaji wa nyumba za makatibu tawala wa wilaya tisa (9), ukarabati wa nyumba za makatibu tawala wa wilaya 18; ukamilishaji wa ofisi za tarafa 11, ukarabati wa ofisi za tarafa 18, ukarabati wa nyumba za maafisa tarafa tatu (3); ujenzi wa majengo 16 mapya ya utawala, ukamilishaji wa majengo 85 ya utawala, ununuzi wa samani katika majengo 38 ya halmashauri; ujenzi wa nyumba moja (1) ya mkurugenzi na ukamilishaji wa nyumba 83 za wakurugenzi na ujenzi wa nyumba 46 za wakuu wa idara na ukamilishaji nyumba saba (7) za wakuu wa idara.

(vi) **Ufuatiliaji na Tathmini**

156. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2025/26 Ofisi ya Rais - TAMISEMI, mikoa na halmashauri imepanga kutumia shilingi bilioni 18.57 kwa ajili ya ufuatiliaji na tathimini wa shughuli zitakazotekelezwa katika ngazi zote ili kubaini mafaniko na changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji na kuweka mikakati ya utatuzi wa changamoto

hizo. Hii itasaidia miradi kutekelezwa kwa ubora na kuhakikisha inakuwa na thamani ya fedha.

(vii) **Fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa Majimbo ya Tanzania Bara**

157. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2025/26 Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepanga kutumia shilingi bilioni 15.99 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Majimbo ya Uchaguzi 214 ya Tanzania Bara.

(viii) **Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati**

158. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2025/26 Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepanga kutumia shilingi bilioni 44.85 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati. Kati ya fedha hizo shilingi 28.75 ni za utekelezaji wa miradi mipya 31 na shilingi bilioni 16.10 ni za miradi 19 inayoendelea.

(viii) **Ushirikishwaji wa Wananchi kupitia Mfumo wa O&OD Iliyoboreshwa**

158. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kuhamasisha wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo katika ngazi za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kwa kutumia Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo Ulioboreshwa. Aidha, mwaka 2025/26 mafunzo yatatolewa kwa wataalamu 184 waliopo ngazi ya kata katika kata 62 ili kujengea uwezo jamii ziweze kushiriki katika shughuli za maendeleo na kufanya mafunzo kwa vikosi kazi 1,288 katika halmashauri 184 na mikoa 26.

(ix) **Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu**

160. ***Mheshimiwa Spika,*** wote tunafahamu kuwa ***"Kila mkopo unahitaji mpango; bila mpango ni kama safari bila ramani"*** Mwaka 2025/26 shilingi bilioni 123.92 zimetengwa na mamlaka za serikali za mitaa kwa ajili ya utoaji wa mikopo kwa wanawake,

vijana na watu wenye ulemavu. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 18.35 zitakopeshwa kupitia Mfumo wa Kibenki katika halmashauri 10 za mfano ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Siha (Uchumi Commercial Benki), Bumbuli (NMB), Itilima (NMB) na Nkasi (CRDB); Halmashauri ya Jiji la Dodoma (NMB na CRDB) na Dar es Salaam (NMB na CRDB); Halmashauri ya Mji wa Newala (NMB) na Mbulu (CRDB); Halmashauri ya Manispaa ya Songea (NMB) na Kigoma (CRDB). Aidha, shilingi bilioni 105.57 zitatolewa kupitia Mfumo wa Serikali Ulioboreshwa kwa halmashauri 174 (***Kiambatisho Na. 5)***.

161. ***Mheshimiwa Spika,*** sehemu ya fedha hizo zitatumika kwa ajili ya utambuzi na uhamasishaji wa wananchi ili kuunda vikundi, utoaji wa mafunzo na ufuatiliaji wa vikundi kabla na baada ya kupata mikopo kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni ya 38(1) na (2) ya Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za Mwaka 2024.

(x) **Uendelezaji Vijiji na Miji**

162. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2025/26 Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepanga kutumia shilingi bilioni 32.04 kwa ajili ya uendelezaji wa vijiji na miji.

163. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na:

(a) Kukamilisha mapitio ya muundo wa Mji wa Dar es Salaam uendane na ukuaji wake kijiografia na kiuchumi ili kuwa Jiji Kuu (*Metropolitan Assembly*) lenye utawala na uendeshaji;

(b) Kuratibu utekelezaji wa Mpango Kabambe Jumuishi wa Jiji la Kibiashara na Uwekezaji la Kwala, Mkoa wa Pwani;

(c) Kukamilisha mapendekezo ya rasimu ya Sera ya Maendeleo Vijijini na Mijini;

(d) Kusimamia uendelezaji wa Miji Midogo Inayochipukia 101 na vijiji vya mfano 284 vilivyoainishwa katika kutekeleza mpango wa kuiendeleza miji ya aina hiyo;

(e) Kuzisimamia mamlaka za serikali za mitaa kutumia Mfumo wa Taarifa za Kijiografia (*Geographical Information System* - GIS) ili ziweze kutambua hali halisi ilivyo kwa wakati husika ya uendelezaji uliopo na mali asilia zilizopo uwandani;

(f) Kusimamia uendelezaji wa Jiji la Dodoma likiwa ndiyo makao makuu ya nchi;

(g) Kufanya mapitio ya Mwongozo wa Utoaji wa Vibali vya Ujenzi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2018 ili kudhibiti ujenzi holela;

(h) Kudhibiti uendelezaji wa ardhi kwa kutoa vibali vya ujenzi kupitia Mfumo wa kielektroniki wa TAUSI;

(i) Kuwezesha ukusanyaji wa takwimu kwa mfumo wa kijiografia kwa ajili ya uimarishaji wa ukusanyaji wa mapato ya ndani;

(j) Kuwezesha usimamizi wa uthamini wa majengo kwenye halmashauri 184;

(k) Kuwezesha ukusanyaji wa taarifa za maeneo ya ukanda wa kijani, maeneo ya wazi na maeneo ya umma kwa mfumo wa kijiografia;

(l) Kuwezesha upatikanaji wa leseni, michoro na picha za anga kwa ajili ya mifumo ya GIS kwenye halmashauri;

(m) Kuwezesha usimamizi wa mazoezi ya uwandani ya uthamini na ukadiriaji wa kodi za majengo, ardhi na mabango;

(n) Uboreshaji wa miundombinu ya masoko na mialo ya samaki katika Halmashauri za Majiji ya Mwanza na Tanga na Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela; na

(o) Utoaji wa elimu kwa makundi mbalimbali ya jamii ya Mwanza na Tanga, ujasiriamali na kutoa mikopo yenye riba nafuu kama mitaji kwa Wananchi wa Mwanza na Tanga.

(x) **Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)**

164. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2025/26, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepanga kutumia shilingi trilioni 1.18 kwa ajili ya ujenzi, matengenezo, ukarabati wa miundombinu ya barabara na usafiri na usafirishaji wa vijijini na mijini. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 257.03 ni za Mfuko wa Barabara, shilingi bilioni 127.50 Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali, shilingi bilioni 325.77 ni za tozo ya mafuta ya petroli na dizeli ya shilingi 100 kwa lita na shilingi bilioni 423.79 ni fedha za nje.

165. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zitakazotekelezwa ni:

(a) Ukamilishaji wa miundombinu ya barabara kwa kiwango cha lami kilomita 33 katika Halmashauri za Wilaya za Iringa (Wenda – Mgama kilomita 19) na Mufindi (Mtili – Ifwagi kilomita 14);

(b) Kuanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kilomita 33 kwa awamu ya pili katika Halmashauri za Wilaya za Handeni, Ruangwa na Mbogwe. Kazi zitakazofanyika ni ujenzi wa barabara na mitaro, uwekaji wa taa za barabarani, ujenzi wa maeneo ya kupaki bodaboda na magari ya abiria pamoja na maeneo ya waenda kwa miguu;

(c) Matengenezo ya barabara kilomita 23,105.78 kupitia Mfuko wa Barabara, Kalavati aina ya boksi 23, makalavati aina ya mabomba ya zege mistari 1,647, drift 2, na mifereji ya maji ya mvua mita 73,405, barabara za

lami kilomita 17, barabara za changarawe kilomita 108.8 na madaraja 2. Kazi hizi zitafanyika katika wilaya 139 Tanzania Bara.

(d) Ujenzi wa barabara kilomita 91.97 kwa kiwango cha lami, kilomita 2,621.40 za changarawe, madaraja 85, boksi kalavati 91, mitaro ya maji ya mvua mita 10,989, drift tano (5), mistari ya kalavati 666 na taa za barabarani 345 katika wilaya 139 Tanzania Bara;

(e) Ujenzi wa barabara kilomita 252.42 kwa kiwango cha lami, kilomita 6,939.41 za changarawe, madaraja 51, boksi kalavati 336, mistari ya kalavati 1,719, drift 2, na mifereji ya maji ya mvua mita 63,836 katika wilaya 139 Tanzania Bara;

(f) Kuendelea na ujenzi wa barabara za lami kilomita 147.50 kwenye miji 12 ya Fungu la Kwanza la Mradi wa TACTIC;

(g) Kuendelea na ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua mita 24,600;

(h) Kuendelea na ujenzi wa masoko tisa (9) katika Majiji ya Mwanza, Mbeya, Arusha, Dodoma, na Manispaa za Songea, Ilemela, Kigoma, Tabora na Kahama;

(i) Kuendelea na ujenzi wa stendi kuu nne (4) za mabasi katika Halmashauri za Majiji ya Arusha, Mbeya na Manispaa za Kahama na Geita na stendi ndogo mbili (2) katika Jiji la Dodoma na Manispaa ya Morogoro;

(j) Kuendelea na ujenzi wa maghala mawili (2) ya kuhifadhia mazao katika Manispaa za Sumbawanga na Songea;

(k) Kuanza ujenzi kwenye Halmashauri za Miji 15 za Fungu la Pili la Mradi wa TACTIC;

(l) Kukamilisha mchakato wa maandalizi ya Mradi wa TACTIC Fungu la Tatu katika Halmashauri za Miji 18;

(m) Kuendelea na uboreshaji wa Bonde la Msimbazi lenye Hekta 5.7;

(n) Kuendelea na ujenzi wa karakana ya mabasi ya mwendo kasi katika eneo la Ubungo Maziwa;

(o) Kuendelea na ujenzi wa tuta kilomita 6.7 katika eneo la Bonde la Mto Msimbazi;

(p) Ujenzi wa Bohari Mpya ya BRT eneo la Ubungo Maziwa;

(q) Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya barabara awamu ya kwanza zenye jumla ya kilomita 132 katika Manispaa za Kinondoni, Ubungo, Temeke, Ilala na Kigamboni;

(r) Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya barabara awamu ya pili ya Mradi wa DMDP zenye urefu wa kilomita 118 kiwango cha lami katika Manispaa za Kinondoni, Ubungo, Temeke, Ilala na Kigamboni;

(s) Kuwasimamia wataalamu washauri wa *Traffic Management and Parking Study* na Utafiti wa Maegesho katika eneo la kibiashara katikati ya Jiji la Dar es Salaam; na

(t) Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwenye miradi yote ya maendeleo ikijumuisha miradi inayotekelezwa kupitia fedha za ndani katika ngazi ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na taasisi zilizo chini yake, mikoa 26 na halmashauri 184.

(xi) **Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam**

166. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam imepanga kutumia shilingi bilioni 4.83 kwa ajili ya

Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 4.10 kwa ajili ya Mishahara na shilingi milioni 731.21 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

167. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni:

(a) Kukamilisha taratibu za ununuzi wa mtoa huduma kwa njia ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ya uendeshaji wa mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Kwanza na ya Pili;

(b) Kuendelea na maandalizi ya usanifu na ujenzi wa miundombinu Awamu ya Tano (V) ya Barabara za Nelson Mandela, Mbagala na Tabata -Segerea – Kigogo zenye urefu wa kilomita 26;

(c) Kuendelea na ukarabati wa mara kwa mara wa miundombinu ya Mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT *system*) na ujenzi wa vituo mlishi (*feeder*);

(d) Kukamilisha ufungamanishaji wa mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji nauli *(Automated Fare Collection System-AFCS)* na mfumo wa kuongozea magari *(Intelligent Transport System-ITS)* ikiwa ni sehemu ya maboresho endelevu ya huduma hii kwa wananchi waishio Dar es salaam;

(e) Kufanya pembuzi yakinifu nne kwa ajili ya upanuzi wa miundobinu ya barabara za nyongeza za Mabasi Yaendayo Haraka za Mbagala Rangitatu – Vikindu (BRT 2) kilomita tano (5), Tegeta - Bunju (BRT 4) kilomita 13, Kimara – Kibaha (BRT1) kilomita 20 na kuunganisha BRT Awamu ya Kwanza na BRT Awamu ya Nne kupitia Barabara ya Mwai Kibaki kilomita saba 7(;) na

(f) Kufanya utafiti na kuibua vyanzo vipya vya mapato ya ndani kwa kuendeleza maeneo ya ushoroba wa mradi *(Transit Oriented Development)* ikiwemo ujenzi wa vitega

uchumi kwenye maeneo ya Mtoni kwa Aziz Ally na eneo la Kariakoo Gerezani.

(xii) **Shirika la Masoko ya Kariakoo**

168. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2025/26 Shirika la Masoko ya Kariakoo limepanga kutumia shilingi bilioni 1.90 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 1.51 kwa ajili ya Mishahara na shilingi milioni 388.22 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

169. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni:

(a) Kuboresha uendeshaji wa biashara wa kisasa kwa kutumia mifumo ya kidijitali itakayosaidia kutoa huduma bora kwa wafanyabiashara na wadau wa shirika;
(b) Kufanya uchunguzi wa udongo pamoja na kuandaa michoro ya majengo kwa ajili ya kuendelea na uwekezaji wa miradi ya kibiashara katika eneo la Mbezi Beach Makonde na Tabata Bima;
(c) Kuboresha utendaji wa shirika kwa kuimarisha rasilimaliwatu na kuhakikisha upatikanaji wa vitendea kazi kwa Watumishi;
(d) Kuwajengea uwezo watumishi wa shirika kupitia mafunzo mbalimbali;
(e) Kuendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato kikamilifu;
(f) Kuimarisha mahusiano na Mamlaka ya Mapato Tanzania, Taasisi za fedha, Taasisi ya kudhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania, Mamlaka ya Uthibiti wa Mbolea, Wizara ya Kilimo, Taasisi za utafiti na vyuo vya kilimo. Vyombo vya Usalama na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa; na
(g) Kuanzisha kituo cha kutolea Habari.

(xiii) **Chuo cha Serikali za Mitaa**

170. ***Mheshimiwa* Spika,** Chuo kimepanga kutumia shilingi bilioni 7.77 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi

bilioni 7.42 kwa ajili ya Mishahara na shilingi milioni 349.30 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

171. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni:

(a) Kudahili wanafunzi 9,300 kuanzia ngazi ya Astashahada hadi Shahada ya Kwanza;
(b) Kuanza kutoa mafunzo ya Shahada ya Kwanza ya Nyaraka na Kumbukumbu kwa kudahili wanafunzi 100 baada ya mtaala kukamilika;
(c) Kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa 40 na Taasisi tano (5) kupitia mafunzo ya muda mfupi ili kutoa huduma bora kwa wananchi;
(d) Kufanya tafiti sita (6) na machapisho 30 ya kitaaluma katika majarida mbalimbali yenye lengo la kuboresha utendaji katika mamlaka za serikali za mitaa na wadau wengine;

(e) Kufanya ukarabati wa mabweni manne (4) ya wanafunzi na nyumba saba (7) za watumishi ikiwa ni pamoja na miundombinu ya maji na umeme ambapo shilingi milioni 575 zimepangwa kutumika; na

(f) Kuendeleza watumishi 27 katika ngazi mbalimbali za elimu. Kati ya hao, Shahada ni watano (5), Uzamili 11 na Shahada ya uzamivu 11.

(xiv) **Shirika la Elimu Kibaha**

172. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Elimu Kibaha limepanga kutumia shilingi bilioni 9.51 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 7.94 kwa ajili ya Mishahara, shilingi bilioni 1.30 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi milioni 276 za Maendeleo.

173. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni:

(a) Kuendelea kutoa elimumsingi kwa wanafunzi 3,282 na elimu ya sekondari kwa wanafunzi 315;

(b) Kuboresha utoaji wa elimu kwa wahudumu wa afya 564 katika fani ya utabibu, uuguzi na ukunga; na uhudumu wa afya ngazi ya jamii kupitia Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Kibaha, sambamba na kutoa elimu ya afya dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza kwa wananchi 500;

(c) Kutoa elimu na mafunzo ya stadi mbalimbali za ujuzi na ubunifu katika fani za umeme wa majumbani, ufundi wa magari, uundaji na uungaji vyuma, ujenzi (useremala, uashi na bomba), kilimo, mifugo, upishi, na ushonaji kwa vijana 400 kwa kozi za muda mrefu na wananchi 500 kwa kozi za muda mfupi; na

(d) Kuendelea na ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha.

(xv) **Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa**

174. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imepanga kutumia shilingi milioni 756.26 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

175. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni:

(a) Kutoa mikopo kwa halmashauri zitakazokidhi vigezo vya kukopeshwa na kufanya uwekezaji kwenye taasisi za fedha ambapo shilingi bilioni 3.51 zitatumika;

(b) Kufanya ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo kwenye halmashauri zilizokopeshwa na bodi ili kukusanya marejesho ya mikopo ya shilingi bilioni 1.25;

(c) Kufanya ufuatiliaji wa ukusanyaji wa mchango wa akiba na nyongeza ya mtaji kwenye halmashauri 104 ambazo bado hazijakamilisha kuchangia mchango kwenye bodi ili kukusanya jumla ya shilingi bilioni 2.12;

(d) Kukamilisha mapitio ya sheria ili kuboresha utendaji wa bodi; na

(e) Kukamilisha taratibu za kuhuisha muundo wa bodi ikiwa ni pamoja na kuifanya bodi iwe taasisi inayojitegemea.

(xvi) **Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2)**

176. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2025/26, tume imepanga kutumia shilingi bilioni 21.84 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 11.79 kwa ajili ya Mishahara na shilingi bilioni 8.11 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, shilingi bilioni 1.94 ni fedha za Maendeleo.

177. **Mheshimiwa Spika,** shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni:

(a) Kutoa barua za ajira kwa walimu wapya 14,648;
(b) Kuhuisha Tange ya Walimu 273,736 kwenye wilaya 139 kutoka mamlaka za serikali za mitaa 184;
(c) Kuchambua taarifa za walimu 14,648 kwa ajili ya kuthibitishwa kazini, 79,777 kupandisha vyeo waliokasimiwa Mwaka 2024/25 na walimu 4,422 kubadilishiwa cheo/muundo baada ya kujiendeleza;
(d) Kuchapisha na kusambaza Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu 14,648;
(e) Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi za tume makao makuu; na
(f) Kuwajengea uwezo watumishi wa tume 509 na wajumbe 9 wa tume kuhusu uendeshaji wa mashauri ya nidhamu na rufaa.

178. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia fursa hii kuwaelekeza waheshimiwa wakuu wa mikoa kuwasimamia wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:

(a) Kuhakikisha ukusanyaji wa mapato unafikia malengo;

(b) Kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya afya ya msingi, elimumsingi na sekondari kulingana na mipango iliyowekwa;

(c) Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Uchumi wa Kidigitali ikiwemo uwekaji na matumizi ya mifumo na miundombinu ya TEHAMA katika mikoa na mamlaka za serikali za mitaa ikiwa ni pamoja na vituo vya huduma za afya na elimu;

(d) Kuhakikisha mapato katika mikoa na mamlaka za serikali za mitaa yanakusanywa kupitia mifumo ya TEHAMA ya Serikali pamoja na kufanya ufuatiliaji wa karibu wa mifumo hiyo ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato;

(e) Mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha inatekeleza Mikakati ya Uchumi wa Buluu, nishati safi ya kupikia na mabadiliko ya tabianchi na utunzaji wa mazingira;

(f) Mikoa na mamlaka za serikali za mitaa iendelee kuimarisha mifumo stahimilivu na endelevu ya utoaji wa huduma bora za afya, ustawi wa jamii na lishe ili kuboresha huduma ambayo ni nguzo muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote; na

(g) Wakuu wa mikoa na wakurugenzi wahakikishe watoto walio chini ya miaka mitano wanajiunga kwenye vituo vya jamii vya kulelea watoto wadogo mchana.

179. ***Mheshimiwa Spika***, kila halmashauri itapimwa utekelezaji wa vipaumbele hivi kwa kuzingatia miradi iliyotengewa bajeti kwa Mwaka 2025/26.

180. ***Mheshimiwa Spika***, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, nitumie fursa hii kuwashukuru wadau mbalimbali walioshirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kufanikisha utekelezaji wa mpango na bajeti ya 2024/25. Vilevile, ninawashukuru wadau wote ambao wametoa ahadi za kuchangia utekelezaji wa bajeti ya 2025/26

kwa mafungu 28. Wadau hao ni pamoja na: Benki ya Dunia, UNICEF, Global Fund, Twiga Barrick Tanzania, EU, JICA, KOICA, GiZ, UNCDF, CDC, SIDA, UNDP, UNFPA, UN Women, Carbon Tanzania, UNEP, WHO, AfDB, WWF, FCDO, DANIDA, CANADA, SDC SWISS, Shirika la Korea - KOFIH, Serikali ya Shirikisho la Ujerumani, Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kupitia *FOCAC*, *Global Facility Financing* na *GAVI*.

181. ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, ninawashukuru viongozi wa Chama Cha Mapinduzi katika ngazi zote kwa kutekeleza wajibu wao wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 katika maeneo yao, watendaji wote ngazi za msingi bila kusahau wenyeviti wa vitongoji, vijiji na mitaa, watendaji wa mitaa na vijiji, watendaji wa kata, maafisa tarafa, wakuu wa idara na vitengo, wakurugenzi wa halmashauri, makatibu tawala wa wilaya, waheshimiwa madiwani, waheshimiwa wabunge, wakuu wa wilaya, makatibu tawala wa mikoa, wakuu wa mikoa na watumishi wote wa tawala za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kwa utendaji kazi wao mzuri.

182. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mara nyingine ninawashukuru sana wananchi wa jimbo langu la Rufiji kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya kitaifa na jimbo na kuniombea kila siku. Ninaahidi kuendelea kuwatumikia na kushirikiana nao kila hatua katika kuleta maendeleo ya jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

183. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee, ninaishukuru kwa dhati familia yangu kwa upendo wao, uvumilivu na maombi yao wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yangu ya kitaifa. Ninawashukuru kwa kusimama nami katika safari hii ya kuleta maendeleo ya Taifa letu.

4.8 Makadirio ya Makusanyo ya Kodi ya Majengo, Maduhuli na Mapato ya Ndani kwa Mwaka 2025/26

184. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2025/26, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, taasisi zilizo chini yake, mikoa 26 ikijumuisha halmashauri 184 inaomba idhini ya kukusanya kodi ya majengo, maduhuli na

mapato ya ndani ya shilingi trilioni moja, bilioni mia tisa ishirini na tano, milioni mia nane themanini na moja, mia tatu ishirini na tatu elfu, mia nne sitini na nne (1,925,881,323,464.00).

185. ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya fedha hizo, shilingi bilioni hamsini na sita, milioni mia moja na nane, mia moja sabini na nne elfu na sitini na nne (56,108,174,064.00) ni mapato ya ndani ya taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, shilingi milioni mia tatu na sita, sabini na tisa elfu na mia nne (306,079,400.00) ni maduhuli ya mikoa na shilingi trilioni moja, bilioni mia sita themanini, milioni mia tano na sita, mia saba sitini na nne elfu (1,680,506,764,000.00) ni za mapato ya ndani ya halmashauri. Aidha, shilingi bilioni mia moja themanini na nane, milioni mia tisa sitini, mia tatu na sita elfu (188,960,306,000.00) ni kodi ya majengo ambayo itakusanywa na mamlaka za serikali za mitaa ambazo zimepewa uwakala wa kukusanya kodi hiyo na kuwasilisha makusanyo hayo Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ***Jedwali Na. 1.***

Jedwali Na. 1: **Makadirio ya Makusanyo ya Kodi ya Majengo, Maduhuli na Mapato ya Ndani kwa Mwaka 2025/26**

Ofisi/Taasisi	**Makadirio ya Makusanyo 2025/26**
Ofisi ya Rais - TAMISEMI	188,960,306,000.00
Taasisi	56,108,174,064.00
Mikoa	306,079,400.00
Halmashauri	1,680,506,764,000.00
Jumla Kuu	**1,925,881,323,464.00**

4.9 Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Mafungu 28) kwa Mwaka 2025/26

186. ***Mheshimiwa Spika,*** sasa naomba Bunge lako likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2025/26 yenye jumla ya shilingi trilioni kumi na moja, bilioni mia saba themanini na mbili, milioni mia tisa themanini na nne, mia mbili na mbili elfu (shilingi 11,782,984,202,000.00) kwa ajili ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na taasisi zilizo chini yake (Fungu Na. 56), Tume

ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2) na Mafungu 26 ya Mikoa (yakijumuisha Halmashauri 184).

187. ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya fedha zinazoombwa, shilingi trilioni saba, bilioni mia nane thelathini na sita, milioni mia moja arobaini, mia saba na nane elfu (shilingi 7,836,140,708,000.00) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida yanayojumuisha Mishahara shilingi trilioni sita, bilioni mia mbili tisini na mbili, milioni mia tano hamsini na saba, mia sita arobaini na nane elfu (shilingi 6,292,557,648,000.00) na Matumizi Mengineyo shilingi trilioni moja, bilioni mia tano arobaini na tatu, milioni mia tano themanini na tatu na sitini elfu (shilingi 1,543,583,060,000.00) ikijumuisha shilingi trioni moja, bilioni sitini na saba, milioni sitini na tano, mia tatu ishirini na nane elfu (shilingi 1,067,065,328,000.00) za mapato ya ndani ya halmashauri.

188. ***Mheshimiwa Spika,*** shilingi trilioni tatu, bilioni mia tisa arobaini na sita, milioni mia nane arobaini na tatu, mia nne tisini na nne elfu (shilingi 3,946,843,494,000.00) zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo kati ya fedha hizo shilingi trilioni mbili, bilioni mia nne tisini na nane, milioni mia tisa thelathini na moja, mia nne sabini na sita elfu (shilingi 2,498,931,476,000.00) ni fedha za ndani, ikijumuisha shilingi bilioni mia sita kumi na tatu, milioni mia nne arobaini na moja, mia nne thelathini na sita elfu (613,441,436,000.00) za mapato ya ndani ya halmashauri na shilingi trilioni moja, bilioni mia nne arobaini na saba, milioni mia tisa kumi na mbili na kumi na nane elfu (shilingi 1,447,912,018,000.00) ni fedha za nje ***Jedwali Na. 2.***

***Jedwali Na. 2:* Muhtasari wa Makadirio ya Mpango wa Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI Mwaka 2025/26**

Maelezo	Makadirio ya Bajeti 2025/26
Matumizi ya Kawaida	
Mishahara	
Makao Makuu	13,460,722,000.00
Taasisi	72,506,144,000.00
Tume ya Utumishi wa Walimu	11,792,001,000.00

Mikoa	90,577,132,000.00
Halmashauri	6,104,221,649,000.00
Jumla ndogo	**6,292,557,648,000.00**
Matumizi Mengineyo	
Makao Makuu	23,582,719,500.00
Taasisi	3,525,430,500.00
Tume ya Utumishi wa Walimu	8,110,307,000.00
Mikoa	119,332,530,000.00
Halmashauri – SK	321,966,745,000.00
Halmashauri – OS	1,067,065,328,000.00
Jumla Ndogo	**1,543,583,060,000.00**
Jumla Matumizi ya Kawaida	**7,836,140,708,000.00**
Matumizi ya Maendeleo	
Ndani	
Makao Makuu	6,724,914,000.00
Taasisi	710,592,035,000.00
Tume ya Utumishi wa Walimu	264,215,000.00
Mikoa	117,058,250,000.00
Halmashauri – SK	1,050,850,626,000.00
Halmashauri – OS	613,441,436,000.00
Jumla Ndogo	**2,498,931,476,000.00**
Nje	
Makao Makuu	144,441,979,794.00
Taasisi	423,798,057,206.00
Tume ya Utumishi wa Walimu	1,678,508,000.00
Mikoa	57,272,703,000.00
Halmashauri	820,720,770,000.00
Jumla Ndogo	**1,447,912,018,000.00**
Jumla Maendeleo	**3,946,843,494,000.00**
Jumla Kuu	**11,782,984,202,000.00**

SK - Serikali Kuu

OS - *Own Source*

189.***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na hotuba hii, yapo majedwali ambayo yamefafanua kwa kina makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa ajili ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na taasisi zilizo chini yake (Fungu Na. 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2) na mafungu 26 ya mikoa (yakijumuisha halmashauri 184).

190.***Mheshimiwa Spika,*** ninapohitimisha hotuba hii ya bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ninaomba tusimame pamoja si tu kama viongozi wa leo, bali kama warithi wa kesho tunaojenga Tanzania mpya kwa misingi ya uwajibikaji, ushirikishwaji na maendeleo yanayogusa maisha ya kila mtanzania kuanzia mjini hadi vijijini.

191.***Mheshimiwa Spika,*** leo hii tumewasilisha si tu makadirio ya mapato na matumizi, bali tumeweka mbele yetu dira ya matumaini, ramani ya maendeleo na ahadi ya uongozi unaowajibika. Kama alivyoandika Nelson Mandela:

"***Education is the most powerful weapon which you can use to change the world."*** Tumewekeza katika elimu kwa watoto wetu wote, bila ubaguzi.

Na Kama alivyosema John F. Kennedy:

"***Let us not seek the Republican answer or the Democratic answer, but the right answer***." TAMISEMI haitafuti sifa ya kisiasa, tunatafuta suluhisho sahihi kwa maisha ya mtanzania wa kawaida.

Na kama alivyosema Mwalimu Julius Kambarage Nyerere: "***Maendeleo Hayataletwa na Mtu Mmoja***. ***Maendeleo ni Kazi ya Pamoja***." Na hivyo, kwa kauli moja, tunatoa wito kwa mikoa, mamlaka za serikali za mitaa na wananchi wote: tushirikiane, tusonge mbele kwa mshikamano.

192.***Mheshimiwa Spika,*** kwa dhamira hii, na kwa imani kubwa katika maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunawasilisha bajeti hii kama zana ya kazi, dira ya matumaini na silaha ya mapinduzi ya

kiutawala, kiuchumi na kijamii. Kwa hiyo, tunasema kwa ujasiri mkubwa:

"TAMISEMI – Ndiyo Msingi wa Maendeleo Endelevu!"

"***Kila Shilingi ina Jukumu, Kila Kiongozi ana Wajibu na Kila Mwananchi ana Nafasi***!"

193. ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba hii inapatikana pia kwenye tovuti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI ambayo ni www.tamisemi.go.tz.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa kuwasilisha hoja hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, haya, wakati Mheshimiwa Waziri akiendelea kujikusanya sasa nimwite Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Justin Nyamoga aje awasilishe maoni ya Kamati.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea naomba taarifa yangu hii iingie katika Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa mezani.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ninatoa shukrani kwako kwa kunipa wasaa ili niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya

Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, maeneo muhimu yaliyoguswa na kuelekezwa katika taarifa hii ni kama ifuatavyo:-

(i) Maelezo na uchambuzi kuhusu ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na uzingatiaji wa Maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(iii) Uchambuzi wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa makadirio ya maduhuli na matumizi; na

(iv) Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, maelezo na uchambuzi kuhusu ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi trilioni 1.6 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 117 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ilitembelea na kukagua baadhi ya miradi hiyo ya maendeleo iliyotekelezwa na Ofisi hii katika mwaka wa fedha 2024/2025. Miradi iliyotembelewa ni miradi ya elimu, afya, masoko pamoja na barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)*.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata wasaa wa kutembelea na kukagua miradi katika Mikoa minne ya Kigoma, Kagera, Geita na Shinyanga ambako jumla ya miradi tisa (9) ilikaguliwa. Taarifa

zaidi kuhusu miradi hiyo inapatikana katika taarifa ya Kamati iliyowasilishwa mezani.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa na utekelezaji wa mpango wa bajeti na uzingatiaji wa maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Baada ya Wizara pamoja na Sekretarieti za Mikoa kuwasilisha bajeti zao kwa Mafungu 28 kuanzia tarehe 19 Machi, 2025 hadi 4 Aprili, 2025, Kamati ilipata wasaa wa kuchambua na kujadili. Pia, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maoni; katika taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni kuhusu bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo 13. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kwa kiasi kikubwa Serikali imetekeleza maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanyia kazi maoni na ushauri huo kama ulivyotolewa na Kamati. Aidha, kwa maeneo ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu, Kamati inaendelea kusisitiza yaendelee kutekelezwa kama yalivyooneshwa kwenye taarifa mbalimbali likiwemo suala la shule za mchepuo wa kiingereza.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Fungu 56 - Makao Makuu ya Wizara, Fungu Na.2 - Tume ya Utumishi wa Walimu na Mafungu 26 kutoka Sekretarieti za Mikoa katika mwaka wa fedha 2024/2025 ilikadiria kukusanya maduhuli ya shilingi trilioni 1.6. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni188.9 zilikadiriwa kukusanywa kutoka Makao Makuu ya Wizara, shilingi bilioni 1.6 zilikadiriwa kukusanywa kutoka Shirika la Elimu Kibaha; shilingi bilioni 21.5 zilikadiriwa kukusanywa kutoka Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka - *DART*; shilingi bilioni 10.5 zilikadiriwa kukusanywa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa; shilingi bilioni 4.1 kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa; shilingi bilioni 5.6 kutoka Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA);* shilingi bilioni 11.9 kutoka Shirika la Masoko ya Kariakoo; Shilingi milioni 315 kutoka Ofisi za Mikoa na shilingi trilioni 1.3 kutoka

katika Halmashauri. Kwa maelezo zaidi tazama kuna kielelezo kama tulivyowasilisha taarifa mezani.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitaarifiwa kwamba, hadi Februari 2025, Wizara na taasisi zake zilikusanya jumla ya shilingi bilioni 879.9 sawa na 54.95%. Maelezo zaidi kuhusu maakusanyo ya maduhuli yanapatikana katika taarifa ya Kamati iliyowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa kati ya taasisi zote zilizo chini ya TAMISEMI, Halmashauri za Wilaya ndizo zilizofanya vema kwenye makusanyo kwa kukusanya maduhuli kwa 60.3%. Aidha, Kamati imebaini kuwa Shirika la Masoko ya Kariakoo ndilo lililokusanya chini zaidi katika makusanyo ya maduhuli. Kamati ilihoji ili kufahamu sababu ya Shirika la Masoko ya Kariakoo kukusanya kiwango cha chini zaidi na kujulishwa kwamba ni kwa sababu ya soko hilo kuendelea na ujenzi baada ya kuungua.

Mheshimiwa Spika, matarajio ya Kamati ilikuwa TAMISEMI pamoja na taasisi zake kufikia 66% ya makusanyo ya maduhuli hadi Februari, 2025. Hata hivyo, hakuna hata taasisi moja iliyofikia kiwango hicho. Hali hii imeisababisha Kamati kuhoji uhalisia wa upangaji wa makusanyo ya maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Taarifa kamili zaidi kuhusu makadirio ya makusanyo ya maduhuli inapatikana kwenye taarifa ya Kamati iliyowasilishwa mezani.

Mheshimiwa Spika, utolewaji wa fedha za matumizi kwa mwaka 2024/2025. Katika bajeti ya mwaka 2024/2025 iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu Juni, 2024 Wizara kupitia Fungu Na. 56, Fungu Na. 02 pamoja na Mafungu yote 26 ya Mikoa iliidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 10.1 Kati ya fedha hizo shilingi trilioni 6.7 sawa na 66.3% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 3.6 sawa na 33% ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, matumizi ya kawaida ni shilingi trilioni 5.5 sawa na 82.3% ni kwa ajili ya mishahara na shilingi trilioni 1.1 sawa na 17.7% ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Februari, 2025 taasisi zake pamoja na Sekretarieti za Mikoa zimepokea jumla ya Shilingi trilioni

6.9 sawa na 67.7% ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 4.8 sawa na 68.4% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 2.2 sawa na 31.6% ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya shilingi trilioni 4.7 zilizoombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, shilingi trilioni 3.6 sawa na 76.3% ni kwa ajili ya matumizi ya mishahara na shilingi trilioni 1.1, sawa na 23.7% ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)*. Aidha, kati ya shilingi trilioni 2.2 za matumizi ya maendeleo zilizopelekwa, shilingi trilioni 1.8 sawa na 82.6% ni fedha za ndani na Shilingi bilioni 383 sawa na asilimia 17.4 ni fedha za nje. Taarifa zaidi kuhusu upokeaji wa fedha unapatikana kwenye taarifa ya Kamati kama ilivyowasilishwa mezani.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake wa randama za Wizara zilizowasilishwa mbele ya Kamati, Kamati imebaini kuwa kwa wastani upokeaji wa fedha hadi mwezi Februari, 2025 ni wa kuridhisha. Kamati imebaini kuwa upelekaji wa jumla wa fedha za Fungu Na. 56, Fungu Na.2 na Mafungu 26 ya Sekretarieti za Mikoa umefikia 67.68%, kiasi hiki ni zaidi ya 66% zilizokisiwa kuwa zimewasilisha hadi Februari, 2025. Kwa upelekaji huu wa fedha Kamati inaipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, mpango wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2025/2026. Kamati ilitaarifiwa kwamba, maandalizi ya mpango na bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka 2025, imezingatia mpango mkakati wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wa miaka mitano pamoja na mipango mingine. Kamati ilielezwa pia kuwa, katika Mwaka wa Fedha wa 2025/2026, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imepanga kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele mbalimbali ilivyojiwekea na hivyo kukadiria bajeti yake ya mapato na matumizi kulingana na vipaumbele hivyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara pamoja na taasisi zake, Fungu Na. 56 - Tume ya Utumishi wa Walimu, Fungu Na.2 pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa Mafungu 26 imekadiria kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi trilioni 1.9. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 188.9 sawa na 10.8% zinakadiriwa kukusanywa kutoka Makao Makuu; shilingi bilioni 1.6

sawa na 0.09% kutoka Shirika la Elimu Kibaha; shilingi bilioni 217 sawa na 1.2% kutoka Wakala wa Mabasi Yaendayo Kasi Dar es Salaam - *BRT,* shilingi bilioni 10.7 sawa na asilimia 0.6 kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa na shilingi bilioni 3.5 sawa na asilimia 0.2 kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa. Shilingi bilioni 7.0 sawa na asilimia 0.4 kutoka Wakala wa Barabara (*TARURA*), shilingi bilioni 11.4 sawa na asilimia 0.66 kutoka Shirika la Masoko ya Kariakoo, shilingi milioni 306 sawa na asilimia 0.017 kutoka Makao Makuu ya Mikoa na shilingi trilioni 1.68 sawa na 96.7% kutoka Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kuna ongezeko la utengaji wa maduhuli kutoka shilingi trilioni 1.6 mwaka 2024/2025 hadi Shilingi trilioni 1.92 mwaka 2025/2026 sawa na ongezeko la Shilingi bilioni 324 ambayo ni sawa na 20.2%. Kamati inaipongeza sana Wizara kwa ongezeko hili. Taarifa zaidi kuhusu makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli kwa Wizara inapatikana kwenye taarifa kama ilivyowasilishwa mezani.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa makadirio ya matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, yanalenga kuchochea maendeleo ya watu na ustawi wa Taifa ili kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa na siha bora ili kuwawezesha kushiriki katika shughuli za ujenzi wa Taifa na kuboresha maisha yao. Makadirio haya ya matumizi ya Wizara yamepangwa ili kutekeleza mipango mbalimbali ya Serikali kama ilivyo chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, kama ilivyoainishwa kwenye mpango wa maendeleo wa miaka mitano na ule wa mwaka mmoja pamoja na miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoainishwa kwenye randama ya Wizara, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa - Fungu Na. 56, Tume ya Utumishi wa Walimu - Fungu Na.2 pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa - Mafungu yote 26, inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi trilioni 11.78. Kati ya fedha zinazoombwa, shilingi trilioni 7.8 sawa na 66.5% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 3.9 sawa na 33.48% zinaombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake, Kamati imezingatia mwelekeo wa Wizara katika hoja yake ya kule siha bora kwa wananchi, Kamati inaamini ili siha bora iweze kuletwa kwa wananchi, uwekezaji katika miradi ya maendeleo ni muhimu ili kuleta urahisi wa utolewaji wa huduma kwa wananchi. Kutokana na hilo Kamati inaishauri Serikali kuongeza utengaji wa bajeti kwenye miradi ya maendeleo ili kuwezesha huduma kwa wananchi kupatikana kwa urahisi na kwa haraka na hivyo kuharakisha maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya pia ulinganisho wa mpango wa bajeti wa mwaka 2025/2026 kwa kulinganisha na bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka 2024/2025, nia ni kuonesha ukuaji wa bajeti na kungezeka kwa utekelezaji wa majukumu ya Wizara na shughuli za umma.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa kuna ongezeko la upangaji wa bajeti ya Wizara kutoka shilingi trilioni 10.2 kwa mwaka wa fedha 2024/2025 hadi shilingi trilioni 11.78 kwa mwaka wa fedha 2025/2026, sawa na ongezeko la shilingi trilioni 1.48 ambalo ni sawa na 14.4%. Aidha, matumizi ya kawaida yameongezeka kutoka shilingi trilioni 6.7 hadi shilingi trilioni 7.83 sawa na ongezeko la shilingi trilioni 1.2 ambayo ni 16.7% huku matumizi ya maendeleo yakiongezeka kutoka shilingi trilioni 3.58 hadi shilingi trilioni 3.9 sawa na ongezeko la shilingi bilioni 405 ambayo ni 11.3%.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilibaini kuwa matumizi ya kawaida upande wa mishahara yameongezeka kutoka Shilingi trilioni 5.5 hadi shilingi trilioni 6.2 mwaka 2025/2026 ambalo ni ongezeko la 13.9%. Taarifa hii inapatikana kwenye taarifa ya Kamati iliyowasilishwa mezani ambayo pia ainaelezea sababu ya ongezeko la mishahara ni ongezeko la ajira za watumishi wapya ambao Serikali imefanya.

Mheshimiwa Spika, ili kujua mwenendo wa kufanya shughuli za wananchi kuwa muhimu kwa maendeleo yao ya kiuchumi na kuboresha siha za wananchi, Kamati ilifanya ulinganisho ili kujua uwiano wa bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na mpango

wa bajeti ya Taifa kwa mwaka 2025/2026. Nia ni kuiwezesha Bunge kuona na kutafsiri ongezeko la namba katika bajeti ya Taifa na kuongeza huduma kwa wananchi ili kuona kama kuongezeka kwa bajeti ya Taifa kuna athari kwa bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa bajeti ya Taifa imeongezeka kutoka shilingi trilioni 50.2 zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 hadi shilingi trilioni 57.4 zilizotengwa mwaka 2025/2026, hili ni sawa na ongezeko la 13.4%.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake Kamati imebaini kuwa, wakati bajeti ya Taifa ikiwa imeongezeka kwa 13.4%, bajeti ya Fungu Na. 56, Fungu Na.2 na Mafungu yote 26 ya Mikoa imeongezeka kwa 14.4%. Aidha, wakati bajeti ya Taifa ya maendeleo ikiwa imeongezeka kwa asilimia 0.1 bajeti ya Fungu Na. 56, Fungu Na.2 na Mafungu yote 26 ya Mikoa kwa ajili ya maendeleo imeongezeka kwa 11.3%. Wakati bajeti ya Taifa ya matumizi ya kawaida imeongezeka kwa 10.4%, bajeti ya matumizi ya kawaida kwa mafungu yote ya TAMISEMI imeongezeka kwa 16.7%.

Mheshimiwa Spika, tafsiri tunayoipata katika uchambuzi huu ni kuwa, ongezeko la mafungu yote kwa pamoja lililowekwa katika Bajeti ya Taifa, linawiana na ongezeko la bajeti ya Wizara hii, Fungu Na. 56, Fungu Na.2 na Mafungu yote 26 ya Mikoa. Hii inaonesha kuwa Wizara hii ni miongoni mwa Wizara zilizopewa kipaumbele katika tengeo la fedha za bajeti. Kamati inapongeza Serikali kwa ongezeko hili la tengeo katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati; baada ya uchambuzi wa bajeti, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara hii katika kuwahudumia wananchi:-

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ni upungufu wa matundu ya vyoo katika shule za misingi na sekondari. Sitara, umaridadi na utulivu wa ujifunzaji katika ngazi za elimu ya msingi

na sekondari ni jambo muhimu kuzingatiwa ili kujenga Taifa lenye siha njema na kulifanya Taifa likue na kustawi kwa utulivu mazingira ya kujifunza ambayo mtoto anakua nayo ni muhimu yawe mazuri na yenye kuleta utulivu wa akili wakati wote wa maisha ya mtoto na wanafunzi katika ngazi ya shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa suala la kuzungumzia matundu ya vyoo kwa karne tuliyonayo ni fedheha kwa Taifa letu. Aidha, wakati wa ukaguzi wa miradi ya elimu nchini katika baadhi ya Halmashauri Kamati imebaini kuwa kuna baadhi ya shule za msingi na sekondari zina vyoo vyenye hadhi ya chini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa uwekezaji mkubwa sana wa ujenzi wa majengo ya shule mbalimbali za msingi na sekondari. Hata hivyo, wakati wa uchambuzi wa taarifa za bajeti za Halmashauri mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati, Kamati ilibaini kuwa kuna upungufu mkubwa wa matundu vya vyoo katika shule nyingi. Kamati inaona kuwa hali hii si nzuri kwa usitawi wa Taifa la Tanzania. Kutokana na hali hiyo Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ifanye tathmini ili kubaini ukubwa wa tatizo la upungufu wa matundu ya vyoo katika shule zake zote za msingi na sekondari nchini;

(ii) Serikali ifanye tathmini ya ubora wa vyoo katika shule zake zote za msingi na sekondari nchini hasa kwenye shule kongwe;

(iii) Serikali iweke mkakati wa kumaliza kabisa katika shule zake za msingi na sekondari nchini na katika kila Mkoa na Halmashauri zake zote zenye upungufu wa vyoo zisimamiwe kwa kuweka mkakati wa kutatua na kukomesha kabisa tatizo la ukosefu wa vyoo pamoja na ubora hafifu wa vyoo katika shule zake za msingi na sekondari nchini.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia fedha zinazotokana na kampuni za uwekezaji kurudisha huduma kwa umma *(CSR)*. Kampuni zinazowekeza katika miradi na biashara mbalimbali nchini zina utaratibu wa kurejesha kwa jamii faida inayotokana na uwekezaji wao *(Corporate Social Responsibilities – CSR)*.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake wa taarifa mbalimbali za Halmashauri zilizowasilishwa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2024/2025 pamoja na mpango wa mapato na matumizi kwa mwaka 2025/2026 kwa Mafungu 26 ya Mikoa; Kamati imebaini kuwa kuna shida kubwa kwenye taratibu za kutoa, kupokea, na kutumia fedha hizo zinazotokana na *CSR*. Kamati imebaini kuwa Mkoa wa Geita pekee una takribani Shilingi bilioni 18 zinazotokana na *CSR* ambazo hazijatumika kwa sababu mbalimbali, ikiwemo mkwamo wa kimanunuzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa suala la utekelezaji wa miradi kwa kutumia fedha zinazotokana na *CSR* bado lina changamoto nyingi za kiutekelezaji. Hali hii inasababisha wananchi kutokupata faida na thamani ya fedha inayotokana na *CSR (value for money)*. Kutokana na hali hiyo Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali isimamie fedha zote zinazotokana na *CSR* zitolewe kwa wananchi kama Sheria inavyotaka;

(ii) Serikali iunde Kamati ndogo itakayokuwa na jukumu la kufanya utafiti wa kutosha na kutoa maoni kuhusu namna bora ya utoaji na matumizi ya fedha zinazotokana na *CSR*. Kamati hiyo pamoja na taa ama Wizara nyingine zinazohusika na TAMISEMI (Hasa Mamlaka zaSerikali za Mitaa; na

(iii) Serikali ione kama kuna haja ya kuipitia na kuifanyia marekebisho Sheria inayosimamia utoaji na matumizi ya fedha za *CSR*.

Mheshimiwa Spika, uimarishaji wa vyanzo vya mapato katika halmashauri nchini. Kamati nyakati zote imekuwa ikiishauri Serikali kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mikakati mbalimbali ya kubuni na kuibua vyanzo mbalimbali vya mapato kwa ajili ya kuongeza wigo wa ukusanyaji wa ushuru ili buboresha mapato ya ndani kwa ajili ya manufaa ya halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inazipongeza baadhi ya halmashauri kwa kuwa wabunifu wa uanzishwaji na ukusanyaji wa ushuru huo. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa bado Halmashauri nyingi nchini, isipokuwa Halmashauri za Majiji, bado zinategemea sana mapato yanayotokana na mazao ya kilimo kutoka kwa wananchi na hivyo wananchi hao kutokupata faida nzuri ya mazao yao kutokana na mzigo mkubwa wa ulipaji wa ushuru.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo Kamati inashauri Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kuendelea kufanya ubunifu wa vyanzo vingine vya mapato mbali na tozo za ushuru wa mazao ambavyo havitawakandamiza wananchi.

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa mazingira ya kupumzika wananchi. Kamati inaendelea kuyapongeza sana Majiji nchini Tanzania, hasa Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Dodoma, Mbeya na Tanga. Hata hivyo Kamati imebaini kuwa maeneo mengi ya majiji hayo hayana maeneo ya mapumziko ambapo wananchi wanaweza kupumzika mara baada ya shughuli za kulijenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri majiji kuweka mikakati ya kutengeneza maeneo mengi kwa ajili ya kuwezesha wananchi kupata mapumziko mara baada ya kazi nzito, hii itasaidia sana kuleta afya ya akili kwa wananchi, majiji yaanze kufikiria hilo.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya kupumzikia ya jamii *(community recreation centers*) yana umuhimu mkubwa sana katika kuongeza na kuboresha thamani ya maisha kwa jamii, binadamu anahitaji kupumzika iwe ni kwa ajili ya uimara wa mwili, au akili mara baada ya kazi za kutwa nzima kwa walio wafanyakazi ama wafanyabiashara au kwa wanafunzi katika ngazi mbalimbali za elimu. Maeneo ya mapumziko kwa ajili ya

jamii yanatakiwa kuwa ya kutosha, kwa hiyo, kuna umuhimu mkubwa wa kuwa na maeneo hayo. Kamati inashauri kwamba, majiji pamoja na miji waendelee kufanya utaratibu wa kuhakikisha kwamba, kwenye maeneo yao kunakuwa na maeneo hayo ya kupumzikia na maeneo ya wazi ambayo wananchi wanaweza kupata mapumziko.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ununuzi wa vifaa vya maabara kwa ajili ya shule za sekondari. Kamati inampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uthubutu wake wa kuwezesha kujenga shule nyingi za sekondari hasa sekondari za wasichana za mikoa na sasa sekondari za wavulana za kanda.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza zaidi hasa hizi shule za sekondari za mikoa kuwa ni shule maalum kwa ajili ya kufundisha watoto wa kike sayansi na hivyo kuongeza idadi kubwa ya wanasayansi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa ili masomo ya sayansi yafundishwe vema na ili wanafunzi waweze kuelewa vyema sayansi, ni muhimu sana kuwepo na maabara pamoja na vifaa vyote vya maabara kwenye shule zote. Hata hivyo, Kamati wakati wa ukaguzi wake kwenye miradi mbalimbali ya shule hizi imegundua kuwa hakuna baadhi ya vifaa vya maabara kwenye shule ambazo ilizitembelea.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati ilibaini kuwa, asilimia kubwa ya shule hizi tayari zimekwishadahili wanafunzi wanaosoma katika shule hizi na kwamba, wengine wanatarajia kufanya mitihani yao ya mwisho mwezi mei, mwaka huu wa 2025. Kamati ina hofu kuwa wanafunzi hao, kama Serikali isipokuwa na mpango wa dharura, watafanya mitihani yao bila kuwa na uwezo wa kufanya mitihani ya mafunzo kwa vitendo *(practical)* kutokana na kutokuwepo kwa maabara. Kutokana na hali hiyo, Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(i) Serikali iweke mpango mkakati wa dharura wa kuhakikisha kwamba, inapeleka vifaa vya maabara

kwenye shule hizi zote 26 za wasichana za mikoa bila kuathiri mipango iliyowekwa ya upelekaji wa vifaa vya maabara katika shule nyingine za sekondari nchini; na

(ii) Kwa kuwa, tatizo la uhaba wa vifaa vya maabara katika shule za sekondari nchini ni la muda mrefu na linaonekana kuwa gumu, kamati inaishauri Serikali itenge fungu maalum kwa kutumia chanzo maalum na cha kudumu, kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maabara, kwa ajili ya shule za sekondari nchini wakati wote vinapohitajika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ujenzi wa Shule za Mchepuo wa Kiingereza. Wakati wa uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti, Kamati ilibaini kuwa, halmashauri nyingi zimeanza kujikita katika ujenzi wa shule maalum za mchepuo wa Kiingereza kwa kutumia fedha ya Serikali na kutoza ada kubwa kwa wanafunzi wanaokuja kusoma katika shule hizi. Kamati haikuridhika kabisa na utaratibu wa halmashauri kujikita katika ujenzi wa shule hizi na kutoza ada kubwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa, kufanya hivyo kunaondoa usawa wa upatikanaji wa elimu kwa Watanzania na hivyo kujenga madaraja nchini. Hii si dhamira ya Serikali na si tamko la elimu la Serikali ambavyo limesema. Kwa sababu hiyo, Kamati inashauri kwamba:-

(a) Halmashauri kuacha kabisa kujihusisha na ujenzi wa shule hizi kwa kutumia fedha yoyote ile ya Serikali na kutoza ada kwa kuwa, inakwenda kinyume na mipango ya Serikali ya utoaji wa elimu bure kwa shule za sekondari.

(b) Kama kuna ulazima kwa halmashauri yoyote kuanzisha shule za mchepuo wa Kingereza, iombe kibali kutoka Wizara ya TAMISEMI.

(c) Aidha, kama kuna ulazima shule hizi kuanzishwa, Kamati inashauri halmashauri ianzishe shule hizi kwa

kutafuta chanzo tofauti nje ya fedha ambazo zinakusanywa kutoka kwenye mapato ya Serikali.

(d) Serikali iwarejeshe walimu wote wazuri waliochukuliwa kutoka shule ze umma na kupelekwa kwenye shule hizi maalum za mchepuo wa kiingereza katika shule zao za awali, ili waendelee kuinua ubora wa elimu katika shule hizi za umma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Uzalishaji wa Madeni Makubwa ya Watumishi katika Halmashauri; Kamati imebaini kuwa, halmashauri nyingi zimekuwa zikizalisha madeni makubwa bila kuyalipa na hivyo kuiweka Serikali kwenye wakati mgumu wa utekelezaji wa majukumu yake. Kamati ilihoji sababu ya uwepo wa madeni hayo na kutaarifiwa kuwa, sababu ni malipo ya uhamisho wa watumishi pamoja na posho mbalimbali za watumishi katika halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Mkoa wa Dodoma peke yake umezalisha madeni yenye thamani ya shilingi bilioni 12 yanayotokana na utumishi. Madeni haya ni makubwa. Hii ni dalili mbaya sana. Kutokana na changamoto hii kutishia ustawi wa halmashauri nchini, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali kuweka mkakati wa ulipaji wa madeni haya kwa wakati ili kuziweka huru halmashauri;

(ii) Serikali kusimamisha uzalishaji wa madeni mengine ya namna yoyote ile katika halmashauri hadi pale madeni yaliyozalishwa awali yatakapokuwa yamekwishalipwa.

Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Utoaji Mikopo ya 10%. Kamati imeabini kuwa, utaratibu wa utengaji wa fedha za 10% unatofautiana kati ya halmashauri moja na nyingine. Kuna halmashauri ambazo zinatenga fedha hizo kwa kutumia mapato yote ya ndani na kuna zingine zinatenga kutokana na mapato ya fedha za maendeleo. Hivyo, utengaji huu wa mapato kutofautiana unaleta mkanganyiko wa uelewa wa utekelezaji wake Kitaifa. Kwa sababu hiyo, Kamati inashauri kuwa, Serikali

itoe mwongozo mmoja utakaotumika, kwa ajili ya kutenga fedha hizo katika halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho; kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu kwako kwa fursa uliyonipa ya kuwasilisha maoni haya ya kamati, lakini pia, kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu. Ninawashukuru sana Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Zainab Katimba, Naibu Waziri na Mheshimiwa Festo John Dugange, Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, aidha, ninamshukuru Katibu Mkuu wa Wizara, Ndg. Adolf Ndunguru, Naibu Makatibu Wakuu wote pamoja na watendaji wote wa Wizara na taasisi zake kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati tangu tulipoanza kufanya nao kazi na kushirikiana nao vizuri kwenye uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kipekee ninawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, pamoja na Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Makamu Mwenyekiti wa Kamati, kwa ushirikiano mzuri ambao ananipa. Wakati wote Wajumbe hawa ni wachapa kazi na wameshiriki kikamilifu katika uchambuzi wa bajeti na kuhakikisha wanahoji ili kupata ufafanuzi wa kina. Ninawapongeza sana na ninaomba kuwatambua kwa majina kama ilivyoambatanishwa kwenye orodha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukurani hizi pia, ninapenda kuwashukuru Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Wakurugenzi wote kwa ushirikiano walioutoa mbele ya Kamati kwa muda wote walipofika kwenye Kamati, kwa ajili ya kufanya mawasilisho mbalimbali. Vilevile, ninapenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Idelphonce Leonard, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema na kwa kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu, ikiwemo uandaaji wa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja. Yaani Fungu 56, 02, 36, 47, 54, 63, 70, 71, 72, 79, 74, 75, 76, 77, 78, 79, 80, 81, 82, 83, 84, 85, 86, 88, 89, 90 na 95 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 ninatoa shukrani kwako kwa kunipa wasaa ili niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, Maeneo muhimu yanayoguswa na kuelezwa kwa kina na taarifa hii ni kama ifuatavyo:-

(a) Maelezo na uchambuzi kuhusu ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(b) Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na uzingatiaji wa Maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(c) Uchambuzi wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 (Makadirio ya Maduhuli na Matumizi); na

(d) Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati.

SEHEMU YA PILI

2.0 MAELEZO NA UCHAMBUZI KUHUSU UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iliidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 1,601,044,595,990.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, Kamati ilitembelea na kukagua baadhi ya miradi hiyo ya maendeleo iliyotelekezwa na Ofisi hii katika mwaka wa fedha 2024/2025. Miradi iliyotembelewa ni miradi ya elimu, miradi ya afya, miradi ya masoko pamoja na miradi ya barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)*.

2.1 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha na kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilifanya ukaguzi wa baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha

2024/2025. Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo zilifanywa kwa kuzingatia Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata wasaa wa kutembelea na kukagua miradi katika Mikoa minne ya Kigoma, Kagera, Geita na Shinyanga ambako jumla ya miradi tisa (9) iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ilikaguliwa. Matokeo ya uchambuzi wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo: -

Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Kigoma (Mradi Namba 4322)

Mheshimiwa Spika, Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Kigoma imejengwa katika Kata ya Uvinza Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza kwa gharama ya Shilingi 4,450,000,000, fedha kutoka Serikali Kuu kupitia Mpango wa Kuboresha Elimu ya Sekondari *(SEQUIP)*. Fedha hizi zilipokelewa katika awamu tatu, ambapo awamu ya kwanza zilipokelewa Shilingi 3,000,000,000 tarehe 29/05/2023, awamu ya pili kilipokelewa kiasi cha Shilingi 1,100,000,000 (tarehe 21/6/2024) na awamu ya tatu kiasi cha Shilingi 350,000,000 kilipokelewa tarehe 21/6/2024.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Kigoma ulianza kutekelezwa kuanzia tarehe 25/09/2023 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 28/03/2025. Ujenzi wa Miundombinu katika Shule hii umetumia Mfumo wa "***Force Account***". Hadi kufikia kipindi cha ukaguzi wa Kamati, Mradi huu ulikuwa umefikia asilimia 85 ya utekelezaji.

Faida ya Mradi

Mheshimiwa Spika, faida zinazotarajiwa kupatikana kutokana na mradi huu ni pamoja na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia na kutoa hamasa ya kujifunza masomo ya sayansi kwa watoto wa kike katika Mkoa wa Kigoma.

Hali ya Utekelezaji wa Mradi

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Kigoma uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kamati ilitaarifiwa kuwa kwa sasa mradi unakadiriwa kufikia asilimia 85. Mradi unatarajiwa kukamilika itakapofikia tarehe 28/03/2025.

Changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa ujenzi wa Shule hii pamekuwa na changamoto mbalimbali zilizosababisha utekelezaji wake kutokukamilika kwa wakati uliopangwa. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo: -

(a) Uwepo wa mvua kubwa zilizokuwa zinanyesha zilisababisha ubovu wa barabara na hivyo kusababisha magari ya kupeleka vifaa vya ujenzi kama vile mawe, saruji, nondo na kokoto, kushindwa kufika uwandani;

(b) Mvua kubwa zilizokuwa zikinyesha zimesababisha mbao zilizopaswa kutumika kwa ajili ya kutengeneza milango pamoja na samani mbalimbali kushindwa kukauka kwa wakati;

(c) Uwezo mdogo wa wa kifedha kwa baadhi ya mafudi kulikosababisha vibarua wanaofanya nao kazi kutokulipwa hadi pale mafundi hao wanapolipwa malipo yao; na

(d) Uwezo mdogo wa kifedha kwa baadhi ya Wazabuni *(Suppliers)* kulikosababisha vifaa kutokupelekwa uwandani kwa wakati.

Uchambuzi wa Kamati

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada ya taratibu za ukaguzi wa miradi, baada ya kupokea taarifa hii ya mradi Kamati ilifanya uchambuzi kuhusiana na utekelezaji wa mradi huu. Katika

uchambuzi wake Kamati imebaini mambo ya msingi kama ifuatavyo:-

(a) Kukosekana kwa vifaa vya Maabara katika Maabara zote tatu za Kemia, Baiolojia na Fizikia

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Kigoma ina maabara tatu ambazo ni za Kemia, Baiolojia pamoja na Fizikia. Katika ukaguzi huo Kamati ilibaini kuwa maabara hizo zote hazina hata kifaa kimoja cha maabara, hali hii imesababisha wanafunzi waliokwishakuandikishwa shuleni hapo kushindwa kabisa kufanya aina yoyote ya majaribio.

Kamati ilibaini kuwa sababu iliyosababisha vifaa hivyo kutokuwepo kwenye shule hiyo kuwa ni vifaa hivyo kutakuwa sehemu ya utekelezaji wa mradi huo na hivyo kukosa makisio.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa kutokuwepo kwa vifaa vya maabara katika shule hii ni kuwafelisha wanafunzi wasichana wanaosoma katika shule hiyo kwa kuwa hawatakuwa na uwezo wa kufanya mitihani yao vyema. Kamati inatambua kuwa shule hii ni ya vipaji maalum kwa mkoa mzima na hivyo inaamini kuwa wanafunzi wanaosoma shuleni hapo ni wale walio na uwezo mkubwa wa akili. Kamati inaona kuwa hali hii ya kukosekana kwa vifaa vya maabara katika shule hiyo si tu kunaua ndoto ya watoto hao bali pia inaua mkakati mzuri uliowekwa na Serikali wa kuwapata wanafunzi wa kike wanasayansi kwa ajili ya mabadiliko ya kisayansi na kiteknolojia nchini.

(b) Milango ya shule kutokuwa imara

Mheshimiwa Spika, Kamati imebini kuwa kuna udhaifu wa uwekaji wa milango na madirisha katika majengo mbalimbali ya shule hii. Kamati imegundua kuwa milango mingi katika shule hii haina ubora aidha kutokana na aina ya mbao zilizotumika au namna milango yenyewe ilivyotengenezwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa majengo ya Serikali yanapaswa kuwa imara na yenye uwezo wa kudumu kwa muda mrefu; kwa kawaida walau kwa miaka 50. Kamati inaona kuwa uwepo wa milango hii yenye kiwango duni kutasababisha milango hii kutokudumu kwa muda mrefu.

(c) Kutokuwepo kwa samani kwenye ofisi ya Mkuu wa Shule pamoja na ofisi ya walimu wengine

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa pamoja na shule kujengwa vizuri na Ofisi ya Mkuu wa Shule kuwa nzuri, ofisi hiyo haina makabati, meza wala viti vinavyoendana na ubora wa majengo hayo. Hali hii inapunguza thamani ya ubora wa shule hii muhimu kwa watoto wa kike katika Mkoa wa Kigoma. Aidha, hali hii inaweza kumuathiri mkuu wa shule kwa kukosa maeneo ya kufanyia vikao akihitaji kuwa na kikao ofisini kwake. vilevile, utunzaji wa mafaili muhimu unaweza ukaathirika zaidi kutokana na kukosa makabati bora. Usiri wa mambo ya siri utaathirika kutokana na kukosa maeneo ya kuhifadhi nyaraka za siri.

Kamati pia imebaini kuwa eneo shule ilipojengwa kuna majimaji na udongo wenye asili ya tope. Hali hii inasababisha wanafunzi kupata ugumu wa kutembea kutoka eneo moja kwenda eneo lingine.

Mheshimiwa Spika, Hata hivyo, Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuwezesha ujenzi huu pamoja na usimamizi uliofanikisha shule hii kujengwa na kufikisha asilimia 85 na kwa kiwango cha kuridhisha.

Maoni na ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi na ung'amuzi wa mambo mbalimbali yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi wa mradi huu Kamati inatoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo: -

(a) Kutokana na shule hii kuwa ni ya muhimu sana kwa watoto wa kike katika Mkoa wa Kigoma na maeneo mengine, kwa suala la kutokuwepo kwa vifaa vya

maabara, Kamati inashauri kuwa Serikali ichukue hatua za dharura ili kuhakikisha kwamba vifaa hivyo vinapatikana na kupelekwa shuleni hapo ili kuwawezesha wanafunzi hao kufanya mazoezi kwa vitendo na hivyo kuwafanya wafaulu mitihani yao;

(b) Kuhusu milango kuwa ya kiwango cha chini Kamati inashauri kwamba Serikali na mamlaka husika ziiondoe milango hiyo na kuweka milango mipya itakayokuwa na uwezo wa kudumu kwa muda mrefu; na

(c) Mkuu wa shule kukosa viti, meza na makabati yenye hadhi kutamfanya asitekeleze majukumu yake ipasavyo. Kamati inashauri Serikali kununua samani mbalimbali kwa ajili ya Ofisi ya Mkuu wa Shule na vile vile kwa ajili ya ofisi nyingine za walimu.

Mradi Na. 4212: Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Uvinza

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Uvinza umetekelezwa kwa jumla ya Shilingi 5,304,963,633.00 ikiwa ni fedha kutoka kwenye vyanzo mbalimbali ikiwemo Serikali Kuu ambayo imetoa kiasi cha Shilingi 5,195,255,300. Kati ya hizo Shilingi 1,205,255300 iliyotumika ni kwa ajili ya kununua vifaa tiba. Aidha, mapato ya ndani ya halmashauri ni kiasi cha Shilingi 17,000,000 huku nguvu za wananchi zikiwa ni Shilingi 3,500,000.00 na fedha kiasi cha Shilingi 89,208,333 ni fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo (Benki ya Dunia). Mradi huu ulianza kutekelezwa tarehe 10 Januari, 2019 na ulianza kutoa huduma za afya tarehe 08 Mei, 2021.

Faida ya Mradi

Mheshimiwa Spika; miongoni mwa faida zinazopatikana kupitia mradi huu ni kama ifuatavyo: -

i) Kupungua kwa rufaa za kwenda Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Maweni kwa huduma ambazo hapo awali zilikuwa

zinapatikana kwenye Hospitali ya Maweni tu, kwa mfano huduma watoto njiti na wale waliozaliwa na uzito pungufu;

ii) Kusogezwa karibu kwa huduma za afya kwa jamii, baada ya huduma hizo kusogezwa karibu yao na kuwapunguzia umbali wa kufuata huduma za afya kwenye Hospitali ya Mkoa ya Maweni, ambapo kwa sasa jamii inatumia muda huo kujishughulisha na shughuli za kiuchui na kuongeza pato la familia na Taifa kwa ujumla; na

iii) Kupungua kwa idadi kubwa ya akina mama kujifungulia nyumbani ambapo sasa wanajifungulia hospitalini hapo kwa ongezeko la asilimia 150%.

Changamoto

Mheshimwa Spika, Kamati imebaini kuwa Hospitali ya Wilaya ya Uvinza inakumbana na changamoto ya utoaji huduma hafifu kutokana na kuwa watumishi wachache.

Uchambuzi wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Wakati wa kutembelea mradi huu Kamati ilibaini mambo mbalimbali kama ifuatavyo: -

i. Upungufu wa nyumba za watumishi.

Hospitali hii ina upungufu wa nyumba za watumishi na kusababisha watumishi wengi kukaa nje ya hospitali na hivyo kusababisha huduma hafifu kwa wananchi kutokana na kutokupatikana kwa urahisi wakati wa dharura;

ii. Uchache wa watumishi

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake Kamati imebaini kuwa hospitali hii ya wilaya yenye ubora mkubwa wa miundombinu ina upungufu wa watumishi. Kamati ilibaini kuwa hospitali hii ina uhaba wa madaktari bingwa kwa asilimia 50 huku upungufu wa wauguzi ukifikia asilimia 85.

Maoni ya Kamati

(a) Kamati ilibaini kuwa hospitali hii ina nyumba moja tu kwa ajili ya watumishi ambayo ina uwezo wa kukaa watumishi watatu kwa pamoja *(three in one)*. Kamati inashauri Serikali kutenga bajeti kwa ajili ya kujenga nyumba za watumishi katika hospitali hiyo ili kuwawezesha watumishi (hasa madaktari) kuishi karibu na hospitali ili kurahisisha utoaji wa huduma, hasa za dharura, kwa wananchi nyakati zote, hasa nyakati za usiku.

(b) Kamati inashauri kuwa Serikali iendelee kutenga ikama itakayowezesha kuwaajiri watumishi mbalimbali wa afya kwa ajili ya hospitail hii ili iwezeshe huduma zote muhimu kwa wananchi kupatikana kama ilivyokusudiwa wakati wa usanifu wa mradi huu; na

(c) Serikali iendelee kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kununua dawa na vitendanishi kwa ajili ya matumizi katika hospitali hii ili kuiwezesha hospitali hii kutoa huduma kwa hadhi yake ya wilaya.

Mradi wa Ujenzi wa Daraja la Mawe na Matengenezo ya Barabara ya Mgaraganza – Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma (Mradi Na. S.10/074/2023/2024/2/10)

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ujenzi wa Daraja la Mawe naMatengenezo ya Barabara ya Mgaraganza – Bweru (Km2.9) kwa kiwango cha changarawe, umetekelezwa katika Kata za Mgaraganza na Kagongo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma Vijijini. Utekelezaji wa Mradi huu ulianza rasmi tarehe 30 Oktoba, 2023 na ulikamilika tarehe 21 Agosti, 2024. Ujenzi wa Daraja hili la Bweru unakamilisha jumla ya madaraja arobaini na nane (48) yaliyojengwa kwa teknolojia ya mawe katika Mkoa wa Kigoma, na kuufanya Mkoa wa Kigoma kuwa kiongozi katika matumizi ya madaraja ya mawe nchini kwa kipindi cha miaka mitano (2019 – 2024).

Mheshimiwa Spika, mradi huu ambao umegharimu Shilingi 101,010,960.00 ulitekelezwa kama sehemu ya Serikali ya kufungua maeneo yaliyokuwa hayafikiki, kuondoa vikwazo vya upitikaji katika barabara za vijijini na kurahisisha usafiri na usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, gharama za mradi huu zimegawanyika katika sehemu tatu, ambapo Serikali Kuu kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)* imechangia kiasi cha Sh. 45,380,000.00, Fedha za Mfuko wa Barabara *(Road Fund Maintenance),* nguvu za wananchi kiasi cha Shilingi 3,371,280.00 na Serikali ya Ubegiji kupitia katika Mradi wa SAKiRP imechangia kiasi cha Shilingi 52,259,680.00. Hadi kufikia wakati wa ukaguzi wa Kamati, mradi huu ulikuwa umekwishakukamilika kwa asilimia 100.

Faida ya Mradi

Mheshimiwa Spika; kukamilika kwa mradi huu kumepelekea faida mbalimbali zikiwemo: -

i) Kufunguka kwa Barabara ya Mgaraganza-Bweru;

ii) kurahisisha usafiri kwa wakazi wa kata za Kagongo, Mwandiga, Bitale na Chankele, kufika eneo la Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, Hospitali ya Wilaya na maeneo ya masoko kama Kigoma Mjini, Kalinzi na Nyarubanda.

Changamoto

Mheshimiwa Spika; Kamati ilitaarifiwa kuwa wakati wa utekelezaji wa mradi huu kumekuwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo: -

i) Kuchelewa kwa fedha za malipo kwa wakandarasi na hivyo kuchelewa kwa utekelezaji wa mradi;

ii) Uhaba wa changarawe katika maeneo ya utekelezaji wa mradi;

iii) Uharibifu wa miundombinu unaosababishwa na wananchi wachache kwa kung'oa alama za barabarani;

iv) Kutembeza mifugo katikati ya barabara; na

v) Wananchi kuweka vizuizi katika mitaro ya barabara ili kukinga mchanga unaosafirishwa na mvua kwa ajili ya shughuli zao za ujenzi.

Uchambuzi wa Kamati

(a) Kingo za daraja kutokuwekewa vizuizi vya mmomonyoko wa udongo

Kamati ilibaini kuwa kingo za daraja hili hazijajengewa vizuizi vya mmomonyoko wa udongo. Kamati inatambua umuhimu wa kujengwa kwa kingo hizi ili kuzuia mmomonyoko zaidi wa udogo na hivyo kulifanya daraja hili kudumu kwa muda mrefu zaidi.

(b) Ubora wa Teknolojia na gharama nafuu

Mheshimiwa Spika, Katika uchambuzi wake Kamati imebaini kuwa teknolojia iliyotumika, ingawa ni ya muda mrefu kwa mataifa yaliyoendelea lakini kwa Taifa letu ni teknolojia rahisi na yenye ubora na inayofaa hasa katika maeneo yetu ya vijijini. Kamati imebaini kuwa teknolojia hii haina ugumu katika kutekeleza wakati wa ujenzi wake, na ni teknoljia ambayo inatumia rasilimali zinazopatikana kwa wingi katika maeneo mengi nchini.

Kamati inaona kuwa kama maeneo mengi , hasa ya vijijini, yatatumia teknolojia hii kuna uwezekano wa kujenga madaraja mengi katika maeneo mengi nchini na hivyo kuondoa kabisa tatizo la madaraja na kuwezesha mawasiliano kati ya eneo moja na lingine na hivyo kuongeza kasi ya maendeleo kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Maoni ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi huo wa Kamati, Kamati inashauri mambo yafuatayo: -

(a) Kwa kuwa teknolojia hii ni rahisi kutekelezeka, na kwamba inapunguza gharama za ujenzi; Kamati inashauri kuwa teknolojia hii itumike maeneo mengine, hasa ya vijijini ili kuwezesha madaraja mengi kujengwa katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu;

(b) Kuhusiana na ujenzi wa kingo za daraja hilo, Kamati inashauri Serikali kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kingo hizo ili kulifanya Daraja hili liishi miaka mingi zaidi.

(c) Kutokana na changamoto ya wananchi kuharibu matumizi ya barabara na daraja hili, Kamati inashauri kuwa elimu itolewe kwa wananchi kuhusu umuhimu wa miradi hii ili kuwafanya waitunze miradi ya umma kwa faida yao wenyewe. Aidha wananchi washirikishwe wakati wa utekelezaji wa miradi hii ili wawe sehemu ya umiliki wa miradi hii.

Mradi Na. 4311: Ujenzi wa Shule Mpya ya Sekondari ya Amali Kata ya Mubunda

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari ya Amali ya Mubunda unatekelezwa katika Kijiji cha Kishoju, Kata ya Mubunda katika Halmashauri ya Wilaya ya Muleba kwa gharama ya Shilingi 584,280,029.00 fedha kutoka Serikali Kuu kupitia Mpango wa Kuboresha Elimu ya Sekondara (SEQUIP). Ujenzi wa shule hii ulianza rasmi tarehe 01/11/2024 baada ya kupokea fedha za utekelezaji wa mradi huo tarehe 30/06/2024.

Hadi wakati Kamati inatembelea mradi huu ulikuwa umefikia asilimia 92 ya ukamilishaji wake. Aidha, mradi huu ulitarajiwa kukamilika tarehe 30 Machi, 2025. Hata hivyo kutokana na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi huu, ilielezwa kuwa matarajio ya kukamilika yatakuwa ni mwezi Mei

2024. Mradi huu unatekelezwa kwa kupitia mfumo wa *force account*.

Faida za Mradi

Mheshimiwa Spika, faida zinazotarajiwa kupatikana baada ya ukamilikaji wa mradi huu ni pamoja na kuwawezesha wanafunzi kujifunza elimu ya amali inayolenga mwanafunzi kupata fani mbalimbali zitakazomwezesha kujifunza kwa vitendo na hivyo kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana. Mradi huu pia utawezesha kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na shule za sekondari na hivyo kuongeza ubora wa elimu na idadi ya wasomi katika Wilaya ya Muleba pamoja na Taifa kwa ujumla

Changamoto

Mheshimiwa Spika; Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa mradi huu ulikumbwa na changamoto kadhaa ikiwemo zifuatazo: -

i) Kupanda kwa gharama za vifaa hasa za viwandani;

ii) Barabara ya kuelekea uwandani kuwa mbovu kipindi cha ujenzi hali iliyochelewesha ufikishaji wa vifaa vya ujenzi sehemu ya ujenzi na kuongeza gharama za ujenzi;

iii) Wazabuni walio wengi kutojisajili kwenye Mfumo wa Manunuzi wa NeST na hivyo kusababisha kukosekana ushindani wa wazabuni pindi zabuni zinapokuwa zimetangazwa;

iv) Changamoto za awali za mfumo wa manunuzi (NeST) kutokuwa hewani kwa kipindi cha Julai, 2024; na

v) Kukosekana kwa umeme kwenye eneo la mradi.

Uchambuzi wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Kamati baada ya kupokea taarifa ya awali kuhusiana na utekelezaji wa mradi huu ilifanya uchambuzi wake na kung'amua mambo mbalimbali kama ifuatavyo: -

i. **Taasisi za Serikali kutokushirikiana wakati wa utekelezaji wa mradi;**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa kutokuwepo kwa miundombinu muhimu kama vile ya umeme, barabara mbaya iliyosababisha upelekaji wa vifaa uwandani kwa ajili ya ujenzi kumesababishwa na taasisi za Serikali kutokuzungumza wakati wa usanifu wa mradi.

ii. **Mfumo wa Manunuzi kushindwa kutekelezeka kwa baadhi ya wazabuni;**

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa Mfumo wa Manunuzi wa NeST bado una changamoto ya uelewa wa namna ya kuutumia kwa baadhi ya wazabuni. Hii ni kutokana na baadhi ya wazabuni kushindwa kuuelewa mfumo huo na namna ya kuutumia. Hali hii imekuwa ikisababisha mradi huu kukosa wazabuni wa kuutekeleza.

Maoni ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi huo wa Kamati, Kamati inashauri Serikali kuendelea kutoa elimu kwa wazabuni mbalimbali, hasa kutoka maeneo ya vijijini, juu ya namna ya kuutumia mfumo huo.

Ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari Kata ya Nyakatanga (Mradi Na. 4311)

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ujenzi wa Shule Mpya ya Sekondari Kata ya Nyakatanga umetekelezwa katika Kijiji cha Biija, Kata ya Nyakantanga katika Halmshauri ya Wilaya ya Mulemba. Mradi huu ambao unatekelezwa na fedha Serikali Kuu kupitia Mpago

wa Uboreshaji wa mazingira ya Ufundishaji na Kujifunza (SEQUIP). Aidha, mradi umegharimu kiasi cha shilingi 584,280,029.00.

Mheshimiwa Spika, fedha za utekelezaji wa mradi huu zilipokewa na Halmashauri ya Wilaya ya Muleba tarehe 23/06/2024 na ujenzi ulianza tarehe 22/03/2025, kwa kutumia mfumo wa Force Account. Mradi huu ambao mpaka wakati wa ukaguzi wa Kamati ulikuwa umekwishakutekelezwa kwa asilimia 86 awali ulipangwa kumalizika mwezi Februari, 2025; hata hivyo, kutokana na changamoto ulizokumbana nazo, Kamati ilielezwa kuwa sasa unatarajia kukamilika ifikapo tarehe 23 Machi, 2025.

Faida za Mradi

Mheshimiwa Spika, faida zinazotarajiwa kupatikana mara baada ya ukamilikaji kwa mradi huu ni pamoja na kuwawezesha wanafunzi wa Kijiji cha Biija na vijiji vya jirani kupata huduma ya elimu ya sekondari karibu, kwani kwa sasa wanafunzi hao wanasoma katika Shule ya Sekondari ya Nyakatanga ambayo iko takribani umbali wa kilomita 6 hadi 10, hali inayowasababishia kutembea umbali wa kilomita 12 hadi 20 kwa siku, Kwenda na kurudi shule.

Changamoto

Mheshimiwa Spika, baadhi ya changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na hizi zifuatazo: -

i) Kupanda kwa gharama za vifaa hasa za viwandani;

ii) Hali ya njia kuwa mbovu kipindi cha ujenzi hali iliyochelewesha ufikishaji wa vifaa vya ujenzi uwandani (site) na hivyo gharama kuongezeka;

iii) Wazabuni walio wengi kutojisajili kwenye Mfumo wa Manunuzi wa NeST na hivyo kusababisha kukosekana ushindani wa wazabuni pindi zabuni zinapokuwa zimetangazwa; na

iv) Kukosekana kwa huduma ya umeme na maji kwenye eneo la mradi.

Uchambuzi wa Kamati

Mheshimiwa Spika, mara baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa mradi huu Kamati ilifanya uchambuzi wake na kubaini mambo mbalimbali kama ifuatavyo: -

i. Taasisi za Serikali kutokuzungumza

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kawaida ilitarajiwa kuwamba miradi ya Serikali inapotekelezwa kunakuwa na mwingiliano wa utolewaji wa huduma zote muhimu kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa mradi husika.

Mheshimiwa Spika, wakati wa utekelezaji wa mradi huu ilitarajiwa kwamba huduma zote muhimu kutoka kwa wadau wanaohusika kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa mradi huu zingepatikana. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa kulikuwa na ugumu wa upatikanaji wa maji wakati wa utekelezaji wa mradi huu. Kamati ilibaini kuwa huduma ya maji haikupatikana wakati wa utekelezaji wa mradi huu na hivyo kusababisha gharama kubwa ya kuchota maji kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za ujenzi. Aidha, Kamati ilibaini pia kuwa kulikuwa na changamoto ya upatikanaji wa umeme kutokana na eneo hilo kutokuwa na miundombinu ya umeme. Hali hii ilisababisha ugumu wa utekelezaji wa mradi na hiyo kuongeza gharama kutokana na kazi za uchomeleaji kufanyika nje ya eneo la mradi.

Barabara, wakati huo huo Kamati ilibaini kuwa barabara inayoelekea kwenye eneo la mradi ni mbovu na hivyo kusababisha changamoto wakati wa upelekaji wa malighafi zilizokuwa zikitumika kwenye ujenzi.

ii. Kukosekana kwa mabweni

Mheshimiwa Spika, mfumo wa uanzishwaji na uendeshaji wa shule za amali una tofauti na sekondari za kawaida (hasa sekondari za

kutwa) kutokana na utaratibu wake wa kuchukua wanafunzi mbali na maeneo shule ilipo. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa shule hii imepangwa kufunguliwa huku mabweni yakiwa hayajajengwa hata moja. Hali hii itasababisha changamoto ya makazi kwa wanafunzi watakaodahiliwa katika shuleni hiyo.

Maoni na Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa kina kuhusu mradi huu Kamati inatoa mani na ushauri wake kama ifuatavyo: -

i. Taasisi za Serikali kushirikiana wakati wa usanifu na utekelezaji wa miradi ya umma

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni rai ya Kamati kila wakati inapopata wasaa wa kutoa maoni yake kwa Serikali kusisitiza haja ya utekelezaji wa miradi katika umoja wake *(holistic approaches)*. Kamati inatambua kuwa miradi ya umma inaanzishwa ili kuuwezesha umma kutatua changamoto za kimazingira zinazowakabili. Hivyo, Kamati inatambua kuwa ili miradi hiyo itekelezwe kwa ufanisi ni lazima taasisi zake zote zinazohusika na utekelezaji wa miradi husika zisomane.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa miradi mingi ya miundombinu ya shule na hosapitali, masoko na stendi inayotelekezwa huwa inakosa usaidizi wa huduma kama za umeme, maji na barabara, Kamati inashauri kuwa Serikali, inaporatibu usanifu wa mradi wowote, aidha wa miundombinu ya shule au hospitali usanifu uhusishe taasisi saidizi za kuhudumia mradi husika kama vile umeme, maji na barabara.

ii. Ujenzi wa mabweni katika shule zote za amali

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa shule hii haina mabweni huku ikitarajiwa kufunguliwa kabla ya ujenzi wa bweni hata moja. Kamati inaamini kuwa hali hii italeta changamoto ya malazi kwa wanafunzi watakaojiunga na shule hiyo. Kamani inashauri Serikali kutenga fedha ya ujenzi wa walau mabweni mawili kabla ya kudahili wanafunzi kwenye shule hiyo.

Ujenzi wa Shule ya Wasichana ya Mkoa wa Geita (Mradi Na. 4390)

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Geita unatekelezwa katika Mtaa wa Upendo Kata ya Bombambili katika Halmasauri ya Manispaa ya Geita kwa fedha kiasi cha Shilingi 4,450,000,000/= kutoka Serikali Kuu, kupitia mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP). Aidha, Diwani ya Kata ya Bombambili ametoa kiasi cha Shilingi 10,000,000/= kwa ajili ya kuchimba kisima kirefu cha maji kwenye shule hiyo, hivyo basi kufanya jumla kamili ya ujenzi wa Shule hiyo kuwa ni Shilingi 4,460,000,000/=.

Mheshimiwa Spika; Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Mkoa wa Geita unatekelezwa kwa mfumo wa *force ccount* katika awamu mbili, ambapo awamu ya kwanza ilianza rasmi tarehe 22/09/2023 na kumalizika tarehe 01/07/2024. Aidha, awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi huu ilianza rasmi tarehe 15/09/2024. Mradi huu ulitarajiwa kukamilika tarehe 15 Aprili, 2025.

Faida ya Mradi

Mheshimiwa Spika; faida zinazotarajiwa kupatikana kutokana na mradi huu ni pamoja na kuboresha mazingira ya ufundishaji na ufundishwaji na kupunguza msongamano wa wanafunzi kwenye shule moja. Aidha, mradi unatarajiwa kuongeza kiwango cha wanasayansi wa kike katika soko la ajira na kukuza sayansi na teknolojia nchini.

Changamoto

Mheshimiwa Spika; baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa mradi huu ni: -

i) Ufinyu wa bajeti kwa baadhi ya miundombinu hasa mabweni;

ii) Uwepo wa mwamba kwenye eneo la mradi uliopelekea kuchelewa kwa mradi na kuongezeka kwa

gharama katika uchimbaji wa msingi kwa baadhi ya miundombinu; na

iii) Mfumuko wa bei za vifaa vya ujenzi na madini ujenzi.

Uchambuzi wa Kamati

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa ya mradi huu Kamati iliichambua na kubaini mambo mbalimbali kama ifuatavyo: -

i) Ukosefu wa vifaa vya maabara

Mheshimiwa Spika, Kamati katika uchambuzi wake ilibaini kuwa shule hiyo tayari imekwishakudahili wanafunzi kwa kidato cha tano na kidato cha kwanza. Hata hivyo Kamati ilibaini kuwa shule hiyo bado haina vifaa vya maabara kwa ajili ya majaribio mbalimbali kwa wanafunzi.

ii) Kutokukamilika kwa jiko

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa jiko la shule hii halijakamilika kwa kiwango cha kufaa kuanza kutumika. Hata hivyo wakati wa ukaguzi Kamati ilibaini kuwa jiko hilo tayari linatumika. Kamati inatia shaka usalama wa matumizi ya jiko hilo ilihali bado linaendelea na ujenzi kwa kiasi kikubwa.

iv) Kutokuwepo kwa samani mbalimbali kwa ajili ya ofisi

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa katika ofisi mbalimbali za shule hii kuna upungufu mkubwa wa samani. Kamati imebaini kuwa hata samani zilizopo hazina hadhi ya kubeba jina la Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Geita. Kamati imebaini pia kuwa Ofisi ya Mkuu wa Shule haina samani za ofisi. Aidha kiti na meza vilivyopo ni vya ubora wa chini kutumika na mkuu wa shule hiyo.

Maoni na Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi wake kwa mradi huu Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo: -

i. Kamati inashauri Serikali kutazama usalama wa matumizi ya jiko hillo;

ii. Kamati inashauri Serikali kuharakisha umaliziaji wa ujenzi wa jiko hilo ili litumike ipasavyo.

iii. Kamati inashauri shule hii itengewe bajeti kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maabara;

iv. Makati inashauri shule hii itengewe bajeti maalum kwa ajili ya ununuzi wa samani mbalimbali kwa ajili ya matumizi shuleni hapo.

Ujenzi wa Barabara ya KM 1.5 kwa kiwango cha lami katika Kata ya Kasamwa eneo la mzunguko wa soko. (Mradi Na. 4946)

Mheshimiwa Spika; mradi huu unatekelezwa katika Kata ya Kalangalala katika Halmashauri ya Manispaa ya Geita badala ya kutekelezwa katika Kata ya Kasamwa kama ilivyokuwa kwenye mpango. Kamati ilielezwa kuwa Sababu iliyopelekea kubadilika kwa eneo la utekelezwaji wa mradi kuwa ni kutokana na Barabara ya Nyanza Sekondari – KASCO kuharibiwa na mvua, hivyo kuleta usumbufu wa kuingia na kutoka kwenye makazi ya viongozi, ofisi za taasisi mbalimbali zilizopo eneo hilo, pamoja na wananchi. Ujenzi wa barabara hii ni wa kiwango cha lami nyepesi yenye urefu wa Km. 1.37, ujenzi wa makalvati mita 57 na ujenzi wa mitaro.

Mheshimiwa Spika; mradi huu unatekelezwa na Halmashauri ya Manispaa ya Geita chini ya usimaizi wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini *(TARURA)* Wilaya ya Geita. Mkandarasi anayejenga Barabara hii ni Evax Construction Ltd wa Muleba. Mradi huu umeanza kutekelezwa tarehe 07 Machi, 2025 na unatarajia kukamilika tarehe 08 Septemba, 2025. Hadi kufikia

kipindi cha ukaguzi wa Kamati mradi huu ulikuwa umekamilika kwa asilimia15%.

Faida za Mradi

Mheshimiwa Spika; kukamilika kwa mradi huu kutaimarisha miundombinu ya barabara katika kukuza uchumi na kuondoa umaskini kwa kuboresha sekta ya usafiri na usafirishaji.

Uchambuzi wa Kamati

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake Kamati imebaini kuwa ujenzi wa barabara hii unawezeshwa na fedha za ndani za Halmashauri. Kamati inaipongeza sana Halmasahuri kwa kutenga fedha zake za ndani kwa ajili ya miundombinu ya barabara. Kamati inampongeza sana mkandarasi kutokana na kasi yake nzuri ya utekelezaji wa mradi huu.

Maoni ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi wake Kamati inaishauri Serikali, hasa mamlaka za Serikali za mitaa kuendelea kutenga fedha za ndani kwa ajili ya miundombinu mbalimbali hasa ya bara.

Ujenzi wa Jengo la Utawala Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe (Mradi Namba 4946)

Mheshimiwa Spika; Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Utawala la Halmashauri ya Bukombe unatekelezwa katika Kata ya Katente, Tarafa ya Ushirombo, Wilaya ya Bukombe kupitia fedha kutoka Serikali Kuu. Mradi huu unatekelezwa na Mkandarasi Gipco Clonstruction Ltd kupitia mkataba namba 83P6/2023/2024/W/03 kwa gharama ya Shilingi 3,497,642,805.22, ambapo hadi kufikia wakati wa ukaguzi wa Kamati tayari fedha, kiasi cha Sh. 444,615,610.83 kilikuwa kimekwishakutumika.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu ulianza kutekelezwa tarehe 11/12/2024 na unatarajia kukamilika tarehe 07/07/2025. Hadi

kufikia tarehe ya ukaguzi wa Kamati tayari mradi ulikuwa umekwishakufikia asilimia 25 ya utekelezaji.

Faida za Mradi

Mheshimiwa Spika, faida zinazotarajiwa kupatikana kutokana na utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na kupatikana kwa ajira za muda kwa vijana na wakazi wa maeneo ya jirani na kusaidia uwepo wa jengo la kisasa lenye mazingira mazuri kwa watumishi kufanyia kazi. Aidha, mradi utaongeza mwonekano mzuri wa mandhari katika Kata ya Katente.

Changamoto

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa mradi umekumbwa na changamoto kadhaa wakati wa utekelezaji wake ikiwa ni pamoja na kuchelewa kwa malipo ya awali kwa takribani miezi saba kuanzia mwezi Mei, 2024 na hivyo kusababisha mradi kusimama katika kipindi hicho na kuvutwa kwa fedha kurudi Mfuko Mkuu wa Serikali.

Uchambuzi wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa mradi huu upo kwenye hatua za awali za utekelezaji wake. Kamati imebaini pia kuwa idadi kubwa ya wafanyakazi katika mradi huu ni wananchi wa eneo la Kata ya Kantente. Kamati inapongeza hatua hii ya kuajiri wawananchi wengi kutoka Kata ya Katente, hali inayowaongezea wananchi wa Katente hisia za umiliki wa mradi huo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushirikishwaji huu wa wananchi katika miradi yao.

Ujenzi wa miundombinu ya soko, stendi pamoja na Barabara na mitaro (Mradi Namba 83P8)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata wasaa wa kutembelea mradi Namba 83P8 unaojumuisha ujenzi wa wa barabara na mitaro mikubwa ya maji katika eneo la kuzunguka Soko Kuu la Sango – Kahama; ujenzi wa barabara na mitaro mikubwa ya maji katika

eneo la kuzunguka Stendi Kuu ya Mbasi Mbulu – Kahama, ujenzi wa Barabara eneo la Zongomela kwa kiwango cha G15 km 2.3 pamoja na ujenzi wa mtaro wa maji ya mvua wa Shunu-Magobekokwa (mita 700).

Mheshimiwa Spika, Mradi huu unawezeshwa na program ya *TACTIC (Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness);* ambao ni mmojawapo ya miradi inayotekelezwa na Serikali kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama umegawanyika katika awamu mbili. Awamu ya kwanza inahusisha ujenzi wa barabara za katikati ya Mji km 12.03, barabara za eneo la Viwanda la Zongomela km 3.06 na ujenzi wa mifereji 2 ya maji ya mvua ya Chelsea - Lyazungu na Shunu Magobeko yenye jumla ya urefu wa km 4.9; na awamu ya pili inahusisha ujenzi wa Kituo cha Mabasi Mbulu, Uboreshaji wa soko la Sango na Ujenzi wa Stendi Ndogo na Soko eneo la Viwanda Zongomela.

Mheshimiwa Spika; Mradi wa Awamu ya Kwanza (Package 01) unatekelezwa na Mkandarasi Kampuni ya *Sichuan Road and Bridge Group Corporation LTD* kwa Mkataba wenye gharama ya Shilingi 20,864,094,611.54 na kusimamiwa na Mtaalam Mshauri Kampuni ya NIMETA Consult ikishirikiana na Kampuni ya NIB Consult kutoka Dar Es Salaam.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia wakati wa ukaguzi tayari kiasi cha Shilingi 5,162,373,416.60 kilikwishakulipwa, ikiwa ni malipo ya awali *(Advance Payment)*. Mradi wa huu ulianza kutekelezwa tarehe 20 Novemba, 2023 na ulitakiwa kukamilika tarehe 19 Februari, 2025 kama ilivyokuwa kwenye Mkataba. Hata hivyo, Mkandarasi ameongezewa muda wa miezi mitatu kutokana na ongezeko la urefu wa mifereji ya maji ya mvua ambapo awali mifereji ilisanifiwa kwa umbali wa km 3.2 hivyo mradi unatarajiwa kukamilika tarehe 19 Mei, 2025.

Mheshimiwa Spika; wakati wa ukaguzi wa Kamati ilielezwa kuwa utekelezaji wa mradi huu katika Awamu ya Kwanza (Package 01) - ulikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji na ulikuwa umefikia asilimia 48, ambapo kazi zilizofanyika zilikuwa ni Kusafisha na kujenga msingi wa barabara eneo la barabara za CBD katika kiwango cha G15 - km 3.45 kati ya km 12.033 (24%); Kusafisha na kujenga msingi wa barabara eneo la Zongomela kwa kiwango G15 km 3.05 kati km 3.05 (49%); Ujenzi wa karavati nne katika eneo la Zongomela kati ya karavati sita (67%); Ujenzi wa mtaro wa maji ya mvua wa Chelsea – Lyazungu kwa mawe (GSP) mita 100 kati ya mita 2,268 (9%); Ujenzi wa mfereji wa maji ya mvua wa Shunu – Magobeko kwa mawe (GSP) mita 700 kati ya mita 2,603 (38%); Ujenzi wa karavati mbili katika mfereji wa Shunu Magobeko kati ya karavati tano (40%) na Ujenzi wa Ofisi kwa ajili ya Msimamizi wa mradi (87%).

Faida za Mradi

Mheshimiwa Spika; Kamati ilielezwa kuwa hadi utakapokamilika mradi utapunguza changamoto za ubovu wa miundombinu ya barabara na utaondoa athari za mafuriko ya mara kwa mara kwenye makazi ya watu, hivyo kuwezesha shughuli mbali mbali za kiuchumi na kijamii kufanyika katika mazingira bora zaidi.

Changamoto

Mheshimiwa Spika; Kamati ilielezwa kuwa wakati wa utekelezaji wa mradi huu umekumbwa na changamoto mbalimbali zikiwemo Maji mengi chini ya ardhi ambayo yapo chini ya msingi wa barabara; udhaifu wa msingi wa barabara katika baadhi ya maeneo kutokana na uwepo wa maji mengi na mkandarasi kutokuwa na uwezo wa kifedha ili kuendesha mradi kwa kasi inayotakiwa.

Uchambuzi wa Kamati

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa mradi huo Kamati imebaini kuwa utekelezaji wa mradi huu uko kwenye asilimia ndogo ya ukamilishaji wake. Kamati imetilia

shaka, kwamba mradi ulianza Novemba, 2023 hadi Machi, 2025 na umefikia asilimia 48. Kamati inatilia shaka asilimia 52 kukamilika ndani ya miezi miwili kuanzia tarehe Kamati ilipotembelea mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati haikuridhika kabisa na maelezo ya mkandarasi kuwa changamoto za kiusanifu na wingi wa mvua ndivyo vilivyosababisha mradi huu kuchelewa. Kamati inatilia shaka uwezo wa mkandarasi kutekeleza mradi huu.

Maoni na Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi wake, Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo: -

i. Mradi huu umeshachelewa kwa kiwango kikubwa. Kamati inashauri Serikali kufanya uchunguzi wa upatikanaji wa mkandarasi anayetekeleza mradi huu kutokana na kuonesha uwezo wake wa chini wa utekelezaji wa mradi;

ii. Kamati inashauri taarifa ya uchunguzi ibainishe hatua stahiki za kuchukuliwa kwa mkandarasi huyu kwa kuwa anapoteza malengo ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuwaletea maendeleo wananchi wake;

iii. Kwa hoja ya kumaliza mradi huu, Kamati inashauri mkataba wa mkandarasi huyu upitiwe upya, na ikiwezeshakana usitishwe ili kuruhusu kupatikana kwa mkandarasi mwingine atakayeweza kutekeleza mradi huu kwa wakati ili wananchi wafaidike.

Ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama (Mradi Namba 4946)

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto Hospitali ya Manispaa Kahama unatekelezwa katika halmashauri ya Mji wa Kahama kwa gharama za Shilingi 6,791,250,594.24 ikiwa ni fedha kutoka Serikali Kuu pamoja na fedha za ndani. Hadi

kufikia wakati wa ukaguzi wa Kamati halmashauri ilikuwa imeshapokea Shilingi 3,300,000,000.00 na kutumia Shilingi 2,219,673,214.48. Mradi unatekelezwa kwa njia ya Kandarasi kupitia Mkandarasi SUMA JKT. Mradi huu ulianza kutekelezwa tarehe 15 Julai, 2022 na unatarajiwa kukamilika tarehe 15 Julai, 2025. Hadi wakati Kamati inatembelea mradi huu ulikwishakukamilika kwa 60% ya utekelezaji.

Faida ya Mradi

Mheshimiwa Spika; mradi unatarajia kuwezesha upatikanaji wa huduma bora za kitabibu za mama na mtoto, kupunguza msongamano wa wagonjwa wodini katika wodi za mama na mtoto zilizopo sasa kwenye majengo ya zamani, na kuboresha mazingira mazuri ya utendaji kazi wa watumishi wa afya katika hospitali hiyo.

Changamoto

Mheshimiwa Spika, Changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji ni pamoja na kusimama kwa mradi kwa zaidi ya miezi mitatu kutokana na marekebisho ya mchoro kuhusu mtiririko wa huduma ya wagonjwa. Aidha mradi pia ulichelewa kutokana na kuchelewesha manunuzi ya vifaa vya ujenzi.

Uchambuzi wa Kamati

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kupokea taarifa kuhusu utekelezaji wa mradi huu, Kamati ilifanya uchambuzi wake na kubaini kuwa mkandarasi (SUMA JKT) ana uwezo mdogo na hivyo kuchelewesha utekelezaji wa mradi huu. Kamati inashauri Serikali kukaa na mkandarasi ili kujua ikiwa ana uwezo wa kuendelea na utekelezaji wa mradi na kisha kuchukua hatua stahiki ili mradi huu uweze kukamilika kwa wakati ili kuwaletea faida wananchi.

Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025

Mheshimiwa Spika, kutokana na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika Mikoa ya Kigoma, Kagera, Geita na Shinyanga, Kamati iliweza kubaini mambo mbalimbali na ingependa kutoa maoni na ushauri wa ujumla kama ifuatavyo:-

i. Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wahakikishe kuwa usanifu wa miradi yote ya elimu na afya inazingatia ujumuishwaji wa miundombinu ya maji, umeme na Barabara tangu mwanzo wa utekelezaji wa miradi;

ii. Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ihakikishe kuwa ujenzi wa shule zote za amali nchini; kabla ya udahili wa wanafunzi; miundombinu muhimu kwa ajili ya karakana na mabweni imejengwa na kukamilika;

iii. Kwa zile shule za wasichana za mikoa ambazo bado hazijaanza kudahili wanafunzi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ihakikishe kuwa inakamilisha maabara zote, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa vifaa vyote vinavyotakiwa kwa ajili ya maabara hizo vimepatikana;

iv. Kutokana na changamoto ya mfumo wa manunuzi kuendelea kukwamisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo mengi, hasa ya vijijini, Kamati inaishauri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ihakikishe kuwa elimu inatolewa mara kwa mara kwa wazabuni mbalimbali ili kuwawezesha kufahamu namna ya kutumia mfumo huo;

v. Miradi mingi iliyotembelewa na Kamati imekuwa na changamoto ya ucheleweshwaji kutokana na sababu mbalimbali ambapo nyingine ni za msingi lakini nyingine si za msingi. Kamati inashauri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuweka utaratibu wa

ufuatiliaji wa karibu ili kuhakikisha kuwa hakuna miradi inayochelewa kutokana na sababu zisizo za msingi;

vi. Serikali iweke utaratibu wa kusimamia na kufuatilia kwa ukaribu utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha ili kuepusha ubadhilifu na hivyo kuwezesha kupatikana kwa thamani ya fedha *(value for money);* na

vii. Ili kuleta umiliki wa miradi kwa wananchi wa eneo husika Kamati inashauri kuwa wakati wa usanifu na utekelezaji wa miradi wananchi wa eneo husika washirikishwe ili kuwafanya waone kuwa ni mradi wao na hivyo kuwa na wajibu wa kuulinda. Elimu ya kutosha itolewe kwa wananchi husika juu ya umuhimu wa mradi husika kwao na kwa Serikali kwa ujumla.

viii. Hoja ya upungufu wa wafanyakazi wa sekta za afya na elimu katika halmashauri ni kubwa na inazidi kuongezeka kila wakati. Kamati imebaini kuwa hii ni kutokana na kukua na kuongezeka kwa idadi ya watu nchini na hivyo mahitaji ya huduma za afya na elimu kuendelea kukua wakati wote. Kamati imebaini pia kuwa Serikali imefanya uwekezaji mkubwa sana kwenye miundombinu ya elimu na afya. Kutokana na mafanikio haya ya uwekezaji huu mkubwa Kamati inashauri Serikali kuweka mipango na mikakati mahsusi ya kuajiri idadi ya kutosha ya wafanyakazi katika sekta za elimu na afya.

SEHEMU YA TATU

3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETINA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

Mheshimiwa Spika, Baada ya Wizara pamoja na Sekretarieti za Mikoa kuwasilisha Bajeti zao kwa mafungu 28 Kuanzia tareh 19 Machi, 2025 hadi 04 Aprili, 2025, Kamati ilipata wasaa wa kuichambua na kuijadili, lakini pia Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na

Mapendekezo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara kama ifuatavyo:-

3.1. Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Mwaka 2024/2025

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni kuhusu bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo Kumi na Tatu (13). Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kwa kiasi kikubwa Serikali imetekeleza Maoni na Ushauri wa Kamati. Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanyia kazi Maoni na Ushauri huo. Aidha, kwa maeneo ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu Kamati itaendelea kuyasisitiza katika taarifa hii likiwemo, suala la shule za mchepuo wa Kiingereza.

3.2. Uchambuzi wa ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia **Fungu 56** (Makao Makuu ya Wizara), Fungu 02 (Tume ya Utumishi wa Walimu) na Mafungu 26 kutoka Sekretarieti za Mikoa katika mwaka wa fedha 2024/2025 ilikadiria kukusanya maduhuli ya **Shilingi 1,601,044,595,990.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 188,960,306,000.00** sawa na **asilimia 11.8** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Makao Makuu ya Wizara, **Shilingi 1,634,835,000.00** sawa na **asilimia 0.1** zinakadiriwa kukusanywa kutoka Shirika la ELimu Kibaha; **Shilingi 21,577,652,305.00** sawa na **asilimia 1.3** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka – Dar es Salaam (DART); **Shilingi 10,535,182,220.00** sawa na **asilimia 0.65** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa; **Shilingi 4,131,215,065.00** sawa na **asilimia 0.25** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa; **Shilingi 5,600,000,000.00** sawa na **asilimia 0.34** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA); **Shilingi 11,948,802,000.00** sawa na **asilimia 0.74** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Shirika la Masoko ya Kariakoo; **Shilingi 315,939,400.00** sawa na **asilimia 0.02** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Ofisi za Mikoa na **Shilingi 1,356,340,664,000** sawa na **asilimia 84.7** zilikadiriwa

kukusanywa kutoka katika Halmashauri. *(Kwa maelezo zaidi tazama Jedwali Namba 1*.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitaarifiwa kwamba, hadi Mwezi Februari 2025, jumla ya **Shilingi 879,899,635,518.15** zilikusanywa, sawa na **asilimia 54.95** ya lengo la makusanyo yote kwa mwaka. Kati ya fedha hizo **Shilingi** 48,957,910,165.36 sawa na **asilimia 3.05** zilikusanywa kutoka Makao Makuu ya Wizara, **Shilingi** 810,710,840.00 sawa na **asilimia 0.05** kutoka Shirika la Elimu Kibaha; **Shilingi 4,969,343,555.00** sawa na **asilmia 0.31** kutoka Wakala wa Mabasi yaendayo Kasi-Dar es Salaa (BRT), **Shilingi 5,063,370,896.00** sawa na **asilimia 3.16** kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa, **Shilingi 598,232,080.07** sawa na **asilimia 0.037** kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, **Shilingi 1,002,864,956.17** sawa na **asilimia 0.06** kutoka Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA); **Shilingi 129,837,745.77** sawa na **asilimia 0.008** kutoka Shirika la Masoko ya Kariakoo, **Shilingi 130,925,932.00** sawa na **asilimia 0.008** kutoka Makao Makuu ya Mikoa na **Shilingi 818,236,439,347.78** sawa na **asilimia 51.1** kutoka halmashauri. **Kielelezo Na. 2 kinatoa mchanganuo zaidi.**

JEDWALI NA 1: ***Hali ya ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka 2024/2025***

Na.	Taasisi	Makisio	Kiasi Kilichokusanywa	Asilimia ya makusanyo
1.	Makao Makuu ya Wizara	188,960,306,000	48,957,910,165.36	25.9
2.	Shirika la Elimu Kibaha	1,634,835,000	810,710,840.00	49
3.	Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar-es-Salaam (DART)	21,577,652,305.	4,969,343,555.00	23
4.	Chuo cha Serikali za Mitaa	10,535,182,220	5,063,370,896.00	48

5.	Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa	4,131,215,065	598,232,080.07	14
6.	Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)	5,600,000,000	1,002,864,956.17	17.9
7.	Shirika la Masoko ya Kariakoo	11,948,802,000	129,837,745.77	1.08
8.	Maduhuli - Mikoa	315,939,400	130,925,932.00	41.1
9.	Halmashauri za Wilaya	1,356,340,664,000	818,236,439,347.78	60.3

***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 16, 2025)*

KIELELEZO NA 1: *Mwenendo wa Makusanyo ya Maduhuli ya OR TAMISEMI (Fungu 56, Fungu 02 na Mafungu 26 ya mikoa kwa mwaka 2024/2025*



***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 16, 2025)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa kati ya taasisi zote zilizo chini ya OR-TAMISEMI Halmashauri za Wilaya ndizo zilizofanya vyema kwenye makusanyo ya maduhuli ambapo zimekusanya maduhuli kwa asilimia 60.3 ya makadirio yake. Aidha, Kamati imebaini kuwa Shirika la Masoko ya Kariakoo ndilo lililo chini zaidi katika makusanyo ya maduhuli. Kamati ilihoji ili kufahamu sababu ya Shirika la Masoko ya Kariakoo kukusanya kiwango cha chini zaidi na kujulishwa kwamba ni kutokana na soko hilo kuendelea na ujenzi baada ya kuungua.

Mheshimiwa Spika, matarajio ya Kamati ilikuwa ORTAMISEMI pamoja na taasisi zake kufikia asilimia 66 ya makuanyo ya maduhuli hadi Februari, 2025. Hata hivyo hakuna hata taasisi moja iliyofikia kiwango hicho. Hali hii imeisababisha Kamati kuhoji uhalisia wa upangaji wa makusanyo ya maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

KIELELEZO NA 2: *Makadirio ya makusanyo ya maduhuli na asilimia ya makusanyo halisi kwa mwaka 2024/2025*



***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 16, 2025)*

3.3. Ulinganisho wa Makusanyo ya Maduhuli kuanzia Mmwaka 2022/2023 – 2024/2025

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa kumekuwa na mwendelezo mzuri wa upangaji wa makisio katika ORTAMISEMI kwa miaka mitatu mfululizo. Hali hii inaonesha kuwa vyanzo vya mapato kwenye OR-TAMISEMI vinaendelea kukua kila mwaka.

Kamati inaamini kuwa hali hii inatokana na kukua kwa uchumi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na hivyo kuchagiza usitawi wa jamii. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuweka mikakati inayosababisha ukuaji huu wa uchumi na maendeleo kwa jamii.

JEDWALI NA 2: ***Makusanyo ya Maduhuli kwa ulinganisho kuanzia Mwaka wa Fedha 2022/2023 – 2024/2025 kwa miaka mitatu mfululizo***

A.	Taasisi	2022/2023	2023/2024	2024/2025
	Makao Makuu ya Wizara	4,500,000	0	0
	Shirika la Elimu Kibaha	4,427,543,000	1,634,835,000.00	1,634,835,000
	Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar-es-Salaam (DART)	4,768,836,700	17,172,749,540.00	21,577,652,305
	Chuo cha Serikali za Mitaa	9,055,627,005	10,437,966,865.00	10,535,182,220
	Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa	2,613,545,000	4,131,215,065.00	4,131,215,065
	Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)	30,447,063,547.5	15,200,000,000.00	5,600,000,000
	Shirika la Masoko ya Kariakoo	0	6,565,654,276.00	11,948,802,000
	Maduhuli - Mikoa	220,683,312	261,890,400.00	315,939,400
	Halmashauri	863,858,000,000	1,143,883,281,000.00	1,356,340,664,000

JUMLA		**1,071,730,886,415.**	**1,199,287,592,146**	**1,601,044,595,**
A.	**Taasisi**	**2022/2023**	**2023/2024**	**2024/2025**
		50		**990**

***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 16, 2025)*

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake pia Kamati ilibaini kuwa kuna ongezeko la utengaji wa makisio ya makusanyo ya maduhuli kutoka **Shilingi 863,858,000,000** zilizotengwa mwaka 2022/2023 hadi **Shilingi 1,356,340,664,000 kwa mwaka 2024/2025,** sawa na ongezeko la **Shilingi 487,482,000,000** sawa na **asilimia 56.4**.

Mheshimiwa Spika, aidha, makusanyo ya maduhuli yameongezeka kutoka **Shilingi 1,071,730,886,415.50** mwaka 2023/2024 na kufikia **Shilinigi 1,192,721,936,870.00,** sawa na Ongezeko la **Shilingi 120,991,050,454.50 ongezeko ambalo ni sawa na asilimia 11.3.** Kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 3.**

KIELELEZO NA 3: *Ulinganisho wa makadirio ya maduhuli na mapato halisi kwa miaka mitatu mfululizo*



***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 16, 2025)*

KIELELEZO NA 4: *Mwenendo wa Upangaji wa maduhuli kwa kipindi cha miaka mitatu (2022/2023)*



***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 16, 2025)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na ya taarifa ya Wizara kwa ulinganisho wa randama za vipindi vitatu tofauti Kamati imebaini kuwa Halmashauri zimeendelea kufanya vyema kwenye utengaji wa ukusanyaji wa maduhuli ambapo unaongezeka kila mwaka wa Fedha. Wakati huo huo, Kamati imebaini kuwa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini ameendelea kushusha makadirio yake ya ukusanyaji wa madhuli. Kamati inazipongeza sana Halmashauri kwa juhudi wanazoendelea nazo. Hii inaonesha kuwa halmasahuri wameendelea kuwa wabunifu katika kuongeza vyanzo vyao vya mapato, na hivyo kuendelea vyema kujenga uwezo wa halmashauri zao katika kuwahudumia wananchi. Kamati inashauri *TARURA* kutazama upya vyanzo vyao vya mapato na kuviboresha ili viweze kuongeza mapato Serikalini.

JEDWALI NA 3: ***Ulinganisho wa mwenendo wa makusanyo ya maduhuli kuanzia mwaka 2022/2023 hadi 2024/2025***

NA.	Taasisi	2022/2023	2023/2024	
1	Makao Makuu ya Wizara	0	0	48,957,910,165.36
2	Shirika la Elimu Kibaha	770,651,194.84	784,156,491.50	810,710,840.00

3	Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar-es-Salaam (DART)	5,860,436,938.75	5,859,457,872.73	4,969,343,555.00
4	Chuo cha Serikali za Mitaa	3,867,429,435.00	4,881,583,363.61	5,063,370,896.00
5	Bodi ya Mikopo ya Serikali za	1,261,101,972.95	437,544,255.44	598,232,080.07
	Mitaa			
6	Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)	10,675,082,691.87	1,555,811,906.48	1,002,864,956.17
7	Shirika la Masoko ya Kariakoo	39,904,100.00	190,185,134.51	129,837,745.77
8	Maduhuli - Mikoa	92,266,789.00	193,798,600.00	130,925,932.00
9	Halmashauri	625,319,158,432.00	742,487,214,848	818,236,439,347.78

***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 16, 2025)*

KIELELEZO NA 5: ***Uwiano wa ukusanyaji wa maduhuli hadi mwezi Februari, 2025***



***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 16, 2025)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na jedwali hapo juu sura ya ukusanyaji wa maduhuli kwa upande wa Halmashauri kwa kila mwaka hadi mwezi Februari ya Mwaka wa Fedha husika (2022/2023 – 2024/2025) umekuwa ukiongezeka wakati huo huo kwenye baadhi ya taasisi makusanyo hayo yamekuwa yakipungua.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa Halmashauri zimefanikiwa kuongeza makusanyo ya maduhuli kwa **asilimia 18.4** na **asilimia 10.2** mtawalia. Kamati inapongeza sana juhudi za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa makusanyo hayo. Wakati huohuo, Kamati vilevile imebaini kuwa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) ukusanyaji wake wa mapato umekuwa ukishuka kwa **asilimia 85** na **asilimia 35.5** mtawalia.

3.4 Utolewaji fedha za matumizi kwa Mwaka 2024/2025

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2024/2025 iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu Juni, 2024 Wizara kupitia Fungu 56, Fungu 02 pamoja na mafungu yote 26 ya mikoa iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 10,125,220,403,167** Kati ya fedha hizo **Shilingi 6,709,975,188,500.00** sawa na **asilimia 66.3** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 3,589,016,688,968.00** sawa na **asilimia 33.7** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida ambazo ni **Shilingi 6,709,975,188,500.00, Shilingi 5,524,636,066,000** sawa na **asilimia 82.3** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 1,185,339,122,500** sawa na **asilimia 17.7** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, hadi Mwezi Februari, 2025 Wizara pamoja na taasisi zake pamoja na Sekretarieti za Mikoa zilipokea jumla ya Shilingi **6,970,248,523,170.17** sawa na **asilimia 67.7** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **4,767,435,152,374.26** sawa na **asilimia 68.4** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 2,202,813,370,795.91** sawa na **asilimia 32.3** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya **Shilingi 4,767,435,152,374.26** za matumizi ya kawaida zilizopokelewa **Shilingi 3,639,138,343,817.08** sawa na **asilimia 76.33** ni kwa ajili ya matumizi ya a mishahara na Shilingi **1,128,296,808,557.18 sawa** na **Asilimia 23.7** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)*. Aidha, kati ya Shilingi **2,202,813,370,795.91** za matumizi ya maendeleo zilizopokewa **Shilingi 1,819,807,974,317.72** Sawa na **asilimia 82.6** ni fedha za ndani na Shilingi **383,005,396,478.19** Sawa na **asilimia 17.4** ni fedha za nje. *Tazama Jedwali Na. 4. pamoja na Kielelezo Na 6(a) na (b)*

JEDWALI NA 4: *Uwiano wa fedha zilizoidhinishwana fedha zilizotolewa hadi Februari, 2025*

TAASISI	FEDHA ZILIZOIDHINISHWA		FEDHA ZILIZOPOKEWA	
	KIASI	ASILIMIA	KIASI	ASILIMIA
Makao Makuu	206,711,047,500	2.04	129,412,098,123.43	63
Taasisi	903,223,935,500	8.9	767,536,780,362	84.9

Tume ya Utumishi wa Walimu	20,742,101,667	0.2	13,028,645,429	62.8
Mikoa	297,814,362,500	2.9	218,444,037,343	73.3
Halmashauri	8,696,728,956,000	85.9	5,841,826,961,907	67
Jumla	**10,125,220,403,167**		**6,970,248,523,170.17**	**67.68**

***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 16, 2025)*

Mheshimiwa Spika, kulingana na jedwali hapo juu inaonesha kuwa kwa wastani upokeaji wa fedha hadi mwezi Februari, 2025 ni wa kuridhisha. Kamati imebaini kuwa upelekaji wa jumla wa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina katika Fungu 56, Fungu 02 na mafungu 26 ya Sekretarieti za Mikoa ni wa **asilimia 67.68**. Kwa upelekaji huu wa fedha Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuwa hizi ni dalili chanya kuwa shughuli za umma na maendeleo ya wananchi yanafikiwa kama ilivyopangwa na kama ilivyo dhamira ya Bunge ya kupitisha bajeti ya mafungu haya.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, uchambuzi zaidi wa Kamati umebaini kuwa Wizara na taasisi zake pamoja na Sekretarieti za Mikoa zimepelekewa fedha nyingi za matumizi mengineyo kuliko asilimia zilizotarajiwa kupelekwa na kutumika hadi mwezi Februari, 2025. Kamati ilibaini kuwa Halmashauri nchini zimepelekewa na kutumia zaidi ya **asilimia 174** zikifuatiwa na Makao Makuu ya Wizara ambako zimepelekewa na kutumika zaidi ya **asilimia 99** ya fedha zilizotarajiwa kupelekwa na kutumika hadi mwezi Februari, 2025. Kamati ilihoji sababu za upelekaji na matumizi haya mengineyo kuwa makubwa katika Halmashauri na Makao Makuu ya Wizara na kujibiwa kuwa ni kutokana na zoezi la uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika mwezi Novemba 2024. Aidha, kwa upande wa upokeaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo Kamati ilibaini kuwa taasisi zilizo chini ya Wizara zimepokea fedha (za nje) kwa zaidi ya asilimia 184 ya fedha zilizopangwa.

KIELELEZO NA 6: *Uwiano wa utolewaji wa fedha za matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo hadi Februari, 2025 (a) na (b)*



Chanzo: *Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 16, 2025)*

KIELELEZO NA 7: *Uwiano wa fedha zilizotolewa kwa ajili ya mishahara, matumizi mengineyo pamoja na miradi ya maendeleo hadi Februari, 2025*



Chanzo: *Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 16, 2025)*

SEHEMU YA NNE

4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NAMATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2025

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitaarifiwa kwamba, maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka 2025/2026, yamezingatia Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026; Mipango Mikakati ya Taasisi; Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati akilihutubia Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021; Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/2026; Sheria ya Bajeti Sura 439; Sera za Kisekta; Maelekezo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; malengo yaliyomo katika Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/2022 - 2025/2026; Dira ya Afrika Jumuiya ya Afrika Mashariki 2050; Dira ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika 2050; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; Agenda Afrika 2063; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 na Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi. Aidha, bajeti ya Wizara hii ni ya mwisho katika utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 (TDV 2025) pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa pia kuwa, katika Mwaka wa Fedha wa 2025/2026, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepanga kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele mbalimbali ilivyojiwekea na hivyo kukadiria bajeti yake ya mapato na matumizi kulingana na vipaumbele hivyo. Kamati ilielezwa kuwa katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara imejipangia kufanikisha vipaumbele vifuatavyo: -

i. Kusimamia shughuli za Utawala Bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma (*D by D*);

ii. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa Huduma za jamii;

iii. Kuratibu na kusimamia Mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato na kudhibiti matumizi yasiyo na tija katika ngazi zote;

iv. Uratibu wa usimamizi wa mifumo ya TEHAMA;

v. Kuendeleza rasilimali watu katika ngazi zote za Ofisi ya Rais - TAMISEMI;

vi. Kuratibu na kusimamia shughuli za kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa Ofiisi ya Rais - TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

vii. Uratibu wa utoaji wa huduma za jamii;

viii. Kuratibu masuala ya michezo;

ix. Kuratibu shughuli za utendaji wa kazi wa Taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI;

x. Kuratibu na kusimamia ujenzi wa miradi ya maendeleo katika ngazi zote za Ofisi ya Rais - TAMISEMI; na

xi. Kuratibu shughuli za uendelezaji wa vijiji na miji kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa mchanganuo wa shughuli hizo za Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama ifuatavyo:-

4.1. UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA UKUSANYAJI WAMADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara pamoja na taasisi zake, (Fungu 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu 02) pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa (Mafungu 26) imekadiria kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 1,925,881,323,464.22.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 188,960,306,000.00** sawa na **asilimia 10.8** zinakadiriwa kukusanywa kutoka Makao Makuu ya Wizara; **Shilingi 1,644,835,000.00** sawa na **asilimia 0.09** kutoka Shirika la Elimu Kibaha; **Shilingi 21,721,743,786.00** sawa na **asilimia 1.2** kutoka Wakala wa Mabasi Yaendayo Kasi Dar es Salaam (BRT), **Shilingi 10,745,182,213.20 sawa na asilimia 0.6** kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa, **Shilingi 3,506,815,065.02** sawa na **asilimia 0.2** kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, **Shilingi 7,000,000,000.00** sawa **na asilimia 0.4** kutoka Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA),* **Shilingi 11,489,598,000.00** sawa na **asilimia 0.66** Shirika la Masoko ya Kariakoo; **Shilingi 306,079,400.00** sawa na **asilimia 0.017** kutoka Makao Makuu ya Mikoa na **Shilingi 1,680,506,764,000.00** sawa na **asilimia 96.7** kutoka Halmashauri za Wilaya kama inavyoonekana kwenye Jedwali Namba 5 na Kielelezo Na. 8.

JEDWALI NA 5: *Taswira ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026*

TAASISI	MAKADIRIO	ASILIMIA
Makao Makuu ya Wizara	188,960,306,000.00	10.8
Shirika la Elimu Kibaha	1,644,835,000.00	0.09
Wakala wa Mabasi Yaendayo Kasi Dar (DART)	21,721,743,786.00	1.2
Chuo cha Serikali za Mitaa	10,745,182,213.20	0.6
Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa	3,506,815,065.02	0.2
Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini	7,000,000,000.00	0.4
Shirika la Masoko ya Kariakoo	11,489,598,000.00	0.66
Makao Makuu ya Mikoa	306,079,400.00	0.017

Halmashauri	1,680,506,764,000.00	96.7
JUMLA	1,925,881,323,464.22	

***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 16, 2025)*

KIELELEZO NA 8: Ulinganisho wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka 2025/2026



Chanzo: *Randama ya Wizara (Aprili, 2025) (Fungu 56) na Usanifu wa Kamati.*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kuna ongezeko la utengaji wa maduhuli kutoka **Shilingi 1,601,044,595,990.00** mwaka 2024/2025 hadi **Shilingi 1,925,881,323,464.22** mwaka 2025/2026; sawa na ongezeko la Shilingi **324,836,727,474,** sawa na **asilimia 20.2.** Kamati inaipongeza sana Wizara kwa ongezeko hili. Aidha, Kamati ilibaini kuwa kumekuwa na ongezeko la makadirio ya maduhuli kuanzia mwaka 2023/2024, 2024/2025 na 2025/2026 kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 9 hadi 10**

KIELELEZO NA 9: *Uwiano wa makadirio ya mapato na matumizi kuanzia mwaka 2023/2024 hadi 2025/2026*



***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 16, 2025)*

Kamati ilibaini kuwa ongezeko hili kwa kiasi kikubwa limetokana na ongezeko katika maeneo matatu ambayo ni Makao Makuu ya Wizara, Shirika la Masoko ya Kariakoo pamoja na Halmashauri.

Kamati inazipongeza sana Halmashauri pamoja na Makao Makuu ya Wizara kwa ongezeko la makadirio ya mapato. Kamati inaishauri Wizara kuendelea kuwa wabunifu wa vyanzo mbalimbali ili kuiwezesha Serikali kutekeleza malengo yake kwa ufanisi mkubwa.

KIELELEZO NA 10: *uwiano wa makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli ya Wizara na taasisi zilizo chini yake (a) na (b)*



***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 16, 2025)*

KIELELEZO NA 11: *Ulinganisho wa ukuaji wa upangaji wa Maduhuli katika Halmashari*



***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 16, 2025)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa Halmashauri za Wilaya zimeendelea kufanya vyema katika ukadiriaji na ukusanyaji wa maduhuli kama inavyoonesha hapo juu na katika data zilizotangulia kuelezwa kuhusiana na ukusanyaji wa maduhuli. Kamati ilitaka kujua ikiwa mapato haya yameongezeka katika utozwaji wa kodi na ushuru katika bidhaa na uwekezaji ule ule wa mwaka uliopita na kuelezwa kuwa ongezeko hili ni kutokana na vyanzo vipya ambavyo Halmashauri imevibuni. Kamati inazipongeza sana Halmashauri nchini kwa kuwa wabunifu wa vyanzo vya mapato, jambo ambalo wakati wote limekuwa likishauriwa na Bunge. Hii ni dalili wazi kuwa halmashauri zina uwezo wa kujitegemea, na hivyo kuwa na uwezo wa kuitekeleza Sheria ya Ugatuaji wa Madaraka kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati pia imebaini kuwa kuna taasisi ama hazikui, kwamba zinabaki pale pale zilipokuwa vipindi viwili mfululizo vya miaka ya fedha au hata kushuka kabisa kwenye ukadiriaji wa maduhuli. Kamati imebaini kuwa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imebaki kwenye ukadiriaji ule ule kwa miaka mitatu mfululizo Sekretarieti za mikoa zikikadiria ongezeko kwa asilimia ndogo. Aidha, Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini amekuwa akiendelea kushuka kwenye ukadiriaji wa maduhuli.

Mheshimiwa Spika, Kamati inazishauri taasisi nyingine ambazo ziko chini ya Wizara ambazo makadirio yake hayakuongezeka, ama yamepungua kuwa wabunifu katika kutafuta vyanzo vingine vya mapato ili kuongeza makadirio na makusanyo ya maduhuli.

JEDWALI NA 6: *Mwenendo wa Makadirio ya Maduhuli ya Wizara, Taasisi zake na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kipindi cha mwaka 2023/2024 hadi 2025/2026*

Na.	MWAKA	KIASI	ONGEZEKO	ASILIMIA
1.	2023/2024	1,199,287,592,146.00		
2.	2024/2025	1,601,044,595,990.00	212,796,697,844	17.7
3.	2025/2026	1,925,881,323,464.22	324,836,727,474	20.2

***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 16, 2025)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa ujumla makadirio ya mapato kwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imekuwa ikiongezeka kwa wastani mzuri kila Mwaka. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuwa wabunifu wa utafutaji wa vyanzo mbalimbali vya mapato ili kuongeza Mapato ya Serikali.

JEDWALI NA 7: *Ulinganisho wa Makadirio ya Maduhuli Fungu 56, Fungu Na.02 na Mafungu 26 ya Sekretarieti za Mikoa kwa miaka mitatu mfululizo (2023/2024, 2024/2025, 2025/2026)*

TAASISI	2023/2024	2024/2025	2025/2026
Makao Makuu ya Wizara	0	188,960,306,000.00	188,960,306,000.00
Shirika la Elimu Kibaha	1,634,835,000.00	1,634,835,000.00	1,644,835,000.00
DART	17,172,749,540.00	21,577,652,305.00	21,721,743,786.00
Chuo cha Serikali za Mitaa	10,437,966,865.00	10,535,182,220	10,745,182,213.20
Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa	4,131,215,065.00	4,131,215,065.00	3,506,815,065.02
TARURA	15,200,000,000.00	5,600,000,000.00	7,000,000,000.00
Shirika la Masoko ya Kariakoo	6,565,654,276.00	11,948,802,000.00	11,489,598,000.00
Makao Makuu ya Mikoa	261,890,400.00	315,939,400.00	306,079,400.00
Halmashauri	1,143,883,281,000.00	1,356,340,664,000.00	1,680,506,764,000.00
JUMLA	1,199,287,592,146.00	1,601,044,595,990.00	1,925,881,323,464.22

Chanzo: *Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati*

4.2. UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa, makadirio ya matumizi ya Wizara katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 yanalenga kuchochea maendeleo ya watu na ustawi wa Taifa ili kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa na siha bora ili kuwawezesha

kushiriki katika shughuli za Ujenzi wa Taifa na kuboresha maisha yao. Makadirio haya ya matumizi ya Wizara yamepangwa ili kutekeleza mipango mbalimbali ya Serikali kama iliyo chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ilivyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na ule wa Mwaka mmoja pamoja na miongozo mbalimbali iliyotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili Kamati imefanya uchambuzi wa aina tatu kama ifuatavyo:-

(a) Uchambuzi wa Mpango wa Bajeti ya Wizara (Fungu 56, Fungu 02 pamoja na Mafungu 26 ya Sekretarieti za Mikoa) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(b) Uwianishaji wa Mpango wa Bajeti ya Matumizi ya Wizara (Fungu 56, Fungu 02 pamoja na Mafungu 26 ya Sekretarieti za Mikoa) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 bajeti ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(c) Uwianishaji wa Mpango wa Bajeti ya Matumizi ya Wizara (Fungu 56, Fungu 02 pamoja na Mafungu 26 ya Sekretarieti za Mikoa) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Mpango na Bajeti Kuu ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

(a) Uchambuzi wa Mpango wa Bajeti ya Wizara (Fungu 56,Fungu 02 pamoja na Mafungu 26 ya Sekretarieti za Mikoa) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoainishwa kwenye randama ya Wizara; katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Fungu 56); Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu 02) pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa (Mafungu 26 ya Sekretarieti za Mikoa) inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 11,780,484,202,000.00.** Kati ya fedha zinazoombwa **Shilingi 7,836,140,708,000.00** sawa na **asilimia 66.5** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 3,944,343,494,000.00** sawa na

asilimia 33.48 zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. *(Tazama kielelezo Namba*

KIELELEZO NA 12: *Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi Fungu 56 – Makao Makuu ya Wizara, Fungu 02 – Tume ya Utumishi wa Walimu na Mafungu 26 ya Mikoa*



Chanzo: *Randama ya Wizara na usanifu wa Kamati (Aprili, 2025)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na kielelezo hapo juu matumizi ya Serikali kwa Wizara (Fungu 56) Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu 02) pamoja na Mafungu 26 ya Sekretarieti za Mikoa yana mwelekeo wa kuhudumia ofisi zaidi kuliko kuwekeza katika miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hali ya bajeti kuonesha kuwa na matumizi makubwa kwenye matumizi ya kawaida kunaleta taswira kuwa uwekezaji kwa ajili ya miradi ya maendeleo uko chini, hivyo boreshaji wa maisha ya wananchi unakuwa chini.

Mheshimiwa Spika, Katika uchambuzi wake Kamati imezingatia mwelekeo wa Wizara katika hoja yake ya kule siha bora kwa wananchi. Kamati inaamini ili siha bora iweze kuletwa kwa wananchi uwekezaji katika miradi ya maendeleo ni muhimu ili

kuleta urahisi wa utolewaji wa huduma kwa wananchi. Kutokana na hilo Kamati inaishauri Serikali kuongeza utengaji wa bajeti kwenye miradi ya maendeleo ili kuwezesha huduma kwa wananchi kupatikana kwa urahisi na kwa haraka na hivyo kuharakisha maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliendelea zaidi na uchambuzi kuhusiana na bajeti ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Wakati wa uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa kati ya **Shilingi 7,836,140,708,000.00** zinazoombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida **Shilingi 6,292,557,648,000.00** sawa na **asilimia 80.3** zinaombwa kuidhinishwa kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 1,543,583,060,000.00** sawa na **asilimia 19.7** zinaombwa kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, kati ya **Shilingi 3,944,343,494,000.00** zinazoombwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo **Shilingi 2,496,431,476,000.00** sawa na **asilimia 63.3** ni fedha za ndani na **Shilingi 1,447,912,018,000.00** sawa na **asilimia 36.7** ni fedha za nje. *(Tazama kielezo Namba 13 na Namba 14 mtawalia)*

KIELELEZO NA 13: *Ulinganisho wa makadirio ya Matumizi ya kawaida kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo (OC) kwa Fungu 56 – Makao Makuu ya Wizara, Fungu 02 – Tume ya Utumishi wa Walimu na Mafungu 26 ya Mikoa*



***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 16, 2025)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa fedha za matumizi mengineyo ndizo zinazowezesha rasilimali watu kufanya kazi kwa

mnyumbuliko na hivyo kufikisha huduma stahiki kwa wananchi. Kamati inatambua kuwa ni kutokana na matumizi mengineyo rasilimali watu inatumika ipasavyo. Ni bajeti hii ndiyo inayoweza kuwafanya watumishi kama vile maafisa ugani, maafisa uvuvi na maafisa mifugo (kwa kutaja wachache) katika halmashauri kutoa huduma stahiki, za kutosha na kwa wakati kwa wakulima, wavuvi na wafugaji kote nchini. Aidha, ni bajeti hii ndiyo inayoweza kununua vifaatiba na vitendanishi kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali za wilaya kote nchini.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati imebaini kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo (asilimia 20 ya matumizi ya kawaida) ni ndogo. Kamati inaona kuwa hali hii inaweza kusababisha watumishi wasitumie zaidi weledi na ujuzi wao kwa ajili ya wananchi kutokana uwezeshwaji mdogo na hivyo kushindwa kutoa huduma kwa wananchi kwa namna ya kutosha. Kamati inashauri Serikali kuendelea kuongeza fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo ili kuweza kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

KIELELEZO NA 14: *Uwiano wa makadirio ya Matumizi ya maendeleo kwa fedha za ndani na nje kwa Fungu 56 – Makao Makuu ya Wizara, Fungu 02– Tume ya Utumishi wa Walimu na Mafungu 26 ya Mikoa*



Chanzo: *Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili, 2025)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya maendeleo Kamati imebaini kuwa maoteo ya bajeti kwa kutumia fedha za ndani yanazidi kuongezeka. Kwa sababu hiyo ni sahihi kusema kuwa bajeti ya Wizara inazidi kuimarika na kufanya vema. Hii ni

kutokana na kwamba maoteo ya bajeti kwa fedha za ndani yanaonesha kuwa nchi ina uwezo wa kutekeleza miradi yake kwa asilimia 63 bila kutegemea fedha za wahisani. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuwa ina nia ya dhati ya kuifanya nchi isiwe tegemezi.

(b) Uwiano wa Mpango wa Bajeti ya Matumizi ya Wizara (Fungu 56, Fungu 02 pamoja na Mafungu 26 ya Sekretarieti za Mikoa) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na bajeti ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya pia ulinganisho wa mpango wa bajeti wa mwaka 2025/2026 kwa kulinganisha na bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka 2024/2025. Nia ni kuonesha ukuaji wa bajeti na kungezeka kwa utekelezaji wa majukumu ya Wizara na shughuli za umma.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa kina kuhusiana na uwiano wa Mpango wa Bajeti ya Matumizi kwa Mwaka 2024/2025 pamoja na Mpango wa Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake Kamati imebaini kuwa kuna ongezeko la upangaji wa bajeti ya Wizara kutoka **Shilingi 10,298,991,877,468.00** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 hadi **Shilingi 11,780,484,202,000.00** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, sawa na ongezeko la **Shilingi 1,481,492,324,532** ambalo ni sawa na **asilimia 14.4.** Aidha, matumizi ya kawaida yameongezeka kutoka Shilingi **6,709,975,188,500.00** hadi Shilingi **7,836,140,708,000.00** sawa na ongezeko la **Shilingi 1,126,165,519,500,** sawa na **asilmia 16.7** huku matumizi ya maendeleo yakiongezeka kutoka Shilingi **3,589,016,688,968.00** hadi Shilingi **3,944,343,494,000.00** sawa na ongezeko la **Shilngi 405,326,805,032,** sawa na **asilimia 11.3**.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilibaini kuwa matumizi ya kawaida upande wa mishahara yameongezeka kutoka **Shilingi 5,524,636,066,000.00** hadi **Shilingi 6,292,557,648,000.00** Mwaka

2025/2026; sawa na ongezeko la **Shilingi 767,921,582,000**, sawa na **asilimia 13.9.** Wakati huo huo matumizi ya maendeleo kwa upande wa fedha za ndani yameongezeka kutoka **Shilingi 2,443,601,938,301.00** mwaka 2024/2025 hadi **Shilingi 2,496,431,476,000.00** Mwaka 2025/2026 sawa na ongezeko la **Shilingi 52,829,537,699** sawa na **asilimia 2.2;** huku matumizi ya maendeleo kwa upande ya fedha za nje yaongezeka kutoka **Shilingi 1,145,414,750,667.00** mwaka 2024/2025 hadi **Shilingi 1,447,912,018,000.00** mwaka Mwaka 2025/2026 sawa na ongezeko la **Shilingi 302,497,267,333** sawa na **asilimia 26.4**; kama inavyoonekana katika kielelezo Namba 16 na Jedwali Namba 8.

KIELELEZO NA 13: *Matumizi ya kawaida kwa ajili ya mishahara, matumizi mengineyo (OC) na matumizi ya miradi ya maendeleo kwa Fungu 56 – Makao Makuu ya Wizara, Fungu 02 – Tume ya Utumishi wa Walimu na Mafungu 26 ya Mikoa*



***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 16, 2025)*

JEDWALI NA 8: *Ulinganisho wa Bejeti (Fungu 56, Fungu 02 na Mafungu 26 ya Mikoa) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Hadi 2025/2026 Kwa milioni*

MATUMIZI	2023/2024	2024/2025	2025/2026
Mishahara	4,626,253.9	5,524,636.07	6,104,221.6
Oc	885,592.4	1,185,339.1	1,543,583.06
Maendeleo Ndani	2,147,686.4	2,443,601.9	2,496,431.5
Maendeleo Nje	1,120,306.2	1,145,414.8	1,447,912.02

***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 16, 2025)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na ukuaji wa bajeti ya maendeleo kwa kutumia fedha za ndani. Hii inaonesha kuwa

kama jitihada zikiendelea kufanyika kwenye upangaji wa bajeti ya maendeleo kwa kutumia mapato ya ndani Taifa litaondokana na utegemezi wa fedha za wafadhili. Aidha, Sura hii ya bajeti inatoa taswira kuwa maisha ya Watanzania yanazidi kuboreka kila mwaka. Aidha bajeti hii inaonesha kuwa Taifa letu liko kwenye mwenendo mzuri wa ukuaji wake na maendeleo ya wananchi. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuendelea kuweka mikakati inayosaidia usitawi wa wananchi nchini.

(c) Uwiano wa Mpango wa Bajeti ya Matumizi ya Wizara (Fungu 56, Fungu 02 pamoja na Mafungu 26 ya Sekretarieti za Mikoa) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Mwaka wa Fedha 2025/2026 dhidi ya Mpango na Bajeti Kuu ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Mwaka wa Fedha 2025/2026

Mheshimiwa Spika, ili kujua mwenendo wa kuzifanya shughuli za wananchi kuwa muhimu kwa maendeleo yao ya kiuchumi na kuboresha siha za wananchi Kamati ilifanya uinganisho ili kujua uwiano wa bajeti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI pamoja na Mpango wa Bajeti ya Taifa kwa mwaka 2025/2026. Nia ni kuliwezesha Bunge kuona na kutafsiri ongezeko la namba katika Bajeti ya Taifa na kuongeza huduma kwa wananchi ili kuona kama kuongezeka kwa bajeti ya Taifa kuna athari kwa Bajeti ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa Bajeti ya Taifa imeongezeka kutoka **Shilingi milioni 50,291,408** zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 hadi **Shilingi milioni 57,040,252** zilizotengwa mwaka 2025/2026. Hili ni ongezeko la **Shilingi milioni 6,748,844** sawa na **asilimia 13.4.**

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi huo, Kamati imebaini yafuatayo:-

i) Wakati Bajeti ya Taifa kwa mwaka 2025/2026 ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 13.4** bajeti ya Fungu 56, Fungu 02 na Mafungu yote 26 ya Mikoa imeongezeka kwa **asilimia 14.4.**

ii) Wakati bajeti ya Taifa ya maendeleo ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 01** bajeti ya Fungu 56, Fungu 02 na Mafungu yote 26 ya Mikoa kwa ajili ya miradi ya maendeleo imeongezeka kwa **asilimia 11.3**.

iii) Wakati bajeti ya Taifa ya matumizi ya kawaida imeongezeka kwa **asilimia 10.4,** bajeti ya matumizi ya kawaida ya Fungu 56, Fungu 02 na Mafungu yote 26 ya Mikoa imeongezeka kwa **asilimia 16.7.**

Mheshimiwa Spika, tafsiri tunayopata katika uchambuzi huu ni kuwa, ongezeko la mafungu yote kwa pamoja lililowekwa katika Bajeti ya Taifa, linawiana na ongezeko la Bajeti ya Wizara hii, Fungu 56, Fungu 02 na Mafungu yote 26 ya Mikoa. Hii inaonesha kuwa Wizara hii ni miongoni mwa Wizara zilizopewa kipaumbele katika tengeo la fedha za bajeti. Kamati inaipongeza Serikali kwa ongezeko hilo la tengeo katika Wizara hii.

JEDWALI NA 9: *Ulinganisho wa Bajeti Fungu 56, Fungu 02 na Mafungu 26 ya Mikoa Dhidi ya Bajeti ya Taifa 2022/2023 na 2023/2024 (kwa milioni)*

	2024/2025	**2025/2026**	**Ongezeko**	**Asilimia**
Bajeti Kuu ya Serikali	**50,291,408**	**57,040,252**	**6,748,844**	**13.4.**
Bajeti ya Wizara	**10,298,991**	**11,780,484**	**1,481,492**	**14.4**

***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 16, 2025)*

JEDWALI NA 10: *Ulinganisho wa Bajeti Kuu na Bajeti ya OR TAMISEMI kwa mwaka 2024/2025 na mwaka 2025/2026*

	BAJETI KUU YA SERIKALI			**BAJETI YA WIZARA**		
	2024/2025	2025/2026	%	2024/2025	2025/2026	%
Mishahara	11,767,675.1	13,174,240.5	11.9	5,524,636.07	6,292,557,648	3.46

Oc	21,618,648	24,394,605.3	12.8%	1,185,339.1	1,543,583.06	9.73
Maendeleo Ndani	12,306,921	13,320,501.9	8.2%	2,443,601.9	2,496,431.5	0.01
Maendeleo Nje	2,699,081	6,150,902.6	127%	1,145,414.8	1,447,912.02	0.26
JUMLA	50,291,408	57,040,252	13.4%	10,298,991	11,780,484	4.14

***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 16, 2025)*

SEHEMU YA TANO

5.0. MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Baada ya Uchambuzi wa bajeti, Kamatiinatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yafuatayo kwa lengo la Kuboresha Utendaji kazi wa Wizara hii katika kuwahudumia wananchi:-

5.1. Ukosefu/Upungufu wa Matundu ya Vyoo katika Shule za Msingi na Sekondari

Mheshimiwa Spika, sitara, umaridadi, na utulivu wa ujifunzaji katika ngazi za elimu ya msingi na sekondari ni jambo muhimu la kuzingatiwa ili kujenga taifa lenye siha njema. Ili kulifanya taifa likue na kusitawi kwa utulivu mazingira ya kujifunza ambayo mtoto anakua nayo ni muhimu yawe mazuri na yenye kuleta utulivu wa akili wakati wote wa maisha ya mtoto mwanafunzi katika ngazi ya shule za msingi na sekondari.

Kamati inaona kuwa suala la kuzungumzia matundu ya vyoo kwa karne tuliyo nayo ni fedheha kwa taifa letu. Aidha, wakati wa ukaguzi wa miradi ya elimu nchini katika baadhi ya halmashauri

Kamati imebaini kuwa kuna baadhi ya shule za msingi na sekondari zina vyoo vyenye hadhi ya chini sana.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza sana Serikali kwa uwekezaji mkubwa sana wa ujenzi wa majengo ya shule mbalimbali za msingi na sekondari. Hata hivyo, wakati wa uchambuzi wa taarifa za bajeti za halmashauri mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati, Kamati ilibaini kuwa kuna upungufu mkubwa wa matundu vya vyoo katika shule nyingi. Kamati inaona kuwa hali hii si nzuri kwa usitawi wa taifa la Tanzania. Kutokana na hali hiyo Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

i. Serikali ifanya tathmini ili kubaini ukubwa wa tatizo la upungufu wa matundu ya vyoo katika shule zake zote za msingi na sekondari nchini;

ii. Serikali ifanye tathmini ya ubora wa vyoo katika shule zake zote za msingi na sekonda nchini (hasa kwenye shule kongwe);

iii. Serikali iweke mkakati wa kumaliza kabisa tatizo la vyoo katika shule zake za msingi na sekondari nchini. Aidha, kila mkoa na halmashauri zake zote zenye upungufu wa vyoo zisimamiwe kwa kuweka mkakati wa kutatua na kukomesha kabisa tatizo laa ukosefu pamoja na ubora hafifu wa vyoo katika shule zake za msingi na sekondari nchini.

5.2. Utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia fedha zinazotokana na kampuni za uwekezaji kurudisha huduma kwa wananchi (Corporate Social Responsibilities – CSR)

Mheshimiwa Spika, kampuni zinazowekeza katika miradi na biashara mbalimbali nchini zina utaratibu wa kurejesha kwa jamii faida inayotokana na uwekezaji wao *(Corporate Social Responsibilities – CSR)*. Katika uchambuzi wake wa taarifa mbalimbali za halmashauri zilizowasilishwa na Wizara ya TAMISEMI wakati wa uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2024/2025 pamoja na mpango wa mapato na matumizi

kwa mwaka 2025/2026 kwa mafungu 26 ya mikoa Kamati imebaini kuwa kuwa kuna shida kubwa kwenye taratibu za kutoa, kupokea, na kutumia fedha hizo zinazotokana na *CSR*. Kamati imebaini kuwa Mkoa wa Geita pekee una takribani Shilingi bilioni 18 zinazotokana na *CSR* ambazo hazijatumika kwa sababu mbalimbali, ikiwemo mkwamo wa kimanunuzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa suala la utekelezaji wa miradi kwa kutumia fedha zinazotokana na *CSR* bado lina changamoto nyingi za kiutekelezaji. Hali hii inasababisha wananchi kutokupata faida na thamani ya fedha inayotokana na *CSR (value for money)*. Kutokana na hali hiyo Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

i. Serikali isimamie fedha zote zinazotokana na *CSR* zitolewe kwa wananchi kama sheria inavyotaka;

ii. Serikali iunde Kamati ndogo itakayokuwa na jukumu la kufanya utafiti wa kutosha na kutoa maoni kuhusu namna bora ya utoaji na matumizi ya fedha zinazotokana na *CSR*. Kamati hiyo pamoja na taa ama wizara nyingine zinazohusika ihusishe Wizara ya TAMISEMI (Hasa Mamlaka za Serikali za Mitaa; na iii. Serikali ione kama kuna haja ya kuipitia na kuifanyia marekebisho Sheria inayosimamia utoaji na matumizi ya fedha za *CSR* nchini.

5.3. Uimarishaji wa vyanzo vya mapato katika Halmashauri nchini

Mheshimiwa Spika, Kamati nyakati zote imekuwa ikiishauri Serikali kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mikakati mbalimbali ya kubuni na kuibua vyanzo mbalimbali vya mapato kwa ajili ya kuongeza wigo wa ukusanyaji wa ushuru ili buboresha mapato ya ndani kwa ajili ya manufaa ya halmashauri husika. Kamati inazipongeza baadhi ya halmashauri kwa kuwa wabunifu wa uanzishwaji na ukusanyaji wa ushuru huo. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa bado halmashauri nyingi nchini, isipokuwa halmashauri za majiji) bado zinategemea sana mapato

yanayotokana na mazao ya kilimo kutoka kwa wananchi na hivyo wananchi hao kutokupata faida nzuri ya mazao yao kutokana na mzigo kubwa wa ulipaji wa ushuru.

Kutokana na hali hiyo Kamati inashauri Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kuendelea kufanya ubunifu wa vyanzo vingine vya mapato mbali na tozo za ushuru wa mazao, na ambavyo havitawakandamiza wananchi.

5.4. Uboreshaji wa mazingira ya kupumzika wananchi

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuyapongeza sana majiji nchini Tanzania, Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Dodoma, Mbeya na Tanga. Hata hivyo Kamati imebaini kuwa maeneo mengi ya majiji hayo hayana maeneo ya mapumziko (leisure, play and recreations places) ambapo wananchi wanaweza kupumzika mara baada ya shughuli za kulijenga Taifa. Kamati inashauri majiji kuweka mikakati ya kutengeneza maeneo mengi kwa ajili ya kuwezesha wananchi kupata mapumziko mara baada ya kazi nzito. Hii itasaidia sana kuleta afya ya akili kwa wananchi.

Majiji yaanze kufikiria Maeneo ya kupumzikia ya jamii *(Community recreation centers)* yana umuhimu mkubwa sana katika kuongeza na kuboresha thamani ya maisha kwa jamii. binadamu anahitaji kupumzika; iwe ni kwa ajili ya uimara wa mwili, au akili mara baada ya kazi za kutwa nzima (kwa walio wafanyakazi ama wafanyabiashara) au kwa wanafunzi katika ngazi mbalimbali za elimu wanahitaji maeneo ya kupumzikia ya jamii *(Community recreation centers)*. Maeneo ya mapumziko kwa ajili ya jamii yakiwa ya kutosha kuna uwezekano mkubwa wa kuboresha afya ya akili kwa jamii na hivyo kujenga taifa lenye utulivu na usitawi kwa maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati imebaini kuwa kuna upungufu mkubwa sana wa maeneo ya kupumzikia wananchi mara baada ya shughuli mbalimbali za siku nzima. Kamati inapongeza baadhi ya majiji kama vile Dar es Salaam na Arusha kwa kujaribu kutenga maeneo na kuyajenga kwa ajili ya

wananchi kupumzika. Hata hivyo, kutokana na wananchi kuendelea kuongezeka kwa kasi maeneo ya kupumzikia wananchi yanazidi kuwa machache. Kutokana na hali hiyo Kamati inatoa ushauri ufuatao.

i. Miji na majiji yote nchini kuweka mkakati wa kutenga maeneo mahsusi kwa ajili ya mapumziko ya wananchi. Maeneo hayo yatengwe kwa kuzingatia umbali kutoka eneo moja kwenda lingine ili kuwapa wananchi uwezekano wa kuyafikia kiurahisi;

ii. Serikali iandae mwongozo wa utengaji, uendelezaji na kuyalinda maeneo hayo ili yasipangiwe matumizi mengine.

5.5. Ununuzi wa vifaa vya maabara kwa ajili ya maabara za sekondari nchini

Mheshimiwa Spika, Kamati inampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uthubutu wake na kuweza kujenga shule nyingi za sekondari, na hasa Sekondari za Wasichana za Mikoa, na sasa Sekondari za Wavulana za Kanda. Kamati inapongeza zaidi hasa baada ya shule hizi za Sekondari za Wasichana za Mikoa kuwa Maalum kwa ajili ya kufundisha watoto wa kike sayansi, na hivyo kuongeza idadi kubwa ya wanansayansi nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa ili masomo ya sayansi yafundishwe vyema, na ili wanafunzi hawa waweze kuielewa vyema sayansi ni muhimu sana kuwepo na maabara pamoja na vifaa vyote vya maabara kwwenye shule zote. Hata hivyo, Kamati wakati wa ukaguzi wake kwenye miradi mbalimbali ya shule hizi imegundua kuwa hakuna kabisa vifaa vya maabara. Aidha Kamati imebaini kuwa asilimia kubwa ya shule hizi tayari zimekwishadahili wanafunzi wanaosoma katikashule hizi, na kwamba wengine wanatarajia kufanya mitihani yao ya mwisho mwezi Mei mwaka huu wa 2025.

Kamati inahofu kuwa wanafunzi hao kama Serikali isipokuwa na mpango wa dharura, watafanya mirihani yao bila kuwa na uwezo wa kufanya mitihani ya mafunzo kwa viendo (practical) kutokana na kutokuwepo kwa maabara. Kutokana na hali hiyo Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

i. Serikali iweke mpango makakati wa dharura wa kuhakikisha kwamba inapeleka vifaa vya maabara kwenye shule hizi zote 26 za wasichana za mikoa; bila kuathiri mipango iliyowekwa ya upelekaji wa vifaa vya maabara katika shule nyingine za sekondari nchini;

ii. Kwa kuwa tatizo la uhaba wa vifaa vya maabara katika shule za sekondari nchini ni la muda mrefu na linaonekana kuwa gumu, Kamati inashauri Serikali itenge fungu maalum kwa kutumia chanzo maalum na cha kudumu kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maabara kwa ajili ya shule za sekondari nchini; wakati wote vinapohitajika.

5.6. Ujenzi wa shule za michepuo ya kiingereza katika Halmashauri nchini

Mheshimiwa Spika, wakati wa uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara (Fungu 56) Fungu 02 na Mafungu26 ya Sekretarieti za Miko) Kamati ilibaini kuwa Halmashauri nyingi zimeanza kujikita katika ujenzi wa shule maalum za msingi za mchepuo wa kiingereza *(English Medium School)* kwa kutumia fedha ya Serikali na kutoza ada kubwa kwa wanafunzi wanaokuja kusoma katika shule hizi.

Kamati haikuridhika kabisa na utaratibu wa Halmashauri kujikita katika ujenzi wa shule hizi na kutoza ada kubwa. Kamati inaona kuwa kufanya hivyo kunaondoa usawa wa upatikanaji wa elimu kwa Watanzania na hivyo kujenga madaraja nchini. Hii si dhamira ya Serikali na si tamko la Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023. Kwa sababu hiyo, Kamati inashauri kwamba: -

i. Halmashauri kuacha kabisa kujihusisha na ujenzi wa shule hizi kwa kutumia fedha yoyote ile ya Serikali na kuzitoza ada kubwa kwa kuwa inakwenda kinyume na mipango ya Serikali ya utoaji wa elimu bure kwa shule za sekondari;

ii. Kama kuna ulazima kwa halmashauri yoyote ile kuanzisha shule za mchepuo wa Kiingereza iombe kibali kutoka Wizara ya TAMISEMI, na TAMISEMI ieleze sababu za msingi zinazolazimisha uanzishwaji wa shule za mchepuo wa Kiingereza katika halmashauri husika,

iii. Aidha, kama pia ni lazima shule hizi kuanzishwa, Kamati inashauri halmashauri ianzishe shule hizi zikiwa na utawala wake tofauti, zisitumie rasilimali watu ya aina yoyote kutoka Serikalini.

iv. Serikali iwarejeshe walimu wote wazuri waliochukuliwa kutoka shule ze umma na kupelekwa kwenye shule hizi maalum za mchepuo wa kiingereza katika shule zao za awali ili waendelee kuinua ubora wa elimu katika shule hizi za umma.

5.7. Uzalishaji wa madeni makubwa ya watumishi katika Halmashauri

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa halmashauri nyingi zimekuwa zikizalisha madeni makubwa bila kuyalipa na hivyo kuiweka Serikali kwenye wakati mgumu wa utekelezaji wa majukumu yake. Kamati ilihoji sababu ya uwepo wa madeni hayo na kutaarifiwa kuwa ni sababu ni pamoja na malipo ya uhamisho wa watumishi pamoja na posho mbalimbali za watumishi katika halmashauri husika. Kwa mfano Mkoa wa Dodoma peke yake umezalisha madeni yenye thamani ya Shilingi bilioni 12 yanayotokana na utumishi. Haya ni makubwa mno. Hii ni dalili mbaya sana. Kutokana na changamoto hii kutishia usitawi wa halmashauri nchini Kamati inashauri kama ifuatavyo: -

i. Serikali kuweka mkakati wa ulipaji wa madeni haya kwa wakati ili kuziweka huru halmashauri;

ii. Serikali kusimamisha uzalishaji wa madeni mengine ya namna yoyote ile katika halmashauri hadi pale madeni yaliyozalishwa awali kuwa yamekwishakulipwa kwa walau asilimia 50.

5.8. Mwongozo wa utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu

Mheshimiwa Spika, Kamati imeabini kuwa utaratibu wa utengaji wa fedha (asilimia 10 ya mapato ya ndani) unatofautiana kati ya Halmashauri moja na nyingine. Kuna Halmashauri ambazo zinazotenga fedha hizo kwa kutumia mapato ya ndani yote na kuna halmashauri ambazo zinatenga kwa kutumia mapato ya ndani yaliyotengwa kwenye fungu la maendeleo. Utengaji huu wa mapato kwa kutofautiana kunaleta mkanganyiko wa uelewa wa utekelezaji wake kitaifa. Kwa sababu hiyo, Kamati inashauri kuwa Serikali itoe mwongozo mmoja utakaotumika katika kwa ajili ya kutenga fedha hizo katika halmashauri zote nchini.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu kwako kwa fursa uliyonipa ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati lakini pia kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu. Ninawashukuru sana Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa (Mb) – Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Zainab Athumani Katimba (Mb) – Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Mheshimiwa Festo John Dugange (Mbe) – Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa kwa ushirikiano wanaoipa Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Wizara ya TAMISEMI, Ndg. Adolf Ndunguru, Naibu Makatibu Wakuu Ndg. Eng. Ndg. na Ndg. Sospeter Mtwale pamoja na watendaji wote wa Wizara na taasisi zake kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati tangu tulipoanza kufanya nao kazi na kushiriki vizuri kwenye uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kipekee ninawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Mheshimiwa Jafari Wambura Chege (Mb), Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa ushirikiano mzuri ambao wananipa. Wajumbe hawa ni wachapa kazi na wameshiriki kikamilifu katika uchambuzi wa bajeti na kuhakikisha wanahoji ili kupata ufafanuzi wa kina. Ninawapongeza sana na ninaomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wetu wa Bunge Baraka Idelphonce Leonard kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema na kwa kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu ikiwemo Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja, **Fungu 56, 02, 36 ,47, 54, 63, 70, 71, 72, 79, 74, 75, 76, 77, 78, 79, 80, 81, 82, 83, 84, 85, 86, 87, 88, 89, 90, na 95** jumla ya **Shilingi trilioni kumi na moja bilioni mia saba themanini na mbili milioni mia tisa themanini nane mia mbili na mbili elfu (11,782,984,202,000).**

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, naunga mkono Hoja.

SPIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, tunakushukuru sana kwa kuwasilisha Maoni ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge inayosimamia hii Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo majina hapa ya Wabunge ambao wameomba kuchangia kwa siku ya leo, kama ilivyo ada. Kabla hatujaanza na huo uchangiaji, wapo wageni waliopata fursa ya kuingia baada ya tangazo la wageni la awali. Nitawatangaza hao wageni kisha tutaendelea na ratiba yetu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na wageni waliopo Jukwaa la Spika; kwanza, ni wageni wangu wanne; hawa ni

Watendaji Wakuu kutoka *Access Bank*. Yupo Ndugu Imani John, Mkurugenzi Mtendaji wa benki; yupo Ndugu Joyce Malai, Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wadogo; Ndugu Abdulrahman Nkondo, Mkuu wa Kitengo cha Taasisi za Serikali na Ndugu Anna Wesiwasi, Mkuu wa Tawi la Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine waliokaa Jukwaa la Spika ni wageni wa Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Hawa ni Waheshimiwa wakuu wa mikoa mbalimbali nchini Tanzania. Tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Balozi Batilda Buriani, Mkuu wa Mkoa wa Tanga; Kanali Ahmedi Abbas, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma; Kamishna wa Polisi Mstaafu, Mheshimiwa Thobiasi Andengenye, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma; Mhe. Daniel Chongolo, Mkuu wa Mkoa wa Songwe; Mheshimiwa Nurdini Babu, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro; Mheshimiwa Queen Sendiga, Mkuu wa Mkoa wa Manyara na Mheshimiwa Said Mtanda, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo Mheshimiwa Anamringi Macha, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga; Mheshimiwa Martine Shigela, Mkuu wa Mkoa wa Geita na Mheshimiwa Paulo Chacha, Mkuu wa Mkoa wa Tabora; sitafafanua hayo makofi ni kwa ajili ya nini, lakini najua Waheshimiwa Wabunge wote wanawaza uchaguzi kwa sasa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia, tunaye Mheshimiwa Mwanamvua Mrindoko, Mkuu wa Mkoa wa Katavi; Mheshimiwa Makongoro Nyerere, Mkuu wa Mkoa wa Rukwa; Mheshimiwa Dkt. Juma Homela, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya; Mheshimiwa Antony Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Njombe; Mheshimiwa Peter Serukamba, Mkuu wa Mkoa wa Iringa; Mheshimiwa Kenani Kihongosi, Mkuu wa Mkoa wa Simiyu na Mheshimiwa Adam Malima, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro. Karibuni sana. Hawa wamekuja kwa uwakilishi wa mikoa yote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni wengine wa Mheshimiwa Mchengerwa. Kwanza ni, Wenyeviti wa Chama Cha Mapinduzi wa Mikoa; hawa sijui wamekaa upande gani?

Wapo Makatibu Tawala wa Mikoa, Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi Taifa, Makatibu wa Chama Cha Mapinduzi wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya, wakurugenzi na watendaji kutoka TAMISEMI, Wenyeviti wa Halmashauri na Madiwani wa Halmashauri ya Mji Rufiji. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia, wapo wageni 105 wa Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, ambao ni wanafunzi kutoka Vyuo Vikuu vya Mkoa wa Dodoma. Karibuni sana.

Wageni wengine watatangazwa kwa kadri watakavyopata nafasi ya kuingia Bungeni.

Sasa tunaanza na uchangiaji. Tutaanza na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, atafuatiwa na Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga ajiandae. *(Makofi)*

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kukushukuru kunifanya mchangiaji wa kwanza na nianze kwa kusema naunga mkono hoja kwa sababu, labda nitasahau baadaye. Hotuba yangu ya leo ambayo ni Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, na wote tunaelewa TAMISEMI ndiyo suluhisho la maisha ya Watanzania, Mheshimiwa Waziri amesema hivyo, ninaomba niigawe mara tatu.

Mheshimiwa Spika, nitaanza kwa shukurani kwa Serikali; pili, nitasema na Serikali kwa dhati kabisa na kwa unyenyekevu mkubwa. Tatu, kama nafasi itatosha nitamwambia Mheshimiwa Rais jambo fulani kubwa sana, akiwa ndiye kiongozi mkuu wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa shukurani kwa Serikali. Kwanza, Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe kwamba, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aliingia madarakani tarehe 19 Machi, 2021. Kwa hiyo, sasa hivi tunzungumza kwamba, Mheshimiwa Rais Samia amemaliza kipindi cha miaka minne. Hakuna Mbunge hata mmoja atakayesimama hapa ndani

aseme Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali ya Awamu ya Sita haikufanya kazi kubwa sana, hayupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niseme ukweli. Ninatoka Mkoa wa Kilimanjaro, una majimbo tisa na kila Mbunge wa Jimbo la Mkoa wa Kilimanjaro anajivunia kazi zilizofanywa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, alipoapishwa ile tarehe 19 Machi, alimtuma Waziri Mkuu jimboni kwangu baada ya mimi kulalamika sana kuhusu ubovu wa jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alifika tarehe 24 mwezi wa tisa, mwaka 2021. Waheshimiwa Wabunge ukimuona Waziri Mkuu amekuja kwako, kama ni Mbunge wa Jimbo, ambaye uko makini ni lazima utachukua nafasi hiyo kusema matatizo ya wananchi wako wote. Yote utayasema, nilisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati huo Waziri Mkuu amekuja jimboni kwangu nilikuwa nina kituo cha afya kimoja, Kituo cha Ndungu, kilikuwa hakina hata *mortuary* ya kuhifadhi maiti. Baada ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuingia madarakani naomba niwaambie ukweli, hapa niliposimama, upande wa afya, jimbo langu lina sura gani?

Mheshimiwa Spika, kwanza, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, na Serikali ya Awamu ya Sita walinijengea Kituo cha Afya cha Mamba Miamba, nikajengewa Kituo cha Afya cha Mtii. Hapa ninapozungumza ninajengewa Kituo cha Afya cha Vunta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mnione mimi ambaye Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, alipoingia sikuwa na kituo cha afya hata kimoja, leo nina vituo vya afya vitatu. Ameniletea *ambulance* tatu, ameniwekea *mortuary* kwenye Kituo cha Afya cha Ndugu. Hivi wananchi wanataka tusimsifu Mheshimiwa Rais Samia? Hapana, anastahili sifa. Waheshimiwa, wananchi huko nje na wote wanaotusikiliza ninaomba niseme kwa nguvu zote,

Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amefanya makubwa sana kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba niseme na Serikali. Hii nchi ina majimbo korofi, lakini katika majimbo korofi, naomba nirudie, Jimbo la Same Mashariki ni jimbo korofi. Jimbo lina tarafa tatu; tarafa mbili ni za milimani mno Waheshimiwa Wabunge. Siyo miinuko, *no,* ni milimani. Wananchi hawa ni wakulima na wana bidii sana.

Mheshimiwa Spika, tena niwaambie Waheshimiwa Wabunge, mimi sina wananchi walevi, nina wananchi wakulima. Wanapoamua kunywa wanakunywa, kupumzika baada ya kazi, lakini siyo ulevi. Sasa tatizo langu kubwa, hili jimbo ni korofi na ukorofi wa jimbo langu ni barabara. Tarafa ya Gonja ina kata nne: Kata ya Vuje, Kata ya Bombo, Kata ya Mtii na Kata ya Luguru. Tarafa hii ina barabara sita. Barabara ya kwanza Maorevuje, barabara ya pili Ndungulugulu, barabara ya tatu Kisangaze – Vumbamtii, barabara ya nne Mpirani – *Dispensary* – Ridindimo, barabara ya tano Maore – Kalungoyo, barabara ya sita Mpirani – Bombo. Niliposimama hapa nikizungumza barabara zote hizi hazipitiki. Ninaishukuru Serikali tena naishukuru mno kwa sababu ilinipatia fedha nyingi sana za kujenga hizi barabara. Tulipewa fedha, lakini jimbo langu lina mvua kubwa sana, milimani kule, barabara hizi zote ninavyosema hapa sasa hivi zote hazipitiki, si kwa pikipiki wala si kwa magari, wananchi wanabeba mizigo kwa shida sana.

Mheshimiwa Spika, jumatatu juzi tarehe 14 Aprili, 2025 wananchi wa Tarafa ya Gonja hapa Lugulu hapa waliamua nao sasa waingie kutengeneza Barabara ya Ndungu - Lugulu. Nimemletea video kwenye *WhatsApp* yake Mheshimiwa Waziri na ameisoma. Nimemletea picha zingine tatu za barabara. Wananchi wameamua kuingia watengeneze barabara wenyewe, vijana zaidi ya 180. Hili si jambo la kawaida kwa sababu Tarafa ya Gonja yote imefunga.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimwambie ukweli kuwa tunajua mimi na wananchi wangu wanajua kwamba wametupa

fedha nyingi sana, lakini sasa wamekwama. Tarafa ya Gonja wote wanakaa kule Gonja wanalima tangawizi, wanalima ndizi hawawezi kupeleka mazao kwenye masoko madogo wala makubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa nina ombi, Mheshimiwa Mchengerwa nina ombi kwa Serikali, nimeleta picha umeona ni kiasi gani wale wananchi wanahangaika pale Lugulu. Ninaomba ili hawa wananchi wa Tarafa ya Gonja japo wapate njia. Ninaomba uongee na *TARURA* mkoa, ongea na Victor, huyu Mkurugenzi wetu mzuri sana ambaye ameketi huko juu; wawapatie hawa wananchi msaada mdogo wawakomboe wananchi wangu wa Tarafa ya Gonja. Ninaona huruma, mimi ni Mbunge wao, ninahangaika nao. Ninaomba niseme ukweli *TARURA* Mkoa wa Kilimanjaro na Wilaya ya Same wanafanya kazi sana, tatizo hakuna fedha sasa hivi. Narudi kwako Mchengerwa, kwa unyenyekevu waangalie hawa wananchi wa Lugulu kwa sababu nimekuletea picha.

Mheshimiwa Spika, nina Tarafa nyingine ya Mambavunda. Hii Tarafa ya Mambavunda Barabara inaanzia Hedaru – Vunda - Miamba mpaka Ndungu. Ninaomba niipongeze Serikali, ahsanteni sana. Ninapoongea sasa hivi mkandarasi yupo kazini anafanya kazi. Ombi langu kwa Mheshimiwa Mchengerwa ni kwamba hii barabara sasa tafadhali wapeleke fedha za kutosha ili iwekwe zege kwenye sehemu zote korofi. Hawa wananchi wa kata tano wamechoka kusafiri kwa pikipiki au na mafuso. Ile barabara waipelekee fedha ili wananchi wangu waweze kusafiri na magari.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimalizie lile nililoomba kumwambia Mheshimiwa Rais. Hili neno ninamwambia Mheshimiwa Rais wetu kama kiongozi wa nchi yetu. Mheshimiwa Rais Samia tarehe 17 Septemba, 2024, alikuja Mkoa wa Kilimanjaro…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ANNE K. MALECELA: Hii ni kengele ya mwisho? Namalizia mama.

SPIKA: Ndiyo ni ya mwisho, dakika moja.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alikuja Mkoa wa Kilimanjaro akasema neno kubwa sana, ninaomba kumnukuu: "Kule kwetu kuna watu wanaitwa Mahulukutabu, watu hawa hawapendi utulivu wala raha. Mheshimiwa Rais akaendelea kusema kwamba, "tutailinda amani na utulivu wa nchi yetu, tutailinda kwa gharama yoyote ile" *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba sisi Wabunge wote tumwambie Mheshimiwa Rais tunamuunga mkono katika kulinda amani ya nchi yetu hatutalala tutashirikiana naye katika kuilinda amani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma ajiandae.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kushukuru sana kwa kupata fursa ili niweze kuchangia Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Pia nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wote wawili, pamoja na Katibu Mkuu na wataalam wote kwa kazi kubwa na nzuri sana wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, nitajielekeza kwenye mambo manne. Jambo la kwanza nitazungumzia Mradi wa *TACTIC*, mradi ambao Dkt. Samia Suluhu Hassan ametafuta fedha kupitia *World Bank,* tumezipata na unakwenda kubadilisha Jiji la Arusha. Barabara za Engosheraton pamoja na Barabara ya Olasiti zimekwishaanza. Ninaomba tu Mheshimiwa Waziri afahamu tu kwamba mkandarasi anasuasua, yuko *very slow* japokuwa fedha zipo. Kwa

hiyo ningeomba ofisi yake ikaongeze nguvu kwenda kumsukuma ili matunda haya watu wa Arusha waweze kunufaika nayo.

Mheshimiwa Spika, pili, kupitia Mradi wa *TACTIC* pia tuliweza kupata *component* ya kujenga Stendi ya Kisasa Jiji la Arusha, kujenga Soko la Kilombero na Soko la Morombo na tarehe 19 Januari, 2024 *tender* ilitangazwa. Jana Mheshimiwa Naibu Waziri ametujibu hapa kwamba mchakato ule ulifutwa kwa sababu mtu aliyepatikana hakuwa na kigezo. Nimeona pale palikuwa na usimamizi hafifu wa wataalamu. Kama wametangaza mwezi Januari mpaka kufika mwezi Juni wangeshajua kama mtu hana kigezo na wakatangaza mtu mwingine aombe, wakasubiri mpaka mwaka mzima ukaisha wakaja kutangaza mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, ningeomba Wizara yako ingekaa karibu sana na wale ambao wanasimamia mradi huu ili uweze kukamilika na kuanza kwa wakati na jana wametupa ahadi kwamba kufikia mwezi Mei, mkandarasi atakuwa *site;* na mimi Mheshimiwa Waziri sina mashaka na wewe kwa sababu alikuja pale Esolongido baada ya kuzungumza kipindi fulani hivi, tumeona yule mkandarasi yuko *site* na kazi inaendelea. Tunaomba na hili pia la stendi mkaliwekee nguvu ili mwezi Mei, 2025 mkataba usainiwe na tumeone mkandarasi akiwa *site*.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili nina angalizo moja tu, kwenye Mradi wa *TACTIC* tunataka tujenge barabara ya lami kutoka eneo la Stendi kuja Barabara ya Mbauda, lakini *TANROADS* pia wamesaini mkataba wa kilometa 70 kutoka kona ya Mbauda kwenda mpaka Oljoro, eneo ambalo ni hilo hilo. Kwa hiyo ninaomba wakae na *TANROADS* waangalie ili kama wao wanajenga hizo fedha zikiokolewa ziende zikaondoe changamoto nyingine ya barabara kwenye maeneo mengine ya Jiji la Arusha.

Mheshimiwa Spika, tunatamani pia Barabara yetu ya Lemala ambayo ina *TBL-TANESCO* pia iingie kwenye Mradi wa *TACTIC* ili iweze kuondoa changamoto hiyo. Pia Barabara ya Kibo na yenyewe iweze kumaliziwa. Vile vile Barabara ya kutoka Engosheraton kwenda mpaka kule upande wa Daraja Mbili.

Mheshimiwa Spika, suala la pili Mheshimiwa Waziri na hili nitaomba anivumilie kidogo, kwa sababu ninaamini mtu ukiwa mnafiki ukiwa kijana, ukizeeka ni lazima utakuwa mchawi na uchawi siyo sifa nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, Arusha wanajenga jengo la utawala, jengo ambalo baadhi ya viongozi wake wanalipigia debe sana. Ninataka nimwombe atume timu yake ikakae pale ikaangalie kinachoendelea pale ndani. Katika jengo la utawala kwanza gharama zake za jumla hazipungui shilingi bilioni tisa; jengo la *floor* nane unajenga kwa shilingi bilioni tisa maana yake ni kwamba kila *floor* moja ni bilioni moja na ushee, kitu ambacho kwa akili ya kawaida hakiwezekani.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia wameingia mkataba juzi juzi hapa wa shilingi bilioni 6.2. Katika mkataba ule kuna baadhi ya vipimo walivyoandika kwenye *BOQ* na kwenye utekelezaji ni tofauti. Wameandika kwenye *BOQ* wana vipimo vyao ni *1128-meter square*, mkandarasi ame-*quote kwa 1128 cubic meter* ambayo imeongeza gharama ya shilingi milioni 252. Wameandika vipimo vyao ni hiyo *7,034-meter square*, mkandarasi ame-*quote* kwa *7,034-meter square* gharama zimeongezeka kwa shilingi bilioni 1.5.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wameingia mkataba wa shilingi bilioni 6.2 gharama halisi zilitakiwa ziwe shilingi bilioni 3.4, kuna ziada ya zaidi ya shilingi bilioni nane. Leo wananchi wa pale Arusha wanapata tabu, vivuko ni shida, barabara za ndani ni shida, watu wanachezea fedha namna hii. Badala viongozi waliowaamini kusimamia na wao wanakwenda kushabikia.

Mheshimiwa Spika, mimi nimemwambia Mheshimiwa Waziri mara nyingi, kwamba sijawahi kuwa na mashaka na usimamizi wake tangu akiwa Wizara ya Michezo, Utumishi na alivyokuja TAMISEMI. Ninaomba aongeze jicho la ziada kwenye usimamizi wa miradi; kwa sababu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anatafuta fedha dunia nzima kwa ajili ya Watanzania. Badala ya kuzisimamia vizuri zinakwenda kuliwa na watu wachache, hilo

jambo halikubaliki. Utasikia Mbunge anagombana na kila mtu, ni kwa sababu ujinga wa namna hii, ninaachaje kugombana na kila mtu? Kwa sababu nimechaguliwa pale kulinda maslahi ya watu, hasa watu wanyonge. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri atusaidie kwa sababu hili jambo ni jambo *very serious.* Kwa mfano hawa wenzetu wa *PPRA* wana *evidence* ya hili jambo ninalolizungumza, lakini hatua hazichukuliwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuliwaambia kuwa kuna wizi ulifanyika pale *CAG* akaleta timu pakawa na *special audit,* madudu ya kufa mtu, hakuna watu waliochukuliwa hatua, wanafanya kuzugazuga tu, wanasimamishwa kidogo, utapigwa siku ngapi, lakini hatua *serious* hakuna. Zile ni fedha za walipa kodi, ni fedha za Watanzania. Kwa hiyo, hili jambo namwomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu nasisitiza kwamba sina mashaka naye, ni imani yangu kwamba atakwenda kuhangaika nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ni kuhusu *TARURA*. *TARURA* bajeti yake Jiji la Arusha ni shilingi bilioni 4.39, ndiyo bajeti ya *TARURA*. Hapa tunaona watu wanachezea shilingi bilioni tisa kujenga jengo moja tu, hizi fedha zingekwenda kwenye barabara na kwenye vivuko haya makelele unayoyasikia Arusha leo yasingekuwepo. Wanataka zije huku kwa sababu wanajua ni rahisi kuzila na wanashirikiana, ni *team work* kwenye kulimaliza lile Jiji la Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina ushauri kwamba mapato ambayo yanapatikana kwenye majiji yetu, hasa haya makubwa, kama Arusha, Mbeya, Dar es Salaam na Mwanza, hebu wakae na watu wa halmashauri wasipange bajeti ki-*traditionally,* wapange bajeti kulingana na changamoto za watu. Leo kule kuna shida ya vivuko, leo kuna shida ya barabara, wanakwenda kutenga fedha shilingi bilioni 1.6 kwa Jiji la Arusha eti kwa ajili ya kwenda kubomoa eneo la stendi ndogo, eneo ambalo linaiingizia mapato halmashauri shilingi milioni 800 kwa mwezi, leo wanakwenda kulibomoa eti wajenge jengo lingine ambalo tayari kuna mapato wanayapata pale. Kwa nini hii shilingi bilioni 1.6 isingekwenda kujenga barabara? Kwa nini hii shilingi bilioni 1.6 isingekwenda kujenga vivuko ili tuondoe changamoto kwenye maeneo yetu?

Mheshimiwa Spika, wanafanya hivyo kwa sababu wanajua wakibomoa pale wakijenga kila mtu atapata kibanda kimoja kimoja au atapata vitu vingine; maslahi binafsi, hawaweki maslahi ya umma kwenye eneo hili. Jambo hili nilisema kwenye Kamati ya Mheshimiwa Waziri na maeneo mengine. Kwa hiyo wanakwenda kubomoa majengo pale na wanatumia shilingi bilioni 1.6, kitu ambacho kiko ndani ya uwezo wa wa Mheshimiwa Waziri; na Mheshimiwa Waziri anaweza akatusaidia kwenye jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, wanataka pia kujenga ukumbi kwa zaidi ya shilingi bilioni tatu. Pale wana *AICC,* ndiyo kazi yao, kwenye masuala ya ukumbi na vitu vingine. Sisi tumejenga jengo letu la halmashauri pale, kuna kumbi zetu za mikutano na vitu vingine. Badala ya sisi kujielekeza kwenye shughuli za maendeleo tunataka tena shughuli nyingine huku za ukumbi na nini; kwa sababu gani? Wanajua tu kwamba shilingi bilioni 3.4 ambayo wamemsainisha mtu watakula mle ndani. Si kwamba wanabuni na kwamba wanalipenda jiji. Maeneo ambayo yanatatua shida za watu fedha hazipelekwi.

Mheshimiwa Spika, wewe leo unaenda kwenye kivuko ambacho kinahitaji gharama ndogo tu, pengine shilingi milioni 50, fedha hazipatikani, lakini unachukua fedha hizo hizo unakwenda kubomoa sehemu ambayo inakupa shilingi milioni 800, stendi ndogo, unaweka shilingi bilioni 1.6 huku hujamaliza shida za wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninaomba kwa kweli tusaidiane kwa sababu tunayo dhamana na jukumu la kumaliza shida hiyo; kwa sababu kuna kama Kituo cha Afya Mkonoo, Mheshimiwa Rais Samia amepeleka pale zaidi ya shilingi milioni 800. Kilikuwa ni kizahanati leo ni kituo kikubwa, lakini kuna barabara mbovu. Tungeweza kuokoa hii 1.6 tungeweka lami pale kwenye kituo cha afya, watu wakaenda zao wakapata huduma na wakaendelea kula matunda ya Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa pia na changamoto barabara yetu ya *AFCON* ile Barabara ya Njolo, kule tunakojenga uwanja wetu wa kisasa wa mpira nako pia barabara ni mbovu. Ni

imani yetu kwamba kupitia bajeti hii tutakwenda kuliangalia ili tuondokane na hizo changamoto.

Mheshimiwa Spika, kingine Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amepeleka shilingi milioni 500 kwa ajili ya kujenga soko la wamachinga miaka miwili iliyopita, mpaka leo hazijatumika. Sasa unajiuliza Arusha hakuna Wamachinga? Kwa nini hela hazijatumika? Katika hali ya kawaida ukienda kwenye masoko, angalia soko la Mbauda pale matope matupu. Milioni 500 ipo Mheshimiwa Rais ameleta lakini imekaa tu. Nenda Soko la Machinga Namba 68 matope matupu, mapaa yale hayaeleweki, milioni 500 ipo ina miaka miwili Mheshimiwa Dkt. Samia ameleta lakini hakuna ambacho kinaendelea pale.

Mheshimiwa Spika, nenda Soko la Samunge hali ni mbaya, karibuni kila mahali. Sasa unajiuliza hao waliowapeleka kwenda kusimamia maendeleo kule wanafanya kazi yao ipasavyo au wana ajenda zao nyingine?

Mheshimiwa Spika, ninajua muda ni mchache masuala ni mengi, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana kwa fursa hii adhimu. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri sekunde moja.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Gambo hapa amechangia amezitaja tuhuma nzito kwa kweli. Pamoja na kwamba hajataja mtu, lakini ni tuhuma nzito, kwamba jengo la shilingi bilioni sita zimezidi sijui shilingi bilioni tatu kwingine shilingi bilioni nane, sasa hiyo kidogo si jambo ambalo tunaweza kuliacha tu liende kwamba ni mchango wa kawaida wa Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge, kwa uzito wa tuhuma hizi Mheshimiwa Waziri tutakapomaliza bajeti yako utuletee taarifa ndogo ya huo ujenzi wa hilo jengo. Nitakupa nafasi hapa Bungeni kwa sababu tuhuma zimetolewa hapa Bungeni. Utakapojibu hapa Bungeni tutaona sasa Bunge lichukue hatua gani kwenye jambo kama hilo, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimesha...

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika,….

SPIKA: Unataka kusema jambo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, nikiri kupokea maelekezo yako, lakini ni vyema tukakumbushana kwamba mipango ya maendeleo katika halmashauri zetu, miji yetu na majiji haipangwi na TAMISEMI, inapangwa kwenye vikao maalum ya Mabaraza ya Madiwani kupitia Kamati za Fedha na Kamati mbalimbali chini ya Mabaraza yetu ya Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili suala la fedha pengine ingeenda kufanya shughuli fulani wanaoamua kutuletea ni Madiwani ambao sisi wote ni wajumbe kwenye vikao hivi vya Madiwani.

Hili lingine nimelipokea tutafuatilia kwa karibu kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameweza kuonesha *concern* yake katika eneo hilo, tutafuatilia kwa karibu na wakati wa kuhitimisha tutakuja na taarifa kamili ya namna tulivyochukua hatua. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana, itatusaidia sana hiyo, itatusaidia sana.

Wako wageni wengine ambao wamekuja baada ya tangazo la pili la wageni.

Kwanza, tunaye Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mheshimiwa Albert Chalamila, nimeambiwa amefika na yeye, karibu sana. *(Makofi)*

Nimejulishwa pia kwamba wapo Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kote, wako 184 na wengine wako upande wa Msekwa. Kwa hiyo, wale ambao wako Msekwa kama mnavyojua utaratibu wetu kule Msekwa nao wanaendelea watu

wengine kufuatilia shughuli zinazoendelea hapa na kwa hivyo tunatambua kwamba na wao wapo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimekwishamtaja Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mheshimiwa Eric James Shigongo ajiandae.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa miaka minne hii katika nchi hii; maendeleo tumeyaona kila jimbo, maendeleo ni makubwa haijapata kutokea, ni makubwa mno, kiasi kwamba tunampongeza pamoja na msaidizi wake Makamu wa Rais na Waziri Mkuu. Kwa kweli maendeleo ya nchi hii yameonekana.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mchengerwa, Manaibu wake, pamoja na Katibu Mkuu. Kwa kweli kuna msemo unaosema, "Upele umempata mkunaji." Kwa kweli, tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mchengerwa kwa kazi nzuri na timu yake wanayoifanya na wasaidizi wao katika hii Wizara ya TAMISEMI, wamesimamia vizuri na mambo yanakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Chama cha Mapinduzi kupitia Kamati Kuu, Halmashauri Kuu, na kupitia Mkutano Mkuu ukiunganisha pamoja na Wabunge hawa kazi waliyoifanya ya kumpitisha bila hiyana kwamba awe mgombea pekee wa Urais ndani ya Chama chetu, waliyaona mambo makubwa anayoyafanya.

Mheshimiwa Spika, vilevile, msaidizi wake, Dkt. Nchimbi kwa kweli sasa hii Ilani ya 2025 - 2030 sasa mambo yanakwenda kuwa ni makubwa zaidi. Vilevile tunampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwinyi, kwani Chama cha Mapinduzi kimefanya kazi nzuri upande wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nielezee mafanikio na changamoto. Nikianza na upande wa elimu, Makambako tumepata sekondari nyingi mpya. Tumepata madarasa upande wa shule za msingi na sekondari. Ombi langu kwa Wizara ya TAMISEMI, walitupatia fedha shilingi milioni 585 za kujenga shule ya ufundi na nina imani na wenzangu wamepata. Sasa mahali ambapo imefikia, tunaomba fedha zilizobaki, shilingi 1,100,000,000 ili iweze kukamilisha hii shule ya ufundi, iweze kuwahudumia Wanamakambako.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa upande wa afya, kuna Kituo cha Afya cha Kitandililo. Kituo hiki tulipata fedha kidogo. Tunaomba tupate fedha nyingine ili kituo hiki kiweze kukamilika, kiweze kufanya kazi iliyokusudiwa katika Kituo cha Afya cha Kitandililo.

Mheshimiwa Spika, pia, tulikuwa tumeahidiwa juu ya kituo kimoja kimoja kila Jimbo, ambapo nilipendekeza kituo hiki kijengwe katika Kata ya Kivavi. Wananchi wa Kivavi au wa Jimbo la Makambo wanaendelea kusubiri Kituo hiki. Tunaomba sana katika mpango huu tuweze kupata fedha kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Kivavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tuna ombi kubwa, tuna maboma mengi yamejengwa kwa nguvu za wananchi, Waheshimiwa Wabunge hawa pia na Waheshimiwa Madiwani. Tunaomba katika bajeti hii kuhakikisha maboma haya yote ya zahanati, shule (madarasa) na kadhalika, yaweze kumaliziwa kupitia bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna zahanati moja ambayo nimekuwa nikiizungumza sana. Zahanati hii iko katika Kijiji cha Mkolango ambapo Waziri alishaniahidi kwamba Wananchi wa Mkolango watapata fedha mwezi huu wa Nne, siyo kwenye bajeti hii, kwenye bajeti ambayo ilishapita.

Mheshimiwa Spika, naomba fedha hizi ziende kwa wakati, kwa sababu wananchi niliwaeleza kama ambavyo Mheshimiwa Waziri Mchengerwa aliniambia mwezi huu wa Nne watapata

fedha kwa ajili ya zahanati hiyo, kwa sababu, wananchi wameshajenga, wameshaezeka kwa nguvu zao, bado sasa Serikali kuweza ku-*support*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine pamoja na kwamba halipo katika Wizara hii, lakini kwa sababu ni Serikali, kuna suala la fidia la umeme wa upepo katika Mji wetu wa Makambako. Suala hili la fidia la umeme wa upepo, wananchi wamekaa wakisubiria zaidi ya miaka 15 hawajapata fidia, hawawezi kuendeleza wala kufanya jambo lolote.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Waziri Mkuu alipokuja alitoa maelekezo, naomba kupitia kikao hiki kuhakikisha Serikali inatenga fedha kwa ajili ya kuwapa fidia wananchi hao ili waweze kupisha ule mradi uweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kuna soko la Kimataifa. Eneo hili lililotengwa kwa miaka mingi, tunaipongeza na tunaishukuru Serikali kwa kulipa fidia zaidi ya shilingi 3,200,000,000. Wapo wananchi 18 ambao bado hawajalipwa fidia, tunaiomba Serikali imalizie kuwalipa wananchi hawa 18 ili waweze kupisha huu mradi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la barabara. Tunaishukuru *TARURA, TANROADS* kwa Makambako Mjini, lakini *TARURA* wanafanya kazi nzuri sana. Ombi langu, fedha ziongezwe pamoja na kwamba fedha zimetengwa hapa kwenye taarifa ambayo imesomwa hapa. Barabara za kwenda vijijini, nina barabara hapa ya kutoka Makambako inaitwa Barabara ya Mgimba – Mlowa - Kifumbe, kwenda kutokea Nkitu mpaka pale Ikelu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii barabara ni kama *ring road* kwa Makambako, kutoka Makambako kwenda kwenye hospitali ya wilaya ni kilometa nane. Tunaishukuru Serikali imetupa fedha za kujenga lami kilometa mbili. Tunaiomba Serikali, barabara hii siyo nzuri hasa kwa akina mama wajawazito na akina mama wagonjwa wanapokwenda hospitali yetu ya halmashauri iweze kutengenezwa kwa wakati ili iweze kupitika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, kwenye hili suala la afya, nimeuliza swali la nyongeza asubuhi kuhusu suala la watumishi. Katika Kituo cha Afya hiki cha Kitandililo nilipofanya ziara hivi karibuni, wananchi wale waliomba angalau, kwa sababu kuna wahudumu wawili tu pale, waongezewe wahudumu ili waweze kuwahudumia wananchi wa Kituo cha Afya cha Kitandililo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Serikali kwa kuhakikisha Jimbo letu limepata umeme kwenye vijiji vyote, sasa hivi Serikali imetupatia karibu vitongoji 18. Wakandarasi wanaendelea kupeleka nguzo na kadhalika, tunaipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, mtu anapofanya vizuri ni lazima apongezwe kama alivyosema Mheshimiwa Mama Kilango. Maono yangu na maono ya Wabunge hawa kwa kweli baada ya uchaguzi wa 2025 kila mahali tumejipanga kuhakikisha Mheshimiwa Rais Dkt. Samia anapata kura za kutosha, na baada ya uchaguzi lazima afikiriwe tena kwa mambo mengine kwa sababu ana maono makubwa sana kwa nchi yetu na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Makambako kwa namna wanavyoniunga mkono, wanavyokuwa nami, na mimi inawajali wananchi wangu. Nawaambia Mungu anipe uzima, 2025 nipo, na 2030 nipo ndugu zangu bila shida yoyote.

Mheshimiwa Spika, namwombea Mheshimiwa Waziri Mchengerwa kama ninavyosema, kwa kazi nzuri anayowatumikia Watanzania na Jimbo lake. Sisi Wabunge tunamwombea Mheshimiwa Mchengerwa kwenye Jimbo lake aweze kurudi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile na Naibu wake, ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Dugange, tunamwombea, kazi anayomsadia Waziri ni kazi nzuri sana…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa haya ahsante sana…

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, bila kukutaja wewe, wewe ni Rais wa Mabunge ya Dunia. Sisi wenzako wa kule Mbeya tunakuombea, tunakuombea Watanzania wa Mbeya wakurudishe tena kwa heshima tuliyopewa. Mungu akubariki, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa, haya ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma atafuatiwa na Mheshimiwa Eric James Shigongo na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga ajiandae.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa maoni yangu. Jambo la kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri alizofanya kwenye kipindi chake cha miaka minne. Kwa kweli mimi kama Mwakilishi wa Jimbo la Geita, mpaka sasa tunasubiri tu tarehe ya kupiga kura ili tuweze kumwekea kura zake, hatuna matatizo na kura zake. Kwa kazi alizozifanya Mheshimiwa Rais kwenye Jimbo langu, naomba nitumie *podium* hii kusema nami nipo bado kwenye kiti hiki, nitaendelea kwa sababu nimefanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana wewe kwa kipindi chote cha miaka mitano umetuongoza vizuri sana. Najua umepokea *form one* wengi, lakini mpaka leo naona wote wako sawa wamekuelewa. Tunakushukuru sana kwa kutuongoza vizuri, Mungu akubariki sana na kwa kweli Wanambeya hatutaki watuangushe.

Mheshimiwa Spika, katika watu tunaowaombea wa kwanza kuongoza kwa kura, ni wewe. Watu wa Mbeya wametuletea mtu sahihi. Najua kulikuwa na maigizo, lakini baada ya kuondoa maigizo, hii ndiyo faida ya kuchagua viongozi wenye busara, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, nampongeza sana Mkuu wangu wa Mkoa, nimemwona, Mheshimiwa Martine Shigela. Najua mimi pamoja na Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Geita tuna mlinzi mzuri sana kwenye Majimbo yetu, hatuna mashaka, hatuna wasiwasi, na hivi nimemwona na rafiki yangu Chongolo, tunamkaribisha sana. Amecheka sana wakati mchangiaji akichangia hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimweleze ndugu yangu, Mheshimiwa Mchengerwa, Mheshimiwa Waziri kwenye majimbo yetu tuliwaahidi watu vituo vya afya. Naomba sana, siyo kwamba vitatukosesha kura, lakini kwa sababu tuliahidi na Serikali yetu ni Sikivu, tunaomba zile fedha kwa ajili ya kujenga vituo vya kimkakati. Tulifanya mikutano tukaahidi, wananchi wangu wa Kata ya Rubanga wananiangalia hapa, niliwaambia tunajenga kituo, sasa naomba ufanye namna yoyote ili tuweze kujenga kile kituo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumze kidogo kwa upole, hapa najua Katiba inaruhusu, siyo dhambi, na Mheshimiwa Rais alitangaza juzi kwamba watumishi wote wanaotaka kuingia Bungeni wamwandikie barua. Nimeona kamsururu kidogo ni karefu, wengi wamemwandikia Waziri wa TAMISEMI na Mawaziri wengine, hatuwaogopi na tunawakaribisha kuja Bungeni. Nataka kushauri, hii nyumba ni nyumba kidogo ya watu wanatakiwa tuwe wasafi siyo kichaka cha watu kujificha.

Mheshimiwa Spika, naomba… *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Musukuma, nasikia kuna watu wanasema orodha hii umeiona wapi?

Waheshimiwa Wabunge, lakini wale ambao wanataka kujua nani kiongozi kwenye eneo lake anagombea, mtamwona Mheshimiwa Musukuma atawajuza.

Mheshimiwa Musukuma, endelea. *(Kicheko)*

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, intelijensia inakua kwa baadhi ya watu, siyo kwa wote, nakushukuru. Nilikuwa nashauri wale ambao wameandika kuja kwa Mheshimiwa Mchengerwa kutaka kuingia kwenye hii *game* ya siasa, tunawakaribisha na ni suala la Kikatiba, lakini kabla hajawapa idhini ya kwenda kugombea, naomba Mheshimiwa Waziri na kupitia Bunge lako hebu wapelekewe *special audit* kwanza. Wawe *clear* kwanza, waje wakiwa wasafi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yaani naona kama tunajikaanga wenyewe, tunatoa kulia tunaweka kushoto na mtu akishaingia humu ameshavaa kinga, hawezi kuitwa. Kabla mtu hajaachia kiti chake kuja kugombea Ubunge, peleka *special audit*. Kichere nimemwona hapa, ili wakija kwako na ile barua kwamba huyu hana matatizo, ndio waje huku. Hawezi kukwapua huko halafu wakaja kugombea Ubunge, haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba sana hilo, vyombo vyote mlizingatie na Mheshimiwa Waziri kabla hajawaruhusu kuja kugombea, wawe na barua zinazotuonesha hawa watu ni safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bahati moja nzuri mimi kwenye Jimbo langu nikiletewa kiongozi kama Mkurugenzi, wa kwanza kwenda ofisini kwake huwa ni mimi. Namwambia, nipe *plan* yako ya baadaye. Unataka kwenda kwenu kugombea Ubunge au unataka Ukurugenzi? Bahati nzuri huwa naletewa watu wanaokaribia kustaafu, hakuna anayesumbua watu kwenye Ubunge, kwa sababu ninajua mimi kahalmashauri kangu ni kachanga, ukianza kukakwapua tena kwenda kutunza za Ubunge utanimaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana, hili suala kwa manufaa ya Wabunge wote, hizi barua za *special audit* zitembee ili tupate viongozi safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nilitaka kutoa ushauri kwenye *TASAF*. *TASAF* iko Utumishi, lakini ukiangalia kazi za *TASAF* nyingi tunazifanya halmashauri. Nilikuwa nadhani, ikiwapendeza *TASAF*

irudi TAMISEMI ili tu-*deal* nao moja kwa moja. Kuna kitu wenzangu mnaotoka vijijini mnafahamu, familia maskini zilizokuwa zinapewa fedha na *TASAF* shilingi 30,000 yaani yamekuja masharti unajiuliza, hawa watu waliotengeneza haya masharti wao wanakaa dunia gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zile familia maskini, wale wazee, ili wapewe zile fedha walizokuwa wanapewa mwanzo, lazima wakalime barabara. Mbunge unafanya ziara, unakutana na bibi wa miaka 70, 65 amepewa hatua 10 za kupalilia. Utaendelea na ziara au inabidi umsaidie! Unajua tuko tofauti, mtu aliyekulia boflo na siagi huwezi kulinganisha na mtu amekulia uji wa muhogo halafu unalima mpaka saa kumi na moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ehee, haya mawazo yanafanyika kwa watu ambao hawafanyi *research* vizuri vijijini. Kule vijijini ukikuta mtu ameshakuwa mzee, kwanza amezaa watoto 16, halafu unaenda kumpimia hatua 10 ili umpe shilingi 30,000. Serikali hii ni tajiri sana. Nilikuwa nadhani haya majukumu yarudi moja kwa moja kwa Wakurugenzi ili tu-*deal* nao.

Mheshimiwa Spika, hawa waliotengeneza huu utaratibu siyo sahihi kabisa. Familia maskini, mtu mzee aliyekimbiwa na watoto wake, amewasomesha wapo mjini wameniga tai, mama analima vibarua, tena vya kulipwa shilingi 30,000. Hili nadhani pia tunahitaji kuliangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Waziri, amezungumza suala la mwendokasi. Kwanza, nashukuru kwa kuwa anachukua maeneo machache machache ya ushauri wetu sisi wazoefu. Mheshimiwa bado tatizo sidhani kama tutalitibu. Kama Serikali, wewe ndiyo unanunua magari halafu unampa mtu kuendesha, kila mtu anatafuta faida. Mimi siwezi kufanya kazi ya bure, lazima nitachukua change, tuje tukutane kwenye makaratasi, kwenye matatizo.

Mheshimiwa Spika, nadhani kama tumeweza kujenga miundombinu ile, jukumu la uendeshaji tuwape sekta binafsi, yeye mwenyewe na kila kitu cha kwake. Hii kazi siyo lazima tuwape

wageni, siyo lazima. Wapo watu ambao ni Watanzania kabisa wanaoweza kufanya hizo kazi kupeleka mabasi Mbagala, kama mtu ana gari mia anapeleka mpaka Rungwe. Yaani kwenda Mbagala, tunahitaji kuleta Wazungu kweli!

Mheshimiwa Spika, hao wanaokuja hawana uchungu na Watanzania, wao wanakuja kuchuma ili waende kwao. Kwa hiyo, hizi kazi ambazo tunaweza kuzifanya wenyewe nadhani kuna umuhimu wa kuwapa watu wazawa ili waweze kufanya hizo kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, tunaenda kwenye uchaguzi na ninashukuru kwanza chama changu kwa kale kameseji kalikotoka jana usiku, kwamba tutachukua tarehe 28. Nakishukuru sana chama changu, Sekretarieti pamoja na waliotoa hayo maamuzi, Wabunge sasa tu-*concentrate* na Bunge. Tufanye kazi ya Kibunge, tukutane hiyo tarehe 28. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuwaambia kwa niaba ya sisi Wabunge tunaotokana na Chama cha Mapinduzi, sisi Sera yetu tunasonga mbele. Hawa wanaosema *no reform,* mimi nashauri kama kuna namna yoyote hata ya kuwapitisha mlango wa nyuma waruhusuni wasaini tukutane nao, hawana cha kutuambia. Kama walitafuta mlango wa kutokea, kutokwenda kusaini, wapeni hata kwa ziada ili tukakutane nao majukwaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kazi zilizofanywa na Serikali ya Mama yangu Samia, mimi sioni hoja. Hata ukizunguka huko mtaani unawaambia watu tuzuie uchaguzi, leta hoja. Mwanzoni kulikuwa na hoja ya *Escrow, EPA,* watu wengi walitoka hata walioenda shule wasomi, lakini leo tunaenda kuzuia uchaguzi kwa sababu ya Madaraka, hapana. Wasitupe jezi tunawasubiri, wasitukimbie tarehe 28 likiachiwa tukutane kitaa wote tunajua kuongea.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Eric James Shigongo, tutamalizia na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipa nafasi ya kusimama ndani ya Bunge. Namshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mambo yote anayoyafanya kwa wananchi wa Jimbo la Buchosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana wewe mwenyewe kwa namna unavyoongoza Bunge letu, Waziri wetu wa TAMISEMI, Manaibu wake, Makatibu Wakuu, Watalamu wote wa TAMISEMI kwa namna wanavyofanya kazi yao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mkuu wangu wa Mkoa wa Mwanza ambaye yuko ndani ya ukumbi huu kwa namna anavyofanya kazi, na binafsi kwa ushirikiano anaonipa. Namshukuru sana Mkuu wa Wilaya yangu, Senyi Ngaga ambaye tunafanya naye kazi vizuri. Nawashukuru sana Baraza la Madiwani, Mwenyekiti wangu wa Halmashauri, na Mkurugenzi wangu wa Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nimshukuru sana Mkurugenzi wangu wa Halmashauri. Huko nyuma niliteseka sana, lakini Mheshimiwa Rais akanisikia, akaniletea kaka yangu Mihayo, tunafanya kazi vizuri na Buchosa imebadilika sana. Nakushukuru sana Mihayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shukrani zangu pia ziende kwa *CEO* wa *TARURA*. Lazima niseme sentensi chache. Nimeshakutana na watu wengi sana kwenye maisha yangu, lakini huyu bwana ni mtu wa tofauti. Anapokea simu wakati wowote na anakupatia kila msaada unaouhitaji. Mungu akubariki sana Seif, endelea kufanya kazi yako vizuri na Mungu ataendelea kukunyanyua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumnukuu mshairi mmoja maarufu duniani anaitwa Dante, aliishi mwaka 1265. Dante alisema maneno yafutayo, nami nitayanukuu. Alisema: *"The hottest places in hell are reserved for the ones who chose neutrality during the times of moral crisis"*. Maana yake ni kwamba, sehemu yenye joto kabisa kule jehanamu imeandaliwa

kwa wale watu walioamua kunyamaza wakati mambo yanaharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi Eric Shingongo, Mbunge wa Buchosa, sipo tayari kwenda kwenye sehemu yenye joto kali kule jehanamu. Ndiyo maana sasa nitazungumza kile ambacho mimi ninaamini kwamba ni ukweli.

Mheshimiwa Spika, wapo watu wanapita wanazungumza maneno ya kwamba hakuna kilichofanyika hapa Tanzania na hakuna kilichotendeka tangu Uhuru wa nchi yetu. Tunawasikia wanapita kwenye majukwaa yao mbalimbali wanazungumza maneno kama hayo ambayo ninaamini ni uongo, labda kwa mtoto wa mwaka 2000, lakini hata mtoto wa mwaka 2000 na yeye anajua kwamba huo ni uongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimezaliwa, nimekulia na nimesomea hapa Tanzania. Mimi ni zao la familia masikini kabisa kwenye nchi hii. Nakumbuka kutembea kilometa tisa kwenda shule na kurudi kwa miguu nikiwa mtoto mdogo. Kwa hiyo, akitokea mtu leo akasema hakuna kilichofanyika, huo ni uongo wa mchana ambao Watanzania ni lazima waukatae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka nitoe *data* chache tu kuthibitisha hicho nilichokiongea. Najua mtakubaliana nami, mwaka 1961 tulipopata Uhuru, *infant mortality rate* (watoto wanaofariki chini ya miaka mitano), ilikuwa ni watoto 141 kati ya watoto 1,000. Leo ninavyozungumza ni watoto 43 tu peke yake wanafariki kati ya watoto 1,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *maternal mortality rate* kwa mwaka 1961 tulipopata Uhuru wa nchi yetu, walikuwa wanafariki akinamama 453 wakati wa kujifungua kati ya akinamama 100,000. Leo ninavyozungumza ni akinamama 104 peke yake ndio wanafariki. Hii imemwezesha Rais wetu kupewa mpaka tuzo ya *Goalkeepers* na *Bill Gates Foundation*. Mtu yeyote akisema kwamba hakuna kilichofanyika, huo ni uongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 1961, *life expectancy,* umri wa Mtanzania kuishi ilikuwa ni mika 43, leo Watanzania tunaishi miaka 67. Hayo mambo yametokea kwa sababu ya huduma bora za afya na elimu kwa watu wetu. Mtu yeyote akisema Tanzania haijapiga hatua, huyo ni muongo, anatakiwa kuzomewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 1961 tulikuwa na Chuo Kikuu kimoja tu Tanzania. Leo kwa taarifa ya *TCU* tuna vyuo vikuu 50 ndani ya nchi yetu. Mtu yeyote akisema kwamba hakuna kilichofanyika, huyo ni muongo, anatakiwa kulaaniwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 1961 tulivyopata Uhuru, Tanzania umeme tulikuwa na megawati chini ya 100. Nimesoma *data* asubuhi ya leo mwaka 1967 tulikuwa na megawati 27. Leo ninapozungumza tuna megawati 3,404. Mtu yeyote akisema hakuna kilichofanyika, huyo ni muongo lazima alaaniwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi nchi yetu katika Afrika ni nchi ya nane kwa wingi wa umeme. Nani anapuuza Tanzania na maendeleo yamefanyika? Mambo mazuri yanafanyika, lazima Tanzania iwe mfano kwa sababu ni Taifa linaloenda mbele kwa kasi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtandao wa barabara, mwaka 1961 tulikuwa na kilometa 1,200. Leo ninapozungumza, tuna kilometa 13,000 tunaenda kilometa 14,000. Mtu yeyote akisema hakuna kilichofanyika, huyo ni muongo, lazima alaaniwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa niseme, John Maxwell alisema kwenye kitabu chake, "*Everything raises of falls on leadership*". Haya yote yanayotokea nchi yetu ya shule niliyoyasema na mengine yote ambayo sijayatamka, yametokea kwa sababu ya uongozi bora wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, anafanya kazi kubwa sana. Sisi wote lazima tukubali ya kwamba ndani ya uongozi wake, pamoja na awamu nyingine zote zilizopita, Mheshimiwa Dkt.

Samia Suluhu Hassan, amefanya kazi kubwa sana, anahitaji kupigiwa makofi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, nizungumzie Jimbo langu. Katika Jimbo la Buchosa, mimi peke yangu nimepokea shilingi bilioni 66.2 ndani ya miaka minne. Tumejenga shule, zahanati, mitandao ya barabara na miradi ya maji. Kila kona ukienda, ninavyozungumza hivi sasa, kutana na Mtu wa Buchosa leo muulize; Buchosa ya leo na zamani ipi ni bora? Atakwambia Buchosa ya leo ni bora kuliko ya zamani. Hakuna barabara ambayo wakati wa masika haipitiki. Ni kweli mvua ikinyesha inaezua barabara, lakini *TARURA* wanafanya kazi kubwa na barabara zinaendelea kuboreshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, naomba niseme bila kuficha, nitaendelea kumtetea Rais wangu, nitaendelea kuitetea nchi yangu, mpaka mwisho wa uhai wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua kuna watu wanaweza wasiamini ninachokisema, lakini Buchosa tumejenga shule tano za *High School,* tumejenga zahanati 24, tuna vituo vya afya vitano. Tuna Chuo cha Ufundi kwa mara ya kwanza, hatujawahi kuwa nacho tangu Uhuru wa nchi yetu. Leo tuna Chuo cha Ufundi kinakaribia kukamilika. Sasa, niseme nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie wananchi wa Buchosa kwamba, wamenituma Bungeni, naendelea kuwawakilisha, na kama alivyozungumza kaka yangu Mheshimiwa Deo Sanga, jambo moja kubwa sana, naomba nikunukuu: "*Bado nipo, nitaendelea kuwepo" (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme jambo moja nikielekea kuhitimisha mazungumzo yangu mafupi, naomba Waheshimiwa Wabunge mnisikilize vizuri. Naweza nikakiri na wengi mtakiri, mimi huwa napenda nizungumze ukweli wakati wote. Wakati mwingine ukweli umeniletea madhara, lakini naomba niseme ukweli ambao ninaamini kwamba ni ukweli.

Mheshimiwa Spika, alipoingia madarakani Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, inawezekana mimi na Watanzania wengine wengi hasa kabila langu hawa Wasukuma, ambao hawajazoea kuongozwa na wanawake walikuwa na mashaka kwamba, ataweza? Kwa sababu kwanza kafiwa na Rais madarakani, uchumi wa dunia umeharibika na amekuta miradi mingi, lakini yaliyotendeka na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan yamebadilisha kabisa mtazamo wangu mimi na Watanzania wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi Watanzania wana imani kubwa sana na wanawake kuliko ilivyokuwa huko nyuma, kwa kazi ambayo ameifanya. Watanzania wana imani kubwa sana na wanawake kwa kazi ambayo wewe Mheshimiwa Spika, umeifanya.

Mheshimiwa Spika, wewe na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan mmeinua sana heshima ya wanawake katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo bila kudanganya na kupindisha maneno, nataka niseme wazi, leo hii akiibuka mwanamke mwingine anataka Urais, hakuna mtu atakuwa na mashaka, hayupo. Najua wanaume watasema na wanaweza wakasema, mwanamke tena. Kwani tangu 1961 mbona ilikuwa wanaume tu.

Mheshimiwa Spika, kwa kazi iliyofanyika akitokea mwanamke mwingine anataka Urais leo, Watanzania tumpe bila mashaka kwa sababu Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya jambo moja kubwa, ambalo hakika…

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

TAARIFA

SPIKA: Mheshimiwa Shigongo kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kunti Majala.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nataka tu nimpatie taarifa mzungumzaji Mheshimiwa Shigongo kwamba siyo Urais tu, sasa hivi Watanzania hata kwenye Majimbo na Kata hawana shida na wanawake kwa kazi kubwa iliyofanyika. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Shigongo, kengele imegonga, lakini nakupatia nafasi, unaipokea taarifa hiyo? *(Vicheko)*

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa hiyo kutoka kwa shemeji yangu, Mheshimiwa Kunti Majala. Kwa kweli ni kweli kabisa Watanzania hatukuwa na uzoefu wa kuongozwa na mwanamke.

SPIKA: Sekunde 30.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Spika, kwa yaliyofanyika wala wanawake msisite sasa hivi, gombeeni nafasi yoyote na tutawaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kusema jambo moja tu la muhimu ambalo mimi ninaamini…

SPIKA: Kengele ilishagonga.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Spika, ilishagonga? Ahsante kwa nafasi hii. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru nami kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia hoja ya Wizara hii ya TAMISEMI ambapo na mimi ni Mjumbe katika Kamati hii ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kunijaalia afya, nimeweza kusimama katika Bajeti hii ya TAMISEMI ambayo ni bajeti ya mwisho katika Bunge hili la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nakushukuru sana kwa kazi kubwa unayoifanya katika Bunge letu. Umekuwa mlezi wetu wakati wote. Katika hii miaka mitano ya misukosuko mikubwa, majina ya ajabu na matusi mengi umesimama pamoja na sisi. Pamoja na matusi yote na nini, lakini umeonesha ukomavu wako, umeweza kusimama pamoja nasi wanawake wenzako na kusema kwamba hili litafanyika kama sheria zitaonesha kwamba tumelifanya kimakosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwenyezi Mungu akubariki na tunakuombea kila la heri katika uchaguzi tunaokwenda kuomba tena ridhaa ya Wanambeya, basi Mwenyezi Mungu akufayie wepesi na uweze kuvuka salama salmini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, namshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiifanya. Yeye pia amekuwa ni sehemu ya wale ambao walikuwa wakimwongeza kwa sisi hapa katika kuwepo kwetu Bungeni.

Mheshimiwa Spika, lakini mama huyu ameendelea kusimamia msimamo wake na amesema kwamba, hawa wanawake wataendelea kuwa Wabunge na tumeendelea mpaka leo tunasimama hapa na kumaliza katika Bunge hili la Kumi na Mbili, tunamalizia bajeti yetu ya mwisho. Tunamshukuru sana kwa kweli kwa uvumilivu wote ambao ameuonesha kipindi chote hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote wanayoyafanya na mimi niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI Mohamed Mchengerwa pamoja na Naibu Mawaziri wake. Pia, wasaidizi wao Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu kwa kweli wamekuwa ni viongozi ambao wameshirikiana vizuri na Bunge hili kupitia Kamati yako ya TAMISEMI, tumeweza kufanya

majukumu yetu na kutekeleza kwa ufanisi na uadilifu mkubwa sana wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee lakini siyo kwa umuhimu namshukuru sana *Engineer* Seff wa *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umeona makofi yamekuwa mengi hapa, siyo kwa sababu nyingine yoyote, lakini niseme tu na mimi kama Mjumbe wa Kamati, *Engineer* huyu amekuwa ni mtu msikivu, anayesikiliza na hata kama fedha hana kwenye eneo ambalo umelisema, lakini yale maneno anayokupatia ukitoka pale unasema kweli Serikali ya Awamu ya Sita inafanya kazi yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninaendelea kumwombea kwa Mwenyezi Mungu, *Engineer* Seff Mungu ambariki aendelee kutekeleza makujumu yake vizuri. Pamoja na changamoto tulizonazo za barabara, lakini amekuwa akijitahidi kwenye maeneo yetu kufanya kile ambacho kinawezekana ili wananchi wetu waweze kuendelea na shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimekuwa ni sehemu ya sisi Wanakamati kukagua miradi mbalimbali na haya ninayoyasema kwa bahati nzuri nimeyaona kwa macho. Serikali hii ya Awamu ya Sita imeongoza kwa ujenzi wa madarasa mengi nchini. Pia, imeongoza kwa ujenzi wa zahanati na vituo vya afya pamoja na Hospitali za Wilaya kwenye maeneo yetu mbalimbali. Haya siyo kwa sababu nimeambiwa na mtu ama kwenye makaratasi, lakini mengi nimejionea mwenyewe na watu wanaweza kuiona thamani ya fedha yao ikiwa huko kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, binafsi nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa dhati kabisa kwa imani yake kubwa kwa wakandarasi wetu ambao ni wazawa. Wakati Mheshimiwa Rais anazungumzia kuhusu wakandarasi wazawa, wengi tulidhani na tulifikiri kwamba itakuwa ni kazi kubwa sana wakandarasi hawa kuweza kutekeleza majukumu yao, aidha kutokana na fedha kidogo walizonazo ama kwa hali nyingine yoyote. Mheshimiwa Rais aliweza kuwatengenezea mazingira bora na akawapa nafasi na

wakandarasi wazawa kwa kweli wameonesha wanaweza wakapewa nafasi na wakafanya mambo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekwenda kukagua miradi mbalimbali ya stendi na masoko. Kuna baadhi ya miradi imejengwa na wakandarasi wazawa, na ukiambiwa kwamba miradi hii imejengwa na wakandarasi wazawa, huwezi kuamini hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, pia, kuna maeneo tumekwenda ni wakandarasi wa nje na unaona kabisa kuna changamoto nyingi sana. Juzi tulikuwa Kahama, tumejionea kati ya mkandarasi mzawa na wa nje; mzawa amefanya kazi nzuri na kubwa kweli kweli kiasi kwamba tulivyoambiwa huyu ni mkandarasi mzawa, tukasema kweli Mheshimiwa Rais alifanya jambo zuri kuwaona hawa wakandarasi wazawa na kuweza kuwatengenezea mazingira mazuri ya kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, kuna miradi ya *TACTIC* inayoendelea nchi nzima sasa hivi, lakini miradi hii tumeona ambavyo Serikali imewaamini wakandarasi wazawa na wameweza kuifanya miradi hii kwa ukamilifu mkubwa. Pia, miradi mingine ambayo inaendelea, inafanywa vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi natokea Tabora. Sisi ni sehemu ambayo tumepata mradi mkubwa wa *TACTIC* ambao ni wa soko. Mradi huu tunaye Mkandarasi mzawa ambaye anaitwa *Sihotech Engineering,* anakwenda kwa *speed* ya hali ya juu, kiasi kwamba hatukutegemea kwamba kwa sasa angekuwa amefikia hatua hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huyu *Sihotech* ameweza kutengeneza miradi ya soko na stendi katika Mkoa wa Mbeya na Shinyanga. Tumekwenda na tumeona kazi nzuri iliyofanyika. Ni imani yangu hata pale Tabora katika soko lile, ule wakati ambao Mheshimiwa Waziri amesema kwamba soko hili litakuwa tayari na wafanyabiashara wetu wataenda kufanya kazi, naiona hiyo ahadi ya Mheshimiwa Waziri kwa jinsi ambavyo Mkandarasi huyu anafanya kazi nzuri kwa weledi na kwa kasi ya hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nami kwa kweli niungane na Mheshimiwa Rais kwa imani aliyoionesha kwa wakandarasi wetu wazawa, wanafanya kazi nzuri na hawa wakandarasi wazawa wengine waendelee kuonesha imani hiyo kwa Mheshimiwa Rais ili waweze kupewa kazi nyingi ambazo zinajitokeza katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, binafsi nizungumzie kwenye Sekta ya Elimu na niseme kidogo kwenye baadhi ya Miradi ya Elimu ambayo imekuja kwenye Mkoa wetu hususan kwenye Jimbo la Tabora Mjini ambalo ninatokea mimi.

Mheshimiwa Spika, tuliomba hapa kwamba kuna shule nyingi sana za msingi sasa ambazo zinahitaji ukarabati, zimeshakuwa za muda mrefu. Kipekee kabisa, naishukuru sana Serikali na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI amepeleka fedha kiasi cha shilingi milioni 316 katika Shule ya Msingi *Town School.* Shule hii ilikuwa ni ya mwaka 1940. Leo tumepewa shilingi milioni 316 kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa kuongeza madarasa katika shule hii ambayo ipo katika Kata ya Gongoni ambapo mimi natokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi ya kukarabati imeanza kufanyika, majengo yale ya zamani yaliyochakaa, sasa wameshaanza ujenzi wa madarasa ambapo unaenda kukamilika na watoto wetu sasa wataanza kusoma katika shule hiyo, ikiwa ni shule inayoonekana mpya, na imefanyiwa ukarabati wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, pia, tumeletewa shilingi milioni 170 katika Shule ya Msingi Kitete iliyo *opposite* kabisa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Leo ukipita katika shule ile, ilikuwa imechakaa kweli kweli, lakini sasa hivi ukipita kama shule mpya. Kwa kweli kwa ukarabati huo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ukarabati huo na shule zetu sasa zimeonekana zikiwa mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunavyo vituo vya afya, pia tunazo zahanati, na bado kuna ujenzi wa zahanati zinaendelea katika Jimbo letu la Tabora Mjini. Kwa hiyo, tuishukuru sana Wizara ya

TAMISEMI kwa kupitia Waziri wake Mheshimiwa Mchengerwa kwa kutuletea fedha.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi sisi Jimbo letu ni kubwa sana, lina kata 29. Tumelalamikia sana kwamba hatuna huduma za afya za karibu. Leo tunapata huduma za afya za karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mchengerwa kwa ahadi yake ya kutupelekea fedha kwa ajili ya kumalizia majengo katika Kituo cha Afya Maili Tano. Amesema kwamba fedha hizi zitakwenda baada ya kuanza kwa bajeti hii ili kujenga majengo ambayo yanakosekana katika Kituo cha Afya Ipuli.

Mheshimiwa Spika, wakituwekea majengo yale, yanaweza kutusaidia kuhudumia wananchi wengi wa maeneo ya mjini katika Jimbo la Tabora Mjini na kwenye kata ambazo zinazunguka kituo kile cha afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na haya, nashukuru pia kwa miradi ya barabara ambayo imekuwa ikiendelea. Tunayo miradi ya *TACTIC* ambayo inaendelea na ujenzi wake. Pia, tunayo miradi ya *TARURA* ambayo kwa kweli wamepata fedha kidogo, lakini wameanza kutekeleza miradi mbalimbali ambayo barabara zilikuwa zimechoka na zimeharibika.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kipekee kabisa kabla sijamaliza, nisipomshukuru sana Mkuu wangu wa Mkoa, ndugu yangu Chacha Matiko, kwa kweli nitakuwa sijamtendea haki. Mkuu wa Mkoa huyu amenipatia amani wakati wote. Nimefanya kazi kwa ujasiri mkubwa sana, na kila ninapohitaji ushirikiano katika Ofisi ya Mkoa, kwa kweli Mheshimiwa Mkuu wangu wa Mkoa na *RAS* wake wamekuwa mstari wa mbele kuweza kunipatia ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata pale nilipokuwa nina changamoto yoyote, nikienda, kwa kweli wamekuwa wakinisaidia ili niweze kutekeleza majukumu yangu kama Mbunge wa Mkoa wa Tabora. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Mkuu wangu wa Mkoa

na *RAS* wetu kwa kuniamini na kuona kwamba, mimi ni Mbunge na ninaweza kutekeleza majukumu yangu katika eneo langu la kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwanza nitoe maelezo. Wakati mwingine Wabunge wanaitwa ambao pengine majina niliyonayo wanaonekana wapo chini, lakini sababu ni kwamba, ukiwa umekaa hapa mbele, Wabunge wana mambo mengi. Wakati mwingine wana wageni, ama wanakwenda hospitali. Wengine ndio kama hivyo, kwa sababu wanataka kubaki humu ndani, basi ana simu nyingi hapo nje.

Kwa hiyo, akiniletea ujumbe hapa mbele, inategemea na ujumbe wenyewe umekujaje. Sikubali kila ujumbe, lakini ukija kwa uzito, basi inabidi yule aliyekaa hapa mbele awapatie kipaumbele wale wanaokuwa wameomba kwamba, wana udhuru ama wana dharura.

Waheshimiwa Wabunge, tutakaporejea jioni leo wachangiaji nitakaowataja hapa ndio tutakaoanza nao. Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, na wengine tutaendelea kuwataja kadri muda utakavyokwenda.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninasitisha Shughuli za Bunge, mpaka Saa11.00 jioni leo.

(Saa 7.20 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

Hapa Mwenyekiti (Mheshimiwa Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu. Tutaanza na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, na Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, ajiandae.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa fursa nami kuweza kuchangia katika Wizara hii muhimu ambayo ni Wizara inayogusa moja kwa moja maisha ya Watanzania. Kabla sijaenda kwenye mchangao wangu, uniruhusu nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposimama na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tueleweke kwamba, lengo ni kushukuru na kupongeza kutokana na matokeo tunayoyaona, tunayoyashuhudia ya kazi kubwa anayofanya katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natokea Mkoa wa Tanga. Miaka minne mitatu iliyopita, Wabunge wote wa Mkoa wa Tanga ilikuwa kila tukisimama hapa tunalalamikia maji, tunalalamikia afya, tunalalamikia barabara. Malalamiko yalikuwa mengi kuliko shukurani, lakini kila anayesimama leo kitu cha kwanza tunashukuru. Tunampongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu tayari tumeona ametutoa

kwenye hatua moja ya maendeleo na ametupeleka kwenye hatua kubwa mpya ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuwashukuru viongozi wengine wote wanaomsaidia Mheshimiwa Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu, Waziri Mwenye dhamana na Naibu Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa namshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, kwa sisi Wabunge, tena mabinti ambao tumeingia kwenye Bunge hili tukiwa tunahitaji malezi ya hali ya juu, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson alijitolea. Leo tunasimama kifua mbele, tuna uwezo wa kujenga hoja tukaeleweka, tuna uwezo wa kusimamia taratibu mbalimbali kwa sababu ya mwongozo na malezi ya Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson. Kwa pamoja tunamwombea afya sana na Mwenyezi Mungu ambariki sana, na watu wa Mbeya Mjini waone hili ambalo sisi tunaliona ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimejikita kwenye hoja moja tu, Elimu ya Ufundi. Nakumbuka wakati tu tumeapa mwaka 2021, mimi ni moja ya Wabunge ambao tulijenga hoja, tulisikitishwa, tulilalamika juu ya mfumo na matokeo ya elimu Tanzania. Mwaka 2021 baada ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuapa, alikuja kuhutubia Bunge hapa. Moja ya eneo ambalo alizungumza na yeye kutoridhika, ni elimu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hotuba yake, Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo mahsusi kwa Wizara zinazohusika kufanya mapitio ya elimu yetu na mwisho wa siku tukaletewa sera na mitaala mipya ya elimu. Tunampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuona kama ambavyo Watanzania tunaona, anaziona changamoto kama Watanzania tunavyoziona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunavyozungumza, tuna mtaala mpya, tuna sera, lakini hapa tulipo tunahitaji kwenda sasa tukaone matokeo ya sera na mitaala mipya ambayo

imeshapitishwa. Tuna mambo makubwa matatu ambayo tunapaswa kwenda kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni kuboresha miundombinu ya elimu ya ufundi katika mkondo wa amali, elimu ambayo kwa Tanzania Bara ni jambo jipya. Elimu ambayo kwa Tanzania Bara bado haijawa na ushawishi wa kutosha, elimu ambayo kwa Tanzania Bara, pamoja na kwamba bado haijawa kwenye mazingira mazuri sana, ni elimu ambayo ina uhitaji mkubwa, na pengine ndiyo njia ambayo Watanzania tunakwenda kutoka, kupitia elimu ya ufundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokwenda ni lazima tukubaliane kama Taifa, tutengeneze vipaumbele. Kipaumbele cha kwanza ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na elimu inayomwandaa Mtanzania kujiajiri, na ndiyo malengo ya kuwa na elimu ya ufundi nchini. Katika malengo hayo, ili uwe na elimu ya ufundi, lazima ujiandae kukuza ujuzi, lazima ujiandae kupanua uzalishaji, lazima ujiandae kupanua soko la ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana umechangia, moja ya eneo ambalo nilikusikia ulisema, hakuna nchi duniani ambayo inaweza kumaliza changamoto ya ajira. Naungana nawe, ni kweli kabisa, lakini ipo namna kama Taifa. Nitakupa mfano, Switzerland, Ujerumani, China, India, Korea, ni Mataifa ambayo yamekuwa na maendeleo makubwa kiuchumi kwa sababu waliwekeza kwenye elimu ya ufundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *enrolment* ya Ujerumani tunavyozungumza sasa, nusu ya wanafunzi wake wanapelekwa kwenye Elimu ya Ufundi. Ukiangalia Switzerland, tunavyozungumza sasa 90% ya wanafunzi wake wanapelekwa kwenye elimu ya ufundi. Lengo ni nini? Lengo ni kukuza uzalishaji, lengo ni kukuza ujuzi, lengo ni kupanua mazingira kwa ajili ya soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, nimeona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 141, Serikali imeshajenga shule 100 za ufundi nchini. Hili ni jambo kubwa sana na tunaipongeza sana. Jambo ambalo sijaliona ni

hizi shule zimeshajengwa, lengo ni kutoa elimu ya ufundi, ziko wapi karakana? Wako wapi walimu wa ufundi? Viko wapi vifaa vya kufundishia vitakavyokidhi elimu ya ufundi tunayoihitaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshakuwa na elimu ya ufundi kwa kipindi kirefu kidogo. Tumekuwa na elimu ya ufundi lakini tuepuke kwenda kwa mazoea. Elimu ya ufundi tuliyokuwanayo, tumefundisha watu kwa nadharia kwa kipindi kirefu. Elimu ya ufundi tunayotamani kuiona sasa ni elimu ya watu kwenda kupewa ujuzi au kufundishwa kazi wanazokwenda kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu akitoka kwenye chuo cha ufundi, awe na uwezo wa kwenda kujiajiri, awe na uwezo wa kwenda kufanya kazi bila kupewa elimu nyingine tofauti na ile ambayo ametoka nayo kule chuoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tungependa kuona hizi shule zilizojengwa kwa elimu ya amali, vyuo vya ufundi vinavyojengwa, *VETA* na maeneo mengine, walimu wenye ujuzi wawepo wa kutosha ili tudhamirie kwa pamoja kutoka kwenye hatua tuliyonayo kwenda kwenye hatua nyingine ambayo itatuletea ule uzalishaji na kupanua soko la ajira, kama ambayo nimesema hapo mwanzoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumzia elimu ya ufundi, ukiboresha elimu ya ufundi, maana yake unaiandaa nchi kuwa nchi ya viwanda. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alitembelea Mkoa wa Tanga, alifanya ziara kwa wiki nzima kwenye Mkoa wa Tanga. Moja ya wimbo wake katika maono yake, maelezo aliyotoa, alitamani kuirejesha Tanga ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanga ya viwanda haiwezi kupatikana bila malighafi. Ni lazima tuwaandae vijana leo kuzalisha malighafi kwa ajili ya viwanda ambavyo vinadhamiriwa. Ni lazima tuandae vijana leo kwa ajili ya kwenda kuajiriwa kwenye viwanda vinavyotegemewa kuanzishwa. Sasa, haya yote yanahitaji uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ni gharama na ndiyo sababu wakasema, kama ukiona elimu ni gharama, jaribu ujinga. Elimu ya ufundi ni gharama kuliko ambavyo tunategemea kuona. Elimu ya ufundi peke yake kwa shule ambazo zipo sasa hivi, zinahitaji shilingi bilioni 135.5 ili ziweze kupata vifaa. Walimu waliopo sasa hivi ni nusu, 50% peke yake, kati ya Walimu ya zaidi ya 2,000 waliopo ni zaidi ya 1,000, nusu ya walimu hatuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tuna dhamira ya dhati ya kwenda kwenye elimu ya kujitegemea itakayoleta manufaa kwa Watanzania kuepuka kupigiwa simu za mara kwa mara kuombwa ajira, ni lazima tujikite kwenye elimu yenye tija kwa kupeleka vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika shule ambazo tumeziandaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko. Nilimtaja Mheshimiwa Mohamed Lujua Monni, na Mheshimiwa Tarimba Abbas Gulam ajiandae.

MHE. MOHAMED L. MONNI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia mjadala huu muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema ambaye ametujaalia afya njema, ametujaalia uhai na leo tupo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais, amefanya kazi kubwa. Kila Mbunge ambaye anasimama hapa, anaeleza mazuri ambayo yametendwa kwenye majimbo yao, anaeleza namna gani Mheshimiwa Rais amewatendea haki Watanzania. Kwangu mimi yamefanyika mambo mengi, nami kipekee kabisa nachukua nafasi hii kumshukuru sana na ninaamini amefanya kazi ambayo Wanachemba wanajua wajibu wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru pia Mheshimiwa Waziri, hotuba yake ilikuwa nzuri sana, amegusa maeneo yote. Nimefurahia kuchangia kwa sababu moja tu. Kila nilipoenda ofisini kwake lifanya kile ambacho kinahitajika kule Chemba, kwa hiyo, leo hapa nina jambo. Mheshimiwa Waziri nakushukuru kwa namna ambavyo unafanya kazi. Nawashukuru Naibu Mawaziri wote wawili pamoja na wataalam wote wakiongozwa na Katibu Mkuu, kwa kazi kubwa ambayo wanafanya. Nafahamu Wabunge wengi hapa wanaguswa na Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, natamani nikishukuru Chama cha Mapinduzi, hasa Mkoa wa Dodoma. Tumekuwa na Mwenyekiti mzuri sana, Alhaj Adam Kimbisa ambaye amekuwa akitekeleza na kusimamia vizuri Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mkoa wa Dodoma kwa Chama cha Mapinduzi ni salama, uko kimya kwa sababu ya Mwenyekiti, anafanya kazi vizuri. Pia, namshukuru Katibu pamoja na wenzake wote ambao wanasimamia Ilani ya Chama cha Mapuinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaye Mkuu wa Mkoa ambaye anaratibu vizuri shughuli za Serikali kwenye Mkoa wa Dodoma, nampongeza sana. Pia nampongeza Mkuu wa Wilaya; vile vile tunaye Mkurugenzi wetu mpya wa Wilaya ya Chemba ambaye tunaona mwelekeo, sasa tunaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, namshukuru Mkuu wa Wilaya kwa kazi, pamoja na kuwa ni wapya, lakini wanafanya kazi nzuri sana. Naomba nichangie kwenye maeneo matatu tu. Naomba nichangie kwenye elimu, afya, pia nichangie kwenye barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Serikali sana, kwa miaka minne hii ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan tumejenga shule mpya saba za sekondari. Tumejenga shule maalum ya zaidi ya shilingi bilioni 4.1. Ninaamini shule ile inaenda kutatua changamoto na kutoa matokeo chanya kwa wanafunzi wetu ambao wamekuwa wakisoma kwenye shule za kutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefungua shule mpya za msingi 13. Tumepokea zaidi ya shilingi bilioni 17 kwenye sekta ya elimu, Msingi na Sekondari. Tumejenga zaidi ya madarasa 145; tumemalizia maboma zaidi ya 60. Tumefanya kazi kubwa sana kwenye elimu, kazi kubwa sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa namna ya kipekee, mara zote ametoa fedha, lakini pia ametusaidia kwenye maeneo ambayo maboma yalikuwa na zaidi ya miaka 13, miaka 15. Nashukuru sana sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumepata kujengewa maabara. Pia, tumepata nyumba za walimu, lakini naishukuru sana Serikali, miaka minne iliyopopita, upungufu wa Walimu kwenye Halmashauri ya Chemba ulikuwa 22%. Leo tunaongea, kwenye *primary school,* tumefika 54%. Nakushukuru sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo ambalo nilitamani sana unisaidie zaidi, mwaka huu tumepata takribani walimu100. Walimu 54 kwa ajili ya sekondari, na walimu 40 kwa ajili ya *primary school*. Tuna upungufu wa zaidi ya walimu 756. Nakuomba sana sana Mheshimiwa Waziri, nilisimama hapa kwa sababu ya upungufu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Chemba ni la kijijini, siyo kama Jimbo la Dodoma Mjini ambalo kukiwa hakuna walimu hapa unaweza ukapata *tuition*. Wapo jamii ya Kisandawe kule, kutoka shule ilipo mpaka kitongoji kilipo ni kilometa 42. Maana yake kama hakuna Mwalimu, hakuna *alternative* yoyote ya kupata masomo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, hebu tunapogawa walimu tuangalie na kipaumbele, ni namna gani tunaenda kugusa maisha ya watu wengi zaidi? Naomba katika hiyo changamoto tuweze kuitatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya pili kwenye elimu ni changamoto ya madawati. Kwa miaka minne hii tumejenga vyumba vya madarasa 147 vyenye madawati. Madarasa yatadumu kwa miaka 50, lakini madawati yatadumu kwa miaka

saba. Ni bahati mbaya sana hatujawahi kuwa na mkakati wa moja kwa moja wa namna gani tunaenda kutibu, baada ya miaka saba yale madawati kuondoka, au madawati kwisha. Ni lazima, hakuna *option*, ni lazima Wizara iangalie namna bora ya kutibu hii changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa Mjumbe wa Kamati ya *LAAC,* wakati huo ukitembelea shule nyingi Tanzania nzima, kuna upungufu mkubwa. Kwangu upungufu wa madawati ni zaidi ya 70%. Ni lazima tuangalia ni namna gani tunaenda kutibu changamoto hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze kwenye sekta ya afya. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, tulikuwa hatuna hospitali ya Wilaya, lakini sasa hospitali ya Wilaya imekamilika. Tumejenga vituo vya afya, vizuri sana. Pia, tumefungua zahanati 11. Nasema hayo ni kazi kubwa sana ambazo zimefanywa na Mheshimiwa Rais Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kuna changamoto kidogo. Kweli tunayo majengo mazuri, lakini kuna upungufu mkubwa sana wa watumishi wa afya. Kwangu mahitaji ni makubwa sana, upungufu ni zaidi ya 71%. Nimesema hapa kwamba, jimbo langu ni la vijijini. Yapo maeneo kutoka kijiji kwenda kitongoji ni kilometa 40. Kijiji kwenda kitongoji! Yaani ili mtu atoke kwenye kitongoji kuja kwenye Kijiji, lazima afanye safari ya siku nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika mazingira ya namna hiyo, ni lazima tuangalie ni namna gani tunapeleka watumishi kwenye zahanati ambazo tumezijenga huko vijijini. Nakuomba sana, umekuwa ukifanya hivyo mara kwa mara, lakini nakuomba tena kwa mara nyingine, ajira za safari hii zizingatie maeneo ambayo yana mahitaji makubwa zaidi na ambao hawana *alternative*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hivyo, wananchi wa kule kijijini hakuna *dispensary* ya mtu, hakuna *private dispensary*, hakuna hospitali ya *private*. Maana yake ni kwamba, kama zahanati yetu haina dawa, zahanati yetu haina mtumishi, maana

yake yule mtu atabaki kuwa na tatizo lile lile bila *alternative* yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo ni la muhimu sana, kuna changamoto kubwa nimewahi kuisema huko nyuma, naomba kidogo Mheshimiwa *Eng*. Seff anisikilize. Hakuna uwiano ulio sawa, kati ya *sealing* zinazotolewa kutoka Halmashauri moja hadi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Chemba ina mtandao mkubwa wa barabara kwa sababu, jimbo ni kubwa sana. Wakati mwingine ukiangalia fedha inazopewa, sisi tuna zaidi ya kilometa 900, ukiangalia *ceiling* yetu ni ndogo kuliko watu ambao wana mtandao wa barabara wa kilometa 400, nami najua *Engineer* Seff ni Mhandisi, anajua *ratio analysis*, sijui ni kwa namna gani unaweza kutenga fedha kidogo kwa mtu mwenye barabara ndefu halafu ukaweka fedha nyingi kwa barabara fupi? Hili jambo linatakiwa liangaliwe upya, liratibiwe upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2024 tulipitisha bajeti hapa ya barabara. Zipo barabara ambazo tulizitengea fedha, moja ya barabara hizo ni Rufati – Muungano, Chemba – Soya, Donsee – Bugani – Kamaziwa, Baaba – Wavada, mpaka leo hazijatangazwa. Ukimwuliza Mhandisi mbona sisi tumepitisha bajeti? Anasema bado sijapata kibali cha kutangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, zipo barabara ambazo zilitangazwa kama Mrijo Juu – Magasi zimesimama kwa sababu, *TARURA* hawajapewa fedha. Nina maombi mawili; kwanza naomba mruhusu hizi barabara zitangazwe kwa sababu, tayari tulishawaambia wananchi kwenye bajeti hii tunaenda kujenga barabara moja, mbili, tatu. Kutokuzijenga ni kutengeneza kutokuaminika wakati mwingine tunaposema tumepitisha bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wakandarasi waliopo kwenye barabara zile kwa mfano, huyu wa Mrijo Juu – Magasa ameondoka, ukimwuliza kwa nini umeondoka *site?* Anasema ni kwa sababu, hajapata fedha. Kwa hiyo, nawaomba, najua fedha

zimeanza kutoka, na huyu mkandarasi wetu alipwe ili angalau barabara hii iweze kutengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna barabara muhimu sana, tangu nimekuwa Mbunge nimekuwa nikiongelea hapa. Nimeuliza maswali zaidi ya mara tatu, lakini nashangaa hujawahi kushituka kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna barabara ya kutoka kwa Mtoro – Sanzawa hadi Mpendo, ni barabara ndefu ya kilometa 54. Bajeti tunayopata *ceiling* ni shilingi bilioni 2.3, hakuna namna unaweza ukatengeneza barabara korofi vile kwa shilingi bilioni 2.5. Tumekuja na maombi maalumu mara kadhaa, namwomba Mheshimiwa Waziri, mimi najua yeye ni bingwa sana, jambo hili anaenda kulitatua. Hebu aangalie namna ambavyo anaweza kusaidia kwenda kutatua changamoto hii ya barabara.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. MOHAMED L. MONNI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naona unaniangalia. Muda wangu umeisha, lakini nikuombe Mheshimiwa Waziri, barabara hiyo ni muhimu sana, maana inaweza kutatua changamoto ya kata nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni. Nilimtaja Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, ajiandae.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya TAMISEMI. Awali ya yote, napenda kusema kwamba, naunga mkono bajeti hii na ninaomba Waheshimiwa wenzangu waweze kuipitisha ili tuweze kuipatia Serikali nyenzo za kwenda kutuletea maendeleo ya haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeagizwa na wananchi wa Kinondoni nije nizungumze mambo mawili ya msingi. La kwanza ni kuipongeza Serikali na hapa ninapoipongeza Serikali, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wakati nagombea Ubunge, nilikuwa na ndoto ya kutaka kuiona ile Kinondoni tunayoitaka, Kinondoni ya mjini, Kinondoni tunayoitaka. Mheshimiwa Rais ametutimizia ndoto yetu na hakika utekelezaji wa ilani ya uchaguzi naweza nikasema imefikia zaidi ya 90% kwa ushahidi wa kile ambacho kilitakiwa kufanyika, kimefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, namshukuru sana ndugu yangu Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, yeye ni mwana Kinondoni mwenzangu. Kwa wale ambao hamjui, Mheshimiwa Mchengerwa ni mwana Kinondoni katika jimbo langu, hivyo namshukuru kwa sababu, umekuwa ni msaada mkubwa sana kwangu. Hivi ninavyozungumza, wananchi wenzake wa Kinondoni niliwapelekea taarifa kwamba, Mheshimiwa Mchengerwa baada ya kumaliza bajeti yake amesema nitaongozana naye kwenda Kinondoni, kuna kazi kubwa ambayo ameniahidi anakwenda kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kwanza ni kwenda kuzindua *dispensary* ya mfano ya mionzi kutokana na fedha za Mfuko wa Jimbo, shilingi milioni 129, tumewekeza katika hospitali ile ambayo tayari inafanya kazi, *Ultrasound* na *X-Ray* za kisasa. Hivyo, Mheshimiwa aje aone, kumbe fedha za Mfuko wa Jimbo zinaweza zikafanya maajabu kiasi gani? Vilevile ameniahidi na nikawaambia wananchi wa Tandale na Ndugumbi kwamba, Mheshimiwa Mchengerwa atakuja hapa kutafuta majawabu ya mto Mwangosi, mto ambao unafurika na kuwasumbua wananchi wa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nikawaambia watu wa Kijitonyama, kule ambapo tuna Uwanja wa *KMC* kwamba, kuna mto unaitwa Mto Kijitonyama na umeahidi tutakwenda tukaangalie, uone ni kwa jinsi gani Serikali inakwenda kusaidia wananchi katika eneo hili na mwisho, pale Mwananyamala sehemu za Msisiri kwenye lile bonde. Bonde lile ma-*engineer*

wengi sana wamefeli kutafuta majawabu. Najua Mheshimiwa Mchengerwa tukienda pamoja pale atajua ni kwa jinsi gani ma-*engineer* waliopo katika Wizara yake watakwenda kutusaidia. Hii ni pamoja na Mto Mzimuni katika Kata ya Mzimuni, pia, nitampeleka kule. Ni kazi ya siku moja au nusu ya siku, atatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetufanyia mambo makubwa. Bonde la Mto Msimbazi, hongera sana kwa Mheshimiwa Rais, ametufanyia kazi. Shilingi trilioni 1.3 zinakwenda bonde la Mto Msimbazi, pamoja na Daraja la kisasa la Jangwani linalokwenda kubadilisha maisha ya wananchi wa Magomeni na maisha ya wananchi wa Mzimuni. Hakika wale wakandarasi wapo mzigoni, na jana nilizungumza na Mheshimiwa Ulega, ameniambia hata fedha za kuanzia wameshapewa. Hivyo ndani ya miaka miwili Magomeni na Mzimuni patakwenda kubadilika pale, sijui tutakuwa kama nchi gani? Siwezi nikaielewa, lakini panaweza pakapendeza kama vile *Young Africans* ilivyo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisemee kidogo changamoto. Leo hii tulikuwa na changamoto ya elimu. Pale kwetu, huwezi ukaamini kwamba katika jimbo kubwa kama lile la mjini, lenye watu takribani laki nne, hawana *high school*, lakini kwa mara ya kwanza, tangu tupate uhuru Kinondoni tunakwenda kuwa na *high school*, ambayo Julai, 2025, keshokutwa, wanafunzi wa kwanza wanakwenda kusajiliwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera sana kwa Mheshimiwa Rais, amenifanya nijisikie, kila ninavyotembea nasema, naam. Mimi nipo sawa, na ndiyo maana wananchi wa Kinondoni watambue kwamba nami nimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunazungumzia shule za *English Medium*. Pale kwetu Dar es Salaam shule hizo unazikuta Upanga, lakini leo mpaka Uswahilini kwetu kule Kigogo kuna *English Medium* za kisasa, Magomeni za kisasa, Kijitonyama za kisasa, sasa tunataka nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa ambacho nawashukuru tena ni tatizo sugu la *secondary school* tulilokuwanalo katika Kata ya Tandale. Hili suala tulimfikishia mpaka Mheshimiwa Rais, akatupatia fedha, sasa hivi ninavyozungumza, Tandale wana *secondary school* ya kisasa na wapo *form two*. Nawashukuru sana Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, walitoa kibali shule ile iitwe *Tarimba Abbas Secondary School*, Alhamdulillah, nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye Kata ya Kinondoni, ambayo ndiyo kata ya nyuma kabisa, leo ina *secondary school* ya kisasa. Hivyo tumeondoa matatizo ambayo yalikuwepo katika jimbo langu, mambo yote, miundombinu ya elimu, yamekwisha hatudaiwi. Mheshimiwa Dkt. Samia hatumdai katika masuala ya elimu, Dkt. Samia hatumdai kwenye masuala ya afya, tumetimia. Tuna vituo vya afya, tuna *dispensary* tena za kisasa. Changamoto iliyopo ni pale Tandale peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Manispaa tumetenga shilingi milioni 600 kwa ajili ya upanuzi wa Kituo cha Afya kile ambacho hupokea zaidi ya watu 1,000 kwa siku. Ukumbuke pale tuna soko la kisasa kubwa la nafaka, hivyo wananchi wanaokuja pale kupata huduma ni wengi sana. Tumeweka shilingi milioni 600 kwa ajili ya kununua eneo, lakini tutaomba Serikali, na hii naomba iwekwe kwamba, tungependa tutanue kile kituo chetu kiweze kuwa kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie matatizo ambayo yapo kule Mwananyamala, yaliyopo Magomeni, Tandale, Makumbusho, ambayo Serikali ya Dkt. Mama Samia imekwenda kutuondolea aibu hii, kwamba, Mto Ng'ombe wakati unajengwa, ambao ndiyo unapitia maeneo mengi sana na kuleta athari kubwa ya mafuriko, alimtuma Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikuja kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alipokuja Mheshimiwa Waziri Mkuu alihakikisha mkandarasi anarudi katika eneo lile, lakini wale ambao walikuwa wanatakiwa kulipwa fidia ili wapishe ule mradi, fedha zile zikatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza, Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Mchengerwa, matatizo ya mafuriko Kata ya Tandale, Makumbusho, Ndugumbi, Magomeni na Mwananyamala, ambayo yalikuwa yanaletwa na ule Mto Ng'ombe yale yameisha. Inyeshe mpaka inyeshe, watu wana-*enjoy* na hata kuamka saa nne wanaweza wakaamka. Hongera sana, Mheshimiwa Rais ametusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda nizungumzie jambo ambalo kidogo lina matatizo, ingawa hili nalo limetuletea mafanikio makubwa. Hakuna kata katika Jimbo la Kinondoni, Mheshimiwa Mchengerwa, ambapo tumeshindwa kujenga barabara hata moja. Kata zote tumeweka miguu yetu. Kuna kata tumefanya barabara nyingi na tumefungua uchumi wa wananchi wa Kinondoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Kigogo kuna masoko ambayo yalikuwa hayafanyi kazi, lakini kuna barabara inaitwa Mapera, tumeijenga ile kwa lami. Sasa hivi wananchi wanaweza kufanya shughuli zao za kibiashara vizuri zaidi na kuwanyanyua kiuchumi. Kata ya Hananasif, ambayo ilikuwa haina mradi, juzi tumewapeleka wakandarasi kwenda kujenga barabara tatu katika kata ile, Kinondoni ambako ndiko kulikuwa kumesahauliwa Barabara ya *Best Bite*. Wengi mnakaa Kinondoni mnaweza mkaiona sasa hivi Kata ya Kinondoni ilivyobadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijitonyama kule anapotoka Mheshimiwa Mwenyekiti wangu, wazawa wa Kamati ya Bajeti tumetengeneza pale Mabatini, palikuwa panatisha. Sasa hata sijui nichangie nini zaidi ya kuwaambia Serikali, ahsanteni sana, Mheshimiwa Mama Samia ahsante sana. Kilichobakia ni kitu kidogo sana na wala sitaki nimsumbue Mheshimiwa Mama Samia, namsumbua huyu Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, ndio nakwenda naye baada ya bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mungu awabariki sana TAMISEMI, wanafanya kazi vizuri sana, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas. Nilimtaja Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, ajiandae.

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza kabisa, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima mpaka tukawepo hapa kuchangia hoja muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, naomba nimpongeze Spika wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, kwa kazi nzuri anazofanya. Jinsi anavyoliendesha Bunge, kwa kweli anastahili pongezi, maana wakati mwingine tunajiuliza, ni wakati gani anapumzika? Unabaki kumshukuru Mungu, kwa ajili yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Waziri, kaka yangu, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa na Manaibu wake wote wawili kwa kazi nzuri. Kwanza kabisa, nampongeza kwa uchaguzi uliopita wa Serikali za Mitaa, ameweza kuendesha vizuri sana, nchi yetu ina amani, tumepata viongozi walio bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii pia kumpongeza Mkuu wangu wa Mkoa, ndugu yangu Makongoro, kwa kusimamia vizuri Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Pia, nakishukuru sana Chama changu cha Mapinduzi, Mkoa wa Rukwa, kimeweza kusimamia vizuri Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nampongeza sana Rais wangu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri anazozifanya katika kipindi chake cha miaka minne, amefanya mambo mengi makubwa na mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wetu wa Rukwa, tulikuwa tuna changamoto sana ya hospitali za Wilaya, lakini

Mama katika kipindi chake ameweza kutupatia fedha za kujenga hospitali za wilaya, wilaya zote nne tumepata hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi kati hapa tumezindua Hospitali ya Isihofu iliyogharamiwa takribani shilingi 4,500,000,000, sasa hivi imeanza kutumika. Pia, *Sumbawanga DC* hospitali imefunguliwa, tulipokea fedha takribani shilingi 4,500,000,000, kwa ajili ya ile hospitali ya wilaya. Tumejengewa hospitali wilaya zote, hongera sana Mama, umeupiga mwingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, Mheshimiwa Rais ametujengea vituo vya afya vizuri. Kipo kituo cha mfano Sumbawanga Mjini. Kile kituo sisi akina mama zamani tulikuwa tuna hofu, ukiwa mjamzito ukiambiwa unafanyiwa operesheni, unajihesabia mawili, aidha kufa au kupona, lakini sasa hivi vituo vya afya vyote, hasa kituo kile, ukienda mjamzito, akina mama sisi tunaomba ufanyiwe operesheni badala ya kusukuma na kuchanika msamba. Sasa hivi hakuna tena kuchanika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madaktari wapo vizuri, ukifanyiwa operesheni siku ya kwanza, ya pili, ya tatu, umeshaamka. Kwa hiyo, mama ametuletea huduma nzuri sana katika vituo vyetu vya afya, lakini pia, huduma zimejitosheleza. Kwenye vituo vya afya majengo ya mama na mtoto yamejitosheleza kabisa, ukijifungua mtoto njiti, mtoto anawekwa vizuri anakua bila wasiwasi. Hongera sana Rais wetu mpendwa, kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie sasa kwenye hoja zangu za msingi, naanza na Kituo cha Afya cha Kirando. Kituo kile ni kikubwa sana, kinahudumia vijiji vingi sana na kata zaidi ya nane; Kata ya Korongwe, Kata ya Kipili, Kata ya Kitete, Kata ya Mkinga, Kata ya Ninde na Kata ya Kirando. Kile kituo cha afya kinahudumia vijiji vingi sana. Tulikuwa tunaomba kipandishwe hadhi iwe hata hospitali ya Wilaya, lakini kituo kile hakina *mortuary*, pa kulaza miili panakuwa na uhitaji. Tunaomba kituo kile kijengewe jengo la *mortuary*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la barabara. Kwanza kabisa, nampongeza Mkurugenzi wa *TARURA,* anafanya

kazi nzuri, lakini nilikuwa naomba kwenye *TARURA* bajeti iongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna barabara nyingi ambazo zinahitaji huduma. Kuna barabara inayotoka Mto Wisa kupitia Ng'ongo kuingia Kristo Mfalme, barabara ile ni muhimu sana. Tulikuwa tunaomba *TARURA* waongezewe fedha kusudi iweze kutengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la maboma. Tunaomba pia, bajeti ya elimu iongezwe kwa sababu tuna maboma mengi ambayo bado hayajakamilika. Kwenye Wilaya ya Sumbawanga kuna maboma mengi sana ambayo hayajaisha, nikianza na maboma ya zahanati, tuna boma pale Kifinga, Msia, Tululu, Kilando, Legeza, Ilemba, Kapewa, Mtetezi na Sikaungu. Tunaomba basi, bajeti ya safari hii haya maboma yaweze kupatiwa fedha na hatimaye yaishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee hoja nyingine ya akina mama. Kwanza kabisa, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutupatia ile 10%, ambayo ni ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. Kwa kweli, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kweli, ile huduma ni nzuri sana, akina mama wanapata mikopo na hiyo huduma inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Jukwaa la Wanawake. Jukwaa hili lilianzishwa kwa ajili ya (Mheshimiwa Waziri naomba unisikilize) uwezeshaji kiuchumi wa akina mama, lakini jukwaa hili naona kama limetelekezwa. Akinamama, viongozi wa majukwaa haya ya uwezeshaji, wanapata tabu sana kwa sababu, hawana fungu, hawana bajeti. Kwa hiyo, inakuwa ni tabu tupu. Nilikuwa naomba Jukwaa la Wanawake la Uwezeshaji kiuchumi lipatiwe fungu na bajeti yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala lingine la mikopo ambayo ilikuwa inaitwa Imbeju. Wanawake waliitikia mwitikio mkubwa sana kupata mikopo inayoitwa Imbeju. Wakachangishwa fedha, wakaambiwa wafunge akaunti, wakaambiwa waandae mihtasari, lakini matokeo yake akina

mama walifungua akaunti, wametoa fedha zao, wamepoteza muda, lakini hamna kinachoendelea kwenye suala zima la mikopo ya Imbeju.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba nayo waifanyie kazi ili akina mama hawa waweze kupata mikopo hiyo. Kama haipo, basi waambiwe kwamba mikopo ya Imbeju haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee pia suala la watumishi. Mama amejenga vituo vya afya, amejenga shule, lakini Mkoa wa Rukwa tuna upungufu wa watumishi kwa 75%. Tunaomba sasa watuongezee watumishi, na watumishi hao wajengewe nyumba; kwa sababu watumishi wengi wakiletwa katika mikoa yetu ya pembezoni na wakipelekwa vijijini wanahama tena kurudi mjini kwa sababu kule kunakuwa na changamoto pengine za nyumba za watumishi. Kwa hiyo, tunaomba watumishi wajengewe nyumba ili waweze kutulia kule. Endapo wanapokuwa wanawaajiri wawe wanawapa mikataba kwamba hakuna kuhama, ndani ya miaka tano hahami mpaka hapo atakapomaliza miaka mitano ndipo afikiriwe jinsi ya kuhama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata. Nilimtaja Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, ajiandae.

MHE. MASACHE N. KASAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nami kupata nafasi ili niweze kuchangia kwenye hotuba hii nzuri sana ya ndugu yangu Mheshimiwa Mchengerwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza, ameweza kuisoma hotuba yake vizuri. Nina hakika Wizara hii wamejipanga vizuri, yeye pamoja na wasaidizi wake, kwa maana ya Manaibu Waziri lakini na Katibu Mkuu pamoja na timu yake yote kwa ujumla. Hakika wanaitendea haki hii Wizara. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nitaendelea kuungana na wenzangu tuendelee kuweza kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo imeendelea kushusha miradi mingi ya kimikakati ya kimaendeleo kwenye kila sekta; wameweza kugusa takriban sekta zote. Hapa kila mmoja akisimama hapa siyo kwenye kata, siyo kwenye vijiji, hakuna mahali ambako mradi haujafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mimi kule Wilayani kwangu Chunya takribani kila kijiji, na kila kata, kila mahali miradi imeenda imetiririka. Tunampongeza Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hakika ameonesha kwamba yeye ni mama na ni mama mwenye shughuli. Ndiyo maana tunasema tunamwongezea mitano tena; na sisi, pamoja na kumwongezea yeye na sisi bado tumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa afya, mimi niseme kwamba kila mmoja amezungumza hapa, lakini sisi kule kwetu Chunya kwenye upande wa afya hospitali ya wilaya tumepata zaidi ya shilingi bilioni 5.7. Leo ukifika pale, na wale ambao hawajafika zaidi ya miaka miwili wakifika pale leo wanapotea kwa namna ambavyo majengo yamejengwa ya kisasa, vifaa tiba vimewekwa pale ndani na huduma sasa zinatolewa za viwango vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine wakifika pale mpaka wanashangaa, kwamba ni hii Chunya tunayoifahamu au nyingine! Sisi ndiyo kazi ambayo alitupatia na tumeendelea kuifanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haijaishia hapo, katika kipindi hiki hapa cha Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na miaka mitano ambayo sisi tulipewa ridhaa hii vituo zaidi ya zahanati 15 tumeweza kuvijenga na vinatoa huduma. Haya kwetu sisi ni mafanikio makubwa kwa sababu tunasema mtu ni afya ndiyo maana afya imekuwa kipaumbele cha kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kana kwamba haitoshi, kwenye upande wa vituo vya afya zaidi ya vituo vya afya vitano vimejengwa ndani ya hii miaka mitano. Kituo cha Afya cha Mamlaka ya Mji Mdogo wa Makongorosi ni kikubwa, kina hadhi ya hospitali ya wilaya. Kimejengwa, kinatoa huduma, kina *facilities* zote, na mpaka huduma ya *mortuary* pale inatolewa na majokofu yamewekwa pale. Wananchi wananufaika kwa huduma hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, hatujatosha hapo, Kituo cha Afya cha Matwiga tulipata fedha na juzi tu takribani kama wiki tatu zilizopita tumepata zaidi ya shilingi milioni 200. Kazi inaendelea pale na huduma zinaendelea kutolewa. Kituo cha Afya cha Mafyeko tulipata zaidi ya shilingi milioni 300, kazi inaendelea lakini pia na huduma zinaendelea kutolewa pale na fedha zinazidi kutiririka kuhakikisha kwamba vituo hivi vinakamilika. Kituo cha Afya Kambikatoto ambacho ni zaidi ya kilometa 260 kutoka Chunya Mjini; kimejengwa kituo kizuri, Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alitupatia hizi fedha wananchi wananufaika pale na gari la wagonjwa tumewapelekea kule. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo imeweza kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi letu moja, haya yameweza kufanyika na mambo mengine bado yanaendelea kufanyika; tunaomba tuzidi kuongeza kwenye upande wa vifaa tiba, tupate vifaa tiba vingi na vya kutosha zaidi. Kana kwamba hiyo haitoshi, tupate pia na wataalamu wa kutosha. Vifaa vipo vichache ilhali pia majengo yapo ya kutosha, lakini tuna upungufu wa wataalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri alichukue hili, atuletee wataalamu wa tiba tukahakikishe kwamba huduma za afya zinakwenda vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa elimu, kila mmoja hapa amekuwa shahidi, ameweza kuzungumza namna ambavyo kwenye upande wa elimu Mama yetu Mheshimiwa Dkt.

Samia Suluhu Hassan alivyoweza kuigusa elimu kwenye jamii yetu. Yamejengwa madarasa ya kutosha, zimejengwa shule shikizi na shule mpya zimejengwa. Tukianza kutaja hapa shule mpya moja moja hatutamaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama amewekeza kuhakikisha kwamba elimu ndiyo mkombozi wa Mtanzania, ndiyo maana amepeleka fedha nyingi sana kwenye elimu. Kana kwamba haitoshi, ndani ya miaka minne ya Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tumeweza kujenga sekondari mpya tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejenga Sekondari mpya Lupa ya Maheka *Girls,* tumejenga Lualaje Sekondari, tumejenga Mafyeko, tumejenga Kambikatoto na tumejenga na Kata ya Nkung'ungu. Hizi sekondari mpya tano zimejengwa na sekondari mpya nyingine mbili zinaendelea kujengwa kwenye Kata ya Upendo na Kata ya Matundasi, kwa maana ya Kijiji cha Itumbi, tunaendelea kujenga. Haya kwetu sisi ni mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeendelea, mwaka huu tumeweza kusajili sekondari nyingine mbili kwenda Kidato cha Tano na cha Sita. Tunategemea kwamba kuanzia Julai zipokee wanafunzi hawa wa Kidato cha Tano na cha Sita. Haya kwetu ni mafanikio makubwa sana. Tunampongeza Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tunaomba tuongeze juhudi sana ili tuhakikishe kwamba kwenye upande wa elimu tutatafanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnavyofahamu, Wilaya yetu ya Chunya ni moja kati ya wilaya kongwe; ilikuwa nyuma kwenye upande wa elimu na ndiyo maana sasa hivi tunakwenda kwa kasi zaidi. Kutokana na ukongwe wake huu, shule zile ambazo zilijengwa zamani, tuna shule kongwe nyingi, zimechakaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwenye mipango hii tunajua tumeanza kupata fedha kwa ajili ya shule chakavu, lakini kwa Wilaya yetu ya Chunya kutokana na ukongwe wake na shule nyingi kongwe tunaomba atuangalie

kwa jicho la huruma ili tuweze kupata fedha nyingi zaidi ili zile shule nyingi kongwe ambazo tunazo ziweze kupata fedha hizi na tuweze kukarabati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba uchumi ili uweze kwenda vizuri zaidi, lazima tuwekeze kwenye miundombinu, hasa miundombinu ya barabara. Wakati Mama Mheshimiwa Dkt. Samia anaingia madarakani sisi Wilaya ya Chunya bajeti yetu ilikuwa shilingi milioni 750 kwa mwaka, lakini leo tunavyozungumza tumefika shilingi bilioni 2.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mafanikio makubwa sana. Ndiyo maana tunaposema Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia mitano tena hatuongei tu kwa kumpamba, ni kwa sababu amefanya kazi na inaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingi zimejengwa na nyingi zimetengenezeka. Barabara ya kutoka Chunya Mjini kwenda Ifumbo imetengenezwa kwa kiwango ambacho hakina mfano wake. Imejengwa kwa moramu, inapitika vizuri. Walikuwa hawana usafiri kule, leo wanalala magari matatu ambayo kila siku yanatoka kuanzia Ifumbo yanaenda sehemu nyingine mbalimbali. Haya sisi kwetu ni mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara kutoka Njiapanda kwenda Sangambi imetengenezwa vizuri, Barabara ya kutoka Lupa kwenda Lualaje, Barabara ya kutoka Lupa - Nkung'ungu na Kambikatoto Sifa na nyinginezo zimefanikiwa vizuri. Pia, madaraja yameendelea kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba haya yamepiga hatua, lakini kwa jiografia ya Wilaya ya Chunya na kwa ukubwa wa Wilaya ya Chunya, leo Wilaya ya Chunya kijiografia ina zaidi ya *square meter* 13,000, ambapo *square meter* 13,000 hizi ukizijumlisha Wilaya ya Kyela, Rungwe, Mbeya Mjini, Mbeya Vijijini bado haijafikia Wilaya ya Chunya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado tunapata bajeti ndogo, hizi shilingi bilioni 2.3. Pamoja na kwamba tumeongezewa,

na tunaishukuru Serikali, tunaomba sana tuangaliwe na jicho la huruma ili tuweze kuongezewa bajeti hii ili tuweze kutengeneza barabara nyingi zaidi. Kwa sababu kwa sasa hivi barabara za kwenda vitongojini, nyingi hazijasajiliwa. Ndiyo kazi tunayoifanya, tuzisajili, ziingie kwenye mtandao wa *TARURA* ili tuweze kuweza kuiombea fedha na hivyo tupate fedha nyingi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kusajili barabara kadhaa, na tunaendelea kuzisajili barabara nyingine kwa sababu kule sasa hivi ndiko kwenye uchumi mkubwa sana hasa kama mnavyofahamu sisi Wilaya yetu ya Chunya ndio wazalishaji wa pili wa dhahabu kwa wachimbaji wadogo kwa Tanzania. Kwa hiyo, muone namna gani ambavyo barabara hizi zinakwenda kule kwenye maeneo ambako uchumi unazidi kufunguka; na ukiufungua uchumi wa kule maana yake ni kwamba, Serikali pia itapata mapato mengi zaidi, wananchi wataweza kunufaika kiuchumi, nasi kwa ujumla wake tutaweza kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya, lakini kupitia mapato ya ndani tumeweza kujenga na tunaendelea ujenzi wa stendi mpya pale Halmashauri yetu ya Wilaya ya Chunya. Naishukuru Halmashauri yangu ya Wilaya ya Chunya, Baraza la Madiwani na Mkurugenzi wetu ndugu yangu Tamim Kambona, anafanya kazi kubwa sana. Tumepata zaidi shilingi bilioni tatu na stendi inajengwa; na inawezekana ndiyo itakayokuwa stendi ya kwanza nzuri ya kisasa kwa Mkoa wa Mbeya inayojengwa kwa kupitia mapato ya ndani ambayo sisi Chunya tunaendelea kuijenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kazi ambayo wananchi walituamini kuifanya, tumeifanya kwa ukubwa wake, tumetekeleza Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi kwa kuhakikisha kwamba haya na mengine yanakwenda vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa 10% ya zile fedha kutoka kwenye Halmashauri, tunamshukuru mama yetu, baada ya kuzirudisha fedha, leo vikundi vingi zaidi vimeweza kunufaika. Awamu ya kwanza zilitolewa zaidi ya shilingi milioni 840 kwa

Wilaya yetu ya Chunya; awamu ya pili ambayo kuanzia mwezi ujao wiki ya kwanza au ya pili tutakwenda kuzikabidhi. Tuna fedha ambazo zipo tayari shilingi bilioni 1.2, hizi zinapokwenda kwa wananchi maana yake tunakwenda kuunyanyua uchumi wa akina mama, vijana na walemavu wa Wilaya yetu ya Chunya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, tunaomba sana haya mengineyo ndiyo sababu inayotufanya leo hii tunaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambayo inaweza kufanya kazi kubwa na nzuri zaidi. Huduma za kijamii zinaendelea kuboreshwa zaidi, na sisi Wanachunya tunaendelea kuwaambia Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia yeye hatudai, ila sisi tuna deni kwake, na hili deni tutampatia mwezi Oktaba kwa kumpa kura nyingi za kishindo zaidi ili aendelee kutumikia na sisi ambao tumechaguliwa na wananchi tuendelee kutumikia zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka. Nilimtaja Mheshimiwa Anna Richard Lupembe na Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, ajiandae.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa, naomba nimshukuru Mungu ambaye ametupa neema kubwa, katika kipindi cha miaka minne tupo humu ndani tukiwa wazima na afya njema. Naomba nimshukuru sana Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo amewafanyia Watanzania katika Tanzania nzima hususan Mkoa wa Katavi pamoja na Jimbo la Nsimbo, amefanya kazi kubwa; ametuletea fedha nyingi na miradi mingi katika Jimbo la Nsimbo, Halmashauri ya Nsimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Mchengerwa pamoja na Manaibu wake wote wawili kwa kazi kubwa nzuri wanayoendelea kuifanya na usimamizi wa Wizara. Hongereni sana Mheshimiwa Waziri Mchengerwa. Nisimsahau Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na Manaibu Katibu Wakuu wote ambao wanafanya kazi kubwa nzuri kwa ajili ya kuendeleza kutuletea fedha katika mikoa yetu tulipokuwa huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee sana naomba nimpongeze Mkuu wangu wa Mkoa wa Katavi Mwanamvua Mrindoko kwa kazi kubwa nzuri anayoifanya katika Mkoa wetu wa Katavi. Anahamasisha na ana maono. Mkoa wetu wa Katavi umetulia. Hongera sana Mkuu wetu wa Mkoa Mwanamvua Mrindoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nisimsahau Mkuu wetu wa Wilaya, Jamila Yusuph, kwa uhamasishaji wake anaoendelea kuufanya katika Mkoa wetu wa Katavi Wilaya ya Mpanda. Anafanya kazi nzuri, anahamasisha, ninaona anachukua kero mbalimbali. Naomba nimpongeze Mkuu wetu wa Wilaya, Jamila Yusuph. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiwasahau Chama cha Mapinduzi Mkoa, Kamati ya Siasa ya Mkoa, Kamati ya Siasa ya Wilaya ambao wanaendelea kusimamia Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Naomba nimpongeze Mwenyekiti wa Mkoa wa Katavi wa Chama cha Mapinduzi na Mwenyekiti wa Wilaya yetu ya Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nampongeza Mkurugenzi pamoja na watendaji wote kwa sababu fedha zote zinakwenda kwenye Halmashauri yangu. Wanafanya kazi vizuri na wanasimamia miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watendaji wote katika kata zote pamoja na Watendaji wa Vijiji wameendelea kusimamia miradi yote inayopelekwa katika maeneo yetu. Tusiwasahau Wenyeviti wa Vijiji pamoja na Wenyeviti wa Vitongoji kwa sababu wao ndio

wahusika wakuu kwa kila kitu walichokuwa wanapelekewa katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiache kuwapongeza walimu, walipelekewa miradi mbalimbali wakaisimamia na leo tunawapongeza kwa kazi kubwa nzuri. Walimu wa shule za msingi, walimu wa shule za sekondari waliyabeba majukumu haya kwa kasi kubwa kwa ajili ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze Madiwani wangu 12 wa kata 12. Nimefanya nao kazi vizuri kwa kipindi chote cha miaka minne. Wote tumehakikisha kuwa miradi ambayo tuliiomba imefanikiwa kwa 100%. Naomba niwapongeze Madiwani wote na Mwenyekiti wa Halmashauri yangu ya Nsimbo kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kupitia mfumo wa manunuzi *(NeST)*. Mfumo huu unasumbua wakandarasi sana, haujawa rafiki. Wakandarsi wengi sasa hivi wanashindwa kuingia kwenye mfumo huu kwa sababu unasumbua. *Tender* zinatangazwa, wanashindwa kuingia kwenye *tender* kutokana na usumbufu wa manunuzi jinsi ulivyo, na kwamba wengi sasa hivi wamekata tamaa. Naomba Mheshimiwa Waziri alitazame hili kwa kuwa mfumo wa sasa hivi siyo mzuri sana na siyo rafiki kwa ajili ya wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, naomba nipongeze kwa ajili ya fedha ambazo tumeletewa kwa ajili ukarabati wa maboma. Naomba tuendelee kufanya kazi hii kwa sababu wananchi wengi wamejenga maboma ya zahanati pamoja na shule za msingi. Naomba sana tupeleke fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa zile shule kongwe, kuna shule kongwe za siku nyingi, za miaka mingi, zimechoka, vyoo vinabomoka, vinatumbukia. Ukiangalia, walimu wanapata shida, nyumba za walimu zimechakaa, na nyingine zinabomoka. Nilikuwa naomba tuangalie kwa jicho la huruma zile nyumba ambazo zilijengwa zamani, kwamba zikarabatiwe ili walimu

waweze kuishi katika maeneo hayo ili tuendelee na kazi ya kujenga Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana *Chief* wa *TARURA* kwa kazi kubwa nzuri anayoendelea kuifanya. Tumepata fedha nyingi, miradi mingi ya barabara imetekelezwa na madaraja yamejengwa. Sasa hivi kule kwenye maeneo yetu mvua mvua zinanyesha; ubovu wa barabara, na bajeti yetu imekuwa ndogo kwa Mkoa wetu wa Katavi. Halafu fedha za mwaka huu bado madeni wakandarasi wetu hawajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, kutokana na kazi kubwa ya wakandarasi wa Mkoa wa Katavi ambao ni wavumilivu, wanatengeneza barabara bila hata kulipwa, sasa wamekaa muda mrefu huku *certificates* zikiwa zimefika. Nilikuwa naomba wakandarasi hawa wanaotengeneza barabara na kujenga madaraja walipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na madeni hayo na kwamba kazi haziendi kabisa sasa hivi, hivyo *TARURA* waruhusiwe kutangaza kazi kwa sababu kazi zote zimesimamishwa. Waruhusiwe kutangaza kazi zote za ukarabati maana barabara sasa hivi kule kwetu Katavi zimeshachimbuka na nyingine zimekatika. Naomba basi ule ukarabati utangazwe na maboresho yaweze kufanyika kutokana na uharibifu wa mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mvua tunaihitaji kwa sababu ndiyo maisha yetu. Tunahitaji kufanya kilimo, wananchi wanahitaji kilimo lakini na hapo hapo kuna upungufu ambao umesababishwa na changamoto zinazotokea. Naomba sasa tuongezewe bajeti kwa ajili ya ukarabati na matengenezo katika Mkoa wetu wa Katavi kwa ujumla wake. Hizi fedha ziende ili zikarekebishe barabara pamoja na madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uharibifu, sehemu nyingine madaraja yamekatika kabisa, na watoto hawaendi shuleni. Kuna Kata kama ya Sitalike watoto sasa hivi wana taribani mwezi mzima hawaendi shuleni kutokana na kukosekana kwa daraja, maji yamejaa. Naomba sana basi tupewe bajeti ya dharura kwa

ajili ya kutengeneza barabara za Mkoa wa Katavi hususan Jimbo la Nsimbo ili watoto waweze kwenda shuleni na mambo ya kijamii yaweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa afya, naomba niishukuru Serikali kwani katika Halmashauri ya Nsimbo kuna Hospitali ya Wilaya ingawa bado haijakamilika, lakini hivi karibuni tumeletwa fedha. Tuna vituo vya afya vinne, lakini vile vituo vya afya bado havijakamilika, bado hatujapata wodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru, hapa karibuni nilipata shilingi milioni tisini tisini katika vituo vya afya viwili. Naomba sana niongezewe fedha kwa ajili ya mahitaji makubwa katika vituo wiwili, Kituo cha Afya cha Ugalla na Kituo cha Afya cha Itenka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa, naomba nishukuru kwa kupatiwa *ambulance* mbili katika Halmashauri yetu ya Nsimbo, lakini kwa bahati mbaya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa walikuwa hawana gari, wakaazima *ambulance* kutoka katika Halmashauri ya Nsimbo katika Kituo cha Afya cha Ugalla. Bahati mbaya walivyoichukuwa ile *ambulance* ikaenda kuanguka, ikapinduka. Sasa matokeo yake tumebaki na *ambulance* moja ambayo inahudumia wilaya na vituo vinne vya afya pamoja na zahanati, ile *ambulance* imebaki moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa sababu hatuiombei ajali hata kidogo, ni bahati mbaya, ile ajali ilitokea ikiwa na mgonjwa akikimbizwa Hospitali ya Rufaa Mbeya, na kwa bahati nzuri gari limeharibika, lakini watu walipata unafuu, walipona. Tumewaombea Mungu wamepona, lakini gari ndiyo hilo limeharibika kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ningepatiwa *ambulance* nyingine kupunguza kasi ya wagonjwa kutoka sehemu nyingine hususan Kata ya Ugalla, kilometa 100 kutoka kata mpaka Makao Makuu ya Wilaya, ndipo kuna Hospitali ya Wilaya. Naomba kupatiwa hiyo *ambulance* ili iweze kukidhi mahitaji ya Wanaugalla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana kazi kubwa inayofanyika na Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan na wasimamizi wake wote, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa anajitahidi kuhakikisha trilioni za fedha zinazokuja na anazisimamia vizuri. Nawapongeza sana kwa kazi kubwa, na pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Mungu awabariki na awasimamie mpite wote kwenye Majimbo yenu na wale Viti Maalum mpite. Amen. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Anna Richard Lupembe. Nilimtaja Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa na Mheshimiwa Salome Makamba ajiandae.

MHE. MICHAEL C. MWAKAMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nami kwa kupata nafasi ya kuchangia kwenye hotuba hii ya Bajeti ya Waziri ndugu yangu, kaka yangu Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni shukrani za pekee kwa Mwenyezi Mungu kutujalia afya, mimi binafsi na Wabunge wenzangu leo tumesimama tena kwenye Bunge hili tukiwa tunatimiza miaka ya kikanuni kabisa ya kuwahudumia wananchi waliotuagiza kuja hapa. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa afya njema na kutufanya tutekeleze majukumu yetu salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, namshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Serikali yake kama ambavyo wenzangu wote wamefanya hivyo. Kiukweli kabisa sisi Wabunge, hasa mimi wa Jimbo la Kibaha Vijijini nina kila sababu ya kushukuru kila nikisimama kwa namna ambavyo Mheshimiwa Rais analitendea Jimbo langu mambo mema na makubwa ambayo miaka kadhaa ya nyuma hayakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia hii imeandikwa na Mheshimiwa Rais kwa sababu ya miradi mingi iliyokuja katika jimbo lile, lakini imenifanya nami Mbunge wa *form one* kuwa na historia ya pekee ambayo haijawahi kuvunjwa kwenye Jimbo letu. Miradi mingi ya kimkakati imetekelezwa, na imetekelezwa tofauti na waliokuwa wanafikiri wao ni ma-*senior* kwenye jambo hili, namshukuru sana, sana, sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na timu yake yote ya TAMISEMI, kwa maana ya kuanzia yeye, Manaibu wake, Watendaji wake Wizarani mpaka kule mkoani, tena kule mkoani Mheshimiwa Waziri ile timu ya kuanzia mkoani mpaka kwenye ngazi ya halmashauri yangu, kwa maana ya Mkuu wa Mkoa kaka yangu Kunenge, ndugu yangu Nickson na Mkurugenzi, dada yangu Bieda, hakika ingekuwa ni *forward* ya timu ya mpira, basi ningesema ile ni sawasawa na timu ya Simba. Inashambulia kwa hatari, na ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri aitazame timu ile ibaki katika mikono salama, imalize shughuli tulizozianza bila kufanya lingine lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli kubwa ambayo Mheshimiwa Waziri ninakuomba sana kwa muda huu, tunakoelekea, acha wamalize kazi kubwa waliyofanya na mimi halafu kama yatatokea mengine mwezi wa Kumi itakuwa ni baadaye, kwa sababu kwa kweli ni timu ambayo inamsaidia Mheshimiwa Rais, inaungana na mawazo ya Mbunge, inasimamia miradi ya wananchi na miradi imekwenda kwa kasi ya ajabu sana. Kwa hiyo, nakushukuru sana wewe kwa sababu, ni imani yangu kwamba, siyo tu kwa sababu unatoka Pwani, ni kwa sababu ameikamata Wizara sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, sisi kule Pwani tuna vitu viwili vinafanana, na kaka yangu Mheshimiwa Mchengerwa na watu wengine wachache wanaweza wakavikumbuka nikiwatajia. Kwetu kuna kitu kinaitwa furu, ni tunda la porini ambalo Mwenyezi Mungu amelileta na sanasana nafikiri linapatikana Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kuna kitu kinaitwa sizi. Mbegu ya furu itakapokuwa inachanua ni ya kijani, hii ni ishara kabisa ya Chama cha Mapinduzi, lakini inapoiva ina tabia ya kujificha kwenye rangi nyeusi. Ukijificha kwenye rangi nyeusi inafanana na sizi. Sizi ni kipande cha mkaa. Sasa kule Pwani wanajua kwamba ukiiweka sizi hapa na ukiiweka furu hapa, kama mtu hatambui kati ya vitu hivi kipi kina ladha, wanaweza wakakimbilia sizi. Vilevile, kule Kibaha Vijijini wanafahamu sizi na wanafahamu furu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na utendaji mkubwa wa Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan na uimara wa Mbunge wa Jimbo la Kibaha niliyesimama hapa ninazungumza, wanafahamu wakati ukifika baada ya ratiba hii iliyobadilishwa juzi, watatambua sizi ni nini na furu ni nini? Mheshimiwa Waziri nibebe hizi kama salamu kwa Mheshimiwa Rais, zifike kwamba Wanakibaha Vijijini wanajua furu yao na wataijaza kwenye makapu yote na mapakacha ya Pwani mwezi Oktoba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea kutoa pongezi, nimesema wakati naanza kuzungumza, wakati naingia hapa mwanzoni kabisa mwa Bunge la Kwanza nilipokuja kama Mbunge, nilijawa hofu kubwa sana, nilipokuwa naangalia awamu ya kwanza ya uendeshaji wa Bunge, lakini nampongeza sana Mheshimiwa Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maana yake ma-*senior* wa humu ndani akiwemo Kaka yangu, Mheshimiwa Kigua, alikuwa ananipa mashaka kwamba hivi nitapata nafasi ya kuuliza hata swali la nyongeza na jina langu halijulikani? Nampongeza sana Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Naibu Spika, na Wenyeviti, ninyi mliomsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila niliposimama kwenye kona hii, jina langu lilitamkwa vizuri na niliwasilisha mawazo ya wananchi wa Jimbo la Kibaha. Uhodari wenu wa kuyashika majina yetu hata kama sio wazoefu ndani ya Bunge hili, nina kila sababu ya kupongeza uongozi wake Mheshimiwa Spika; na kwa sababu

yupo ndani ya Bunge hili, naona aangalie kwa vitendo bila kusikia sauti yangu, makofi haya ni kwa ajili yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu waliotangulia kusema wamejaribu kueleza namna miradi mikubwa iliyofanyika Jimboni, sina tofauti nao. Ili nisiweze kula muda wangu katika kueleza kila mradi uliofanywa, nihitimishe maneno haya ya kupongeza miradi kwa kumwambia, yaliyofanywa Jimboni ni ya hatari, ni makubwa, ni mengi na wananchi wanatambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa ninayotaka kuifanya hapa leo, kwanza ni kutoa mifano michache ya mambo makubwa ambayo hayajawahi kufanyika, lakini pia nitatoa maombi maalumu na ushauri kidogo Serikali ikafanye utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mifano michache ninayopenda kuitumia kwenye sekta ya elimu. Jimboni kwangu Kibaha kuna mabadiliko makubwa sana, miaka mitano hii, shule nane za sekondari zimejengwa na watoto wanaendelea kudahiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiichukua sekta ya afya na sekta ya elimu msingi na sekondari, kwa miradi yake iliyotekelezwa kwenye sekta hii imetumika shilingi bilioni 19.57. Ni kitu ambacho hakijawahi kufanyika kwenye Jimbo la Kibaha kwa muda mrefu, japo yapo maneno ya kufikiri kwamba watu hawaijui furu au sizi, wakidhihaki jitihada hizo wakiamini vitu hivi vinashuka tu. Nataka niwaambie, Wanajimbo la Kibaha, kila king'aacho basi ujue kimesafishwa na anayekitunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kazi ya miradi hii iliyofanyika Jimboni, haina tofauti na haina kipingamizi kumwambia Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Mwakamo, Watendaji wa Serikali pamoja na Madiwani wa Jimbo hilo kwa awamu yetu, tumetekeleza wajibu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa shukrani hizi na kueleza michango hii ya miradi iliyotendeka kwa ufupi huo,

naomba niseme, kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri leo amelizungumzia Jiji la Kwala. Kwanza naipongeza Serikali na kama Mheshimiwa Rais asingekuwa na utashi binafsi wa kutupendelea, asingekuwa na sababu kuifanya Kwala iwe kwenye vinywa na mipango mikubwa ya Serikali kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa yapo maeneo mengine yana ardhi kubwa na yanaweza kufanya miradi ambayo Kwala imekusudiwa, lakini Mheshimiwa Rais ametupendelea na amesema lianzishwe jiji maalumu litakaloitwa Kwala litakalokwenda kuwa kongani la viwanda, na linalokwenda kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwenye hili Jiji la Kwala, wakati Serikali inaendelea kuliandaa, nawaomba mliandae na miundombinu yake. Jiji la Kwala lipo pembezoni kidogo mwa barabara kubwa ya Dar es Salaam, lakini limepitiwa kabisa na reli zetu mbili; ipo reli ya *SGR* na ipo reli yetu ile ya zamani. Kwa hiyo, naomba sana, tutengeneze barabara kama ambavyo tumeanza kutengeneza barabara ya lami kutoka Vigwaza kwenda Kwala, zipo barabara kama ya kutoka Kwala kwenda Ruvu, ni muhimu ikashughulikiwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo barabara ya kutoka Kwala kwenda Gumba kutokea Chalinze, ni muhimu ikashughulikiwa kwa wakati. Ipo barabara ya kutoka Kwala – Kimara Misale inakwenda Morogoro Vijijini. Hii ni muhimu ikashughulikiwa kwa wakati. Barabara hizi zikifunguka tafsiri ya kuitengeneza Jiji la Kwala linakwenda kuwa la kishindo kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, yapo maombi maalumu ambayo nayawasilisha hapa kwa ajili ya kuomba utekelezaji wake. Kwanza, kuna hii tafsiri tunaizungumza wengi, kwa sababu zile barabara hazikamiliki. Kwanza nampongeza Kiongozi wa *TARURA* ndugu yetu Seff kama ambavyo amepongezwa na wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakataa kwamba siyo kweli kwamba *TARURA* ina bajeti ndogo sana. Nitatoa mfano mdogo

sana. Kwa mwaka Mkoa wa Pwani, *TARURA* inapokea shilingi bilioni 32, hebu zidisha shilingi bilioni 32 mara idadi ya mikoa ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nina ushauri kidogo. Tunaziona fedha hizi ndogo kwa sababu ya namna tunavyozitumia. Kila mwaka mkoa unatumia shilingi bilioni 32 kufanya ukarabati kwenye barabara ambazo ikinyesha mvua moja ya masika, hujui kama umeifanyia ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, tungeweza kutengeneza utaratibu, na kupanga ni kuchagua. Leo hii sisi *SGR* imefika Dodoma, tunafurahia kipande ambacho tunakitumia na watu walioko Katavi na walioko Mwanza wanaifurahia na wanaisubiri ifike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *TARURA* tungekuwa na utaratibu kwa mfano, fedha zinazokwenda kwenye mkoa, tukatafakari katika fedha zile zisigawanywe katika mazingira ya kidogo kidogo, tuamue tunashambulia barabara ngapi za kimkakati kwa mkoa. Kama ni barabara mbili za Mkuranga, kama moja ya Kibaha Vijijini, lakini ni barabara ya kimkakati, tukiimaliza japo kwa lami nyepesi, maana yake miaka 10, miaka 15 tutakuwa haturudi hapa, tutakuwa tunakwenda kufanya kazi kwenye barabara nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivi, kwa mfano kwa hii shilingi bilioni 32 ya Mkoa wa Pwani, mimi na wewe na ndugu yangu yupo pale pembeni Bwana wa Kibiti, ninaamini kabisa tukikubaliana wenyewe kwenye mkoa wetu, tukazielekeza shilingi bilioni 32 za mwaka mmojawapo, tukashambulie kwangu mimi kwa mfano, halafu tukaja kwako ninaamini kabisa baada ya miaka mitano hizi kilometa zinazotajwa za mkoa, kilometa 5,172 zitakuwa zime… *(Makofi/Kicheko)*

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. MICHAEL C. MWAKAMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tulia kaka, muda umekwisha, naunga mkono hoja. Ahsanteni kwa kinisikiliza. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. MICHAEL C. MWAKAMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante kwa kunisikiliza.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba ajiandae.

MHE. NICHOLAUS G. NGASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, nami kupata nafasi ya kuchangia jioni Bajeti yetu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii ambayo nimeipata jioni hii kuongea katika Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango yangu itakuwa itakuwa imejikita na sehemu tatu. Sehemu ya kwanza nitakuwa nikieleza mafanikio, upande wa pili nitakuwa nikieleza changamoto lakini pia upande wa tatu nitakuwa ninatoa ushauri nini kifanyike ili tuweze kusonga mbele; na ndiyo faida ya kuwa na Wabunge vijana ambao bado akili zinachemka vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo letu la Igunga tulipata bahati, kati ya mwaka 2021 mpaka 2025 tulipata ziara ya viongozi wakuu watatu wa nchi hii. Tarehe 17 Mwezi wa Kumi, 2023 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya ziara kwenye jimbo letu. Mheshimiwa Rais alikuta umati mkubwa sana wa watu,

walimpokea kuanzia saa mbili asubuhi mpaka saa kumi na mbili jioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye uwanja tulioutumia unaitwa Uwanja wa Barafu, historia inaonesha kwa mara ya mwisho ule uwanja ulijaa mwaka 1993 mimi nikiwa Darasa la Kwanza, kipindi hicho walikuja Wazungu kuonesha sinema zile. Waliweka pale sinema, tulijaa sana pale kipindi kile wakati wanatoa elimu ya mambo mbalimbali ya afya ya jamii. Uwanja ule ndiyo ulijaa kwa mara ya mwisho na ukajaa kuvunjwa rekodi alipokuja Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi walijitokeza kwa wingi ikiwa ni shukurani kwa Mheshimiwa Rais kwa miradi mikubwa ya maendeleo ambayo ametufanyia takribani shilingi bilioni 100 zimeingia kwenye Jimbo letu la Igunga. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tarehe 8 Oktoba, 2024 Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Makamu wa Rais pia alipita Igunga; na tarehe 12 Machi, mwaka huu 2025 Mheshimiwa Waziri Mkuu alipita. Tunawashukuru sana viongozi wetu hawa wakuu kwa kutenga muda wao kufika katika Jimbo letu na Wilaya yetu ya Igunga ambapo waliweza kujionea kwa uhakika na kwa uhalisia yale ambayo tumekuwa tukiyasema kila mwaka wameyafanya makubwa katika kipindi hiki cha miaka mitano. Tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hoja yangu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, nina mambo kama manne au matano nitachangia. Jambo la kwanza ni sekta ya elimu, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mchengerwa pamoja na Manaibu wake, Makatibu Wakuu pamoja na Watumishi wote wa Wizara, wamekuwa wakifanya kazi vizuri sana usiku na mchana. Unapoongelea TAMISEMI, nadhani shughuli takribani 80% za menejimenti ya Serikali zipo chini ya mikono yao. Wamekuwa mkipambana sana usiku na mchana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa hongera sana Kaka yangu Mheshimiwa Mchengerwa, hongera dada yangu Mheshimiwa Zainab, Kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Dugange na wasaidizi wako wote mmetutendea haki. Kwa kweli siku hizi vijana wanasema, hamna baya. Nasi tunasema hamna baya kwa kweli, mlikuwa mnafikika muda wote. Pia, tunawatakia heri katika majukumu yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya elimu tumefanya makubwa sana, elimu msingi na elimu sekondari. Hakuna Jimbo nchi hii ambalo halijajengewa madarasa, hakuna Jimbo nchi hii ambalo halijajengewa maabara, hakuna Jimbo nchi hii ambalo halijajengewa shule shikizi, miundombinu ya kila aina kwenye elimu, elimu bila malipo, uendelezaji wa walimu, ajira za walimu lakini pia na uboreshaji wa miundombinu mbalimbali ya elimu, kujenga vyoo na kila kitu. Wamefanya makubwa sana katika sekta ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa ushauri, changamoto ambayo imebaki pamoja na kwamba tumejenga madarasa mengi, kuna changamoto kubwa ya ujenzi wa nyumba za walimu, vyoo vya wanafunzi na vyoo vya waalimu. Sasa hii changamoto mbele nafikiri Mheshimiwa Mchengerwa mnaweza mkaumiza vichwa. Mimi ninawapa ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mashirika ya ujenzi ambayo yapo chini ya majeshi yetu, tuna *Police Cooperate Society,* tuna SHIMA lipo chini ya Magereza lakini tuna *SUMA JKT*. Tengenezeni *model* mwingie nao mikataba hawa watu waweze kujenga nyumba za walimu nchini au vyoo, tuachane na tatizo la vyoo kwenye shule zetu nchini na nchi nzima kwa ujumla. Mnaweza mkawapa mkataba wa muda mrefu hata wa miaka mitatu kwa sababu ni mashirika yaliyo chini ya Serikali yetu, mtakuwa mnaenda mnalipana taratibu kutokana na makusanyo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuachane na habari ya kuja huku tunasema tunaomba vyoo au tunafika kule kwenye ziara za viongozi tunaanza kusema hakuna vyoo. Haya mashirika ni ya

wazalendo, na yapo chini ya majeshi yetu. Mnaweza mkaingia mkataba mkubwa hata kama ni wa miaka mitano, lakini mna-*assurance* kwamba mtakuwa mnawalipa kidogo kidogo kutokana na makusanyo ya nchi. Itakuwa ni mfumo mwingine wa *Force Account* ambao uta-*deliver* kwa uhakika katika nchi nzima kwa wakati mmoja. Hilo ni jambo moja kwenye sekta ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kwenye suala la barabara za mijini na vijijini. Nawapongeza kiukweli TAMISEMI, mmesimamia vizuri sana *TARURA*. Moja ya eneo kubwa ambalo Mheshimiwa Rais hata alipokuja Igunga nilimwambia na kumshukuru, alipofanya uamuzi wa kuamua fedha za barabara kila jimbo lipatiwe na liamue linaenda kutengeneza barabara za aina gani, Mheshimiwa Rais alifanya uamuzi mkubwa sana na hili jambo limetusaidia kwa kiwango kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejenga madaraja mengi kwenye mito ya msimu na mito ya wakati wote na tumetengeneza barabara za lami. Kwa mfano, sisi pale Igunga kwa sasa tuna mtandao wa barabara za lami pale mjini takribani kilometa 20 wakati zamani lami ilikuwa historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mtandao wa barabara za mataa. Barabara za vijijini tumetengeneza za changarawe na kila eneo tumegusa. Kuna madaraja ya kwenye mito yalikuwa yameshindikana kwa muda mrefu, lakini tumeweza kuyatengeneza kutokana na huu uamuzi makini wa Mheshimiwa Rais wetu wa kuhakikisha kwamba tunapatiwa fedha kwenye jimbo, tunakaa na wataalamu na tunaamua nini cha kufanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ambayo nimeiona bado ipo kwenye huu utaratibu ambayo nadhani Mheshimiwa Waziri anaweza akaumiza vichwa na wataalamu wake wakalitafutia ufumbuzi, ni michakato ya kupata wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba kuna utaratibu wa Sheria ya Manunuzi, lakini kwa upande wa *TARURA* imekuwa ni ya muda mrefu sana. Wamekuwa na changamoto,

wakipata wakandarasi baadaye wanarudi wanasema mkandarasi hakukidhi vigezo. Tumejikuta jambo dogo linatumia muda mrefu sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri na wataalamu wake kwenye hili waumize vichwa ili kutatua hili tatizo kwa sababu linatukwamisha kwa muda mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza kutoa mfano, Mheshimiwa Rais alipotoa zile fedha za dharura kutengeneza zile barabara, zilichukua muda mrefu sana mpaka zikaanza kuleta kelele humu Bungeni mwaka 2024, lakini ni kutokana na huu mfumo wa upatikanaji wa wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalieni hili mlitatue ili tuweze kutatua changamoto. Barabara inapokatika, tunahakikisha ndani ya miezi miwili au mitatu tunakuwa tumeweza kuimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nashauri, mnaweza mkatengeneza mwongozo na *component* ambayo baadaye mnaweza mkaiweka kwenye *regulations.* Tunapopeleka fedha za barabara, kuwe na *percentage* fulani, kwenye kila shilingi tunaweza tukakubaliana 10% au 30% ibaki kwa ajili ya *maintenance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia sana inaponyesha mvua kwa dharura, kwa sababu tunaelewa mvua za nchi hii nyingi ni za ukanda, na ni za muda mfupi. Inaponyesha mvua ya dharura, ikitokea changamoto kwenye barabara tusisubiri tena *financial year* inayofuata ndiyo waje watatue tatizo la ile barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajikuta tumengeneza barabara kilometa 20, imekatika kipande cha mita 100 na barabara inaacha kupitika mwaka mzima. Mheshimiwa Waziri, hii inakuwa haina *value for money,* hivyo mtengeneze mwongozo ambao utakuja kutusaidia, zinapotokea changamoto tunazimaliza kwa wakati na haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine unakuta linatokea tu eneo korofi dogo, lakini *TARURA* Wilaya, *TARURA* Mkoa hawana

fedha ya kutengeneza maeneo korofi. Sasa mkiweka, kutakuwa na kile kikapu pembeni cha fedha ya uhakika. Kama barabara imetoboka au imetoka shimo, itakuwa siyo mpaka kusubiri *financial year* inayofuata ili iweze kutengenezwa. Hilo ni kwa upande wa eneo la barabara vijijini na mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kwenye ujenzi wa masoko ya kimkakati. Ukiangalia katika maeneo mengi sana kumekuwa na utaratibu wa kujenga haya masoko ya kimkakati. Sasa mimi ninashauri kitu kimoja. Jambo la kwanza, ili nyie TAMISEMI muweze kushusha huu mzigo, toeni maelekezo kwa halmashauri inayohitaji kujenga soko la kimkakati, itafute eneo liwe katikati ya mji kabisa. Tuachane na ile biashara ya kujenga soko la kimkakati kilometa 15 kutoka mjini, mkijidanganya kwamba tunavuta mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kuvuta mji, mtajenga soko na litakosa biashara. Watafute eneo katikati ya mji na mwaambie waanzishe kama tulivyokuwa tunajenga maboma halafu wakifika kwenye lenta nyie TAMISEMI ndiyo muingie kumalizia. Tutajenga masoko yote na yatakuwa na ufanisi kabisa. Tutaachana na kujenga masoko nje ya mji, yanachosha wananchi. Matokeo yake wananchi wanaenda kwenye magenge na mmejenga soko la bilioni limekaa halina kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waambie kama ni halmashauri itafute kiwanja katikati ya mji hata kama ni cha kununua kwa kulipa fidia. Maana yake katikati ya mji litakuwa na tija na kila mtu atakwenda. Hilo ni upande wa masoko ya kimkakati. Mheshimiwa Waziri, Mawazo yangu ni hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu Sekta ya Afya. Nawapongeza sana kwenye Sekta ya Afya. Tumejenga vituo vya afya vingi, zahanati nyingi, tumetoa *ambulance*, vifaatiba, na tumejenga mpaka hospitali zenye *ICU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi lgunga zamani tulikuwa tunakwenda Bugando Mwanza. Sasa hivi tuna *ICU* ya maana kabisa na ya kisasa inayoweza kuhudumia wagonjwa 10 mahututi

kwa wakati mmoja hata kama wamepata ajali. Tuna wodi za mama na mtoto za kila aina. Sisi tuna wodi ya mama na mtoto inayoweza kuhudumia akinamama 55 kwa wakati mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu. Ameweka *commitment* kubwa kwenye Sekta ya Afya. Unapoongelea ustawi wa nchi, maana yake unaanza na afya ndiyo inafuata elimu. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa changamoto ambayo bado ninaiona kwenye Sekta ya Afya ni ndogo sana. Kwenye Sekta ya Afya changamoto ni *customer care* tu. Wale wahudumu wa afya bado maneno yao siyo mazuri kwa Watanzania na kwa wananchi hususan kwa akinamama wanaojifungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa ni suala tu la uwajibikaji na wasimamizi wanaowasimamia. Muwape miongozo na uwajibikaji uwe wa kiwango cha juu ili tuweze kupunguza. Wananchi wanapokuwa *harassed*, wanatukanwa na wanapewa maneno mazito mazito wanajikuta wanawachukia viongozi kwa sababu ya chuki na hasira za mtu mmoja ambaye unakuta amegombana na mume wake, lakini anaenda kutukana akinamama wanaojifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tano ni suala la mafunzo ya watumishi wa halmashauri. Hili linahusiana kidogo pia na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, lakini kwa kuwa asilimia kubwa ya watumishi ni wa kwenu, jitahidini sana kuweka mkazo katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifanya tathmini, watumishi wa umma wengi wanaosoma na kujiendeleza sasa hivi, wengi wanajisomesha kwa gharama zao wenyewe na wanajiendeleza kwa gharama zao wenyewe. Sasa Mheshimiwa Waziri mliangalie hili. Kama pale Wizarani mna kitengo au mna dawati linalohusiana na masuala ya mafunzo, basi muwape kipaumbele sana watumishi hususan kada za chini na kada za kati. Wasiwe

wanasubiri mpaka Tume ya Uchaguzi wanakuja na shughuli zao, ndiyo wanarudi mjini wanafundishwa wanaondoka. Mwawekee elimu ambazo zinaendana na ujuzi, taaluma na kazi wanazozifanya ili kuweza kujenga *capacity* za watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa umuhimu mkubwa natoa shukurani na pongezi kwa Mheshimiwa Spika wetu Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson; Naibu Spika, Mheshimiwa Zungu; Wenyeviti na watumishi wa Bunge kwa ushirikiano mkubwa ambao wamekuwa wakitupatia katika kipindi chote hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapoongea neno 'Bunge', inakuja picha ya Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson ambaye ni Spika mpenda haki sana. Mara nyingi unaposema neno 'haki' ukiwa katika viwanja hivi, basi unaona picha ya Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Spika alikuwa muungwana sana hususan kwa sisi Wabunge ambao ni vijana tunaokua, ametuvumilia lakini ametulea na amekuwa mlezi mwema.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. NICHOLAUS G. NGASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa. Nilimtaja Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma ajiandae.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie katika bajeti hii muhimu ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia, napenda kuanza kwa kunukuu kauli ya Mheshimiwa Waziri aliyeitoa kwenye ukurasa wa 138 wa hotuba yake akisema, "Naomba tusimame pamoja, siyo tu kama viongozi wa leo, bali

kama warithi wa kesho tunaojenga Tanzania mpya kwa misingi ya uwajibikaji, ushirikishwaji na maendeleo yanayogusa maisha ya kila Mtanzania kuanzia mijini hadi vijijini." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri tangu mwanzo mpaka mwisho unaona kabisa dhamira ya dhati ya Wizara ya TAMISEMI kutaka kuunganisha Taifa, kuwatumikia Watanzania na kuhakikisha kwamba katika kuliunganisha Taifa, kila mtu atashiriki katika zoezi hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitayaunganisha hayo maneno yangu na mifano michache ambayo nimeiona katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Ninaanza na namna ambavyo Wizara hii imeanzisha mfuko maalum kwa ajili ya kuwasaidia fedha za mitaji wakandarasi wazawa wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko huu uliopewa jina la Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan, unaitwa Mfuko wa *Samia Infrastructure Bond*. Mfuko huu walitegemea kuuza hisa zenye thamani ya shilingi bilioni 150. Hisa hizi zimenunuliwa na Watanzania. Mwitikio mkubwa waliouonesha Wananchi wa Kitanzania wa kawaida sana, lengo lilikuwa ni shilingi bilioni 150, lakini mpaka tunavyozungumza hivi leo, tumekusanya zaidi ya shilingi bilioni 300 katika *Samia Infrastructure Bond*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki wa wananchi katika kununua hisa za Mfuko wa *Samia Infrastructure Bond* unaonesha ushirikishwaji wa Watanzania wa kawaida katika kuchangia kwenye maendeleo ya nchi na ndiyo maana nilianza na ile *quotation*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili limekuwa na kelele nyingi sana zikihusisha na namna ambavyo wakandarasi wazawa wamekuwa wanarudi nyuma kwa kukosa mitaji, wanarudi nyuma kwa kutokulipwa kwa wakati na wanarudi nyuma kwa kukosa uwezo au kutokujengewa uwezo wa kifedha ambao utawafanya watekeleze majukumu yao katika miradi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya TAMISEMI ambayo kimsingi mimi ninahudumu kama Mjumbe wa Kamati, jambo hili lilikuwa linatuumiza vichwa sana, lakini leo wakandarasi wetu wazawa watapata fursa ya kupata mitaji, tena ambayo haina ukiritimba, kwa sababu wataweza kuomba mitaji hii kupitia mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani mkandarasi ataomba *then* fomu ile itakwenda moja kwa moja *TARURA* kupitia mtandao. *TARURA* watathibitisha, itatoka pale itakwenda moja kwa moja kwenye Benki ya *CRDB* na Benki ya *CRDB* baada ya ku-*assess* watampatia mkandarasi mtaji bila ya kuwa na haja ya kuonana naye uso kwa uso. Jambo hili siyo la kubeza. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Wizara ya TAMISEMI kwa kazi nzuri waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kujua dhamira ya dhati ya mtu, utaiona kwenye matendo yake. Katika kipindi hiki kifupi ambacho nimehudumu katika Kamati ya TAMISEMI, tumekagua shule za sekondari za wasichana za sayansi nchi nzima zenye thamani ya kuanzia shilingi bilioni nne mpaka shilingi bilioni tano na kitu ambazo kimsingi Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan amejitoa kwa hali na mali kuhakikisha watoto wa kike wanaweza kushiriki na kusoma masomo ya sayansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama mwanamke kusema ukweli, niseme kazi kubwa imefanyika. Hivi tunavyozungumza leo, watoto wetu wa kike wako shuleni katika shule ambazo ni za kisasa zenye mabweni, mabwalo, maabara na maktaba za kisasa wanasoma masomo ya sayansi. Shule hizi zinafanya kazi sasa hivi nchi nzima. Hili ni jambo la kupongeza na ninasema ukweli, iko haja ya Waheshimiwa Wabunge wote hapa kupata fursa ya kuzishuhudia shule hizi ili tuweze kujua kazi kubwa iliyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Manispaa yangu ya Shinyanga kuna shule inaitwa Rajani Sekondari. Ile shule iko jirani sana na ninapoishi mimi. Ile shule ilikuwa ina changamoto kubwa sana ya miundombinu. Kilio kikubwa cha Mheshimiwa Mbunge

wa jimbo ilikuwa ni kupandisha hadhi ile shule. Leo tunavyozungumza, mabweni yameshajengwa, miundombinu ya madarasa imeshajengwa, wanamalizia kuweka maabara na shule ile wanaipandisha hadhi iende kuwa shule ya Kidato cha Tano na Sita. Haya ni mambo makubwa ambayo hatuwezi kuyabeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali hasa kwenye Sekta ya Elimu, kwanza shule hizi za sayansi zipelekewe vifaa vya kisasa vya maabara badala ya kutegemea kununua vifaa hivi kwa kutumia fedha za ndani za halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu moja tu, tayari wanafunzi wako shuleni, lakini vifaa vilivyopelekwa havitoshi na watoto hawa wamekaribia kuanza kufanya mitihani na ni lazima wafanye mitihani ya *practical*. Naishauri Serikali wapeleke vifaa vya maabara kwa haraka ili watoto waweze kufanya mafunzo kwa vitendo tayari kwa kujiandaa na mitihani yao ya kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu, umuhimu wa kupeleka vifaa vya maabara kwa haraka, hizi shule zote ni mpya na mwisho wa siku unavyoanza ndivyo watu watakavyokuchukulia. Shule hizi zisipokuwa na ufaulu mzuri, zitashusha lile lengo kuu la Serikali la kutaka kuzifanya shule hizi ziwe *special* na la kutaka kufanya shule hizi zionekane ni za mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kuishauri Serikali ihakikishe inapeleka vifaa vya maabara vya kutosha ili watoto wafanye *experiment* ili *wale best students* ambao tumewachagua katika maeneo yale waweze kuonesha uwezo wao katika mitihani yao ya Kidato cha Tano, Kidato cha Sita na Kidato cha Nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri, katika eneo la mikopo ya 10%, mwaka 2024 wakati Mheshimiwa Waziri anawasilisha bajeti yake, hapa alitupa ahadi nzuri sana kwamba sasa wanakwenda kutoa mikopo ya 10% na akatuahidi kwamba kuna baadhi ya maeneo watatoa mikopo hiyo kwa kutumia benki

na maeneo mengine watatoa mikopo hiyo kwa kutumia halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hili linasuasua sana na mpaka sasa tunavyozungumza huu ni mwaka wa mwisho katika Bunge hili la Kumi na Mbili. Nadhani kama kuna jambo kubwa ambalo Wizara ya TAMISEMI inaweza kulifanya na kuacha alama baada ya bajeti hii ya mwisho, ni kuhakikisha vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wanapata mikopo ya 10%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ni nyingi sana. Takribani shilingi bilioni 123 ziko kwenye akaunti zimezuiliwa, zinasubiri wanawake, vijana na watu wenye ulemavu waweze kufaidika. Nadhani ipo haja ya TAMISEMI kuchukua hatua madhubuti ya haraka. Nimeona katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri anasema tunakwenda kuanza kutoa mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumebakiza mwezi mmoja hapa, utasikia mara mifumo haifunguki, mara sijui *NeST* imefanyaje. Hebu waharakishe hili zoezi la kutoa mikopo ya 10% ili tuweze kuyasaidia haya makundi maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, nataka nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wangu wa Shinyanga. Pale Shinyanga, Manispaa ya Shinyanga Mjini ndiyo imeongoza kwa usafi, na kitaifa imekuwa ya pili kwa usafi. Sasa hili halitokei hivi hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo adha kubwa sana ya miundombinu. Juzi nilimwona Mheshimiwa *DC* Mboni kule Kahama anahangaika kukagua miundombinu ya barabara baada ya kukuta barabara nyingi zimeharibiwa na mvua. Hebu fikiria kwa 11% ya bajeti ambayo *TARURA* wamepelekewa, wamefanya kazi kubwa na leo humu ndani kila mtu anampongeza *Engineer* Seff. Je, wangepelekewa kwa asilimia ambazo zinatakiwa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, ipeleke fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya barabara katika maeneo yetu kwa sababu hali siyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho, siyo kwa umuhimu, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Spika Dkt. Tulia Ackson. Daktari huyu siyo tu kwamba ni Daktari wa Sheria, maana ni mwalimu wangu, nina-*declare*. Siyo tu Daktari wa Sheria, lakini ameweza kumudu kuwa Daktari wa Siasa Kitaifa na Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ambao tunajifunza kutoka kwake, tuna mengi ya kuendelea kujifunza. Niseme ukweli, mwanzoni tulikuwa tunamwona kama mkali hivi, lakini sasa hivi tunaiona tija. Kwa sisi ambao tunawakilisha Bunge ndani na nje ya nchi, tunaonekana namna ambavyo tumenyooka kwenye namna tunavyojenga hoja na tumenyooka kwenye namna ambavyo tunaweza kutetea Taifa letu Kitaifa na Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kazi kubwa aliyoifanya, mimi ninamwombea sana aendelee kuwa Spika wetu hata katika Bunge la 13. Mwenyezi Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba. Kabla sijaendelea na mchangiaji mwingine, naomba niwatangaze wageni ambao wapo Bungeni muda huu.

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Kuna wageni 12 wa Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ambao ni Wakurugenzi wa Halmashauri. Karibuni sana wageni wetu ambao ni Wakurugenzi wa Halmashauri. *(Makofi)*

Pia, tuna wageni 30 wa Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga ambao ni Wajasiriamali wa Kisabato kutoka Magu Mkoani Mwanza. Karibuni sana wageni wetu kutoka huko Magu Mkoani Mwanza. *(Makofi)*

Pia, tuna mgeni wa Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mbunge, ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Wauguzi kutoka Mkoa wa Mwanza, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Ni wageni 80 kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo kutoka Jijini Dodoma. Wanafunzi wetu kutoka Hombolo, karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mchangiaji ambaye nilimtaja, Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, na Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga wajiandae.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba iliyoko mbele yetu. Awali ya yote, napenda sana kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Ukarimu anayejalia neema ndogo ndogo na kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kwa pongezi kwa Mheshimiwa Rais wetu Mama yetu kipenzi Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya katika Taifa lake la Tanzania. Mheshimiwa Rais amekuwa hatulii usiku na mchana ndani na nje ya Tanzania kwa ajili ya kuwatafutia neema wananchi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kukubali ama kuuteua Mkoa wetu wa Pwani unaoongozwa na Mkuu wa Mkoa wetu, Alhaji Musa Kunenge kupewa heshima kubwa ya kuwa mwenyeji wa uzinduzi wa Mbio za Mwenge Kitaifa ambapo tumezindua tarehe 02 Aprili, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwani kupitia Mwenge wa Uhuru tumeukimbiza, tumemulika na tumekagua miradi yenye takribani thamani ya shilingi bilioni 45. Hivyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Mwenge unasimama

kwa niaba yake na Mwenge ule umemulika na kukagua miradi yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pasi na shaka, mwaka huu Mkoa wa Pwani tutaongoza, na katika hizi Mbio za Mwenge ndiyo tutashika namba moja kwani miradi mikubwa imetekelezwa na imetekelezwa kwa umahiri wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumpongeza Mbunge wangu wa Jimbo la Rufiji na Waziri wetu wa TAMISEMI, Kaka yangu Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, kule kwa Wandengereko wanamwita a.k.a. MMK katika maana ya Mchengerwa Mtu Kazi, nampongeza sana, amepatiwa kazi kubwa ya kumsaidia Mheshimiwa Rais, na anafanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu ya TAMISEMI ndiyo Wizara ambayo inashughulika na maendeleo ya watu katika miji, vijiji na vitongoji, lakini Mheshimiwa Mchengerwa amekuwa akifanya kazi ya kumsaidia Mheshimiwa Rais, lakini bado amekuwa yuko *bennet* na wananchi wake wa Rufiji. Napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wake kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba namshukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kuniteua na kuniweka kuwa Mjumbe wa Kamati ya *LAAC* kwa kipindi cha miaka miwili na nusu. Kupitia Ujumbe wangu wa Kamati hii ya *LAAC,* nimepata fursa na nafasi ya kutembea karibia nchi yote ya Tanzania. Nadhani nimetembea Halmashauri ama niseme mikoa yote, nilibakiza Mkoa wa Kigoma tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ziara za *LAAC* zimenipa nafasi ya kuwa shuhuda kujionea miradi mikubwa ya kimaendeleo ambayo imetekelezwa katika Halmashauri zetu, katika Wilaya zetu na katika Majimbo yetu. Nikisema nitolee mfano katika sekta ya elimu, sote ni mashuhuda, shule za wasichana zimejengwa ambazo zina thamani ya shilingi bilioni nne mpaka shilingi bilioni tano katika mikoa yote ya Tanzania. Kwa hiyo, tunaweza

tukafanya hesabu kwamba shilingi bilioni nne mpaka shilingi bilioni tano tukizidisha mara mikoa yote ya Tanzania tutaona ni kiasi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu shule za wasichana, Mheshimiwa Rais kwa kuwa ni mama, kwa kuwa ni mlezi, kwa kuwa ni mvumbua vipaji, ameona ipo haja na tija ya kuanza na zoezi la kujenga shule za wavulana. Shule saba tayari za wavulana zimejengwa kila moja yenye thamani ya shilingi bilioni 4.450.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, shule 29 za amali zenye thamani ya shilingi bilioni 1.6 na zenyewe zimejengwa. Kwa wale watakaoshindwa kwenda kwenye mfumo rasmi, basi waende kwenye huu mfumo wa amali. Mwisho wa siku Mheshimiwa Rais hajamwacha kijana yeyote wa Kitanzania pembeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine wa mambo makubwa yaliyofanywa na Rais wetu katika sekta hii ya elimu ni Shule za Kata. Shule mpya za Kata takribani 734, zenye thamani ya shilingi milioni 470 kila moja zimejengwa katika hili Taifa letu la Tanzania. Hivyo napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwani elimu ndiyo ufunguo wa maisha na elimu itatusaidia Taifa na vijana wa Tanzania kuondoka gizani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Mwenyezi Mungu amlipe sana Mheshimiwa Rais wetu. Kwa hiyo, kazi kubwa aliyoifanya kuwafanya watoto waondokane na ujinga, katika Dini yetu ya Kiislamu tumeambiwa *"Iqraibi-ismi rabbika allathee khalaq."* Katika maana ya kwamba, "Twende Tukasome kwa Jina la Mola." Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais anafanya kazi ambayo ameamrishwa na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija katika upande wa sekta ya afya, Mheshimiwa Rais wetu amefanya kazi kubwa na kazi nzuri, kwani hospitali, vituo vya afya na zahanati zimejengwa. Tunazo hospitali mpya takribani 129 katika halmashauri zetu 129. Kwa hiyo, hili ni jambo la kumshukuru sana Mheshimiwa Rais. Pia kama

hiyo haitoshi, tunazo hospitali kongwe 48 ambazo zimefanyiwa ukarabati pamoja na vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Rais amegundua kwamba afya ndiyo msingi wa Taifa la Watanzania na afya ndiyo msingi wa maisha ya mwanadamu, ndiyo maana kwa makusudi ameamua kuwekeza katika hii sekta ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda katika Mkoa wangu wa Pwani, katika Mkoa wetu wa Pwani ni Mkoa wa kielelezo, Mkoa ambao una mifano tosha ya mambo makubwa na mazuri yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu katika shule ya sayansi ya wasichana kule Wilayani Rufiji katika Kata ya Chemchem, tumepatiwa kiasi cha shilingi 4,800,000,000 kwa ajili ya kujenga shule nzuri, shule ya kisasa ili kuweza kuibua vipaji vya watoto wa kike ama vipaji vya wasichana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hii ama hakika tumeipa jina la heshima Bibi Titi Mohamed. Ni shule ambayo itakuja kutoa mabinti ambao ni Marais wa baadaye, Wenyeviti wa baadaye, Maspika wa baadaye na Mawaziri wa baadaye. Hivyo tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili pia nampongeza sana Mbunge wa Jimbo la Rufiji, kwani mbali na kwamba Mheshimiwa Rais ametupatia fedha, tumejenga shule nzuri ya kisasa. Yeye hakusita kuwawekea mfumo wa gesi ili waweze kupikiwa chakula katika majiko ya kisasa na katika bwalo ambalo ni zuri. Nafikiri katika sehemu zote tulizotembea hakuna bwalo zuri kama bwalo la kule Wilayani Rufiji, bwalo lile limejengwa vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ningependa kusemea ni mikopo ya 10%. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, hii mikopo ya 10% ilifika mahali ilisitishwa, kwa sababu ya baadhi ya watumishi kutokuwa na nia njema na baadhi ya vikundi hewa ambavyo vililetea Taifa hasara. Mheshimiwa Rais alisitisha kwa nia

ya kwamba vichakatwe upya, viangaliwe upya ili irejeshe mikopo ambayo ina tija na afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii mikopo iliyorudishwa ya mfumo wezeshi, naipongeza sana Wizara ya TAMISEMI. Hii mikopo, kwanza imewekwa katika *category* tatu, mwisho wa siku hakuna mjasiriamali, awe mdogo, awe wa kati, ama mkubwa ashindwe kunufaika na hii mikopo. Nikitolea mfano wa Halmashauri yangu ya Wilaya ya Kibaha, mkopo mdogo wameweka kati ya shilingi 500,000 mpaka shilingi 10,000,000 ili vijana, wanawake na watu wenye ulemavu waweze kukopa. Kwa sasa mtu mwenye ulemavu ameruhusiwa kwenda kuchukua mkopo huu pekee yake, lakini kwa wale watu ambao wanaweza wakakopa mkopo wa kati ni kati ya shilingi 10,000,000 mpaka shilingi 50,000,000 na mkopo mkubwa ni kati ya shilingi 50,000,000 mpaka shilingi 150,000,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake ni kwamba vijana wa Kitanzania, wanawake, akina mama, akina mamalishe, pamoja na wauza mboga mboga, neema imefunguliwa na Rais Samia. Kwa hiyo, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri jambo hili kama kuna mambo madogo, madogo niliona katika halmashauri zetu kadhaa Mkoa wa Pwani walizindua hundi za kimfano kwa ajili ya kutoa hii mikopo kwa akina mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo lenye tija, ni jambo lenye afya, ambapo Wabunge wa Viti Maalum tunapata nafasi kubwa na nzuri ya kumsemea Rais wetu kwa namna alivyotenda kwa wanawake wenzie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kumpongeza Spika wetu Dkt. Tulia Ackson kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. Wabunge wa Viti Maalum tunamshukuru kwa vile vikao vya kila Alhamisi, alikuwa anatuita vikao vya kila Alhamisi kutuandaa maandalizi ya 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemwelewa Mheshimiwa Spika, tumemfahamu, tutafuata ushauri na Bunge lijalo tutarudi kwa

wingi, namba ya wanawake itaongezeka, vikao vya Alhamisi haviwezi kwenda hivi hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, licha ya kutuheshimisha wanawake wenziwe, Mheshimiwa Spika ameheshimisha Bara la Afrika. Hii ilijidhihirisha pale Mheshimiwa Spika alipowakatalia Wazungu kwa kuona bado tuko kwenye masuala ya ukoloni. Ni kwamba tumeshamalizana na ukoloni, Afrika ni huru, tunasonga mbele na tunachapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma. Nilimtaja Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, ajiandae.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia jioni hii ya leo. Naomba nimtangulize Mwenyezi Mungu katika mchango wangu. Naomba katika mchango wangu tumwombee Mheshimiwa Rais kwa Zaburi ya 25, ningeisoma lakini kwa sababu ya muda, basi naomba kila mtu akaisome. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Hassan kwa mambo makubwa sana ambayo ameyafanya katika nchi yetu. Ameiaminisha dunia kwamba wanawake tunaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nampongeza sana Mheshimiwa Spika wetu Dkt. Tulia Ackson ambaye ni Rais wa Mabunge ya Dunia. Kwa kweli, tunawashukuru sana, Tanzania imetambulika kwamba kuna wanawake jasiri, wanawake ambao wanaweza wakaongoza nchi, wanawake ambao wanaweza wakafanya mambo makubwa katika hii dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna usemi wa Wanyamwezi ambao unasema kwamba "mzigo mzito, mpe Mnyamwezi" lakini tunaubadilisha usemi huu kwamba mzigo mzito sasa hivi apewe

mwanamke, kwa sababu wanawake tunaweza na tumekuwa tukibeba mizigo mizito sana bila kuidondosha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nikipongeze Chama cha Mapinduzi kwa kumteua Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Mgombea wa Urais 2025, pamoja na Mgombea Mwenza Dkt. Emmanuel Nchimbi. Pia Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, nawapongeza sana. Tuna imani nao sana kwamba wataweze tena kuiongoza nchi yetu kwa kipindi kijacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niendelee kumpongeza Waziri wetu wa TAMISEMI Mheshimiwa Mchengerwa, nampongeza na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Dugange pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Zainab Katimba, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika hii Wizara ya TAMISEMI na kuhakikisha kwamba nchi yetu inakwenda vizuri katika miundombinu yote ya barabara, afya na elimu na mambo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nichukue pia nafasi hii kumpongeza Mkuu wangu wa Mkoa Mheshimiwa Peter Serukamba ambaye kwa kipindi kifupi ameweza kufanya kazi nzuri sana katika Mkoa wetu wa Iringa. Tunaamini kwamba tunamwombea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nampongeza Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi wa Mkoa, M-*NEC* wetu *ASAS* ambaye kwa kweli kwa kushirikiana na viongozi wetu wa Chama wamesimamia vizuri sana katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba nianze na uchangiaji wa barabara za *TARURA*. Niungane na wote waliompongeza *Engineer* Seff ambaye ni Mtendaji Mkuu wa *TARURA* kwa kazi nzuri sana ambayo amekuwa akiifanya, kwa kweli tunamwombea Mwenyezi Mungu aendelee kumweka na aendelee kufanya utumishi katika Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nipongeze uanzishwaji wa Hatifungani ambayo ni Samia *Bond*. Tunaamini kabisa *bond* hiyo sasa itasaidia malipo kwa Wakandarasi wetu nchini na barabara nyingi sasa zitaweza kupitika na uchumi sasa utaweza kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Iringa tumepokea fedha nyingi sana kwa ajili ya ujenzi wa barabara za *TARURA,* lakini sasa kutokana na mvua nyingi, barabara nyingi zimekuwa zinaharibika kwa kipindi kifupi tu na hazipitiki kabisa wakati wa mvua na kusababisha mazao kutofika kwa wakati katika masoko, lakini pia pembejeo kutofikishwa kwa wakati katika mashamba vilevile baadhi ya wagonjwa wengine kutofika kwa wakati katika vituo vya afya, pia gharama za usafiri zinakuwa kubwa sana kwa kipindi hicho, kwa sababu barabara nyingi sana zinakuwa mbovu na nyingine hazipitiki kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitaje tu baadhi ya barabara ambazo zinasumbua sana wakati wa mvua. Kuna barabara inayokwenda Idete – Itonya – Muhanga – Mgeta kilometa 18, barabara hii inaunganisha Mkoa wa Morogoro. Kuna barabara ile ya Ipalamwa – Naupwega – Kimara, ujenzi wake unasuasua. Tunaomba jitihada ili barabara ziweze kupitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna ile barabara ya Kidabaga – Magome – Ndengisivili – Kimara. Katika barabara hii kuna maeneo kama mawili yanasumbua, tunaomba Serikali iangalie ili barabara iweze kupitika kwa sababu wananchi wanapata shida sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ile barabara ya Lulindi – Ukwega – Boma la Ng'ombe, pia kuna barabara nyingine ya Masisiwe – Isanga, kuna barabara ya Kihesa Mgagao – Mwatasi, kuna barabara ya Ihimbo – Itimbo – Kising'a, na kuna barabara ya Mtandika – Ilula kilometa 22.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mtandika – Msosa kilometa 16, Barabara ya Ihimbo – Kitelewasi, barabara ya Mtandika – Nyanzwa, barabara ya Ilula – Image – Ibumu, hii

barabara ingepewa heshima kabisa ya *Engineer* Mfugale kwa sababu ni sehemu ambapo amejenga makazi yake pale, ingesaidia ikajengwa hata kwa lami, lakini sasa hivi haipitiki ni mbovu. Pia kuna barabara ya Mahenge – Ilindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu sasa tunaomba barabara hizi Serikali ingefanya upembuzi yakinifu, maeneo yale ambayo ni korofi, yaweze kujengwa ili hizi barabara ziweze kupitika wakati wote wa mwaka ili kutokuleta usumbufu ambao umekuwa ukijitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye sekta ya afya. Naomba niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa tuzo aliyoipata ya kupunguza vifo kwa akina mama nchini, kwa kuleta fedha nyingi sana katika ujenzi wa hospitali zetu za Wilaya, vituo vya afya na zahanati zilizosheheni kila kitu. Sera ya Serikali ni ujenzi wa vituo vya afya kila Kata, lakini naiomba Serikali kuleta fedha katika baadhi ya Kata ambazo hazina vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, naweza nikataja Kata chache za Wilaya ya Kilolo ambazo hazina vituo vya afya. Kata ya Ukumbi, Kata ya Ihimbo, Kata ya Udekwa, Kata ya Ibumu, Kata ya Image, Kata ya Idete, Kata ya Ilole, Kata ya Lugalo, Kata ya Ng'ang'ange, Kata ya Boma la Ng'ombe, Kata ya Masisiwe, Kata ya Kising'a, Kata ya Mlafu, Kata ya Wambingeto, na Mahenge. Hivi vituo havijajengwa pia barabara zake hazifikiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa wakati mwingine zinasababisha hata akina mama wajawazito kwenda katika vituo vya afya kwa shida sana. Hata pikipiki hazifiki, zinabebwa mgongoni kwa sababu hazipiti wakati wa mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaomba maboma ya vituo vya afya na zahanati ambazo zimejengwa kwa nguvu za wananchi, basi angalau Serikali ilete fedha ili kuweza kumalizia, pia nyumba za madaktari na watumishi. Watumishi bado hawatoshelezi katika vituo vya afya na zahanati na katika hospitali zetu za Wilaya. Tunaiomba Serikali izingatie hilo ili tuweze

kuboresha afya na kuondoa kabisa vifo vya akina mama na watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya elimu, naomba niwapongeze walimu wote nchini, bila kuwasahau walimu wetu waliopo katika Mkoa wetu wa Iringa, wamefanya kazi nzuri sana. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa ujenzi wa shule za watoto wa kike ambazo zipo 26 nchini ikiwepo katika Mkoa wetu wa Iringa ambayo imejengwa katika Wilaya ya Kilolo, Shule ya Lugalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nalipongeza Bunge letu kwa kujenga shule za shule za sekondari za watoto wa kike na wa kiume kwa kuleta ubunifu, nao pia wameweza kuongeza juhudi nawapongeza sana. Hata juzi tulikuwa kwenye *Marathon* ya Bunge kwa ajili ya ujenzi wa shule zetu za watoto wa kike na wa kiume. Hii tumetoa alama Wabunge, kwamba na sisi tunaweza tukajenga shule za watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto nyingi sana kwa shule zetu za msingi. Shule zetu za msingi nyingi ni kongwe sana, unakuta watoto wanasoma kwenye mazingira magumu. Mkoa wetu wa Iringa ni Mkoa wenye baridi sana, unakuta shule nyingi hazina madirisha, hazina milango, hazina *ceiling board*, hazina *floor*. Kwa hiyo, watoto wetu wanasoma kwenye mazingira magumu sana, ni nyingi hata kuzitaja siwezi. Sasa ningeiomba Serikali iangalie na itoe uzito shule hizi ziweze kukarabatiwa ili vijana wetu waweze kusoma katika mazingira mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba kuchukua nafasi hii kushukuru Chama changu cha Mapinduzi kupitia Jumuiya ya UWT inayoongozwa na Mheshimiwa Mary Chatanda. Pia katika Mkoa wangu, Zainab Mwamwindi ambao kwa kweli wamenilea, wamenifunza mpaka leo hii naweza kufanya kazi vizuri. Nawaomba wananchi wa Iringa, nikienda kuomba tena, kwa maana tunamaliza, tuna-*graduate,* nikienda tena waniamini kwamba ninaweza na sitawaangusha, nitafanya kazi kwa uaminifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati. Nilimtaja Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso ajiandae.

MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kukushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais ambaye kwa kweli ndiye mwenye hii Wizara, kwa namna ya pekee ambavyo anaendelea kutupatia fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi yetu. Mheshimiwa Rais anafanya kazi nzuri na kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Mheshimiwa Mchengerwa, tangu aingie kwenye hii Wizara, mabadiliko makubwa ya kiutendaji tumeyaona. Tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake, Naibu Mawaziri hao wawili wanamsaidia sana. Kuna mambo hatufiki kwake, yanamalizwa na Naibu Mawaziri wake, hasa mimi nikiwa nimekaa hapa wakipita wananiuliza Magu kuna tatizo gani? Naweka mambo yangu hapo. Tunampongeza yeye pamoja na Naibu Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza Katibu wake Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, nao wanamsaidia sana kwa kweli, kwa sababu wakati wote siyo lazima tufike kwake, tunaishia kwa Watendaji mambo yanakwenda vizuri. Katibu Mkuu, pamoja na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Mativila anayekusaidia kwenye miundombinu kwa kweli wakati wote ninamsumbua sana. Nimewahi kumpigia simu akasema, niko nje ya nchi, lakini akatoa maelekezo ya mipango ikaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunampongeza Ndugu Seff? Ni kwa sababu anajali Wabunge wote. Hakuna Mbunge ambaye ameenda kwa Ndugu Seff akashindwa kusaidiwa na hata kushauriwa kwa ajili ya barabara. Kwa hiyo, nilitaka nipongeze hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Magu tumepata stendi na soko, nami nawapongeza sana TAMISEMI pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, akiwemo Mheshimiwa Tax pamoja na Mheshimiwa Mary Masanja, haya yote tumeyasukuma kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa kweli, niombe sasa maelekezo, TAMISEMI itoe hili jambo la manunuzi kwa stendi ya Magu Mjini na soko lianze mara moja kwa sababu, umeshatoa idhini na maelekezo tu ya manunuzi ili stendi na soko la Magu yaweze kujengwa. Kwa kweli, wananchi watakuwa wamepata stendi ya muda mrefu, ni stendi ambayo kwa kweli imechakaa, ni stendi ambayo ina madimbwi. Kwa hiyo, kwa fedha ambazo mmetupa kwa bajeti hii tunayomalizia, zitakwenda kusaidia sana maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunacho Kituo cha Afya cha Lutale, ni kati ya vituo ambavyo mlituambia Waheshimiwa Wabunge tutafute vya mkakati, ni Kituo cha Lutale. Nashukuru kwamba, mmeshakubali kutoa fedha, naomba sasa na Waheshimiwa Wabunge wengine kwa sababu mmesema kwamba, fedha mmepata, pelekeni fedha, ili hivyo vituo vianze kujengwa na vianze kusaidia wananchi wetu. Tunayo imani na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ukiiongoza wewe Mheshimiwa Mchengerwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, mahitaji tunayo, ni mengi. Maboma ya zahanati zetu bado hayajakamilika, nayo tuombe kama kuna namna ya kupata fedha, kwa ajili ya maboma ndugu yangu Mheshimiwa Mchengerwa, hebu tupatie fedha Waheshimiwa Wabunge tukakamilishe maboma ambayo yameanzishwa na wananchi pamoja na halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa niwapongeze Waheshimiwa Madiwani wa Wilaya ya Magu wakiongozwa na Mwenyekiti, pamoja na Mkurugenzi na Wataalamu wake, kwa namna fedha za mapato ya ndani zinavyofanya kazi kwenye miradi ya maendeleo. Kwa namna ya pekee nawapongeza kwa sababu, fedha za miradi ya maendeleo wanazipeleka kama ambavyo

zimekusudiwa. Hebu sasa zile fedha shilingi milioni 50, 50 kila boma, nami nimeleta maboma 20 tu, yakipata shilingi bilioni moja tunamaliza, na wananchi wanapata huduma ya msingi huko. Kwa hiyo, naombe sana hili jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikiri kwamba, tangu Mwenyezi Mungu aumbe dunia, kuna maeneo yalikuwa hayajawahi kupata barabara na sasa hii kwenye Serikali ya Awamu ya Sita yamepata barabara. Kwa hiyo, tunapompongeza Mheshimiwa Rais, tunamaanisha, tunapokupongeza Mheshimiwa Mchengerwa na Waheshimiwa Manaibu wake, tunamaanisha, hata tunapowapongeza Makatibu Wakuu pamoja na Ndugu Seff, tunamaanisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Kabale – Jijimidi tangu Mungu aumbe ulimwengu, haijawahi kujengwa. Sasa barabara ipo, na wananchi wanaona. Barabara ya Nkumbulu – Kayenze B tangu Mungu aumbe ulimwengu haijawahi kutokea, sasa ipo na Barabara ya Mwamanga – Kisesa B, hasa pale Inolelwa ambapo kuna daraja, niombe fedha; wakandarasi wameshaleta *certificate,* wapewe ili waweze kumalizia hizo kazi ambazo wamebakiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, ni kazi kubwa imefanyika, lakini tunayo mahitaji. Barabara ya Kabila – Nobola – Kabale – Mahaha – Nyasato ni barabara muhimu sana. Mwaka 2024 mvua ilinyesha kubwa, tulikuwa tumeijenga barabara vizuri, imeharibika. Nimeomba fedha za dharura, sikupewa; nimeomba tena mara ya pili, sikupewa; niombe sasa Mheshimiwa Mchengerwa, kama kuna mabakimabaki hapa yaliyobaki, hebu mwambie Ndugu Seff sasa aweze kurekebisha huko maneno yaweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo Barabara ya Muhaha – Mwamnemba kwenda pale Itilima kwa rafiki yangu Mheshimiwa Njalu. Ni barabara ambayo inatuunganisha Wilaya ya Magu na Wilaya ya Itilima, nayo tumeiombea kwenye bajeti hii na kwa kweli, najua kwamba itapita iweze kujengwa ili angalau wananchi waweze kupata barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Mahaha kwenda Bariadi kunahitajika daraja tu pale, hatuhitaji fedha za barabara kwa sababu, barabara imejengwa kutokea Magu mpaka Mahaha, tunakosa daraja la kuunganisha kwenda Bariadi kule Tubhukilo. Hebu tupatieni fedha ya daraja ili tuweze kuunganisha Bariadi na wananchi waweze hasa kufungua uchumi wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikilia hapa kwamba, Mji wa Kisesa na Bujora ni miji mikubwa sana. Idadi ya wananchi kwa mujibu wa sensa ni takribani watu 63,000 ukiongeza ongezeko kwa sababu Mwanza na Ilemela yote inapumulia Kisesa na Bujora, hebu uangaliwe ule mji kwa fedha ambazo mnapata kutoka *World Bank*, *TACTIC* na mashirika mbalimbali yanayotoa fedha, tuuangalie ule miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, Ndugu Seff alifika pale akatuma wataalamu wake wa ku-*design* waka-*design* barabara zote akatuambia tuanze na zipi? Tumeshaleta, tunahitaji fedha, ili angalau hizo barabara, hata kama siyo lami, zijengwe kwa kiwango cha mitaro na *gravel*, ili ziweze kupitika wakati wote kwa sababu, maji yote yanayokusanywa kwenye nyumba za bati yanamwagika na kukata barabara, niombe sana jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Magu ina miji mingi. Ukienda pale Nyambuge, ni mji unakua, ukienda pale Lugeni mji unakua, ukienda pale Ilumbu ni mji unakua na Mji wa Magu wenyewe, Mji wa Kabila na Mji wa Mahaha. Hebu wataalamu muitazame hii miji, wananchi wanatutangulia sana, sisi tunabaki nyuma kwamba, tuangalie mji ulivyo sasa na baada ya miaka 10 ijayo hiyo miji itakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wananchi watakosa kabisa barabara kwa sababu, wanajenga holela na hakuna barabara, tunaomba hii miji itazamwe kwa namna. Tunapozungumza hapa, sisi tunaomba mtuelewe, tunajua TAMISEMI kazi kubwa imefanyika, lakini bado mahitaji ya Watanzania ni mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo Barabara ya Matela – Nyakasenge. Barabara hii inaunganisha kutoka kwenye lami, *trunk road,* kwenda *TANROADS*. Kwa hiyo, tungeomba hizi barabara kwa kweli, ikiwezekana zipandishwe hadhi, zina sifa, inatoka *trunk road* kwenda *TANROADS*. Maana yake ni kwamba, ina sifa zote za kwenda *TANROADS*. Kama siyo hivyo, basi mtutengee fedha kwa sababu, zinapitika na watu wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Barabara ya Kisesa kwenda Kayenze, nayo ni *trunk road,* inaungana na *TANROADS,* barabara ambayo inatoka *airport* kuja Nyanguge. Hebu nayo muone namna ambavyo mnaweza kutusaidia kwa kweli. Barabara hizi ni muhimu sana kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nishauri kwamba tunaweza kujipa muda, tunajua fedha hizi tunazopata ni kidogo, siyo nyingi sana, na mahitaji ya Watanzania ni makubwa, hebu tujipe muda kwamba, mwaka huu tunamaliza maeneo gani, hasa ambayo yanasaidia wananchi kiuchumi, ili kuhakikisha kwamba, tunawakomboa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipongeze sana kwenye elimu. Kwa kweli, kazi kubwa imefanyika, kila Mbunge hapa ni shahidi. Sasa kinachohitajika hapa, nami niseme tu kwamba, kule Magu sasa tumeshatoka kwenye sekondari za kata, tumekwenda kwenye sekondari za vijiji na sekondari nyingi wakati wowote tutazifungua. Sasa walimu ni wa muhimu sana. Ajira mmetoa, lakini bado upungufu wa walimu ni mkubwa. Naomba hilo pia lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya kazi kubwa kwenye afya, vituo vya afya tumejenga vingi na vifaatiba tumepeleka, lakini bado wataalamu wanahitajika. Serikali ya Awamu ya Sita imejitahidi kwa yote, imepeleka wataalamu, lakini bado wataalamu wanahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie sasa kwa kusema kwamba, kwa kweli, Mheshimiwa Rais hakukosea kuiunda vizuri Wizara hii ya TAMISEMI kuanzia kwa Mheshimiwa Waziri, wasaidizi

wake na watalaamu. Kule TAMISEMI kuna mtu anaitwa Ndugu Cheyo, mtaalamu mzuri wa mipango, hakuna asiyemjua, hakuna asiyemsikiliza. Kwa kweli, TAMISEMI ina watu waliobobea, watu makini, tuendelee kuwatumia, kwa ajili ya kutusaidia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niunge mkono hoja, japo nilikuwanayo mengi. Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa *Eng.* Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho, ajiandae.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii. Awali ya yote, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameifanya ya kuleta fedha nyingi ndani ya Halmashauri yetu ya Wilaya ya Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais, ndani ya kipindi cha miaka minne halmashauri yangu imepata fedha nyingi sana za maendeleo. Zaidi ya shilingi bilioni 400 zimepatikana kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, ni hatua nzuri sana ambazo zimefanyika kwenye maendeleo, kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, nawapongeza Waheshimiwa Manaibu Waziri wote wawili ambao wanafanya kazi ya kumsaidia Mheshimiwa Waziri kufanya shughuli za maendeleo ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali kwenye upande wa elimu. Kwenye sekta ya elimu tumepata fedha nyingi za maendeleo, ndani ya kipindi kifupi ambacho Mheshimiwa Rais amekuwa na dhamana tumepata fedha za kujenga shule nyingi za msingi, shule za sekondari, tuna zaidi ya shule mpya 33 zimejengwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, na vyumba vya madarasa zaidi ya 150 vimejengwa kwenye Wilaya hiyo ya Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na sekondari ambazo zimejengwa karibu kila kata, sasa tuna sekondari kinyume na ilivyokuwa huko nyuma, tumepata ujenzi wa Chuo cha *VETA* kwenye eneo la Wilaya ya Tanganyika, ambapo tulikuwa hatuna kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni maendeleo makubwa sana ambayo yamefanywa na Serikali ndani ya kipindi hiki ambacho Mheshimiwa Rais amepewa dhamana. Eneo hili tungependa kuishauri Serikali na kuomba msisitizo suala zima la kukamilisha maboma ambayo yameanzishwa na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi wamejitolea, tunayo maboma mengi ndani ya Wilaya ya Tanganyika ambayo yameanzishwa kwa ajili ya kujenga Shule za Msingi na kuongeza madarasa kwenye Shule za Sekondari. Naiomba Serikali kupitia kwako Mheshimiwa Waziri, uweze kufanya jitihada kwenye bajeti hii, uweze kuleta fedha kukamilisha hayo maboma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo Serikali imefanya kazi kubwa sana ni sekta ya afya. Kwenye afya tuna Hospitali ya Wilaya ya Tanganyika, hospitali nzuri sana, vifaatiba tumeanza kuvipata na tunavyo vituo vya afya. Kabla ya hapo, tulikuwa na vituo vya afya vitatu, lakini tunavyoongea, sasa hivi tulishakuwa na vituo vya afya 10. Kati ya hivyo, saba vinafanya kazi na vitatu vinahitaji kumaliziwa ili viweze kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hapo, wananchi wengi wamejitolea sana kujenga zahanati kwenye vijiji mbalimbali. Eneo hili tunaomba Serikali iweze kubeba yale maboma. Tumeanzisha ujenzi wa zahanati Kijiji cha Mgamsa, Kijiji cha Kisubangala, Kijiji cha Kabanga na vijiji vinginevyo ambavyo vimejenga zahanati bado kuna hatua ya mwisho ambayo inahitaji kusaidiwa na Serikali. Matumaini yangu ni kwenye bajeti hii yale maboma yote ambayo yapo kwenye eneo la sekta ya afya mtayafanyia kazi, ili wananchi waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeleta huduma ya vitendeakazi, hasa vifaatiba, kwenye vituo vya afya. Bado tuna tatizo kubwa sana la Watumishi wa Serikali Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika. Mfano tu ni kwamba, baada ya kuleta *X-Ray, Ultra Sound* na vifaa vingine vyote ambavyo vinahitajika hatuna mtaalamu, ambaye anaviendesha vile vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaweza tukafanya mazuri tukashindwa kutekeleza kwenye eneo ambalo linasimamia huduma ambayo kimsingi ndiyo inayohitajika. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, tunahitaji sana watumishi waje kwenye eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika kwa sababu, vile vifaa tunavyovipeleka vinaenda kulundikwa na havifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaye mtaalamu mmoja tu ambaye anashindwa kugawanyika aende kwenye vituo vyote hivyo vya afya akasimamie na afanye kazi kwenye hospitali ya Wilaya, kitu ambacho hakiwezekani kufanyika. Naombe eneo hili lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala zima la watumishi kuna wimbi ambalo lipo kwenye Ofisi ya TAMISEMI, watumishi mnaowaleta wakishafika kwenye vituo vyao vya kazi mnatoa vibali tena kuwarudisha kwenye maeneo mengine. Hili ni tatizo kubwa sana na tunaomba Mheshimiwa Waziri alisimamie kwa sababu, wale watumishi wanaowapelekwa kule ni sehemu ya kwenda kutoa huduma kwa Watanzania. Hivyo, tunasisitiza eneo hili lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kuzungumzia ni suala la *TARURA*. Kwanza nawapongeza sana wasimamizi wote ambao wamesimamia suala zima la kupeleka miundombinu kupitia *TARURA*. Nawapongeza sana Manaibu Katibu Wakuu, akiwemo ndugu yangu Matibila, kwa kazi kubwa sana ambayo ameifanya kusukuma miradi ya maendeleo, lakini bila kumsahau *Engineer* Seff, ambaye ametusaidia sana kwenye eneo hili la kupeleka miradi ya maendeleo, hasa ya miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Engineer* Seff alikuja Mkoa wa Katavi, amekuja kwenye eneo ambalo kulikuwa hakujafunguliwa barabara, alijionea na pale alitusaidia akatupa fedha za kujenga daraja, shilingi bilioni 1.5 na ile barabara kwa sasa kutoka Kambanga kuja Infisi, Infisi kwenda Bugwe imefunguliwa na inapitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo ambalo ni la faraja na tumeokoa maisha ya Watanzania walio wengi kwenye maeneo haya, lakini alienda kule ukanda wa ziwa, ameenda kuangalia daraja kwenye Kijiji cha Kapalamsenga kwenda Itunya, lile daraja nalo limekamilika. Sasa kazi kubwa ambayo inahitajika kufanywa, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, ipo ahadi ambayo iliahidiwa na Serikali ya kuunganisha Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Kigoma kupitia Wilaya ya Tanganyika na Wilaya ya Uvinza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya kutoka Kapanga kwenda Bujombe - Bujombe kwenda Kalya, hii barabara iliahidiwa kipindi kile na Mheshimiwa Waziri Ummy, yenye thamani ya shilingi bilioni 1.5. Naomba Mheshimiwa Waziri, ahadi ambayo ilitolewa na Serikali aifanyie kazi na ni kiungo muhimu sana kwenye barabara inayounganisha Wilaya ya Tanganyika na Wilaya ya Uvinza. Eneo hili ni muhimu na mawasiliano hayapo kwa sasa, ikifika masika wananchi hawafanyi kazi. Kwa hiyo, tunaomba maeneo haya yafanyiwe kazi na mtoe fedha, kwa ajili ya kukamilisha hii barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie kuwapongeza sana Serikali, hasa kwenye kufungua barabara. Barabara zimefunguliwa nyingi sana. Jimboni kwangu tunazo barabara nyingi, lakini tatizo lililopo kwa sasa ni wakandarasi waliofanya kazi hawajalipwa. Tunaomba Serikali iwalipe wale wakandarasi, mwatie moyo ili waweze kufanya kazi na kukamilisha ile miradi waliyoianzisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo jingine ambalo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaomba wakaangalie maeneo ya kufanya maboresho hasa kwa upande wa madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nawashukuru na kuwapongeza wote ambao wamefanya kazi nzuri, ahsanteni sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso. Nilimtaja Mheshimiwa *Engineer* Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, ajiandae.

MHE. ENG. DKT. LEONARD M. CHAMURIHO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniruhusu nami nichangie hoja hii muhimu ya Wizara yetu hii muhimu ambayo inashughulika na wananchi, hasa wa ngazi ya chini kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutuongoza vizuri hasa kwa falsafa zake za *4R* ambazo zinasababisha twende vizuri, kwa utulivu na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, napenda kumpongeza Rais wetu kwa kuhakikisha kwamba Wizara hii ambayo iko chini ya ofisi yake ina ufanisi mzuri; na vilevile kwa kuendelea kuitafutia rasilimali ya kuweza kuifanya Wizara hii ifanye kazi kama inavyotakiwa. Tunampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuiongoza Wizara kwa usimamizi wake mahiri, na kwa kuandaa bajeti nzuri ambayo inatia matumaini mazuri katika utekelezaji wa majukumu ya sekta hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ningependa kuwapongeza wasaidizi wa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange na Mheshimiwa Zainab Katimba kwa kazi nzuri wanayoifanya ya

kumsaidia Mheshimiwa Waziri, na vilevile Katibu Mkuu wa Wizara hii, Ndugu Adolf Ndunguru na Naibu Makatibu Wakuu wote na wataalam wote kwani tunaamini kabisa kwamba kazi hii nzuri iliyofanywa inawajumuisha hao wote katika utendaji kazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI ina majukumu mengi lakini mchango wangu wa leo utajikita kwenye usimamizi na uendelezaji wa miundombinu ya usafiri. Ningependa kutoa pongezi kwa Serikali kwa kuanzisha chombo mahsusi cha *TARURA* ambacho ndicho kinachosimamia miundombinu ya usafiri katika Wizara hiyo. Uamuzi huo umezaa matunda, hivyo pongezi hizo ni dhahiri inabidi zielekezwe huko. Chini ya uongozi wake Mhandisi Victor Seff kwa kweli TARURA imefanya kazi ya mfano wa kuigwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, napenda kusisitiza kwa Waziri kwamba chombo hiki ni budi tukiwezeshe ili kiweze kuendelea kutekeleza majukumu yake vizuri. Uendelevu wa matunda bora ya *TARURA* unahitaji vitu vitatu. Kwanza rasilimali ambayo ina watu na fedha; pili, ina ubunifu hasa huu wa teknolojia; na tatu, ningesema ni uzingatiaji wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kwenye rasilimali watu, mfano mzuri uko kwa kiongozi mwenyewe wa *TARURA,* Mhandisi Victor Seff ambaye ninamfahamu vizuri. Huyu amefanya uhandisi kuanzia Kidato cha Kwanza kule *Moshi Technical* akatoka pale akasoma *Dar Technical* kabla ya kujiunga na vyuo vikuu. Kwa hiyo, hakuna wasiwasi na umahiri na ujuzi alionao. Kwa hiyo, katika rasilimali watu, wamekaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile anayesimamia miundombinu ya ujenzi na usafiri, Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Rogatus Mativila, naye ni mhandisi mzuri ambaye anaaminika katika kazi hizo. Hivyo, tunaona kwamba kwenye upande wa rasilimali watu kinachotakiwa ni kuwaongezea watu wenye weledi ili mipango yao na utekelezaji viweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru na kumpongeza, kwa sababu nikiangalia katika ukurasa wa 164 wa hotuba yake

ametenga shilingi bilioni 7.97 kwa ajili ya ajira mpya. Basi katika hili tunamwomba asisitize kuzingatia kwamba hao watakaoingizwa pale wawe ni wale wenye weledi wa kuweza kumsaidia katika kutekeleza jukumu hilo la kutunza miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye jambo la pili la rasilimali fedha, kwanza ningependa kumpongeza kwa kuongeza fedha kwenye mtiririko wa Wizara yake katika eneo hili. Kwa kweli kazi za ujenzi, ukarabati na matengenezo ni kubwa sana. Ni kweli kwamba hata siku moja hii bajeti haitatosha. Hivyo, inabidi tuzingatie kwamba vyanzo vya mapato vinavyoelekeza bajeti hiyo vinaongezwa na pia vinalindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia randama ya Wizara hii ukurasa wa 15 kwenye maduhuli ambayo yanatokana na hifadhi za barabara, nimeona kwamba kufikia Februari mwaka huu ni asilimia 58.8 tu ndizo zimekusanywa, na sababu imetolewa pale, sababu ni kwamba tumeshusha ushuru wa kukodisha zile hifadhi za barabara kutoka dola 1,000 kwa kilometa hadi dola 200. Hiki kilikuwa chanzo muhimu. Tusipovilinda vyanzo hivi tunaweza kupata changamoto huko mbele za kupata fedha ya kuweza kuendesha miundombinu hii inayosimamiwa na *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ukiangalia katika mipango, jedwali la pili ukurasa wa 41 utaona tena kwamba chanzo hicho hicho mwanzoni kilikuwa kimepangiwa shilingi bilioni 5.6, lakini kwa mwaka huu kimepangiwa shilingi bilioni 7.0. Sasa unajiuliza kwamba ikiwa kile chanzo kule kimepungua, mbona matarajio ya makusanyo yameongezeka? Kwa hiyo, tunapata changamoto hapo kwamba tusipokuwa makini kuangalia vyanzo hivi tunaweza kupata shida katika kutekeleza majukumu yaliyopangwa kwa *TARURA*. Hivyo, vyanzo tuvilinde na tutafute vyanzo vipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupongeze na kutoa hongera kwa *Samia Infrastructure Bond* ambayo imekuja kwa ajili ya kusaidia wakandarasi ili waweze kupata mitaji mikubwa. Shida kubwa ya hawa wakandarasi siyo mitaji. Shida kubwa ni *cashflow,* kwamba wanapofanya kazi, wanatakiwa walipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii *Samia Infrastructure Bond* ukiiongeza ili vilevile ishughulikie na kulipa wakandarasi, itakuwa na manufaa makubwa zaidi kuliko kuwapatia mitaji tu. Shida kubwa zaidi ni kwamba wakishafanya kazi wanakuwa hawajalipwa. Kwa hiyo, hizi *bonds* kama zitatumika katika kuwalipa itakuwa imeleta tija kubwa sana katika kwenda kwenye hiyo miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo nilikuwa nataka nilizungumzie katika hiyo ni ubunifu. Fedha za ujenzi hazitoshi katika miundombinu hiyo, kwa hiyo, inatakiwa kuwe na ubunifu mkubwa sana katika kupunguza gharama. Kwenye *level* ya miradi tunasema ni *value engineering*. Kwa hiyo, hiyo ikikuzwa ikaenda hadi kwenye *level* ya mipango, utaona kwamba tunaweza tukafanya kazi kubwa zaidi kwa kutumia rasilimali chache tulizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia *TARURA,* imeshaanza na tunaipongeza, kwani imerudi kule nyuma kwenye kutumia teknolojia ya mawe. Tumeona imeanza kujenga madaraja ya mawe ili kupunguza gharama za ujenzi ili tuweze kupata miundombinu mingi zaidi kwa fedha iliyopo. Vilevile, tumeona, na ukiangalia ukurasa wa 29 wa bajeti ya Mheshimiwa Waziri inaonekana kwamba anatumia teknolojia mpya ya *EcoRoads, Ecoenzyme* na *Polyster*. Teknolojia hizi lengo lake ni kupunguza gharama za miradi. Hivyo, ubunifu huo tunaomba uendelee na wapate wafanyakazi wenye weledi wa kuweza kufanya hizo tafiti ili teknolojia hizi mpya ziweze kuwasidia katika kupunguza gharama kwenye miradi hiyo mbalimbali…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. ENG. DKT. LEONARD M. CHAMURIHO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Eng. Dkt. Leonard Chamuriho. Nilimtaja Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, ajiandae.

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hotuba ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambazo anaendelea kuzifanya katika Taifa letu. Kama ambavyo wenzangu wameshasema, hakika kuna miradi mingi sana iliyopatikana kwenye maeneo yetu. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi, tunapongeza kwa uimara wake kama ambavyo wenzangu wameshasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane nao kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi anazofanya katika nchi yetu. Leo wana Busega wamenituma nije nimshukuru sana kwa miradi mkubwa ya maendeleo, ambapo tumepata zaidi ya shilingi bilioni 67 katika miaka minne ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mama Samia Suluhu Hassan. Hakika haya ni mafanikio makubwa sana kwa wana Busega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, mtani wangu, kaka yangu Mheshimiwa Mchengerwa kwa kazi kubwa anayoifanya. Hakika Wizara imepata mkunaji; na anafanya kazi nzuri pamoja na wasaidizi wake, Comred Dugange pamoja na dada yangu Zainabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tuwapongeze sana kwa kazi kubwa wanazozifanya katika Wizara yetu ya TAMISEMI. Pia kuna wasaidizi wao ambao ni Katibu Mkuu pamoja na timu yake. Tunawapongeza sana kwa kazi nzuri wanazozifanya kwenye hii Wizara yetu ya TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane na wengine ambao wamempongeza Mkurugenzi wa *TARURA,* kaka yangu Seff, na

mimi nampongeza sana. Kwa kweli baba huyu amekuwa ni msikivu na anatusikiliza Waheshimiwa Wabunge. Hata ukienda kwake, hawezi kukukataa, atakwambia nipe muda nitafanyia kazi, na kweli anakuja kufanyia kazi. Hakika mtu huyu ni mtu sahihi, endeleeni kumshikilia ili alisaidie Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, nichukue nafasi hii kumpongeza sana kijana mwenzangu Mkuu wetu wa Mkoa wa Simiyu, kaka yangu Kenani Kihongosi, kwa kweli ni kijana ambaye ameendelea kuwa imara sana katika Mkoa wetu wa Simiyu, na ameendelea kuonesha vizuri kwamba mkuu huyu wa Mkoa ameamiwa akiwa kijana, kwamba kijana anaweza, na hata wengine wataendelea kuaminiwa kwa kuwa yeye ni moja ya *sample* ya vijana ambao wameaminiwa na wameweza kuhudumia Mkoa wetu wa Simiyu vizuri. Hakika amesimamia miradi mingi ya maendeleo katika Mkoa wetu wa Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nampongeza sana Mkuu wetu wa Wilaya, dada yangu Faiza Salim, hakika Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Mchengerwa ametuletea Mkuu wa Wilaya kwa wakati sahihi, na mtu sahihi. Hakika sisi kazi yetu ni kukaa hapa Bungeni, mambo ya usimamizi wa miradi ya maendeleo Mkuu wa Wilaya yupo kule Busega anafanya kazi vizuri. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri amwangalie kwa jicho la pili. Pale Busega bado tunaye na tunataka tutambe naye kwa kazi nzuri ambazo ameendelea kuzifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza Wakurugenzi, nimeona wamekuja kwa wingi hapa, wanaendelea kusimamia miradi yetu ya maendeleo, akiwemo na Mkurugenzi wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, nami nilete ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Rais aliwaahidi wana Lamadi stendi na soko, na ninaamini katika mpango wake ameviongelea. Kwanza nampongeza kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Rais angalau kuanza na fedha zaidi ya shilingi bilioni moja kwa ajili ya miradi hii miwili. Sasa ametupa sisi tuchague. Sisi tunachagua

kipaumbele cha kwanza kwenye miradi hii ya kimkakati, mradi wa stendi pale Lamadi kwa sababu hakuna kabisa stendi, na ni barabarani, watu wamekuwa wakigongwa na magari, wanakufa, wanapoteza maisha mahali pale. Sasa ni vizuri tukianza na stendi ili wananchi wetu waweze kuondokana na adha kubwa ambayo wanayo pale Lamadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza kwa sababu ameiweka kwenye mpango, nasi tunamshukuru sana, na tunamshukuru pia Mheshimiwa Rais. Watakapopata na fedha nyingine, basi tuangalie na hili soko ili tuweze kumaliza hii miradi ambayo ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, na stendi ambayo sasa inaenda kuanza katika mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kuanza na hii shilingi bilioni moja ambayo nimeiona imewekwa kwenye mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Zainab kwa kuniletea memo ikionesha kabisa kwamba sasa Serikali na Wizara ya Fedha imetoa kibali kwa ajili ya stendi hii ya Lamadi. Wana-Lamadi tunawapongeza sana na wana-Lamadi wanasema wanatamba na Mheshimiwa Rais, wanaye na wanaendelea kumshikilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, pale Lamadi tulileta andiko letu kwa ajili ya kituo cha afya. Ni imani yangu kwamba kwenye orodha ya vituo vya afya watatuletea fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya pale Kabita. Kata ya Kabita ina zaidi ya wananchi 36,000. Sasa ni muda muafaka wa kupatiwa kituo cha afya ili waweze kuwa na sehemu ambako wanapata matibabu kwa urahisi kuliko sasa ambapo wanakwenda kata nyingine, zaidi ya kilometa kumi, kwenda kutafuta matibabu. Tukiwapatia kituo cha afya litakuwa jambo la msingi na wananchi wa Kabita wataendelea kunufaika na suala zima la kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikiuzungumza hapa zaidi ya mara tatu nikimtania rafiki yangu Mheshimiwa Dkt. Dugange. Wakati akiwa *RMO (Regional Medical Officer)* kule Shimiyu; Mheshimiwa Mchengerwa kama ulikuwa hujui, huyu

alikuwa Mganga Mkuu Mkoa wa Simiyu. Yeye mwenyewe kwa mwandiko wake alikipandisha hadhi Kituo cha Afya pale Lukungu Kata ya Lamadi. Akapandisha hadhi zahanati iliyokuwa pale Kiloleli na kuwa kituo cha afya, lakini bahati mbaya sana amepandisha kwa jina tu, lakini miundombinu haifanani na vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine naendelea kumwomba, tuviangalie kwa mara ya pili, kwa sababu viliidhinishwa na Naibu Waziri mwenyewe; na kwa sababu yupo, basi aandike tu pale ili sasa tuweze kupata wodi mbalimbali ambazo zinahusika kwenye vituo vyetu vya afya, zikiwemo wodi za wazazi, akina mama, watoto, wodi ya wanaume na wodi nyingine ambazo zinatakiwa kuwa kwenye vituo vya afya. Hilo ni ombi langu sana. Kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Dugange hawezi kukwepa hapa, kwa sababu ni moja ya watu ambao walipandisha hadhi eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine la pili kwa Kata yetu ya Kabita, wametuletea *ceiling* ya ujenzi wa shule mpya shilingi milioni 584. Nawashukuru sana kwa *ceiling* hii kwa ajili ya bajeti ya mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Mheshimiwa Mchengerwa, kwenye Kata yetu hii ya Kabita tuna shule ambayo imeanzishwa na wananchi. Shule hii ina majengo machache. Sisi kama Wanabusega, kama Wanakabita, tunawasilisha andiko kwake, fedha hizi shilingi milioni 584 ziende zikaboreshe eneo hili ili shule hii ya Venance Mabeyo ambayo imepewa jina la *CDF Mstaafu*, iweze kupata miundombinu mingi na iweze kuhudumia wananchi ambao wako kwenye haya maeneo ya Kata yetu ya Kabita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kuhusu *TARURA*. Nawashukuru sana, jana yule mkandarasi ambaye alikuwa anadai shilingi milioni 133, yeye mwenyewe amenipigia simu kwamba amelipwa fedha zake, nami kwa mamlaka yangu ya kawaida nimemwambia kwamba siku mbili awe *site,* na

tumekubaliana ndani ya siku mbili atakuwa *site* kwa ajili ya ujenzi wa daraja la wananchi wetu wa Kata yetu ya Rutubiga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nahukuru sana kwa ajili ya fedha hizi, shilingi milioni 133. Kwa kweli mkandarasi huyu atakapomaliza zoezi hili la ujenzi wa daraja, litakuwa mwarobaini wa Kata hii ya Rutubiga, hasa kwenda kwenye vijiji vya pale Rutubiga pamoja na Mwasamba. Daraja hili litaenda kuunganisha mawasiliano ya barabara. Pamoja na hapo, tutakapomaliza daraja hilo, tutatengeneza barabara ya kilometa 4.2, na wananchi wa kata yetu ya Rutubiga watafurahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna barabara moja ambayo itabaki maeneo yale kutoka pale Rutubika kwenda pale Mwakiroba. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri ahakikishe kuwa barabara hii nayo inaingia kwenye mpango ili wananchi wa maeneo hayo nao wanufaike na barabara hii ambayo tayari daraja lake linakwenda kumalizwa kujengwa kwa fedha ambazo ametuletea na ambazo zimeidhinishwa na Mama Samia ambazo ni kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Busega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna barabara nyingine za kimkakati. Barabara ya kutoka pale Ngasamo kwenda kule Kisesa nayo imeharibika sana kwa sababu ya mvua. Barabara hizi nazo zinatakiwa zitafutiwe fedha ya dharura ili tuweze kutengeneza kwa sababu zimeharibiwa sana na mvua. Barabara nyingine ni kutoka pale Ngasamo kwenda kule Sanga na yenyewe imeharibika. Hivyo, nayo itafutiwe fedha ya dharura ili wananchi wetu waweze kunufaika na barabara ambazo ni za kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana. Nirudie maneno ambayo niliyasema katika bajeti iliyopita. Mama Samia tunaye na tunatamba naye. Hata maneno ya Biblia yako wazi. Ukisoma Ufunuo wa Yohana 3:11 iko wazi kabisa inasema, " Shika sana ulichonacho, adui asije akatwaa taji yako."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuendelea kumshikilia sana Mama Samia kwa sababu hata maandiko yameandika kwamba

shika sana ulichonacho. Sisi Wanabusega tunamshikilia Mama Samia mpaka kieleweke. Tunaye na tunatamba naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile. Nilimtaja Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mheshimiwa Samwel Xaday Hhayuma, ajiandae.

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja ya Wizara ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ambayo inaongozwa na mdogo wangu Mheshimiwa Mchengerwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kwanza kumpongeza Mwenyekiti wa Chama chetu cha Mapinduzi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwa Tanzania. Vilevile, kwa kazi kubwa ambayo ameifanya katika Jimbo la Morogoro Kusini na Halmashauri ya Morogoro Vijijini. Zaidi ya shilingi bilioni 180 zimepelekwa katika Halmashauri yetu kwa ajili ya kuleta maendeleo kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mchengerwa na wasaidizi wake; Naibu, Dada yangu Mheshimiwa Katimba, na Mheshimiwa Dkt. Festo, Katibu Mkuu na watendaji wote katika taasisi ambazo ziko chini ya Wizara hiyo; *TARURA* na nyingine zote, kwa kazi kubwa ambazo wanazifanya katika kumsaidia Mheshimiwa Rais, kutimiza maono yake. Maana ukiangalia tu Wizara hii inaitwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ni kwamba imebeba mambo makubwa katika ustawi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utaanza kwenye upande wa *TARURA*. Nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika kuipatia *TARURA* fedha za kusaidia kuleta maendeleo ya barabara katika majimbo yetu. Nikikumbuka kwamba wakati Mheshimiwa Rais anaingia, na

wakati mimi naingia katika Bunge hili la pili, Halmashauri ya Morogoro Vijijini ambayo ina majimbo mawili; la kwangu na la mdogo wangu Mheshimiwa Tale, tulikuwa tunapata shilingi milioni 880 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunavyozungumza, kila Jimbo tunapata shilingi bilioni mbili na *point*. Hii ni kielelezo tosha kwamba kuna kazi kubwa imefanywa na kuna mambo makubwa yamefanyika. Ukiangalia barabara za wakati ule zilizokuwa zinatengenezwa na za sasa hivi zilizotengenezwa ndani ya kipindi cha miaka minne, kuna kazi kubwa imefanyika. Ukiangalia kule Bungu, Kibungo Juu, Kasanga, Kolelo, Tawa, na Kibogwa kuna mambo makubwa yamefanyika na yanastahili kupongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali, Halmashauri ya Morogoro Vijijini, katika kilometa za barabara tulizokuwa nazo ni 700 kwa majimbo mawili. Jimbo langu tupu lina kilometa 305. Hata hivyo, katika jimbo langu kuna kata 17, kata tisa ziko milimani. Tunashukuru kwa kiasi hiki cha fedha tulizopewa, lakini naomba Serikali iangalie ni jinsi gani tunaweza tukaongezewa fedha hasa kwa kata hizi za pembezoni (milimani) ili tuweze kujenga barabara na wananchi wetu wakafikika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijaribu kuangalia barabara za milimani, zinahitaji kujengwa kwa zege na zinahitaji kujengwa kwa mawe kama tulivyofanya kwenye barabara ya Dakawa, kama tulivyofanya kwenye barabara ya kwenda Bwakila Juu, barabara ya kwenda Kibogwa na barabara ya kwenda Kibungu Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, hebu tusaidieni kutuongezea bajeti. Katika Halmashauri ya Morogoro Vijijini, tunahitaji bajeti ya karibia shilingi bilioni saba mpaka shilingi bilioni nane. Sasa hivi tunapata shilingi bilioni nne, hebu tusaidieni kutuongezea walau tufike hata shilingi bilioni saba, pengine tunaweza tukatatua changamoto za watu na kuweza kusaidia kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, niipongeze *TARURA* kwa kazi zinazoendelea. Pia, niendelee kumwomba ndugu yangu Seff,

nilikwenda ofisini kwake kuomba fedha kwa ajili ya ujenzi wa Barabara ya Konde – Kiswila ambapo kule kuna kiwanda kikubwa cha karafuu ambacho tunategemea kujenga. Sasa, tuliomba fedha kiasi kama cha shilingi bilioni moja, tupate ili tuweze kutengeneza barabara hiyo ijengeke ili kiwanda kile walau kijengeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakuomba kupitia Bunge lako, *TARURA* waangalie jinsi gani wanaweza kutupatia fedha hizo ili zikafanye kazi hiyo na kutusaidia kuondokana na changamoto ambazo wananchi wetu wanazipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa barabara, naomba hebu tujaribu kuangalia, kila mwaka tunatenga fedha za kujenga barabara kwa kiwango cha changarawe. Sasa kuna wengine wamesema lami, lakini kwetu sisi wa milimani tungeomba tuongezewa fedha na twende tukatengeneze barabara zetu kwa kiwango cha zege na mawe ambazo zitakuwa zinapitika mwaka mzima na vilevile, wananchi wetu watakuwa wanafaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo langu la pili ambalo ningependa kuzungumzia ni kwenye suala la afya. Nina kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya kwenye upande wa afya nchi nzima. Wakati tunaingia Bungeni, kwenye Bunge hili la pili, kwenye halmashauri yetu ya Morogorogo Vijijini tulikuwa hatuna Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya. Hata hivyo, hivi tunavyozungumza tumepelekewa zaidi ya bilioni ambayo imeweza kujenga Hospitali ya Wilaya, lakini wameweza kukamilisha jengo la utawala la hospitali, tumeweza kufikia mpaka kuweka vifaatiba kama *X-Ray* na mambo mengine. Vilevile, tumeweza kujenga zahanati tano mpya: Zahanati ya Kisemu, Zahanati ya Kisaki, na Zahanati ya Kasanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, katika zile zahanati nyingine ambazo tulikuwa tumeambiwa tunaweza tukapata, ombi langu kwa Serikali, mtusaidie kujenga zahanati katika kata za milimani ikiwemo Kata ya Singisa, Kata ya Bwakila Juu, na Kata ya Kolero ili tuweze kuwafikishia huduma wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri kata zote hizo tayari nimeshazipeleka kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Mchengerwa. Ni imani yangu kuwa muda ukifika katika vile vituo vya afya ambavyo kila Mbunge atapewa, basi fedha ziende na wananchi wakapate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili napongeza kwenye suala la afya. Tumeweza kujenga zahanati mpya Mwambani, Ngong'olo, Gozo, Kiswila na Mgata, zahanati ambazo wananchi walijenga na TAMISEMI ilipeleka shilingi milioni 50 ambapo tumekamilisha bila tatizo na zinatoa huduma kwa wananchi wetu. Tuna kila sababu ya kumpongeza Mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, tuna changamoto kwenye suala la afya, kwa upande wa watumishi. Tumekamilisha majengo, lakini tunahitaji kuwa na watumishi. Tatizo kubwa tulilokuwanalo katika Halmashauri yetu ya Morogoro Vijijini, tuna changamoto ya Madaktari wa Usingizi na Madaktari wa Meno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna changamoto ya ukarabati wa vituo vya afya ambavyo viko kwenye Jimbo langu ambavyo ni Kituo cha Afya cha Tawa, Kituo cha Afya cha Dutumi, Kituo cha Afya cha Ngerengere kwenye jimbo la pacha wangu na Kituo cha Afya cha Mkuyuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna changamoto ya magari. Tunahitaji gari jipya la *ambulance* katika Hospitali ya Wilaya. Nashukuru na ninatoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais kwa *ambulance* ambayo ametupatia, ambayo kwangu niliipeleka kwenye Kituo cha Afya cha Dutumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa elimu, tuna kila sababu ya kumpongeza Mama Samia Suluhu Hassan. Ndani ya kipindi kifupi amefanya mambo makubwa. Kubwa zaidi ambalo nataka niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mama huyu toka ameingia, miaka ya nyuma kila ilipofika mwezi Desemba, Madiwani tulikuwa na hangaiko la kuwachangisha wananchi wetu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, ambapo kulikuwepo na watoto wanaingia kwa *first selection* na

second selection, lakini ndani ya kipindi cha Mama Samia, hakuna jambo hili. Watoto wote walikuwa wanaingia kwa wakati mmoja na hivyo hata ufaulu ulikuwa unaweza kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejenga shule mpya tano za sekondari. Tumejenga katika Kata ya Bungu, Kata ya Kisaki, Kata ya Kongwa ambayo ni ya ufundi, lakini Dutumi tumeongeza shule maalum ya akina mama. Dakawa tumeongeza shule nyingine kwa ajili ya kupunguza watoto kutembea umbali mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali, pamoja na mafanikio haya, bado kuna changamoto. Mimi ninakotoka ni katika Jimbo ambalo lina changamoto kwa sababu liko milimani. Kule milimani hatuwezi kuongeza shule nyingine za sekondari kwa sababu watoto ni wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kutoka kwenye Makao Makuu ya Kata kwenda kwenye vijiji ni mbali. Ombi langu kwa TAMISEMI, katika yale majengo ambayo mnataka kuyajenga kwa ajili ya mabweni, tunaomba mtupatie mabweni kwenye Shule ya Sekondari ya Kibogwa, Shule ya Sekondari Kibungo Juu, Shule ya Sekondari Bwakila Juu na Shule ya Sekondari ya Singisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda kulizungumzia na ambalo niliombe kwako Mheshimiwa Mchengerwa, kuna maboma mengi ambayo wananchi wameyajenga na wangependa Serikali itie nguvu. Kuna maboma kwa ajili ya madarasa, nyumba za walimu na maboma kwa ajili ya zahanati. Ombi langu kwako, naomba zile fedha ambazo zimetengwa zije katika Jimbo la Morogoro Kusini na katika Halmashauri ya Morogoro, tukakamilishe kazi ya wananchi ili wakati ukifika tufanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nina ombi moja lingine. Kuna wataalamu wa sekta mbalimbali kwenye halmashauri zetu na kata zetu. Sasa hivi TAMISEMI tunapeleka fedha nyingi kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya ujenzi, na tunawakabidhi madaktari na walimu ambao hawana utaalamu huo. Ombi langu ni

kwamba tuangalie uwezekano wa kuajiri vijana waliosomea fani ya uhandisi wakasaidie kusimamia fedha hiyo na matokeo yake yakaonekane kuwa mazuri.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninaunga mkono hoja. Nataka kusema tu kwamba, miaka mitano kwa Mama Samia, haina mjadala. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris. Nilimtaja Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo na Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, wajiandae.

MHE. SAMWELI X. HHAYUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye bajeti yetu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia uzima, afya na hatimaye tumeweza kuwatumikia wananchi wetu kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Mwenyeiti, vilevile, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pia, namshukuru Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Mchengerwa na Naibu Mawaziri ambao siku zote tumekuwa tukishirikiana nao; Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, pamoja na ndugu yetu Mheshimiwa Katimba; watumishi wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI wakiongozwa na Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na watumishi wote. Vile vile kwenye ngazi zetu za mikoa tumekuwa tukishirikiana nao vizuri katika kusimamia miradi ambayo tunapata fedha kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa maana ya Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya dada yangu Almishi,

tunashirikiana naye vizuri, Mkurugenzi, Theresia Irafay anasimamia miradi na anasimamia watumishi wake vizuri. Pia nawashukuru sana Waheshimiwa Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji ambao mara zote tumekuwa tukishirikiana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka 2025, hii ni bajeti ya tano ambayo sisi tunapitisha kwenye Bunge hili la Kumi na Mbili. Shughuli nyingi zimefanyika na ndiyo maana nawashukuru wote wakiongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kazi aliyoifanya ni kazi ya kupigiwa mfano na tunasema kwa kazi hii aliyoifanya yote ambayo sisi tunapaswa kulipa Oktoba wakati wa kurudisha *change*, tutarudisha *change* ya kutosha. Wanahanang wanaahidi kwa yote ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameyafanya, sisi tunalo deni na deni hilo tutalilipa kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu niseme machache. Kwenye sekta ya afya, sisi tulikuwa na hospitali ya wilaya ambayo imechoka sana. Kwa sasa tumepeleka zaidi ya shilingi bilioni 2.5 ambapo tumeboresha majengo yaliyopo, tumejenga majengo mapya ikiwemo jengo la *emergence, maternity complex* na tumeweka vifaatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejenga vituo vya afya vipya vitano kwenye kipindi hicho kifupi, lakini tumekamilisha zahanati ambazo tumeombea fedha; Zahanati ya Gabadaw, Garawja, Gisiyal, Garbapi, pamoja na Dang'aida. Hizi tukizijenga tunafikisha zahanati 15 ndani ya muda huo mfupi. Maana yake ni kazi kubwa imefanyika kwenye sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo kwenye sekta ya elimu tumeboresha Shule ya Nangwa *High School; Mulbadaw Secondary* majengo yaliyopo pale ni ya kisasa sana. Vilevile, Katesh ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya hatukuwa na *high school*, lakini kwa sasa imepandishwa hadhi tuna *high school.* Ukizichanganya pamoja tuna *high school* nne na tunatarajia nyingine mbili zipande hadhi, baada ya hapo tutakuwa na *high school* sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajengewa *VETA* pale Nangwa, lakini tumejenga shule za sekondari mpya. Tukikamilisha shule inayojengwa Dawar, Jorodom na baada ya kujenga Shule Gendabi, ndani ya muda huo tutakuwa tumejenga jumla ya shule sita za sekondari. Vilevile, tumeboresha shule za msingi kwa maana ya kuongeza madarasa, shule mpya pamoja na kukarabati shule. Hii ni kazi kubwa ndani ya muda huo mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Mji wa Katesh ambao ndiyo makao makuu ya wilaya, pale tunakamilisha ujenzi wa stendi mpya ya kisasa. Kanda nzima ya Kaskazini huwezi kuona stendi nzuri kama hiyo. Stendi ile pale Katesh Mjini imepewa jina la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Vilevile, tumeomba fedha kwa ajili ya kujenga jengo jipya la Halmashauri. Tumeidhinishiwa fedha za awali, tunachoomba tu ni fedha hizo zitolewe kwa wakati, ujenzi ule uanze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ukienda Katesh Mjini hatukuwa na kilometa hata moja ya lami inayoingia pembeni. Kwa sasa tumejenga zaidi ya kilometa 4.5 ndani ya muda huo mfupi. Pamoja na kwamba tuliomba kilometa 10, unaona kazi ikiendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa barabara tumefungua barabara mpya zaidi ya 10 kwa kipindi kifupi. Nitaje barabara chache ambazo kwa kweli kwa Wanahanang ilikuwa ni kilio kikubwa. Tuna barabara inayoanzia Waama, inakwenda Diloda inatokea Mureru, wananchi wale walikuwa wanapata shida sana wakitaka huduma za afya, wakitaka kusafirisha mazao yao changamoto ilikuwa kubwa kwa sababu ya barabara hii lakini sasa barabara hiyo imefunguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna barabara ya Masakta – Lambo – Ng'alda kwenda Masqaroda, wananchi wanafurahia huduma ya barabara kwenye eneo hilo. Hata hivyo, tuna Kata ya Mulbadaw na Kata Bassodesh, kabla mvua ilikuwa ikinyesha Kata ya Bassodesh inakuwa kama kisiwa, kwa sasa tumeunganisha na barabara. Barabara hizo zimeendelezwa na kuhudumiwa nazo ziko kwenye hali ambayo inaridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio haya kwenye eneo la barabara, tunayo changamoto kidogo ambayo Mheshimiwa Waziri Mchengerwa, yeye anaifahamu. Nimemwandikia barua mwenyewe kwa mkono wangu, nimempelekea ofisini kwake, tumekaa na kujadiliana. Tuliomba fedha kwa ajili ya kukarabati zile barabara ambazo ziliathirika na maporomoko ya Mlima Hanang. Barabara hizo ni Barabara ya Endasak– Dawar, Barabara ya Mogitu – Gendabi, Barabara ya Jorodom – Nangwa, Barabara Nangwa – Gitting, Barabara za Mji wa Katesh, Barabara ya kutoka Katesh – Dumbeta – Mureru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliomba fedha za barabara hizo na Mheshimiwa Waziri ulivyochakata akasema, basi tutawaidhinishia shilingi bilioni 4.7. Mpaka sasa hizo fedha tunazisubiri. Tunachoomba sisi Wanahanang, atuharakishie ili hatimaye tuweze kurekebisha hizo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingine ambazo ziliharibika na mvua iliyonyesha kwenye msimu wa 2023/2024 na 2024/2025, kwa kweli tuliomba fedha za dharura. Barabara ya Mogitu – Balang'dalalu, tuliomba shilingi milioni 800; na Barabara ya Endagaw – Gidahababieg, tuliomba kama shilingi milioni 600. Barabara hizo kwa sasa hazipitiki kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huu ni wakati wa mavuno. Tunachoomba, zile fedha za dharura tulizoomba ukijumlisha kwa pamoja zinakuwa kama shilingi bilioni tisa hivi. Kwa sababu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameleta ubunifu wa kisasa wa *bond* ambazo mlitarajia kukusanya za shilingi bilioni 150, mmepata zaidi ya shilingi bilioni 350, hizo fedha zije ziwasaidie wananchi na kukarabati hizo barabara na hatimaye tupate raha ya kutumia Mji wetu wa Katesh na maeneo yale ambayo maporomoko yaliathiri barabara zake ziweze kutengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna changamoto kwenye upande wa sekta ya afya. Tumejenga, lakini tunazo kata kubwa kwa mfano Kata ya Gitting ambayo ina watu zaidi ya 17,000, inahitaji kujengewa kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija Kata ya Gendabi, pale kuna Kituo cha afya cha *private*. Wananchi wamelalamikia kwa muda mrefu kuhusu suala la gharama kubwa kwenye eneo hilo. Vilevile, ukija kwenye eneo la Balang'dalalu, hiyo ni kata kubwa kweli kweli na ina watu zaidi ya 19,000, na ni Makao Makuu ya Tarafa ya Balang'dalalu. Tunaomba kwenye eneo hilo tujengewe kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Hidet ambalo kwa kweli jiografia yake kwenda kwenye Makao Makuu ya Tarafa ya Simbay ni ngumu sana. Wakati tunafikiria kuendelea kujenga barabara, kabla ya hapo tujengewe kituo cha afya kwenye eneo la Kata ya Hidet.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha, kazi kubwa imefanyika. Namshukuru sana *Chief* wa *TARURA*, mara zote tukienda kwake amekuwa akitusaidia. Barabara tulizoomba za mwaka 2024/2025, barabara ziliidhinishwa kwa 60% tu zitangazwe. Nina barabara yangu moja muhimu ya kuunganisha Makao Makuu ya Tarafa na Kata ya Gehandu, barabara inayotoka Balang'da – Gidabwanja inakwenda Gehandu, barabara hiyo ilikuwa haijawekewa fedha. Nimekwenda nimeomba, na akawa ameahidi kwamba atatafuta fedha na nimepata taarifa kuwa zimepitishwa shilingi milioni 200 kwa ajili ya kujenga barabara hiyo. Naomba hizo fedha zipatikane kwa wakati ili ujenzi huo uanze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nasema Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi ambayo amefanya, nimesema sisi tuna deni naye na Wanahanang kwa yale mazuri aliyotufanyia wakati ule wa maafa. Wanahanang wameniambia, nenda ukamshukuru na sisi tutamshukuru vizuri zaidi Oktoba na wakati ule atakapotutembelea kudai *change* yake ambayo kwa kweli *change* sisi tunayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Samwel Xaday Hhayuma. Tunamalizia na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, atakuwa wa mwisho.

MHE. PRISCUS J. TARIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii niliyoipata kwa ajili ya kuchangia bajeti hii kubwa kabisa ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa miradi mingi sana ambayo sitaitaja hapa ambayo imekuja Moshi Mjini. Ninachoweza kusema tu ni kwamba Mheshimiwa Rais kwa Moshi Mjini sisi hatumdai. Hata kwenye bajeti hii ninachoomba ni ile ya kujazia juu ya keki wanasema *icing,* lakini ambavyo vimeshakuja kule vinatosha kabisa kufanyia kazi na Mungu ambariki ampe afya ili tufikie Oktoba na tuweze kumu-*endorse* kwa kura nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mawaziri na Watendaji wote. Napenda tu kusema, wengi wametaja timu nyingi nyingi lakini hiyo timu yao hapo ninavyoiona ni kama timu ya Barcelona vipindi viwili tofauti: kipindi alipokuwepo Messi, Neymar na Suarez na kipindi hiki ambacho yupo Lamine Yamal, Raphinha na Lewandowski. Kwa hiyo, nawapongeza sana, Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wote wawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa ushauri. Kule tulikotoka kwenye upungufu wa watumishi hasa kwenye kada mbalimbali, nina maoni hapa ambayo najua yanaweza yakasaidia. Upungufu wa watumishi kwa mfano nichukulie kada ya Watendaji wa Mtaa na wa Kata. Jambo la kwanza ambalo naliona, kwa sababu nilishawahi kufanya nao kikao, ni suala la mshahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu mwenye *Diploma* ambaye ameajiriwa kama Mtendaji wa Mtaa mshahara wake ni karibu nusu ya mtu mwenye *Diploma* aliyeajiriwa kwenye kada nyingine kwa mfano pale uvuvi. Walinipa mfano unakuta mtu anaanza na shilingi 480,000/=, kule mtu anaanza na shilingi 700,000/= mpaka shilingi 900,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini sasa kunakuwa na upungufu kila mara kwetu, katika kada zote TAMISEMI? Kwa sababu mishahara iko chini, watu wanaomba kule hata kama ana vyeti vingi. Unakuta ana *Masters,* lakini anaomba kwa kutumia hiki cha *Diploma* ili aingie apate *check number;* akishaingia pale anapambana kutafuta maeneo mengine ya kuhamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wenzetu wa utumishi wakiweza kufanya msawazo kwamba mishahara ya kuanzia kama ni *Diploma* Serikalini waanzie kiasi labda ni hiki kwa wote. Hilo kwanza, litaanza kupunguza upungufu kule kwenye maeneo yetu hasa TAMISEMI. Kwa mfano Watendaji wa Mitaa na Watendaji wa Kata walikuwa na maombi *specific*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku nimeona mmeongelea masuala ya nyumba zao, wao wamesema angalau pikipiki kama usafiri wa kuwasaidia kuzunguka kwenye ile mitaa, vijiji na kata kama walivyofanyiwa wale wa Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nimeona linaweza kusaidia ni kuona namna ambavyo baada ya muda wale walioanzia kwenye kada hiyo wanapata *promotion* ikiwemo pamoja na teuzi mbalimbali. Kwa hiyo, yule mtu anaweza akaamua abaki, lakini asubiri kwamba kuna neema hapo juu lakini anapobaki halafu haoni kuna neema, wanakuwa wanaendelea kuomba maeneo mengine na unajua siku hizi watu wanajisomesha, akipata eneo lingine anaondoka. Kwa hiyo, kule tunaendelea kubaki na upungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo nilikuwa ninafikiria hasa yale maeneo ya kijijini ambayo watu wamekuwa wakihama sana, tulikutana nalo kwenye Kamati ya *LAAC,* tulitoa ushauri, sasa hivi Tanzania nzima ina wasomi. Yale maeneo yenye shida sana, watu wanahama sana, kwa sababu huko nyuma kidogo tuangalie namna ya kuajiri wenyeji wa kule kwa sababu sasa hivi watu wenye *Diploma* na *Degree* sasa hivi Tanzania nzima wapo. Inaweza kupunguza ile morali ya kutaka kutoka hapo kwenda sehemu nyingine kwa sababu ameajiriwa eneo la

nyumbani na *cost* yake ya maisha inaweza ikawa ni ndogo. Kwa hiyo, nimeona kwa watumishi nianze na hilo, linaweza likatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri, sisi tuna hospitali ya wilaya, namshukuru sana Mheshimiwa Rais Mama Samia. Pia, naishukuru Wizara wanaendelea kutupatia fedha. Tofauti yetu na maeneo mengine yote Tanzania, hospitali yetu ya wilaya hatukuwa na eneo. Tumelijenga eneo la ekari sita, kwa hiyo, tumejenga kwa ghorofa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukipatiwa *portion* ile ile kwa mwaka, kazi ambayo unakuta tumeifanya kwa fedha ambayo wenzetu watakuwa wameenda mbali, sisi inakuwa kazi ndogo. Kwa hiyo, tunaomba ile *lumpsum* ya kuja kwa kila mwaka watuongozee au ikiwezekana watuhamishie kabisa Hazina tulipwe kwa *certificate,* itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, tumeshakwenda Wizarani pale, mimi Mstahiki Meya, Mkurugenzi, Afisa Mipango wetu, tukakutana na Cheyo. Nilishawahi kumfuata yeye binafsi zaidi ya mara moja na Naibu Waziri kuhusu Stendi ya Nganga Mfumuni wale *CRJE* imekwama kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale *CRJE* wana kazi nyingine maeneo mengine. Mkiwapa *commitment* na kwa sababu Wizara ya Fedha imeshakubali kulipa, watarudi *site*. Lile ni eneo letu la muhimu, Serikali imeshaingiza shilingi bilioni saba na ni chanzo cha mapato. Tunaomba sana mliangalie ili tuweze kuli-*jump start* limalizike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine, kipindi ambacho tuliunguliwa na Soko la Mbuyuni, nilimfuata Waziri tukiwa hapa kwa sababu liliungua tukiwa hapa, nikamwomba atusaidie fedha kwa ajili ya kwenda kulijenga upya lile soko na akaniahidi kwamba atanipatia, lakini tuliporudi kule, Mkurugenzi, Mstahiki Meya pamoja na Madiwani tukajibana tukatafuta fedha pale tukalijenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu tulilijenga kwa fedha zile za ndani, ile fedha iliyokuwa atupatie namwomba sana atusaidie iende kwenye Soko la Manyema ambalo lilikuwa ni ahadi ya viongozi wawili wakubwa. Alikuja Mheshimiwa Chongolo wakamlilia akasema atakuja kuomba na ameshaleta hayo maombi na alipokuja Dkt. Nchimbi pale Moshi pia walimwomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huyu Mheshimiwa Dkt. Nchimbi ni Makamu wa Rais ajaye, na ni Mgombea Mwenza. Sasa ahadi yake isipotekelezwa inaweza ikatuletea ugumu kidogo. Haitatuzuia kwa chochote, lakini kama ile fedha ambayo ilikuwa tupatiwe kwa ajili ya soko la Mbuyuni tutapatiwa, itatusaidia sana pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *option* ya pili ambayo naweza kuomba, kama bado hamjapata fedha, mtupe *commitment* ya fedha kwa sababu ilikuwa ni karibu shilingi milioni 600, kwamba mtaleta pale ili fedha ambayo itajenga vibanda Mbuyuni, tukae na halmashauri tuibadilishe iende ijenge Manyema. Hiyo fedha ambayo anatupatia ije kwenye vibanda kwa sababu pale Manyema tutakuwa tumefanya kazi kubwa zaidi kwa sababu wafanyabiashara pale ni kama 1,400.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukijenga vibanda 50 kwa shilingi milioni 500 tunaenda kuweka wafanyabiashara 50 tu pamoja na kwamba ni chanzo cha mapato. Kwa hiyo, hizo *option* mbili mojawapo akiweza kuifanya, atakuwa ametusaidia sana na soko letu la Manyema litakuwa linafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi niliuliza swali kuhusiana na Barabara ya *YMCA – KCMC*. Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye maadhimisho ya miaka 51 ya Hospitali ya *KCMC* aliombwa barabara mbili na alikubali zote na barabara moja ilikuwa imeshakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka *YMCA* kwenda *KCMC* ilikuwa imetengewa fedha, yalipotokea mafuriko ya *El-Nino* ikaondolewa. Barabara ile hatuwezi kuijenga kwa mapato ya ndani kwa sababu inajengwa kwa *double road* na itahitaji fedha

nyingi. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba sana kama inawezekana kwa sababu ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, basi tutafutiwe ile fedha ili tuijenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema ni muhimu kwa sababu gani? Kwa sasa hivi barabara ya Moshi – Arusha inajengwa kwa *double road,* barabara ya kuingia mjini kuanzia *YMCA* kwenda *roundabout* ya *NBC* inajengwa kwa *double road*. Kwa hiyo, kinakuwa kimebaki kipande hicho cha *YMCA – KCMC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ile ni muhimu kwa sababu ina taasisi zaidi ya 10. Ina *CCP,* Chuo cha Ushirika, Chuo cha Mwenge, *Uru Seminary*, *Old Moshi Secondary*, Hospitali ya Kibosho, *Kibosho Girls*, *Mweka Wild Life College* na kadhalika. Ni barabara ya muhimu sana kwetu sisi Moshi Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo wenzangu wengi wameshalitaja ni vile vituo vya afya. Nilikuwa naomba sana, vile vituo vya afya vya kimkakati Moshi Mjini niliomba kwa ajili Kiborloni. Nimeshawaambia na wanasubiri, na Kiborloni ni eneo lenye watu wengi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri afanye hima ili tuipate ile, Kituo cha Afya kiende Kiborloni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa vile vituo vya afya vya mapato ya ndani, naomba mtusaidie vikamilike kwa haraka kwa sababu sisi tulienda kujenga kule kwenye Kata ya Msaranga pale Mandaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la muda mrefu na nimeona kwenye ukurasa wa 119 kuhusiana na majiji. Nilishaleta maombi haya mara nyingi na bahati nzuri wakati wa mchakato wa Moshi Mjini kupanua mipaka yake au kuwa jiji, nilikuwa Diwani na nilishiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimtumia Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri *GN number* 219 ya tarehe 25 mwezi wa Sita mwaka 2016 ambayo ilisainiwa na Mheshimiwa Lukuvi. Kwa hiyo, sisi tulikuwa tumeshamaliza hatua zote. Hatua ile ilisimamishwa hivyo, tunaomba sasa turejeshewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyoomba hili, Moshi Mjini hatuombi kwa ajili ya *prestige*. Makaburi yamejaa, hatuna mahali pa kuweka makaburi mengine. Madampo yamejaa, tumeenda kununua Moshi vijijini zaidi ya kilometa 16, hatuna maeneo ya uwekezaji. Tuna uhitaji huo sana. Mheshimiwa Mchengerwa naomba sana hili la Moshi kuwa Jiji na kupanua kwenye ile mipaka ambayo tumeshamaliza hatua zote, utupe baraka tulikamilishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa ni kuhusiana na ushauri kwa *TARURA*. *TARURA* imekuwa *very efficient,* lakini kuna eneo moja lina changamoto ambalo ni eneo la ku-*repair*. Sasa unakuta wanatoa *tender* ya *repair* labda kipindi cha mwanzo wa mwaka. Mtu anachukua *tender* baadaye unakuta kuna *repair* ndogo ndogo hawawezi ku-*repair* kwa sababu wanahitaji mpaka watoe *tender*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tutafute *mechanism* aidha ya kuwa na mtu ambaye atakuwa ni *responsible* mwaka mzima au *TARURA* wawezeshwe kwa vifaa vidogo vidogo ili waweze kufanya hizo *repair* wenyewe.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. PRISCUS J. TARIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na ninaunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Priscus Tarimo. Tunamalizia na Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima.

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, niungane na wenzangu kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nampongeza pia Mheshimiwa Waziri na timu yake. Nina imani kwa uadilifu na uchapaji kazi wake, sina mashaka kwenye Wizara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mkuu wangu wa Mkoa Mheshimiwa Halima Dendego kwa usimamizi mzuri wa miradi yetu yote ya maendeleo na tuwakaribishe Mei Mosi inafanyika Singida Kitaifa. Tutakuwa na *Kuku Festival* siku moja kabla. Kwa hiyo, tunawakaribisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Singida Mjini wamenituma nije nimshukuru Mheshimiwa Rais kwenye jukwaa hili ambalo kwa miaka yote minne nimekuwa nikiomba fedha za miradi. Sasa nitumie jukwaa hili kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa kabla sijaeleza hayo, naomba nifanye rejea kwenye vitabu vyetu viwili vitukufu. Nikianza na *Quran*, inasema, "Kiongozi mzuri ni yule anayewa-*inspire* watu wake kwa matendo mema." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kwenye Bibilia ukirejea hadithi ya Yohana Mbatizaji akiwa gerezani alipotembelewa na wafuasi wake, naye aliamini kwamba, kwa kuwa yuko gerezani na Yesu anaweza kila kitu, angeweza kutoka kwa miujiza, akawatuma, "Nendeni mkamwulize yeye ndiye au tumsubiri ajae?" Bwana Yesu akawaambia, "Nendeni mkamwambie wafu wanafufuka, viwete wanatembea na vipofu wanaona," na akamalizia, "Heri yule asiyechukizwa nami." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema nini katika rejea hii? Ni kwamba, kiongozi anapimwa kwa matendo na siyo maneno. Kwa hiyo, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi ya vitendo ambayo ameifanya na sisi Wanasingida Mjini tunafaidika nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Singida Mjini tumepokea fedha za miradi zaidi ya shilingi bilioni 182. Ni fedha nyingi sana. Hatukuwa na Hospitali ya Wilaya, leo tunayo. Tumebakisha tu jengo la *OPD*. Kwa heshima ya Mheshimiwa Rais Mheshimiwa Waziri tuletee fedha tutengeneze jengo letu la *OPD*. Tulikuwa na kituo cha afya kimoja, leo tunavyo vinne. Katika elimu tulikuwa na shule moja ya sekondari, Mwenge Sekondari ya *Advanced Level*. Leo tutakuwa na shule sita za Kidato cha Tano na Sita, hii haijawahi kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu, leo tumejenga shule nne mpya za *O'Level* ambapo ilikuwa ni maajabu sana kujenga shule hizi. Jambo kubwa zaidi, tuna shule ya amali, Shule ya Sekondari ya Ufundi. Zimeletwa shilingi 1,600,000,000 katika Mkoa wa Singida. Lazima tumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miradi hiyo ambayo ametuletea Singida Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo nataka nishauri ni eneo la elimu, na nitafanya rejea ambayo Mheshimiwa Waziri amekuja nayo. Kwanza, amesema elimu yetu ni uhai wa Taifa letu. Hii ni *according to* Mheshimiwa Mchengerwa. Ni jambo jema sana. Pia, amekuja na rejea nyingine, "*Education is the most powerful weapon which you can use to change the world.*" Hii imetokana na Nelson Mandela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukirejea hizi *quotation* kubwa mbili maana yake unauona umuhimu wa elimu kwenye Taifa lolote duniani. Sasa nataka kusema nini? Elimu peke yake tumeshatengeneza miundombinu ya kutosha. Hatuna deni kwenye jambo hili. Tayari tuna shule, madarasa na kila kitu. Changamoto tuliyobakinayo ni ajira kwa walimu na hapa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ametuambia vizuri, Serikali imeajiri walimu 45,803. Hili ni jambo jema sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, mahitaji ya walimu mpaka sasa tunavyozungumza hayapungui 200,000, walimu wanaotakiwa kuwepo. Kama tunahitaji walimu 200,000 mpaka leo maana yake tuna-*deficit* ya walimu 200,000. Kwa hili, bado tuna kazi kubwa. Ni lazima Serikali ije na mkakati wa kuona namna ya ku-*accommodate* haya mahitaji ya walimu na wanafunzi wetu ama shule zetu ziweze kupata walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kushauri nini hapa? Nataka niishauri Serikali vizuri sana kwamba, sasa hivi kwa walimu hawa tulionaonao, vyuo bado vinaendelea kuzalisha na kuleta walimu. Bado tutakuwa na *gap* kubwa sana. Wakati inaendelea na utaratibu wake wa kuajiri, inaweza kutoa maelekezo, mwongozo

au waraka kwenye halmashauri zetu, wakatoa ajira ya muda kwa walimu ambao wanahitaji kufanya hii kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoa ajira ya muda kwa walimu hawa, utakuwa umepunguza hili *gap* ambalo tunalo na watoto wetu wanaweza kufundishwa kwa kile ambacho wanastahili. Tutatoa wanafunzi wazuri kuliko ambavyo sasa hivi tunasubiri ajira ambayo tunaitoa kidogo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza *education* ni *powerful weapon* ambayo inaweza kubadilisha dunia kuipeleka kwenye mwelekeo mzuri na chanya, tukiacha hivi maana yake hii silaha inaweza kuwa bomu la nyuklia ambapo baadaye litakuwa ni hatari zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuishauri Serikali itoe waraka. Waraka huu utafanya nini? Huku chini tuchukulie mathalan tu Manispaa ya Singida, sasa hivi kwa mwaka mzima tunakusanya kama shilingi bilioni sita. Katika shilingi bilioni sita, *category* yetu sasa hivi ni 60% fedha za maendeleo; tumetoka kwenye 40%. Maana yake kila mwezi tunakusanya shilingi milioni 500 na 60% yake ni shilingi milioni 300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi tunahitaji 20% tu kwa sababu tayari miundombinu imejengwa ya kutosha, 40% inatosha unaweza kuajiri walimu wa muda 200 ambao wanahitaji shilingi milioni 40. Wewe tayari kwa mwezi unapata shilingi milioni 60. Jambo hili litakuwa limetusaidia na hapa nimechukua *category* ya Manispaa. Sijagusa majiji mengine ambayo inawezekana kufanya zaidi ya hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri, wala hapa hahitaji kutumia nguvu. Sisi tayari tumeshajenga shule. Mheshimiwa Rais kajenga shule, kajenga madarasa na yote yana madawati, hivyo kashamaliza kazi yake. Siyo tu madawati, watoto leo wanasoma kwenye *tiles*. Maana yake kila kitu kiko vizuri. Tunahitaji walimu, na hao walimu wapo wala hatuendi kuwatafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutoe tu mwongozo wa kuzitaka halmashauri zetu kuweka utaratibu wa kutenga fedha kwa ajili ya ajira ya muda ambapo pia inawezekana kwa mapato ya ndani. Hoja yangu nilikuwa nataka nisimamie hapo, na niwaombe sana tufike mahali tuone umuhimu wa kupunguza hili *gap*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unapunguza kwenye eneo la walimu maana yake unaweza kupunguza pia kwenye eneo la afya na watumishi wengine ili kuweza kuleta ufanisi wa kazi kwenye maendeleo ambayo tunayatarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunalo soko moja kubwa sana Soko la Ipembe. Ndiyo tumebaki hapo. Mheshimiwa Waziri mimi nina jambo moja tu limebaki ambapo Soko hili la Ipembe nakumbuka mwaka 2024, Naibu Waziri kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Dugange alijibu swali akasema wakandarasi wataingia Desemba kwa ajili ya kuanza ujenzi wa soko hilo. Mpaka sasa hawajaingia, na sasa tumeingia kwenye bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, tumebakiza soko tu ili mji huu sasa, kesho tukuombe uwe jiji. Maana yake Soko hili la Ipembe lijengwe kuwa soko la kisasa. Tunahitaji fedha tu kwa ajili ya kujenga Soko hili la Ipembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tumebakiza kituo kimoja cha afya ambacho tayari kuna kata kama nne zinaizunguka kata moja, na katika vile vituo vya afya vya kimkakati tuliweka Kituo cha Afya cha Kata ya Kisaki. Hapa tayari tuna Kata ya Mwankoko ambayo ina zahanati, Kata ya Unyanga ina zahanati pamoja na Kata ya Unyamikumbi ina zahanati. Hii ukijenga kituo cha afya ita-*accommodate* hizi kata nyingine nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na wananchi wangu tumeshafanya juhudi za kutosha. Tumeshajenga jengo la *OPD* na Serikali ilituletea shilingi milioni 50. Tumebaki kwenye suala la umaliziaji ili tuwe na kituo cha afya. Naiomba Serikali iweze kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, huyo ndiye mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo. Nawashukuru wachangiaji wote kwa kazi nzuri mliyoifanya tangu asubuhi.

Pia, nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri, naona timu yote ipo hapo na mnachukua vizuri sana maoni ya Waheshimiwa Wabunge.

Baada ya kusema hayo, nawatakia jioni njema na ninaahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 2.17 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 17 Aprili, 2025, Saa Tatu Asubuhi)